# MAISHA NA HUDUMA YA YESU

Mwandaaji:
Dr. Randall McElwain

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

Hakimiliki· 2019 Shepherds Global Classroom
Toleo la Pili.

Haki zote zimehifadhiwa. Isipokuwa kwa kurasa za majaribio, hakuna sehemu yeyote katika kitabu hiki itakayotengenezwa au kutawanywa kwa njia yeyote ile ya – elektroniki, mbinu za utunzi mfupi, kunakili, kurekodi au vinginevyo- bila kibali kutoka Shepherds Global Classroom (SGC). Kila linaponunuliwa toleo la mtaala wetu wa SGC Kiswahili au Kiingereza kunatusaidia kufanya tafsiri kwa lugha nyingi ili kuvigawa kwa Viongozi wa Kikristo duniani kote. Kwa kuwasiliana na SGC au kuchangia katika maono haya ya kuvutia sana, ingia kwenye tovuti yetu: www.shepherdsglobal.org.

Labda iwe imeelekezwa vinginevyo, nukuu za maandiko yote zinatoka katika Biblia Takatifu, toleo la King James. Maandiko yaliyonukuliwa na kuwekewa alama "ESV®" yanatokana na tafsiri ya Biblia Takatifu ya Kiingereza ("English Standard Version®"), hakinakili © 2001 ya Crossway, huduma ya uchapaji ya Good News Publishers. *Tafsiri ya Maandiko "yaliyonukuliwa" kutoka chapisho la Kiingereza kwa ajili ya chapisho hili la Kiswahili yanatoka katika Biblia Takatifu ya Kiswahili, "Swahili Union Version Bible" (SUVB®)."* Yametumika kwa kibali. Haki zote zimehifadhiwa,

Tafsiri ya chapisho la Kiswahili:
Askofu Wilbert Alfayo Ngowi,
Arusha, Tanzania, East Africa.
E-mail: revwangowi@gmail.com

# Yaliyomo

Maelekezo Kwa Wakufunzi wa Darasa ........ 5

Ramani ya Palestina wakati wa Yesu ........ 6

(1) Maandalizi ya huduma ........ 7

(2) Kuomba kama Yesu ........ 25

(3) Kuongoza kama Yesu ........ 43

(4) Kufundisha kama Yesu ........ 63

(5) Kuhubiri kama Yesu ........ 83

(6) Yesu na Ufalme wa Mungu ........ 101

(7) Kuwa na upendo kama Yesu ........ 123

(8) Msalaba na Kufufuka ........ 143

(9) Kuacha Urithi ........ 169

Kiambatisho: Injili kuhusiana na Ufalme (Mahubiri) ........ 185

Vianzo Vilivyopendekezwa ........ 196

Kumbukumbu ya Kazi Zilizofanywa ........ 197

# Maelekezo Kwa Wakufunzi wa Darasa

Kozi hi ni ya kujifunza maisha na huduma ya Yesu kama kielelezo cha kuigwa katika maisha na huduma kwa wakati wa sasa. Siyo tu utafiti wa kina wa Vitabu vya Injili. Badala yake, kozi hii inaangalia katika vipengele kadhaa vya huduma ya Yesu ili kupata mafunzo kwa ajili ya huduma za wakati wa sasa. Kama una matarajio ya kujifunza kwa undani maisha ya Yesu, ninapendekeza ujipatie mojawapo ya vitabu vilivyooredheshwa kwenye Vianzo Vilivyopendekezwa kwenye mwisho wa kitabu hiki.

Kama ni kujifunza katika kikundi, mnaweza kupeana nafasi ya kusoma mafundisho haya. Inabidi msimame kwa wakati fulani ili kupeana nafasi ya kufanya majadiliano ya darasa. Kama kiongozi wa darasa, unao wajibu wa kuhakikisha kwamba majadiliano hayayumbishwi kutoka kwenye mada inayojadiliwa. Itasaidia kuwa na kiwango cha muda kwa kila kipindi cha majadiliano.

**Maswali yanayohusiana na mjadala** na shughuli za ndani za darasa zimeonyeshwa kwa alama hii. ► Endapo utakutana na alama hii, uliza swali au maswali yanayofuata mbele yake na utoe nafasi kwa wanafunzi kutoa majibu. Tafadhali chukua mud ili kupata majibu yaliyo sahihi na yenye maana. Bila kufanya hivyo, wanafunzi wanaweza kuyaunganisha mafundisho haya ya huduma ya Yesu na huduma zao leo.

Aya nyingi za **maandiko** zimeorodheshwa kwenye kozi yote, kwenye mafundisho ya msingi na kwenye tanbihi. Aya ambazo itapaswa zisomwe kwa sauti zimeonyeshwa pia kwa alama ya ►. Wanafunzi wanapaswa wazisome hizi aya ndefu kabla ya darasa kuanza. Aya fupi zitasomwa darasani.

Sehemu zilizoonyeshwa "**Angalia kwa kuzingatia**" zinaelekeza kwenye mada maalumu zinazohusiana na somo linalojadiliwa.

Kila somo litahusisha kazi moja au mbili za kufanya. Kama mwanafunzi atahitaji kupata **cheti cha kufuzu mafunzo kutoka Shepherds Global Classroom**, atapaswa ahudhurie vipindi vyote vya darasa na amalize kufanya kazi zote zilizotolewa. Fomu imetolewa mwisho wa kozi hii kwa ajili ya kuweka kumbukumbu ya kazi za kufanya zilizomalizika.

Kusudi mojawapo la kozi hii ni kuwaanda wanafunzi kuwa waalimu. Kiongozi wa darasa anapaswa kuwapa wanafunzi nafasi ya kuinua viwango vyao vya kufundisha. Kwa mfano, kiongozi wa darasa mara kwa mara atapaswa kumpa mwanafunzi nafasi ya kufundisha sehemu fupi ya somo katika darasa.

**Ramani ya Palestina wakati wa Yesu**

Tafadhali fanya marejeo kwenye ramani hii katika mwendelezo wa kozi nzima.[1]

(1) Tiro

(2) Kaisarea Filipi

(3) Galilaya (mkoa)

(4) Kana

(5) Kapernaumu

(6) Nazareti

(7) Dekapoli (mkoa)

(8) Samaria (mkoa)

(9) Mto Yordani

(10) Emmau

(11) Yerusalemu

(12) Bethlehemu

(13) Nchi tambarare ya pwani


(14) Milima ya Kati

(15) Jangwa la Yudea

(16) Bahari ya Chumvi

(17) Ziwa Galilaya

(18) Bahari ya Kati




[1] "Map of Israel" was created by SGC with open data from NED, SRTM, NASA, and Bible Geocoding (CC BY 4.0), available from https://www.flickr.com/photos/sgc-library/52344178339, public domain (CC0)

# Somo la 1
# Maandalizi ya Huduma

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi atapaswa:

(1) Atambue kwamba Yesu ndiye kielelezo cha kuigwa kwa ajili ya huduma.

(2) Akubaliane na uwezo wa Mungu wa kuwaanda wale anaowachagua kwa ajili ya huduma.

(3) Kujisalimisha kwa ajili ya wito wa Mungu aliokuitia.

(4) Kufuata nyayo za Kristo za ushindi dhidi ya majaribu.

## Maandalizi ya Somo

*Soma Mathayo 1-4, Luka 1-3, na Yohana 1.*

## Kanuni ya Huduma

Mungu huwaanda wale anaowaita kwa ajili ya huduma ile aliyowaitia.

## Utangulizi

Katika *Maisha na Huduma ya Yesu Kristo*, tutajifunza kuhusu Yesu kama kielelezo chetu cha kuigwa kwa wakati wa leo. Yesu alisema. "Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo."[2] Maisha ya Yesu hapa duniani yalikuwa ni kielelezo kwa ajili ya wafuasi wake.

Paulo aliielewa kanuni hii. Aliposikia mgogoro kati ya Wakristo na Wafilipi, Paulo aliwapeleka kwenye mfano wa Yesu. "Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu."[3] Paulo alijua kwamba kama Wakristo watafuata mfano wa Yesu, unyenyekevu wao utatatua migogoro ndani ya kanisa.

Katika safari yake ya kuja Afrika, Mwandishi wa Kiyahudi, Daudi Plotz, alikwama kwenye uwanja wa ndege wa Malawi. Akiwa pale alikutana na mchungaji wa Kiafrika ambaye alimpeleka nyumbani kwake, akamtunza kwa siku mbili, na akamshuhudia kuhusu Yesu Masihi. Daudi Plotz baadaye aliandika."Siamini katika lolote ambalo huyu baba anaamini, lakini ninaogopa kwa msimamo wake. Anajisikia jinsi Kristo anavyotembea ndani yake, ndiyo maana alimchukua mgeni asiyemjua, akamhudumia kwa malazi na chakula, na

---

[2] Yohana 13:15
[3] Wafilipi 2:5, *Toleo la Biblia ya Kiswahili (SUBV)*

akamvisha." Huyu mchungaji wa Kiafrika alielewa kwamba tumeitwa kwa ajili ya kuwa kilelezo cha Yesu.

Kozi hii siyo utafiti wa kina wa maisha ya Yesu. Badala yake, tutajielekeza katika vipengele vinavyohusiana na maisha ya Yesu ambavyo vinatoa kielelezo kwa ajili ya huduma zetu za leo. Tutajifunza jinsi ya kuunda huduma zetu kwa kutumia mfano wa Yesu.

Katika somo hili la kwanza, tutaona maandalizi ya Yesu kwa ajili ya huduma. Hii inaonyesha kanuni kwamba Mungu humwandaa kila mtu anayemwita kwa ajili ya huduma ambazo wameitiwa.

## Mungu aliandaa Msingi wa Mwanzo wa familia ya Mtumishi wake.

► Fikiria msingi wa mwanzo wa familia yako na maisha ya awali. Ni kwa jinsi gani Mungu ameutumia mwanzo wako kukuandaa kwa huduma?

Mtiririko wa vizazi katika Vitabu va Injili unaonyesha kwamba Mungu mwenye enzi aliandaa njia kwa ajili ya watu wake karne nyingi kabla Yesu hajazaliwa. Kitambo kirefu kabla ya Yesu kuzaliwa, Mungu aliandaa njia ya kuja kwake.

Mtiririko wa vizazi unajibu swali hili, "Je! Yesu ni nani?" Mtiririko huu wa vizazi unaonyesha umuhimu wa Abrahamu na Daudi. Abrahamu ni muhimu katika ukoo wa Yesu kwa sababu Mungu alimwahidi Abraham kwamba, "katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa."[4] Ahadi hii ilitimia kupitia Yesu wa Nazarethi.

Daudi ni muhimu katika mtiririko wa vizazi kwa sababu Mungu alimwahidi Daudi kwamba, "Nacho kiti chako kitafanywa imara milele."[5] Wakati wa kuzaliwa kwa Yesu, ilikuwa ni zaidi ya miaka 500 imepita tangu utawala wa Daudi ulipokuwa madarakani. Mathayo na Luka wanaonyesha kwamba Yesu alikuwa ni mkamilishaji wa ahadi iliyokuwa imetolewa kwa Daudi.

### Yesu alikuwa ni Mwana wa Daudi (Mathayo 1:1-17)

Katika Agano Jipya ya Kiyunani, maneno mawili ya mwanzo ya kitabu cha Mathayo ni *biblios genesis,* maneno ambayo yangekumbusha wasomaji wa mwanzo wa Mathayo juu ya kitabu cha Mwanzo. [6] Kama vile kitabu cha Mwanzo kinavyoelezea ukuu wa Mungu dhidi ya uumbaji, kitabu cha Mathayo kinaelzea ukuu wa Mungu dhidi ya historia. Mtiririko wa vizazi katika kitabu cha Mathayo unaonyesha kwamba historia yote ya Israeli ilielekezwa kwenye kuzaliwa kwa Masihi.

---

[4] Mwanzo 12:3
[5] 2 Samweli 7:16
[6] Mwanzo 2:4; 5:1

Mtiririko wa vizazi katika kitabu cha Mathayo unaonyesha makundi matatu ya watu kumi na nne. Hili lilikuwa ni jambo la kawaida kwa Wayahudi la kusaidia kukumbuka. Makundi mbalimbali ya kawaida ilisaidia wanafunzi kukariri orodha ndefu za majina. Wasomaji wa mtiririko wa vizazi katika kitabu cha Mathayo wanapaswa watambue kwamba orodha hii haikumhusisha kila babu aliyekuweko kati ya Abrahamu na Yusufu. Neno la Mathayo "akamzaa" linaweza kurejewa kwa babu yeyote. Mtiririko wa vizazi wa Wayahudi mara nyingi uliepuka kutaja baadhi ya vizazi vingine. Mathayo anajielekeza kwenye makundi muhimu ya vizazi vya Yesu na kuacha majina mengine.

Kwa kuwa Mathayo aliacha baadhi ya vizazi vingine, majina aliyoingiza kipekee ni ya kuvutia sana. Mathayo aliyachagua majina hayo kwa kusudio maalumu. Kwa mfano, Mathayo anaorodhesha wanawake wanne. Hili lilikuwa siyo jambo la kawaida kwenye mtiririko wa vizazi vya Wayahudi. Majina haya kila moja lilikuwa na hoja ya misingi ya huko nyuma. Rahabu na Ruthi walikuwa wageni. Tamari, Rahabu, na Bathisheba walihusishwa katika aibu ya kashfa ya uzinzi.

Hali kadhalika, baadhi ya wanaume katika orodha hiyo walikuwa wamepatikana na mambo ya aibu. Yuda alimtendea Tamari mambo ya aibu. Kizazi cha Yehokonia kiliondolewa katika uhalali wa kuwa katika kiti cha ufalme cha Israeli.[7] Kinachoonekana zaidi, Mathayo anamtambua Daudi siyo katika yale mambo makubwa aliyofanikisha, lakini kama "Baba wa Sulemani kutoka kwa mke wa Uria."

Majina haya yanamtambulisha Yesu katika ubinadamu wa dhambi. Mungu alimleta Mtoto wake duniani siyo kutoka katika familia ambayo haikuwahi kuwa na doa, bali kama mzaliwa katika ukoo wa watenda dhambi wa kawaida. Wayahudi walidhihaki kuzaliwa kwa Yesu kusikokuwa na heshima, na wakamkataa kama asiyestahili.[8] Mathayo anaonyesha, "Kama Masihi anaweza kuzaliwa kutoka katika kizazi cha ukoo wa aina hii, anaweza akawa mkombozi kwa watu wa aina zote, hata wale ambao wanaonekana hawastahili."[9]

► Katika mila zetu, ni vipengele gani vya mambo ya nyuma ya mtu vinavyoweza kutufanya tumfikirie kama mtu aliye na uwezo mdogo?

Mara nyingi Mungu huwaita watu kutoka katika mazingira mbalimbali ya nyuma yasiyotegemewa kwa ajili ya huduma yake. Hakuna mtu ambaye ataachwa kutumiwa kutokana na historia ya mambo yake ya nyuma. Vipengele vya mambo ya nyuma vinavyotufanya sisi tumwone mtu kama mwenye uwezo mdogo, havijalishi kwa Mungu.

---

[7] Mathayo 1:12; Yeremia 22:30
[8] Yohana 8:41, 48
[9] Craig L. Blomberg, *Jesus and the Gospels.* (Nashville: Broadman & Holman, 1997), 199

**Yesu alikuwa Mwana wa Adamu (Luka 3:23-38)**

Mathayo anafuatilia asili ya mtiririko wa vizazi vya Mfalme wa Wayahudi hadi Abrahamu. Luka anafuatilia asili ya mtiririko wa vizazi vya Yesu hadi Adamu. Hii inakubaliana namkazo wa Luka juu ya Yesu kama "Mwana wa Mtu." Mtiririko wa vizazi wa Luka unawekea mkazo kwenye ubinadamu wa Yesu. Luka anauweka mtiririko wa vizazi kabla ya kujaribiwa kwa Yesu. Hii inamkumbusha msomaji kwamba Yesu, Adamu wa pili, alifanikiwa mahali ambapo Adamu wa kwanza alishindwa.

**Angalia kwa kuzingatia: Mtiririko wa vizazi vya Mathayo na Luka**

Kitabu cha Mathayo 1 na Luka 3 vinatoa mtiririko wa vizazi vya Yesu unaotofautiana. Mathayo anauchuua mtiririko wake kutoka kwa Abrahamu kuja kwa Mfalme Sulemani hadi kwa Yusufu. Luka anatoa mtiririko wake kutoka kwa Yusufu kuja kwa Nathani (mtoto mwingine wa Daudi) hadi kwa Adamu.

Mtiririko wa vizazi unafanana kati ya Abrahamu na Daudi. Hata hivyo, kati ya Yusufu na Daudi, vizazi viwili vinachukua mikondo mingine. Uwezekano wa maelezo ya tofauti hii ni kwamba Mathayo anachukua kumbukumbu za mtiririko wa ukoo wa Yusufu, na Luka anachukua kumbukumbu za mtiririko wa ukoo wa Mariamu.[10]

Ukoo wa Yusufu katika kitabu cha Mathayo ni wa mtiririko wa vizazi ya "kifalme" ukianzia nyuma kwa mfalme Sulemani. Hii inakubaliana na dhamira ya Mathayo ya Yesu kama Mfalme. Huu ni ukoo halali wa kisheria wa Yesu – ambao ni lazima utoke kwa Yusufu.

Ukoo wa Mariamu katika kitabu cha Luka ni wa mtiririko wa vizazi vya "kimwli" ukianzia nyuma kwa Nathani, mtoto wa Daudi. Mtiririko huu wa uzazi unakubaliana na dhamira ya Luka ya Yesu kuwa "Mwana wa Mtu." Ili kuonyesha hili, Luka anafuatilia mtiririko wa vizazi kimwili wa Yesu kupitia Mariamu. Na bado anaanza na neno "Mwana wa Yusufu" kwa sababu mtiririko wa vizazi wa Wayahudi ulitumia wanaume, hata pale ilipotakiwa kufuatilia mtiririko wa nasaba za wanawake.

Nasaba ya Mariamu inaonyesha muunganiko wa damu kutoka kwa Daudi. Nasaba ya Yusufu inaonyesha haki za kifalme kupitia kwa Sulemani.

**Yesu alikuwa Mwana wa Mungu (Yohana 1:1-18)**

Injili ya Yohana inaanza na mtiririko wa vizazi vya kiungu; Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. "Maisha ya Yesu hayakuanza mara tu alipozaliwa." Alikuja duniani kutoka katika maisha ya roho kabla ya mtu kuzaliwa ili kutimiza kazi maalumu. "[11]

---

[10] Kwa ufafanuzi mwingine wa ziada tembelea, http://www.gotquestions.org/Jesus-genealogy.html, iliyopatikana March 22, 2021.

[11] J. Dwight Pentecost, *The Words and Works of Jesus Christ.* (Grand Rapids: Zondervan, 1981), 28

Katika Agano la Kale, utukufu wa Mungu wa *shekinah* ulijaa miongoni mwa Israeli katika hema ya kuabudia. Kwa sasa, utukufu wa Mungu unakaa miongoni mwetu katika mtu Yesu Kristo.[12] Utukufu wa kiungu wa Mungu sasa uliachiliwa kupitia mfumo wa kibinadamu.

Neno lilikuwa la milele: "Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu."[13] Baba na Mwana waliishi katika ushirka wa milele.[14] Kwa nini yesu alikuja katika dunia yetu? Kumdhihirisha Baba. Hakuna mtu aliyewahi kumwona Baba, lakini Yesu "alimfanya afahamike" kwetu.[15] Tunapomwona Yesu, tunamwona Baba.

Kwa sasa, watu wengi wanamwona Yesu kama rafiki mwenye upendo, na Baba kama hakimu mkali. Hata hivyo, kitabu cha Yohana 1 kinaonyesha kwamba tabia ya Yesu ni sawa na tabia ya Baba. Tunapomwona Yesu, tumemwona Baba.

### Mungu Alimwandaa Mtumishi wake kwa kuzaliwa Kimiujiza

Yesu alikuwa amezaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi takribani mwaka wa 5 B.C.[16] Yusufu alikuwa amesafiri hadi Bethlehemu ili kujiandikisha kwa ajili ya kuhesabiwa. Kusudi la zoezi la kuhesabiwa ilikuwa ni kuweka kumbukumbu kwa ajili ya kulipa kodi kwa kila jimbo lililokuwa chini ya mamlaka ya Kirumi.

Utaratibu wa kawaida wa Kirumi wa kuandikisha watu katika miji ulikuwa ni kuwaandikishia pale wanapoishi na kufanyia kazi. Hata hivyo, ili kuimarisha Amani na jamii ya Kiyahudi ambayo ilikuwa wepesi sana kwao kuasi, utawala wa Kirumi uliruhusu jimbo la Yudea kufuata taratibu za uandikishaji za Kiyahudi katika mji wa kabila la mababu zao. Matokeo yake, Yusufu na Mariamu iliwabidi wasafiri kilomita 100 kutoka Nazarethi hadi Bethlehemu. Ingawaje ni mwanaume kiongozi tu wa nyumba aliyekuwa anahitajika kujiandikisha, Yusufu aliambatana na mkewe katika safari hiyo hadi Bethlehemu. Inawezekana kwmba Yusufu hakutaka kumwacha Mariamu nyuma wakati kukiwepo na minong'ono ya majirani zake katika kitongoji chake cha Nazarethi.

Kwa upande mwingine, suala la kuhesabiwa kwa ajili ya kulipa kodi lilikuwa ni wazo la utawala wa Kirumi. Hata hivyo, Mungu alikuwa anaiandaa njia kwa ajili ya mtumishi wake. Mungu hufanya kazi kupitia matukio ya kidunia ili kutimiza kusudi lake. Mungu kwa mamlaka yake alisababisha mfalme wa kipagani "kuchagua" kuwepo na zoezi la kuhesabiwa kwa Wayahudi ili kutimiza kusudi la Mungu. "Moyo wa mfalme huwa katika

[12] Yohana 1:14
[13] Yohana 1:1
[14] Yohana 1:3 anakataa madai ya mashahidi wa Yehova kwamba Yesu alikuwa kiume aliyeumbwa. Yesu alikuwepo wakati wa uumbaji. "Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika."
[15] Yohana 1:18
[16] Kalenda ya Gregori ilikuwa bado haijaanziswa hadi mwaka 1582. Kalenda hiyo iko katika mfumo wa takribani na siyo kwa uhakika. Herode mkuu alifariki takribani mwaka wa 4 K.K. Kwa kuzingatia hili, kuzaliwa kwa Yesu ilikuwa ni takribani kati ya mwaka 5-6 K.K.

mkono wa Bwana; Kama mifereji ya maji huugeuza po pote apendapo."[17] Kama watendakazi wa ufalme wa Mungu, itupe ujasiri na uhakikakwamba Mungu hutimiza kusudi lake hata pale inapotokea kwamba watu waovu wako madarakani.

Hesabu hii kwa ajili ya kodi ni mfano mmoja katika mifano mingi inayoonyesha jinsi Mungu alivyokuwa ameuandaa ulimwengu kwa ajili ya kuzaliwa kwa Yesu. Mungu alifanya kazi nyuma ya misingi ya kikabila ya Mfalme wa Kiyunani, nyuma ya taratibu za kisheria za Utawala wa Kirumi, na nyuma ya kanuni za kidini za imani ya Wayahudi kuuandaa ulimwengu kwa ajili ya kuzaliwa kwa Masihi. Ili uweze kujifunze misingi hio, tafadhali rejea kwenye somo la kwanza la kozi ya Shepherds Global Classroom, *Kuchambua Agano Jipya*.

### Kutembelewa na Wachungaji wa Kondoo (Luka 2:8-20)

Watu wa kwanza kabisa kupokea taarifa za kuzaliwa kwa Yesu walikuwa wachungaji wa kondoo nje ya Bethlehemu. Hili ni la kutazamwa sana kwani wachungaji wa kondoo walikuwa ni watu wa kutengwa na Wayahudi wengi wa karne ya kwanza. Wachungaji wa kondoo walikuwa wakitazamwa kama watu wa hali ya chini sana katika jamii kiasi kwamba hata ushahidi wao ulikuwa haukubaliki katika mahakama za Kiyahudi. Kwa kuwaangalia hawaa wachngaji wa kondoo, Luka anamaanisha kwamba, "kama wachungaji wa kondoo wameweza kukaribishwa, basi *kila mtu* anakaribishwa kwenye ufalme wa Mungu!" Malaika alisema kwa Wachungaji wa kondoo, "ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa **kwa watu wote**."[18]

Injili haiko tu kwa ajili ya taifa moja (la Israeli) au kwa ajili ya jamii ya daraja fulani tu; injili ni kwa ajili ya watu wote. Dhamira hii inaonekana katika Injili yote ya Luka. Luka anatoa angalizo maalumu kuhusiana na huduma ya Yesu kwa wanawake, Wasamaria, na kwa watu waliotengwa na jamii kama Zakayo.

### Kutembelewa na Mamajusi (Mathayo 2:1-12)

Injili ya Mathayo ilikuwa hapo kwanza imeelekezwa kwa wasikilizaji wa Kiyahudi. Wakati ujumbe wa Luka ulilenga kwa watu wote, ujumbe wa Mathayo ulilenga kwanza kwenye mambo ya ufalme wa Mbinguni. Badala ya wachungaji wa kondoo, Mathayo anaonyesha kukaribishwa kwa watu wenye hekima na akili, mamajusi. Ujio huu ulitokea baada ya familia ya Yesu kuhamia kwenye makazi yao ya kudumu, yumkini miezi michache baada ya kuzaliwa Yesu.[19] Hili linaungwa mkono na tukio la amri ya mfalme Herode ya kutaka wauawe watoto wachanga wote waliokuwa na umri chini ya miaka miwili.

---

[17] Mithali 21:1
[18] Luka 2:10
[19] Mathayo 2:11

Mamajusi walikuwa wamefunzwa kusoma mambo ya anga wakichuguza mienendo ya nyota isiyokuwa ya kawaida. Wakati wakiwa katika safari yao ngumu na ya hatari, walitembea umbali mrefu kuchunguza alama ya ajabu waliyokuwa wameiona angani.

Mamajusi walikwenda kwanza Yerusalemu, mahali ambapo ndipo palipotakiwa papatikane mfalme. Wakati habari za kuzaliwa mfalme mbadala zilipomfikia Herode, "alifadhaika, na Yerusalemu (yote) pia pamoja naye."[20] Neno "Yerusalemu *(yote)*" linaashiria kukataliwa baadaye kwa Yesu na viongozi wa kidini wa Yerusalemu.

Kutembelewa na Mamajusi kulikuwa ni ishara ya kwanza ya uwakilishwaji wa Masihi kwa Wamataifa. Ukilinganisha na wale waliokuwa Yerusalemu ambao walikuwa "wamepata shida" kwa kuiona ile alama, Mamajusi waliitikia kwa imani. Yesu alikuja kama mfalme kwa mataifa yote, na siyo mfalme kwa ajili ya Waisraeli tu.

Mathayo hatoi taarifa ni mamajusi wangapi walikwenda kumsujudia Yesu. Mila ya "Watu watatu wenye hekima" inahusiana na zawadi tatu zilizotajwa katika Mathayo 2:11. Kila zawadi ikiwakilisha kipengele kimoja katika huduma ya Yesu.

- Dhahabu ni zawadi kwa ajili ya malme. Hata hivyo, Yesu hatainukia kutawala kutoka kwenye kiti cha enzi bali kutokea msalabani.
- Uvumba ni zawadi kwa ajili ya mchungaji. Uvumba ulikuwa unatumika kama manukato. Yesu alikuja kama mchungaji aliyewezesha watu wote waweze kuingia mbele ya uwepo wa Mungu.
- Manemane ilitumika kama dawa ya kutia kwenye maiti ili isioze.Yesu alizaliwa ili afe kwa ajili ya wanadamu wote.

**Mungu alimlinda Mtumishi wake.**

Kabla ya kuzaliwa kwa Yesu, malaika alizungumza na Yusufu katika ndoto ili kumfunulia mipango yake. Baada ya kutembelewa na mamajusi, malaika alimwonya Yusufu akimbilie Misri. Familia hii ilikaa Misri hadi baada ya kifo cha Herode (takribani mwaka wa 4 K.K.)

Kwa namna nyingi Herode Mkuu alikuwa mtawala mzuri. Aliwaheshimu Wayahudi, hata kwa kufuata sheria za vyakula za Kiyahudi nje ya utukufu wake aliokuwa nao kwa wale aliokuwa anawatawala. Alianza kulifanyia ukarabati wa hekalu ambao uliendelea katika kipindi chote cha maisha ya Yesu. Wakati wa njaa ya mwaka wa 5 K.K., alitumia fedha zake mwenyewe kununulia chakula kwa ajili ya walioathirika na njaa ile katika Yudea.

Hata hivyo, Herode alikumbwa na uwazimu usiotibika. Alimwua mmojawapo wa wake zake, Mariamne, na mama yake Alexandra, alipohisi kwamba walikuwa na njama za kumhujumu. Herde alikuwa na watoto watatu waliouawa kikatili walipofikia umri wa

[20] Mathayo 2:3

kuonekana kwamba wanaanza kuwa tishio kwa utawala wake. Kwa mwanamume aliyefikwa na uwazimu kama Herode, kuchinjwa kwa watoto wachanga Bethlehemu kulikuwa siyo jambo la kushangaza. Mauaji wa dazeni za watoto wachanga kwa ajili ya kulinda nafasi yake ya ufalme lilikuwa ni jambo la usumbufu mdogo sana kwake.

Ukatili wa Herode uliendelea hadi wakati wa kifo chake. Alipokuwa anakaribia kifo chake, Herode aliamuru kwamba raia wote mashuhuri katika Yerusalemu wakamatwe wauawe wakati wa kufa kwake. Aliamini kwamba kwa kufanya hivyo, siku ya kufa kwake ingekuwa siku ya maombolezo makuu. (Badala yake, mjane wake na Herode aliwafungulia wafungwa wote, ikasababisha siku ile iwe ni ya kusherehekewa sana katika nchi yote ya Palestina.)

Baada ya Herode kufa, eneo lake la utawala liligawanywa kwa watoto wake watatu wa kiume. Antipasi alipewa eneo la Galilaya na Perea. Filipo alipewa kutawala eneo la Kaskazini Mashariki mwa Palestina; Arkelau aliteuliwa kuwa mtawala wa Yudea, Idumea na Usamaria. Wanahistoria wa zamani wanasema kwamba Arkelau alikuwa na madhaifu yote ya baba yake na hakuchukua tabia zozote nzuri za baba yake. Alichukiwa na Wayahudi na akaondolewa katika madaraka yake mwaka wa 6 B.K. kutokana na malalamiko ya Wayahudi kwa Kaisari, Baada ya hili, Yudea ilitawaliwa na mawakili wa Kirumi kama Pointio Pilato

Baada ya kifo cha Herode, malaika kwa mara nyingine alimjia tena Yusufu katika ndoto kumpa maelekezo ya kurejea Israeli. Hata hivyo, kwa kuwa Arkelau alikuwa ni mtu wa hatari kama Herode Mkuu, Yusufu aliipeleka familia yake Nazarethi kuliko kurejea tena Yerusalemu.

► Akiwa mtoto mdogo, Yohana Wesley aliokolewa kimiujiza katika nyumba yao iliyokuwa inateketea kwa moto. Aliamini kwamba Mungu alikuwa amemlinda kwa kusudi maalumu. Wesley alijitafakari mwenyewe kama "kijiti kiwakacho kilichonyakuliwa motoni." Waalike wanafunzi wa darasa lako mshirikishane visa ambavyo Mungu ameweza kuwalinda kwa ajili ya huduma – aidha kupitia ulinzi wa miujiza au kupitia majaliwa ya Mungu.

### Angalia kwa kuzingatia: Mathayo 2:23

Zaidi ya Injili nyingine zote, Mathayo anaonyesha kwamba huduma ya Yesu ilitimiza unabii zilizokuwa katika Agano la Kale. Akiwaandikia wasikilizaji wake wa Kiyahudi, Mathayo anaonyesha kwamba Yesu alikuwa ndiye Masihi aliyekuwa ametabiriwa:

- Kuzaliwa kwa Yesu na bikira (Mathayo 1:22-23) ilitimizwa kutoka Isaya 7:14.
- Kuzaliwa kwa Yesu Bethlehemu (Mathayo 2:5-6) ilitimizwa kutoka Mika 5:2.
- Kukimbilia Misri (Mathayo 2:14-15) ilitimizwa katika Hosea 11:1.
- Kuuawa kwa watoto wachanga Bethlehemu (Mathayo 2:16-18) ilitimizwa kutoka Yeremia 31:15.

- Kuingia Yerusalemu (Mathayo 21:1-5) ilitimizwa kutoka Zakaria 9:9.

Mojawapo ya mifano migumu kabisa ya kutimizwa kwa unabii uko katika Mathayo 2:23. Mathayo anaandika, "Akaenda, akakaa katika mji ulioitwa Nazareti; ili litimie neno lililonenwa na manabii, Ataitwa Mnazorayo."

Tatizo ni kwamba hakuna kumbukumbu yeyote kutoka kwenye unabii wa Agano la Kale unaosema kwamba Masihi ataitwa "Mnazorayo." Kuna mawazo ya aina mbili nyuma ya hii aya:

1. Kwa wakati ule wa Yesu, Nazarethi kilikuwa ni kijji ambacho kilikuwa hakina uthamani wowote. (Yohana 1:46). Wayahudi walitegemea Masihi angetoka Yudea na siyo katika mkoa wa kibiashara wa Galilayan(Yohana 7:41, 52). Ukweli kwamba Yesu alitoka katika eneo lililokuwa limedharaulika kama Nazarethi ilikamilisha unabii kama wa Isaya 49:7 na 53:3.
2. Isaya 11:1 alitabiri kwamba Masihi takuwa "tawi." Neno la Kiyunani la tawi *(Netzer)* linatamkika kama sawa na "Nazarethi." Wayahudi wasomaji wa kitabu cha Matayo wangelitambua huu ulimbuaji wa maneno.

**Mungu aliandaa njia kwa Mtumishi kwa njia ya Mtangulizi wake**

Yohana Mbatizaji alikuwa binamu wa Yesu. Maelezo kuhusiana na Yohana yanaanzia wakati baba yake Zakaria alipokuwa anafukiza uvumba kwa niaba ya taifa, mojawapo ya jukumu lililokuwa linaheshimika sana kwa kuhani.[21]

Wakati Zakaria alipokuwa akifanya jukumu hili takatifu, malaika alitokea upande wa kulia wa madhabahu wa kufukizia uvumba. Kwa utamaduni wa Kiyahudi hapa ndipo Mungu alipokuwa anasimama wakati wa kutoa sadaka. Malaika Gabrieli alimwambia Zakaria kwamba maombi yake kwa ajili ya kupata mtoto yamejibiwa.

Kwa kuwa Elizabethi alishapitiliza umri wake wa kuweza kuzaa, Zakaria aliionea shaka ahadi ya malaika. Kutokana na kutoamini kwake, malaika alimfanya awe bubu hadi pale alipozaliwa Yohana. Kama kuhani na mwanafunzi wa maandiko, Zakaria alizijua habari za Hana na Raheli na alipaswa kuamini ahadi ya Mungu kwamba kwa miujiza angelilifungua tumbo la uzazi la Elizabethi.

Miaka thelathini baadaye, Yohana alianza huduma yake. Kuliko atumike kama kuhani katika Yerusalemu, Yahana alitumika kama nabii katika maeneo ya jangwa la Yudea. Yohana alikuwa ametumwa kama mtangulizi wa Masihi. Yohana alipokuwa akihubiri, watu walikuwa wakiulizana, "Je! Yohana ndiye yule Masihi aliyeahidiwa?" Yohana alijibu, "yuaja mtu mwenye nguvu kuliko mimi, ambaye mimi sistahili kuilegeza gidamu ya viatu

---

[21] Luka 1:9

vyake."[22] Mojawapo ya jukumu la chini sana la mtumwa lilikuwa ni kushughulika na viatu vya bwana wake, lakini Yohana alisema, "anayekuja yuko juu sana kuliko mimi, kiasi kwamba sisitahili kwake hata kwa jukumu hili la chini." Yohana anawakilisha aina ya utumishi wa unyenyekevu.

Katika maandiko yote, Mungu hutumia watu kuandaa njia kwa ajili ya mtu mwingine. Angalia mfano wa Barnaba na Paulo. Wakati Sauli alipokuwa akiwauawa Wakristo, tayari Barnaba alishakuwa kiongozi wa kanisa anayeheshimika. Barnaba alimwamini Paulo wakati ambapo Wakristo wengine wachache wangeweza kumwamini huyu muuaji na mtesaji wa kanisa.

Wakati walipoanza safari ya kwanza ya kimishenari, Kitabu cha Matendo kinairejea timu hii kama ya Barnaba na Sauli."[23] Muda siyo mrefu, wakatambulika kama Paulo na Barnaba."[24] Barnaba alikuwa "mtangulizi" lakini alikuwa amehiari kumwachia Paulo uongozi.

Wakati mwingine jukumu lako linaweza kuwa ni lile la Yohana Mbatizaji au la Barnaba, la kuandaa njia kwa ajili ya mtu mwingine. Uko tayari kwa hiari yako mwenyewe kuwa "mtangulizi" kuliko kutaka kuwa "mtendaji mkuu"? Wakati wowote Mungu akitaka kukutumia, jitoe kwa kilebora ulicho nacho. Kama Mungu atakuweka kwenye eneo la kutoa msaada, usiikatae huduma hiyo. Unaweza kumwamini Mungu akutumie katika njia ya mafanikio makubwa sana.

Tumeuona unyenyekevu wa Yohana wakati alipowaelekeza wafuasi wake kwa Yesu.[25] Lengo la Rabi lilikuwa ni kuwapata wanafunzi ambao wangemfuata na kumheshimu mwalimu wao. Badala yake, Yohana Mbatizaji aliwaelekeza wafuasi wake kwa mwalimu mkuu. Alielewa kwamba jukumu lake ni kuelekeza wengine kwa aliye mkuu kuliko yeye. Yohana alikuwa akiangalia wafuasi wake wakimwacha yeye na kwenda kumfuata Yesu. Lengo laku lilikuwa ni ufalme wa Mungu, na siyo utukufu wake mwenyewe. Kama watumishi wa Kikristo, hatupaswi tusahau kwamba lengo letu ni kuwaelekeza watu kwa Yesu, na siyo kutafuta mafanikio kwa ajili yetu wenyewe.

### Angalia kwa kuzingatia: Inamaanisha nini Kutubu?

► Soma Mathayo 3:1-6.

Yohana alihibiri ujumbe wa kutubu. Kwa wakati wa sasa, baadhi ya watu wanasema kwamba kutubu ina maana tu ya kubadili mawazo. Wakristo wengi walioonyesha kuukiri Ukristo huonyesha dalili chache za maisha yaliyobadilishwa.

---

[22] Luka 3:16
[23] Matendo 13:2
[24] Matendo 13:43 na kuendelea.
[25] Yohana 1:35-37

Hata hivyo, neno “kutubu” linamaanisha jambo muhimu zaidi kuliko uamuzi wa akili tu. Waandishi wa Agano Jipya walitumia neno la “kutubu” sawa na walivyokuwa wanatumia manabii Waebrania. Ilimaanisha kubadilisha kabisa “mfumo wa maisha.” Katika Agano Jipya, kutubu inamaanisha:

- Kuwa na mabadiliko ya mawazo na imani, **na**
- Kuwa na mabadiliko ya matendo a mfumo wa maisha.

Hivi karibuni nilisoma kuhusu muimbaji mmoja nyimbo za miondoko ya polepole aliyejulikana kwa mfumo wa maisha yake ya dhambi. Huyu mwimbaji alisema, “Nimekuwa Mkristo na nimejazwa nguvu za Roho Mtakatifu. Ninandelea kuishi maisha niliyokuwa naya hapo mwanzo, lakini sasa mimi ni Mkristo. Kama nikifa, nitaenda mbinguni.” Hii ina maana kwamba “kutubu” kwa mwanamume huyu hakujaleta mabadiliko yeyote katika mfumo wake wa maisha. Hii siyo toba ya kweli.

Yohana alifundisha kwamba toba inabadilisha mfumo wote wa maisha. Yohana aliwataka wahitimu wake “watoe matunda yapatanayo na toba.”[26] Kwa maneno mengine, aliuliza, “Kuna ushahidi gani kwamba umebadilisha maisha yako?” Ubatizo haupaswi ufanyike kuwa ni ibada tupu: “Nimeamini, kwahiyo sasa nibatize.” Ubatizo ni lazima uw ushuhuda wa toba ya kweli na maisha yaliyobadilishwa

## Mungu alimwandaa Mtumishi wake kupitia majaribu.

Ushindi wa Yesu dhidi ya majaribu unaonyesha mfano wa kuigwa tunapofikwa na majaribu. “Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi.”[27] Jaribu lilitokea muda kidogo tu kabla ya kuanza huduma yake rasmi hadharani. Kabla hajaanza kuhubiri kwa watu wengine, Yesu alidhihirisha utii wake kamili kwenye mapenzi ya Baba.

Mathayo anaielezea taarifa hii ya jaribu mara tu baada ya Yesu kubatizwa. Majaribu yetu makuu mara nyingi hufuatiliwa na ushindi wa kiroho. Mara tu baada ya ushindi wa Elia katika mlima Karmeli, Tunamwona akijariwa hadi kufikia kiwango cha kukataa tama na hofu akiwa anakimbia kusalimisha maisha yake.[28]

Luka anaielezea taarifa hii ya jaribu baada ya kufuatilia ukoo wa Yesu kutokea Adamu. Luka anaonyesha kwamba mahali ambapo Adamu alishindwa, Yesu Mwana wa Mtu alikuwa mshindi. [29] Yesu alijidhihirisha mwenyewe kwa unyenyekevu na mfano wa kuigwa wa jinsi ambavyo Mkristo wa kawaida anaweza akapata ushindi dhidi ya dhambi.

---

[26] Luka 3:8
[27] Mathayo 4:1
[28] 1 Wafalme 18-19
[29] Luka 3:38

**Majaribu**

> "Tunawapongeza wale wanaosema kwamba, "Nitaithibitisha nguvu yangu kwa kusimamia haki zangu. 'Lakini mtu mkamilifu huonyesha kwamba nguvu ya kweli inategemea mwanadamu kuachana na mapenzi yake mwenyewe na kutegemea mapenzi ya Mungu."
> - Nukuu kutoka kwa G. Campbell Morgan

***Jaribu la kugeuza mawe yawe mkate***

Shetani alimjaribu Yesu atumie uwezo wake wa kiungu ili aweze kugeuza mawe yawe mkate. Hili lilikuwa ni jaribu la kutumia **uhuru** wa mtu. Shetani alimjaribu Yesu atumie uwezo wake kwa faida yake mwenyewe badala ya kumtegemea baba yake. Yesu alisalimisha "haki" yake ya chakula kwa Mungu.

Akiwa anakabiliwa na tunda lililokataliwa, Adamu wa kwanza alimwasi Mungu. Akiwa anakabiliwa na mkate uliokatazwa, Adamu wa pili alikuwa mwaminifu.

***Jaribu la kuruka kutoka kwenye kinara cha Hekalu***

Shetani alimjaribu Yesu kwa kumwambia aruke kutoka kwenye kinara cha hekalu (mita 91 juu ya bonde la Kedari). Hili litawashangaza watu wakati wakiwa katika kujaribu ulinzi wa Mungu.

Shetani alinukuu andiko la ahadi la Zaburi ya 91:11-12 kumjaribu Yesu avunje ahadi za Baba yake. Kwa jaribu hili, Yesu angemfanya Baba yake kwamba ni mtumishi wake – sawa na madai yake na matazamio yake. Hili lilikuwa ni jaribu la **ufidhuli.**

Yesu alikataa kutumia ahadi ya Zaburi 91 katika mazingira ambayo ahadi haingeweza kutumika. Katika kumjibu Shetani, Yesu alinukuu andiko kutoka katika Kumbukumbu la Torati 6:16, "Msimjaribu Bwana, Mungu wenu." Kama watoto wa Mungu, hatuwezi kumwingiza Baba yetu wa Mbinguni kwenye jaribu.

**Angalia kwa kuzingatia: Imani au Ufidhuli?**

Baadhi ya Wakristo husema, "Kila ahadi katika Kitabu ni yangu." Wakati kila ahadi iliyoko kwenye Maandiko ni kweli, ni lazima kila siku tujiulize, "Je! ahadi hii inaendana na mazingira yaliyopo?" Yesu alijua kwamba ahadi iliyokuwemo katika Zaburi ya 91 haikuwa kwenye mapenzi ya Mungu katika mazingira aliyokutana nayo pale jangwani. Tunawezaje kuwa na uhakika kwamba tunazidai ahadi za Mungu katika imani ya kweli kuliko katika ufidhuli?

**(1) Ni lazima tuwe na ufahamu wa Neno la Mungu***.*

Kwa kiwango kile ninachoweza kujua maudhui ya ahadi za Mungu za kibiblia na mazingira yanayohusiana na ahadi hizo, nitaweza kupima matumizi yake katika mazingira yangu yaliyopo.

Ahadi nyingine zilitolewa kwa watu maalumu na katika mazingira maalumu. Katika Agano la Kale, Mungu aliahidi baraka za mwilini kama Israeli wangekuwa watiifu kwenye agano lake. Ardhi yao itatoa matunda mengi, ghala zao za nafaka zitafurika, na watashinda katika vita vyao. Ahadi za Agano Jipya mara nyingi ni za kiroho katika asili yake. Baadhi

ya watu wanakatishwa tamaa wakisikia haya, lakini tunapaswa tuwe na furaha. Mafanikio ya kimwili thamani yake ni ya muda tu; mafanikio ya kiroho ni yenye thamani ya mbinguni. Ufidhuli (kiburi) vinaondoa ahadi za Mungu kutoka kwenye maudhui ya kibiblia na kuzifanya zitumike kwenye matamanio binafsi; imani humtumainia Mungu atimize ahadi zake kama apendavyo.

**(2) Ni lazima tutambue tofauti iliyopo kati ya ahadi maalumu na ahadi za ujumla.**

Tunaposoma kigezo mantiki cha ujumla, ni lazima tuulize kama Mungu anatoa kigezo mantiki kwa ajili ya mazingira yetu maalumu. Vigezo mantiki vingine ni vya ujumla tu na siyo kwa ajili ya wakati wote.

Zaburi 103:3 inamsifu Mungu "atuponyaye magonjwa yetu yote." Baadhi ya Wakristo wameichukulia kauli hii kama ahadi ya wakati wote kwa ulimwengu kwamba Mungu ataponya magonjwa yote ya kila Mkristo aliyeamini. Hata hivyo, Maandiko yanaonyesha kwamba siyo kila ugojwa wa mwili unaponywa. Paulo aliomba kwa ajili ya uponyaji, na Mungu akamwambia, "Hapana."[30] Mara nyingine Mungu huchagua kuwaponya watoto wake na ugonjwa; mara nyingine huchagua kuwapa neema ya kuhimili maumivu.

Tunapaswa tuwe na majibu kama yale ya vijana watatu wa Kibrania. Wakati mfalme Nebukadineza alipotishia kuwatupa kwenye tanuru la moto, walisema, "Kama ni hivyo, Mungu wetu tunayemtumikia aweza kutuokoa na tanuru ile iwakayo moto; naye atatuokoa na mkono wako, Ee mfalme. **Bali kama si hivyo,** ujue, Ee mfalme, ya kuwa sisi hatukubali kuitumikia miungu yako, wala kuisujudia hiyo sanamu ya dhahabu uliyoisimamisha."[31] Walijua kwamba Mungu alikuwa na uwezo wa kuwaokoa, lakini kama Mungu atachagua iwe vinginevyo, walikuwa na utayari watumikie kwa uaminifu.

Mungu anaweza kuwaokoa watoto wake, lakini siyo kila wakati anachagua njia ya kupitia. Hadi hapo Mungu atakapoweka wazi kwamba kigezo mantiki cha kibiblia ni maalumu tu kwa ajili yako, mwamini Mungu afanye kama atakavyochagua yeye. Mtume Yohana alitoa kigezo mantiki kwamba, "Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba."[32]

Ufidhuli (kiburi) hudhania kwamba kila kigezo mantiki cha kibiblia kinafanya kazi kwa ajili ya mazingira yangu maalumu. Imani inasema, "Nitaomba 'sawasawa na mapenzi yake.'" Nitashawishika kuingia kwenye ufidhuli kama nitachukulia kwamba kila kigezo mantiki ni changu binafsi. Badala yake napaswa niulize kama kigezo mantiki kimekusudiwa kwa ajili ya mazingira yangu.

[30] 2 Wakorintho 12:7
[31] Danieli 3:17-18
[32] 1 Yohana 5:14-15

**(3) Ni lazima tuombe kwa "Jina la Yesu."**

Yesu aliahidi, "Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana."[33] Kuomba kwa "Jina la Yesu" kunamaanisha kuomba kulingana sawa na mapenzi yake na tabia yake. Inamaanisha kuomba "kwamba Baba aweze kutukuzwa." Ufidhuli unatafuta mapenzi binafsi, imani inatafuta utukufu wa Mungu.

Kuomba "kwamba Baba aweze kutukuzwa" kunamaanisha kwamba tunajiweka kabisa chini ya makusudi ya Mungu katika maisha yetu. Mungu alitoa ahadi kwa Israeli, "Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho."[34] Tunapaswa tukumbuke kwamba kigezo mantiki hiki kilitolewa kwa ajili ya Israeli ikiwa inatumikia miaka sabini ya utumwa katika nchi ya Babeli. Hata utumwa ndani ya Babeli utatimiza kusudi la Mungu kwa watu wake; katika dhiki yao, Israeli itamwita Mungu naye atawasikia.

Je, ahadi hii inafanya kazi kwetu leo? Ndiyo! Tabia ya Mungu haijabadilika; analeta mambo mema kwa watoto wake. Siyo kila kitu kitakachofanyika kitakuwa kizuri, lakini tunaweza kuomba kwa uhakika katika "Jina la Yesu" kwa sababu tunajua kwamba Mung analitendea kazi kusudi lake katika yale yote yanayotendeka katika maisha yetu.

## Mungu alimwandaa Mtumishi wake kupitia Majaribu (Inaendelea)

### *Kuahidiwa milki za dunia*

Jaribu la mwisho la Shetani lilikuwa ni ahadi ya **makubaliano,** njia ambayo Yesu angekubaliana nayo ili apewe utawala wote ujao bila njia ya msalaba. Kama Yesu atamsujudia Shetani, angeweza kuvuka maumivu makali ya msalaba. Yesu alimjibu kufuatana na andiko la Kumbukumbu la Torati 6:13, "Mwabudu Bwana Mungu wako, na umtumikie yeye peke yake."[35]

### Ushindi wa Yesu dhidi ya Majaribu

Ili tufaidike na mfano wa Yesu dhidi ya majaribu, ni lazima tukumbuke kwamba Yesu alikuwa mwanadamu kamili. Alijaribiwa "sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi."

► Soma 1 Wakorintho 10:13 na Waebrania 4:15. Wanafundisha nini kuhusiana na majaribu?

Katika 1 Yohana 2:16, mtume anatambulisha njia tatu za majaribu, "tamaa za mwili, tamaa za macho na kiburi cha maisha." Yesu alijaribiwa katika kila eneo.

---

[33] Yohana 14:13
[34] Yeremia 29:11
[35] Mathayo 4:10

- Shetani alimjaribu katika tamaa za mwili wakati Yesu alipokuwa na njaa ya kupata mkate.
- Shetani alimjaribu katika tamaa za macho kwa kumuonyesha milki za dunia.
- Shetani alimvutia kwenye kiburi cha maisha kwa kumjaribu Yesu kwa kitendo cha ajabu cha kuvutia ambacho kingeshangaza halaiki za watu.

Ushindi wa Yesu dhidi ya majaribu haukupatikana kwa kutumia nguvu zake za kiungu. Yesu alikuwa mwanadamu kamili na aliyashinda majaribu katika ubinadamu wake. Ushindi wake unatoa mfano wa kuigwa kwetu sisi katika nyakati zote za kujaribiwa. Hapa unatakiwa utambue zana tatu Yesu alizotumia kupata ushindi dhidi ya majaribu:

***Nguvu ya Roho Mtakatifu***

Yesu alitembea katika uongozi na maelekezo ya Roho Mtakatifu. Alifanya kile ambacho Roho alimwongoza kukifanya. "Yesu, hali amejaa Roho Mtakatifu, alirudi kutoka Yordani, akaongozwa na Roho muda wa siku arobaini nyikani."[36]

Kwa muda wote wa huduma yake hapa duniani, Yesu alitenda kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Alitoa mapepo kwa uweza wa Roho.[37] Mungu alimpaka mafuta Yesu wa Nazarethi kwa Roho Mtakatifu na uweza. Alipita kila mahali akitenda mema na kuwaponya wale wote waliokuwa wamegandamizwa na shetani, kwa kuwa Mungu alikuwa pamoja naye."[38]

Yesu alitimiza huduma yake chini ya uweza wa Roho Mtakatifu. Kama tunataka tuwe na nguvu mbele ya uso wa majaribu, ni lazima tuishi ndani ya uweza wa Roho Mtakatifu.

***Nguvu ya maombi***

Yesu alijaribiwa kufuatia siku arobaini za kufunga na maombi.Maombi yalimwandaa kwa vita vya kiroho. Kwenye somo litakalofuata, tutaona undani wa maombi kwenye maisha na huduma ya Yesu. Kama Yesu alitegemea maombi, sisi tutategemeaje tupate ushindi wa kiroho nje ya maombi?

Shetani mara nyingi hutupiga vita baada ya kuanza kuwa wazembe katika maisha yetu ya maombi. Anajua kwamba kama hatuimarishi maisha yenye nguvu ya maombi tutakuwa wavivu katika kukabiliana na majaribu yanayotujia mbele yetu

***Nguvu ya Neno***

Yesu alijibu kila jaribukwa kutumia aya za Maandiko. Aliyajuaje haya maandiko? Watoto wa Kiyahudi walikuwa na desturi ya kukariri Torati kama sehemu yao ya elimu ya utotoni.

[36] Luka 4:1
[37] Mathayo 12:28
[38] Matendo 10:38

Wakati Yesu alipojaribiwa, maneno katika maandiko hayo yalikuja haraka kwenye akili yake.

Kama Wakristo, ni lazima tuoteshe mbegu ya Neno la Mungu ndani ya mioyo yetu. Kwenye nyakati za majaribu, maandiko yatatupa nguvu ya kukabiliana na hayo majaribu.

Katika kukabiliana na majaribu, Yesu alitumia zana zinazofanana na tulizo nazo. Tunapaswa kukabiliana na majaribu kama Yesu alivyofanya, Kwa uweza wa Roho Mtakatifu, Kwa uweza wa maombi, na kwa uweza wa Neno. Bila ya kuwa na silaha hizo, tutajikuta tumeangukia kwenye mashambulizi ya Shetani.

### Angalia kwa kuzingatia: Kupata mwili kwa Yesu Kristo

Wakristo wa mwanzo duniani kote walikubaliana kwamba Yesu alikuwa na hadhi ya kiungu. Ingawaje wazushi kama Ariasi alikataa uungu wa Yesu, Wakristo wa madhehebu ya Kiothodoksi walifundisha kwamba Yesu alikuwa na uungu.

Wakristo Waothodoksi walifundisha kwamba Yesu alikuwa pia mwanadamu kamili. Imani hii mara nyingi ilikataliwa na wazushi. Hata sasa, waamini wengi wa kiinjili hawauzingaqtii kwa umakini ubinadamu wa Yesu. Wakristo wengi wanajaribu kuwa na hisia kwamba Yesu alikuwa na uungu kamili, lakini ubinadamu wake siyo uliokamilika. Wanafikiri kwamba "aliazima" mwili wa kibinadamu, lakini hakuwa mwanadamu kamili.

Baadhi ya maelezo ya mahubiri yanachangia katika wazo hili potofu. Baadhi ya wahubiri huelezea hadithi ya mfalme aliyejifanya raia wa kawaida akasafiri. Hata hivyo, Yesu hakuwa *akijifanya* kuwa yeye ni mwanadamu. Alikuwa ni mmoja wetu.

Imani ya Yesu kuwa mwanadamu ni muhimu sana kwa uzoefu wa maisha ya Kikristo. Kama Ysu hakuwa mwanadamu kamili, maisha yake hayawezi kuwa mfano halisi wa kuigwa. Mwanatheolojia aliliweka likae hivi, "Kama Yesu kwa uhalisia hafanani na sisi, basi sisi tunasameheka kwa kutofanana na yeye."[39]

Watu wengi wanaamini kwamba ni lazima mara kwa mara tuanguke katika dhambi za kujitakia. Yesu alionyesha katika maisha yake kwamba, Wakristo wa kawaida wanaweza kudumisha maisha ya ushindi dhidi ya dhambi kupitia uweza wa Roho Mtakatifu.

Kama Yesu alifanyika sehemu ya ubinadamu wetu mdhaifu, kama alipitia katika mahtaji yetu kwa uweza wa Roho Mtakatifu, na kama alijaribiwa kama nasi tunavyojaribiwa, basi ushindi wake dhidi ya majaribu unatuonyesha sisi jinsi ya kuwa washindi dhidi ya dhambi katika maisha yetu ya kila siku. Kwa uweza wa Roho Mtakatifu, tuna uwezo wa kuishi maisha ya ushindi.

---

[39] Cherith Fee Nordling, "Open Question" *Christianity Today,* April 2015, 26-27

► Ni lipi gumu kwako kufahamu, imani ya uungu wa Yesu au imani yay eye kuwa mwanadamu? Jadili ni kwa jinsi gani kila mojawapo ya imani hizi ni muhimu kwetu katika maisha yetu ya Ukristo na huduma.

**Hitimisho: Mungu huwaandaa Watumishi wake.**

Katika somo hili, tumeona ni kwa jinsi gani Mungu alivyoandaa njia ya huduma ya Yesu. Kutokea ukoo wake, hadi kupitia Utawala wa Kirumi, kupitia kuzaliwa kwa muujiza, kupitia huduma ya Yohana Mbatizaji na hata kupitia katika majaribu, Mungu aliandaa njia kwa ajili ya Yesu.

Tunauona ukweli huu mara nyingi katika Biblia yote. Angalia katika mfano wa Paulo. Paulo alikulia katika jiji la Roma la Taso. Kuanzia utotoni, alikuwa na marafiki mataifa. Tofauti na Wayahudi wengi, Paulo alikuwa ameridhika sana na kuwa na watu a mataifa.

Baba yake na Paulo alkuwa raia wa Kirumi, kwa hiyo Paulo alithamini sana haki za uraia za Kirumi. Mama yake alikuwa Myahudi, kwahiyo Paulo alipata mafunzo ya awali ya Maandiko ya Agano la Kale. Alikuwa na akili sana na alijifunza teolojia ya Kiebrania (Kiyahudi) chini ya mwalimu mkuu Gamalieli. Akiwa na asili yake ya Kirumi, alijifunza Kiyunani na mafundisho ya Wanafalsafa wa Kiyunani.

Kutokana na asili hii, siyo jambo la kushangaza kwamba Mungu alimwita kuwa mmishenari kwa mataifa. Tangu kuzaliwa, Mungu alimwandaa Paulo kuwa mmishenari wa kwanza kwa mataifa. Jaribu kutafakari maandalizi ambayo Mungu aliyafanya kwa ajili ya huduma yake:

- Kwa Paulo kuwa raia wa Kirumi kulimpa uhuru wa kusafiri bila matatizo.
- Mafunzo ya Paulo ya Kiebrania na Kiyunani yalimpa nyenzo kubwa ya kuandika vitabu vyenye maarifa mengi vya Agano Jipya.
- Kwa Paulo kujifunza falsafa ya Kiyunani, kulimwezesha kuzungumza na watu wa maarifa mengi ya kufikiri waliokuwa katika maeneo kama ya Athens.

Yumkini unasema, "Mungu hakunipa elimu kubwa kama ya Paulo. Sina historia kubwa ya nyuma ya familia yangu." Yote ni sawa! Mwangalie kiongozi mwingine wa kanisa la karne ya kwanza.

Simoni Petro alikulia katika maisha ya uvuvi wa biashara. Hakuwa na elimu au maarifa kama ya Paulo. Kwa hakika, baadaya Petro alikiri kwamba Paulo ameandika mambo mengi "ambayo ni magumu kueleweka."[40] Lakini Mungu alimtumia Petro kwa kiwango cha nguvu sana. Watu ambao wangeweza kujazwa kwa maneno yenye nguvu na maarifa ya Paulo, walikuwa wanaweza kuelewa mahubiri mepesi ya Petro.

---

[40] 2 Petro 3:15-16

Mungu amekuandalia wewe kwenye sehemu yako ya utumishi. Ukisalimisha mafunzo yako kwake, historia yako ya nyuma, na yote ambayo Mungu amekukirimia, atakutumia wewe katika kutimiza kusudi lake. Mungu huwaandaa wale aliowaita kwa ajili ya huduma.

**Kazi za kufanya Somo la 1**

(1) Katika somo hili, tumeona mfano wa Yesu wa ushindi dhidi ya majaribu. Orodhesha mifano mitatu ya kibiblia ya watu ambao waliweza kudumisha ushindi wao dhidi ya majaribu. Onyesha jambo moja ambalo liliweza kuwapa nguvu ya kukabiliana na majaribu.

| Mifano ya ushindi dhidi ya Jaribu | Andiko | Nini kilichosababisha ushindi? |
|---|---|---|
| Yusufu (usafi dhidi ya zinaa) | Mwanzo 39 | Alimtegemea Mungu (Mwanzo 39:9) |
| | | |
| | | |
| | | |

Orodhesha mifano mitatu ya kibiblia ambayo watu walianguka dhidi ya majaribu. Katika kila moja, onyesha kipengele kimoja kilichosababisha kuanguka kwao.

| Mifano ya kuanguka dhidi ya Jaribu | Andiko | Nini kilichosababisha kuanguka? |
|---|---|---|
| Petro kumkana Yesu | Luka 22:54-62 | Kujiamini kupita kiasi (Luka 22:31-34) |
| | | |
| | | |
| | | |

(2) Kutokana na mifano uliyoorodhesha, andaa andiko la mahubiri au la kujifunza Biblia kuhusiana na majaribu. Unganisha mfano wa Yesu pamoja na hii mingine uliyoorodhesha kwenye jedwali lako.

# Somo la 2
# Kuomba kama Yesu

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi atapaswa:
(1) Atambue umuhimu wa maombi katika maisha na huduma ya Yesu.
(2) Aelewe kanuni za maombi kutoka katika mafundisho ya Yesu.
(3) Aelewe umuhimu wa maombi katika huduma yetu kwa wakati huu.
(4) Kukuza kwa vitendo hatua zote za kuwa mtu wa maombi.

## Kanuni ya Utumishi

Kama tunataka tuhudumu kama Yesu, ni lazima tuwe waombaji kama Yesu.

## Utangulizi

Kwenye jujmbe wa mahubiri kuhusiana na maombi, Profesa Howard Hendriki alitoa taarifa hii ya kusadikisha kama ifutavyo:

> Shetani hajali kama unasoma Bibilia, *ila tu usiombe* kwa sababu Andiko haliwezi kubadilisha maisha yako. Linaweza hata likakupa tatizo kubwa la kiburi cha uzima kwa sababu unalijua sana.
>
> Shetani hana cha kujali kama unaishirikisha imani yako kwa wengine, *ila tu usiombe* kwa sababu anajua kwamba ni jambo muhimu zaidi kuongea na Mungu kuhusu wanadamu kuliko itakavyokuwa kuongea na watu kuhusu Mungu.
>
> Shetani hana cha kujali kama unajihusisha na huduma ya kanisa la mahali, *ila tu usiombe* kwa sababu utakuwa mshughulikaji sana lakini kwa uhakika hutafanikisha matarajio mengi.[41]

"Maombi ni ukumbi wa michezo ya mazoezi ya roho."
- Samuel Zwemer,
"Mtume kwa Uislamu"

Maombi yalikuwa ndio kiini cha huduma ya Yesu hapa duniani. Hakuna kilichochukua umuhimu zaidi kuliko maombi. Huduma ya Yesu ilizungukwa zaidi na uhusiano wake na Baba wa Mbinguni. Uhusiano huo uliimarishwa kupitia maombi na ushirika wake wa karibu na Mungu.

[41] Nukuu kutoka kwa Howard G. Hendricks, "Prayer – the Christian's Secret Weapon." Reprinted in *Veritas*, January 2004.

► Kabla ya kujifunza somo hili, fanya tathmini ya dhima ya maombi katika maisha na huduma yako. Jiulize:

- Je! maombi yangu ni endelevu?
- Ni lini mara ya mwisho nilipata jibu halisia la maombi?
- Kuna changamoto gani kubwa katika maisha yangu ya maombi?
- Je! ninaendelea kukua katika maisha yangu ya maombi?

## Mfano wa Yesu wa Maombi

Katika kipindi chote cha huduma ya Yesu, tunamwoana akiwa amejikita katika nyakati ngumu za maombi. Vitabu vya Injili vinatoa taarifa za matukio maalumu kumi na tano ambayo Yesu aliomba. Maombi kamwe hayakuwa nafasi ya pili kwake; maombi yalikuwa kiini cha maisha yake.

Luka anaonyesha kwa ufasaha huduma ya Yesu ya maombi kuliko mwandishi mwingine yeyote. Ni Luka peke yake anayetuambia kwamba Yesu aliomba usiku kucha kabla ya kuchagua wanafunzi wake kumi na mbili. [42] Ni Luka peke yake anayetueleza jinsi Yesu alivyobadilika mwili wake alipowachukua Petro, Yakobo na Yohana kwenda nao mlimani kwa ajili ya maombi. [43] Msisitizo huu unaendelea katika Kitabu cha Matendo kwa Luka kuandika mara thelathini na tano kuhusu majukumu ya maombi katika kanisa la mwanzo.

### Maombi katika Maisha ya kila siku ya Yesu

► Soma Marko 1:32-39.

Taarifa hii kutokea mwanzoni mwa huduma ya Yesu inaonyesha jinsi maombi na huduma vinavyohusiana. Chukulia maanani mwendelezo wa masimulizi haya. Jioni iliyopita, watu walikusanyika nje ya nyumba ya Yesu aliyokuwa akiishi, na aliwaponya wengi wao.

Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka akaenda zake "mahali pasipokuwa na watu" akaomba huko. Simoni Petro alikuja kumtafuta kwa sababu "Watu wote wanakutafuta." Yesu akawaambia, "Twendeni mahali pengine, mpaka vijiji vilivyo karibu, nipate kuhubiri huko nako; maana kwa hiyo nalitokea." Mfumo wa huduma ya Yesu ulikuwa ni *maombi yakifuatiwa na kazi ya utumishi.*

Hii inatakiwa iwe ndio mfumo wa huduma. Bila ya maombi, huduma yetu inakuwa imechoka kiroho. Bila ya utumishi, maombi yetu yanakuwa niya binafsi ; hatufanyi juhudi ya kuhudumia mahitaji ya wale wote wanaotuzunguka. Yesu ananonyesha kwamba maombi na utumishi ni lazima viunganishwe pamoja.

---

[42] Luka 6:12
[43] Luka 9:28

**Maombi katika nyakati za kufanya Maamuzi**

► Soma Luka 6:12-16.

Moja ya maamuzi muhimu sana wakati wa huduma ya Yesu ilikuwa wakati wa kuchagua mitume kumi na wawili. Kutoka katika maelfu ya wasikilizaji wa mahubiri yake, wengine walikuwa karibu sana naye hata kuweza kuitwa "mitume."[44] Wafuasi wake sabini na mbili walikuwa karibu naye sana kiasi cha kuweza kumwakilisha Yesu katika safari yake ya kwenda kuhubiri.[45] Lakini Yesu alichagua hapo kumi na mbili tu kuwa "mitume."

Hawa mitume kumi na mbili walichukuwa muda mrefu kukaa na Yesu. Walikuwa pamoja na Yesu mwishoni mwa huduma yake ya hapa duniani. Baada ya kupaa kwake, mitume kumi na moja walikuja kuwa viongozi katika kanisa la mwanzo. Uchaguzi wa mitume kumi na wawili ulikuwa ni uamuzi uliokuwa mkubwa sana. Yesu hakuwahi kuandika kitabu chochote au kuanzisha mashule. Urithi wake aliwaachia watu hawa.

Yesu alifanya nini kabla ya kuchagua hawa kumi na mbili? Aliomba. Akiwa anakabiliwa na uamuzi mgumu, Yesu alitumia usiku mzima akiwa anaomba. Kama Mwana wa Mungu aliomba kwa kumaanisha kiasi hicho kabla ya kufanya maamuzi magumu, ni kwa jinsi gani maombi yanaweza kutufanyia mambo makubwa katika kufanya maamuzi yetu!

**Maombi unapokabiliana na Mateso**

► Soma Mathayo 26:36-46.

Masaa machache kabla ya kukamatwa kwake, Yesu alikwenda Getsemane kuomba. Alijiandaa kukabiliana na mateso kwa kuomba. Yesu kamwe hajautumia uungu wake kukwepa mateso ya ubinadamu wake. Badala yake aliyategemea maombi kwa ajili ya kutiwa nguvu za kupambana na mateso.

Maombi ya Yesu kule bustanini ni mfano wetu wa kuigwa leo. Maombi yake hayakuwa ya kinafiki; Yesu alikuwa anakabiliwa na mateso ya kweli. Je, hii inakutia moyo kutambua kwamba Yesu alikumbana na njia zote za maumivu anazopitia mwanadamu? Ili kukabiliana na mateso, Yesu aliomba angalao apatiwe unafuu:

> Kule bustanini hajaomba kwamba, "Ee Mungu, ninakushukuru kwamba umenichagua mimi kupata mateso kwa niaba yako." Hapana. Alijisikia kuelemewa na masikitiko, hofu, kuachwa, na kitu kinachomjia cha kumtaka akate tamaa. Lakini bado, aliendelea kwa sababu alijua kwamba katikati ya dunia Baba yake yupo, Mungu wa upendo ambaye anaweza kumtegemea yeye bila kujali mambo yatakavyojitokeza. [46]

---

[44] Yohana 6:60, 66
[45] Luka 10:1
[46] Philip Yancey, *The Jesus I Never Knew.* (Grand Rapids: Zondervan, 1995), 161

Mbele ya mateso, hatupaswi kujifanya kwamba tunazo nguvu kuliko tulivyo. Kama Ayubu, tunaweza kulia tunapokabiliana na maumivu. Katika hali yake ya kibinadamu, Yesu alifanya vivyo hivyo! Hata hivyo, kama ilivyokuwa kwa Yesu, tunaendelea kubakia kuwa waaminifu kwa sababu tunajua kwamba Baba yetu wa upendo aliye mbinguni bado ameshikilia mamlaka yote.

Ni katika maombi tu tunaweza kuyakubalimapenzi ya Mungu. Msingi mkubwa wa maombi ya Yesu katika kukabiliana namateso, na msingi mkubwa wa maombi yetu katika mateso ni kujisalimisha kwenye mapenzi ya Baba: "Hata hivyo, siyo kama nitakavyo mimi, bali mapenzi yako yatimizwe."

## Mafundisho ya Yesu kuhusiana na Maombi

Yesu hakuonyesha tu umuhimu wa maombi kwakupitia mfano wake, bali alitumia muda mwingi katika kufundisha kuhusu maombi. Yesu alijua kwamba maisha ya kiroho ya wafuasi wake yangetegema sana maisha ya maombi. Kwa sababu ya hiyo, aliwafundisha wanafunzi wake kuomba

### Mafundisho ya Yesu katika Hotuba ya Mlimani

► Soma Mathayo 6:1-18.

Katika hotuba ya mlimani, Yesu alifundisha maeneo matatu yanayohusiana na utendaji wa kiroho: kutoa kwa ajili ya maskini, kuomba na kufunga kwa maombi. Ni wazi kutokana na mafundisho yake kwamba Yesu alitegemea haya yawe ni harakati za kawaida kwa wafuasi wake. Yesu hakusema, "kama mtatoa kwa ajili ya maskini,…" au "kama mtaomba…" au "kama mtafunga kwa maombi…" alikuwa anawategemea wafuasi wake wawe watoaji kwa hiari, waombaji na wanafunzi wenye nidhamu binafsi.

Yesu alionyesha kwamba shughuli zote hizi nzuri zinaweza zisiwe na maana yeyote kama zitatokana na malengo mabovu. Katika ulimwengu wa zamani, "mnafiki" au "hypocrite" ni jina la muigizaji aliyekuwa akivaa vinyago mbalimbali ili aweze kucheza kwenye nafasi mbalimbali. Inawezekana kabisa "kucheza kwenye nafasi ya kidini" mbele ya watu wengine.

- Inawezekana kutoa kwa ajili ya maskini ili kuwavutia wengine na ukarimu wetu. Yesu alisema, "Wameipokea thawabu yao."
- Inawezekana kuomba ili kuwavutia wanaotuangalia kwa maneno yetu ya kupendeza. Yesu alisema, "Wameipokea thawabu yao."
- Inawezekana kufunga kwa maombi ili kuwavutia wengine kwa uchamungu wetu na nidhamu binafsi. Yesu alisema, "Wameipokea thawabu yao."

Katika kila kipengele, mtu aliyetoa kwa ajili ya maskini, aliyeomba au kufunga kwa maombi amefanya hivyo kwa ajili ya watu wengine. Watu walivutiwa; hiyo ndiyo thawabu yake. Kwa hiyo, hatapokea thawabu kutoka kwa Mungu.

Makusudio katika harakati hizi za kiroho ni lazima ziwe zenye kumpendezesha Baba yetu wa mbinguni. Aidha iwe ni kutoa kwa ajili ya maskini, kuomba au kfunga kwa maombi, thawabu yetu ni Mungu mwenyewe. Hatupaswi kuzifanya harakati hizi za kiroho kwa ajili ya kuufurahisha ulimwengu. Badala yake, ni lazima tuyafanye haya kutoka katika kina chetu cha ndani cha matamanio na maombi yetu kwa Mungu.

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake jinsi ya kuomba kwa njia rahisi na iliyo wazi:

> Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu. Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele.[47]

Haya siyo maombi ya kufanywa kiholela tu bila kufikiria kama zile "aya tupu" Yesu alizoshutumu katika Mathayo 6:7-8. Badala yake, maombi haya hutengeneneza maadili ya tabia ambazo zinapaswa ziongoze maombi yetu:

### *Mahusiano*

"Baba yetu uliye mbinguni" inaonyesha uhusiano wetu wa karibu uliopo na Mungu. Kuliko kuonekana ni Mungu aliye mbali, tunamtambua kama Baba anayetupenda na anayetupa mema kama watoto wake. [48] Kifungu hiki kwa pamoja kinaonyesha ukaribu ("Baba Yetu") na mamlaka ("uliye mbinguni.") Mungu ni adhimu na aliye binafsi.

### *Heshima*

"Jina lako litukuzwe" linaonyesha tofauti iliyopo kati yetu sis na Baba yetu "aliye mbinguni." Ingawaje Mungu ni wa upendo, yeye ni mtakatifu.[49] Kama mwenye hekima katika kitabu cha Wimbo ulio bora alivyojifunza, ni lazima uende mbele za Mungu kwa heshima na hofu.[50]

### *Kujisalimisha*

"Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni," kunawakilisha kujisalimisha kwetu kwa hiari kwenye mamlaka yake. Kama vile mapenzi ya Mungu yanavyotimizwa kwa ukamilifu huko mbinguni, tunapaswa na sisi tuombe yatimizwe kwa ukamilifu hapa duniani.

---

[47] Mathayo 6:9-13
[48] Mathayo 7:11
[49] Neno "kufanywa wakfu" linamaanisha "takatifu" au "kilichotengwa."
[50] Wimbo Ulio Bora 5:2

### *Utoaji*

"Utupe leo riziki yetu" kulikuwa na umuhimu maalumu katika dunia kabla ya kuwepo kwa majokofu au umeme. Chakula kilitolewa mara moja kwa siku. Kifungu hiki kinaonyesha uaminifu wetu kwa Baba wa kila siku. Kama watoto wake, tunamwamini kwa utoaji wa mahitaji yetu.

### *Kukiri*

"Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu." Katika Luka 11:2-4, ombi hili hili limetamkwa, "Utusamehe dhambi zetu, kwa kuwa sisi nasi tunamsamehe kila tumwiaye." Kwa kuwa dhambi yetu ni "deni" tunalowiwa kwa Mungu, maana zote ni sawa katika Mathayo na Luka.[51]

Kwa kuunganisha msamaha wetu kwa watu wengine na ule wa Mungu kwetu, Yesu hajatufundisha kwamba "tufaidi" msamaha. Badala yake, sisi ambao tumesamehewa kwa mapenzi ya hiari, tuwasamehe wale wote wanaotukosea. Mfano wa Yesu wa yule mtumishi aliyekataa kusamehe unaonyesha uhusiano uliopo kati ya msamaha wetu sisi na hiari yetu ya kusamehe watu wengine.[52]

### *Ushindi*

"Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu" ni maombi ya ushindi dhidi, ya majaribu na mitihani ya maisha. Mungu kamwe hawajaribu watoto wake,[53] lakini kila mmoja wetu atakabiliwa na nyakati za majaribu na mitihani ya maisha.[54] Katika nyakati hizo, Mungu hawezi kuruhusu sisi tujaribiwe kupita vile tuwezavyo kustahimili.[55]

## Mafundisho ya Yesu kuhusiana na Kuomba kwa Bidii

► Soma Luka 11:1-13.

Luka anaifuatilia Sala ya Bwana kama mfano unaotufundisha sisi jinsi ya kuomba kwa bidii kwa Baba ambaye anapenda kuwapa watoto wake thawabu nyingi. Katika Mashariki ya Mbali, ilikuwa ni jambo la kawaida kwa mtu kukopa kutoka kwa jirani kwa ajili ya kumhudumia mgeni. Kama mtu mhitaji ataomba kwa bidii, jirani yake atampa chochote kilichokuwa kinahitajika. Kwa mila hii, ilikuwa inachukuliwa kama ni ukatili kusema "Hapana" kwa ombi lililotolewa. Hata kama huyo jirani hakutaka aisumbue familia, hataweza kukataa wito wa kusaidia.

---

[51] Wakolosai 2:14
[52] Mathayo 18:21-35
[53] Yakobo 1:13
[54] 1 Petro 1:6-7
[55] 1 Wakorintho 10:13

Katika hatua nyingine ya juu zaidi, Mungu anapenda kuwapa thawabu njema watoto wake wanaoomba kwa bidii. Kama vile iliyokuwa kwa huyu mtu katika huu mfano alivyoomba kwa bidii, tunaweza kumwendea Baba yetu wa mbinguni kwa ujasiri. Kwa nini? Siyo kwa sababu Mungu ataona aibu kuyakataa maombi yetu, bali ni kwa sababu tumepewa kibali cha "kuomba, kutafuta na kubisha hodi."

***Angalia kwa kuzingatia: Mitindo ya Kufundisha ya Kiebrania***

Katika Luka 11:1-13, Yesu anaelezea habari ya mtu mmoja ambaye hataki kuamka kitandani ili amsaidie jirani yake aliyekuwa anahitaji kukopa kwa ajili ya mgeni wake.

Ili kuelewa fumbo hili, ni lazima uelewe mtindo wa kufundisha wa Kiebrania – hoja ya "ndogo kuwa kubwa." Aina hii ya ufundishaji inasema kwamba, "Kama A (ndogo) ni kweli, basi ni kiasi gani cha B (kubwa) lazima kitakuwa kweli." Kwa wakati wa leo, tunaweza kusema. "Kama mtu atamlisha chakula mgeni mwenye njaa (A), ni kwa jinsi gani zaidi Mungu wa upendo anaweza kuwalisha watoto wake (B)."

Unaposoma mfano huu, usifikiri kwamba, "Mungu ni kama jirani mkaidi. Ni lazima nimshawishi yeye aweze kujibu maombi yangu." Badala yake, Yesu anamlinganisha rafiki mkaidi na Baba wa mbinguni aliye tayari. Kama jirani wa duniani anaweza kushughulika na ombi lililoombwa kwa bidii, ni kwa jinsi gani zaidi Baba wa mbinguni anaweza kushughulika kwa ajili ya watoto wake!

***Maombi ni mahusiano***

Mungu anataka ajibu maombi ya watoto wake, ni kwa nini mara nyingine majibu yake huchelewa? "Kuomba, kutafuta na kubisha hodi" ni maagizo ya wakati uliopo.Hii inamaanisha kwamba tunapaswa tuendelee "kuomba, kutafuta na kubisha hodi." Kwa nini?

> "Maombi siyo kuhusiana na vitu na kupata vile tunavyotaka. Maombi ni kumtafuta Mungu mwenyewe na kupata kile tunachohitaji."
> - Philipo Yancey

Sababu mojawapo ni kwamba maombi ni zaidi ya kutoa orodha ya msururu wa mahitaji. Maombi ni uhusiano endelevu kati yetu na Baba wa Mbinguni. Kama vile Paulo alivyotuamuru "tuombe bila kukoma,"[56] Yesu naye anatuamuru sisi tuendelee kuomba, kutafuta na kubisha hodi. Kutokana na mazungumzo endelevu na Mungu, mahusiano yetu na Mungu yanzidi kukua zaidi. Maombi ni zaidi ya orodha ya msururu wa mahitaji; maombi ni mahusiano.

**Mfano wa Maombi ya Kung'ang'ania**

Katika Luka 17, Mafarisayo walimuuliza Yesu ufalme wa Mungu utakuja lini. Aliwajibu akawaambia kwamba wasitegemee kuuona kwa kchunguza alama. Badala yake, "ufalme

[56] 1 Wathesalonike 5:17

wa Mungu umo ndani yenu."[57] Ufalme wa Mungu tayari ulikuwa ndani ya wale ambao walikuwa wamemfuata Yesu.

Kisha Yesu aliwageukia wanafunzi wake na kuanza kuwafundisha kuhusu ufalme wa Mungu. Walimtegemea Yesu aanzishe kwa haraka ufalme wa kisiasa, lakini Yesu aliwaandaa kusubiri hata baada ya kifo chake. Wakati wa kungojea, walipaswa kuendelea na maombi siku zote na "siyo kukata tamaa." Kisha Yesu akawaelezea habari iliyohusiana na maombi ya uaminifu

► Soma Luka 18:1-8.

Katika miji mingi ya zamani, makadhi walikuwa wadhalimu. Hakuna aliyeweza kusikiliza shauri bila ya kupokea rushwa. Huyu mjane hakuwa na fedha za kumpa rushwa huyu kadhi, kwa hiyo alikataa kusikiliza shauri lake. Hata hivyo, dada huyu mng'ang'aniaji hakutaka kabisa kukataa tama. Mwishowe, yule kadhi dhalimu akasema, "kwa kuwa mjane huyu ananiudhi, nitampatia haki yake."

Mfano huu unatumia mtindo wa "ndogo kuwa kubwa" kama mfano ule wa jirani aliyeomba kwa bidii. Unapousoma mfano huu, elewa kwamba:

- Mungu siyo mwamuzi asiyetenda haki. Mungu wetu anapenda "kutoa haki kwa kila mteule wake."
- Sisi siyo wajane. Yeye alikuwa mgeni, sisi ni watoto wa Mungu.

> "Maombi siyo kushinda Mungu kuchelewa kujibu. Maombi ni kuweza kijishikilia kwenye mapenzi ya Mungu."
> - Martini Luther

- Hakuweza kupata kibali kwa yule kadhi; kupitia kwa Yesu, tunacho kibali kwa Mungu.

Huu ni mfano wa ulinganifu. Kama kadhi madhalimu ataweza kumskiliza mjane aliyeng'ang'ania, ni kwa jinsi gani zaidi Baba yetu wa mbinguni anaweza kujibu maombi ya watoto wake?

**Mfano kuhusu Maombi ya Unyenyekevu**

► Soma Luka 18:9-14.

Mfano mwingine wa Yesu kuhusu maombi ulitolewa kwa "watu waliojikinai ya kuwa wao ni wenye haki, wakiwadharau wengine wote." Mfano huu unafundisha tabia halisi katika maombi.

Msingi mkubwa wa mfano huu uko pale mwishoni: "kila ajikwezaye atadhiliwa, naye ajidhiliye atakwezwa." Mafarisayo walidhania maombi yanajibiwa kwa sababu ya kuwa na haki yao wenyewe. Yesu anaonyesha kwamba maombi yanajibiwa kwa sababu ya neema

[57] Luka 17:20-21

ya Mungu kwa wale ambao hawana haki yao wenyewe. Hakuna hata mtu mmoja anayestahili maombi yake yajibiwe; Mungu hujibu maombi kwa sababu ya neema yake tu kwa wale wasiostahili lolote.

## Matumizi: Maombi katika Maisha ya Mkristo

Watu wanaomfanania Kristo ni watu wa maombi. J.C. Ryle, Askofu wa Liverpool wa karne ya kumi na tisa, alijifunza maisha ya Wakristo maarufu katika historia. Alisema kwamba baadhi yao walikuwa matajiri, wengine walikuwa maskini, waengine walikuwa wasomi; wengine hawakusoma kabisa. Wengine walikuwa Wakalvini; wengine walikuwa Waarminia. Baadhi yao walitumia liturugia, wengine walikuwa huru. "Lakini walikuwa na jambo moja la pamoja. Wote walikuwa watu wa maombi."[58]

Wakati wote wa historia ya Kanisa, watu waliomfananaia Kristo wamekuwa ni watu wa maombi. E.M.Bounds, Kiongozi mashuhuri wa Kikristo, aliomba kuanzia saa 10 alfajiri hadi saa moja asubuhi. Aliandika kitabu kilichopewa jina "Roho Mtakatifu hashuki kupitia taratibu zilizowekwa bali kupitia wanadamu. Hashuki kwa mashine bali kwa wanadamu. Haachilii upako wake kwenye mipango bali kwa wanadamu – tena wanadamu wa Maombi."[59]i

George Müller alisimamia vituo vingi vya yatima vya maelfu ya watoto. Aliamua kwamba kamwe hataomba msaada kutoka kwa mwanadamu mwingine lakini atategemea maombi peke yake. Alipokea zaidi ya dola 7,000,000 za Kimarekani kupitia maombi peke yake. Siyo tu kwamba aliweza kutoa msaada kwa vituo vyake vya yatima wake, bali Müller alitoa maelfu ya dola kwa ajili ya huduma nyingine. George Müller aliijua nguvu iliyoko katika maombi.

### Kwa nini tunaomba?

#### *Tunaomba kwa sababu sisi ni tegemezi kwa Mungu.*

> "Kama unaweza kufanya jambo lolote bila ya maombi, je, inafaa kufanya hivyo?"
> - Dr. Howard Hendricks

Katika ubinadamu wake, Yesu alitegemea maombi kama kiunganishi cha mawasiliano kati yake na Baba yake. Maombi ni kitendo cha kuwa tegemezi kwa Mungu. Inaonyesha kwamba hatujitegemezi wenyewe kwa maombi bali kwa Mungu.

► Soma Mathayo 26:31-46.

Kuanguka kwa Simoni Petro kunaonyesha umuhimu wa maombi. Yesu aliwaonya wanafunzi wake kwamba, "Ninyi nyote mtachukizwa kwa ajili yangu usiku huu." Kwa

---

[58] Imenukuliwa kutoka Matt Friedeman, *The Accountability Connection.* (Wheaton, Illinois: Victor Books, 1992)
[59] Edward M. Bounds, *Power Through Prayer.* (Kenosha, Wisconsin: Treasures Media, n.d.), 2

uwazi zaidi, Yesu alimwonya Simoni Petro, "Simoni, Simoni, tazama, Shetani amewataka ninyi."[60] Petro alianguka kwa sababu ya madhaifu mawili:

1. **Petro alijiamini kupita kiasi.** Alisisitiza, "Wajapochukizwa wote kwa ajili yako, mimi sitachukizwa kamwe,… Ijaponipasa kufa nawe, sitakukana kamwe!"[61] Kiburi kilimpa Petro kujiamini sana kwa kutegememea nguvu zake mwenywe.

2. **Petro alishindwa kuomba.** Kwa sababu alijiamini sana katika nguvu zake mwenyewe, Petro hakumtegemea Mungu. Adala ya kuungana na Yesu katika maombi, Petro alilala. Tunaomba kwa juhudi tunapotambua utegemezi wetu kamili kwa Mungu. Dick Eastman aliandika, "Ni katika maombi tu tunasalimisha matatizo yetu kabisa kwa Mungu."[62]

***Tunaomba ili kumjua Mungu kwa ukamilifu Zaidi.***

Mojawapo ya madhaifu makubwa ya kanisa la leo ni upeo wetu mdogo wa kuwa na ufahamu kuhusu Mungu. Mara nyingi, haja za maombi yetu zimehusika tu na mahitaji ya vitu na utoshelevu wa mambo binafsi. Tulio wengi tunatumia muda wetu mwingi tukiomba, "Mungu, nakuomba uwasaidie watoto wangu waweze kupata kazi" kuliko kuomba, "Mungu, saidia kuwatengeneza watoto wangu wawe katika mfano wako." Tunaomba kwa juhudi sana kwa ajili ya kupata uponyaji wa mwili kuliko uponyaji wa kiroho. Hii inaonyesha ni kwa jinsi gani tulivyo na ufahamu mdogo kuhusiana na maana halisi ya maombi.

> "Tunayaangalia maombi kama njia ya kujipatia chochote kwa ajili yetu wenyewe; wazo la Biblia kuhusu maombi ni kwamba tuweze kumjua Mungu Mwenyewe."
> - Oswald Chambers

Mojawapo ya makusudi ya msingi ya maombi ni kumjua Mungu kwa ukamilifu zaidi. Katika maombi, tunapatanishwa na moyo wa Mungu. Maombi siyokumtaka Mungu afanye kama tunavyotaka sisi afanye. Maombi hutupa ufahamu mpana wa moyo wa Mungu hadi tutakavyopata kama vile atakavyo yeye.

Tunapofikia katika hatua hii, Yesu alisema, "Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu."[63] Kwa kuwa mioyo yetu iko kwenye uelewano na moyo wa Mungu hatutaomba kutoka katika malengo yasiyofaa, au katika mambo yanayopingana na mapenzi ya Mungu.[64] Ufahamu huu wa moyo wa Mungu unakuja kupitia maombi thabiti.

Watu wa Tohara husema kwamba ni lazima "kuomba hadi tuwe tumeomba." Kwa maneno mengine, tunapaswa kuomba kwa muda mrefu na kwa uvumilivu mkubwa ili kupita

---

[60] Luka 22:31
[61] Mathayo 26:33, 35
[62] Dick Eastman, *The Hour That Changes the World.* (Grand Rapids: Baker Book House, 1995)
[63] Marko 11:24
[64] Yakobo 4:3 and 1 Yohana 5:14

kutoka maneno matupu hadi kuingia kwenye uwepo wa Mungu. Ni lazima tuombe hadi tufurahishwe katika Bwana.

► Elezea kuhusu wakati ambao maombi yaliweza kukupa wewe ufahamu wa ndani kuhusiana na Mungu pamoja na mapenzi yake.

**Tuombe kwa namna gani?**

Kwa kujifunza mfano wa Yesu kuhusiana na maombi, tunajifunza masomo muhimu kuhusiana na maombi yenye ufanisi.

***Tunaomba kwa uvumilivu.***

Yesu alikuwa Mwana wa Mungu.Mtu anaweza kutarajia maisha yake ya maombi kuwa ni jambo rahisi la kusema, "Baba, unataka mimi nifanye nini? Na kutarajia kupata jibu la haraka! Badala yake, tunamwona Yesu akiwa katika maombi ya usiku kucha kabla ya kuchagua wanafunzi wake Kumi na mbili. Tunamwona aking'ang'ana na maombi katika bustani ya Getsemani. Maombi, hata kwa upande wake Yesu, yalihitaji uvumilivu na muda. Maombi ni kumngojea Mungu.

Akiandika kuhusu umuhimu wa kungojea katika maombi, Glenn Patterson alisema, "Kitu Mungu anachofanya ndani yetu wakati tukiwa tunangojea ni muhimu kama kile tunachongojea. Kungoja ni sehemu ya mchakato wa Mungu wa kutufanya tuwe kama atakavyo yeye." Kwa jinsi tunavyoendelea kumsubiri Mungu, tunazidi kujifunza kumjua vyema zaidi.

> "Mwanadamu anaweza kukataa kwa dharau rufaa zetu, akatupilia mbali meseji zetu, akapingana na hoja zetu, akawanyanyasa watu wetu; lakini hawawezi kufanya lolote kinyume na maombi yetu."
> - J. Sidlow Baxter

Zaburi ya 37:1-9 inafundisha masomo muhimu kuhusiana na maombi. Angalia maamrisho haya:

- Usikasirike.
- Umtumaini Bwana.
- Ujifurahishe kwa Bwana.
- Umkabidhi Bwana njia yako.
- Umtumaini yeye.
- Ukae kimya mbele za Bwana.
- Umngojee kwa saburi.
- Ukomeshe hasira.
- Usikasirike. (kwa mara nyingine tena!)

Maamrisho haya yanalenga katika uaminifu wenye uvumilivu kwa Mungu anayekujali wewe na ambaye "atakupa haja za moyo wako." Kupitia maombi yenye saburi, tunakuwa watu tunaoaminika ambao ndiyo Mungu anatutaka sisi tuwe.

### *Mfano wa kuigwa wa Maombi Endelevu*

Mapema kabisa kwenye masisha yake ya Ukristo, George Müller alianza kuomba kwa ajili ya kuongoka kwa mafiki zake watano. Baada ya miezi mingi, mmojawapo miongoni mwa wale rafiki zake akakubali kumpa Bwana maisha yake. Miaka mingine kumi baadaye watu wengine wawili waliongoka. Ilichukua takribani miaka mingine ishirini na tano kabla yule rafiki yake wa nne hajampa Yesu maisha yake.

Müller aliendelea katika maombi hadi alipofariki kwa ajili ya rafiki yake wa tano.Kwa miaka hamsini na mbili, hakukata tamaa kumwombea huyu rafiki yake ili aweze kumkubali Kristo! Siku chache baadaye baada ya mazishi ya Müller, rafiki yake wa tano aliokoka. Müller aliamini katika maombi endelevu.

### *Tunaomba kwa Unyenyekevu.*

Yesu aliomba, "Walakini si mapenzi yangu, bali yako yatendeke."[65] Yesu alijua kwamba anaweza kumtegemea Baba yake katika mapenzi yake kamili.

Maombi ni kitendo cha unyenyekevu. Tunaomba kwa ajili ya watu wengine kwa sababu hatuna uwezo wa kuwasaidia katika hekima zetu; ni lazima tumtegemee Mungu. Tunajiombea wenyewe kwa sababu hatuwezi kuyamudu maisha kwa nguvu zetu wenyewe; ni lazima tumtegemee Mungu.

Maombi yanatambua haja yetu ya kupata msaada wa Mungu. Tunapojisikia tuna uthabiti katika uwezo wetu kukabiliana na matatizo ya maisha, haipingiki kwamba hatuwezi kuomba kwa kumaanisha. Tunapojitambua kwamba hatuwezi kuyakabili maisha kwa nguvu zetu wenyewe, tunaomba kwa unyenyekevu.

Maombi yetu ni lazima yafanyike kwa "unyenyekevu wa ujasiri." Tunapokuwa tunamngojea Mungu kwaajili ya majibu, tunaweza kuwa na uhakika na amani kwa sababu tunaomba kwa Baba yetu wa mbinguni ambaye anatupenda na anatutakia yaliyo mema kwa ajili ya watoto wake. Katika msongamano wa maisha na huduma, maombi ya unyenyekevu yanatupa tumaini la utulivu kwa Mungu.

### *Tunaomba Kibinafsi.*

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuanza maombi yao kwa kumtanguliza Mungu kibinafsi., "Bab yetu." Maombi ya kweli ni ya binafsi. Paulo Miller aliandika kwamba, "Watu wengi wanajitahidi kujifunza kuomba kwa sababu wanazingatia juu ya maombi na siyo juu ya Mungu."[66] Mara nyingi "tunaongea maombi" kuliko kusema na Mungu. Hili lilikuwa onyo la Yesu kutoka moyoni juu ya kutumia "misemo mitupu. "[67]

---

[65] Luka 22:42
[66] Paulo E. Miller, *A Praying Life: Connecting with God in a Distracting World.* (Colorado Springs: NavPress, 2009)
[67] Mathayo 6:7

Fikiria mtu anayekuja kwenye meza ya chakula cha jioni akiwa na kundi la hotuba zilizokaririwa. Anasema, "Ninataka kufanya mazungumzo na familia yetu, kwa hiyo nimeandaa maneno yaliyokaririwa." Haya siyo mazungumzo ya kweli! Tunategemea mtu awe na mazingatio na watu walioko mezani na siyo juu ya maneno atakayotumia.

Ni kwa njia hiyo hiyo, maombi yanazingatia juu ya Mungu kuliko juu ya mafungu ya maneno yaliyokaririwa. Maombi siyo mfumo; maombi ni mahusiano. Maombi ni lazima yawe ya binafsi.

**Ni kwa jinsi gani tunafanyika kuwa Watu wa Maombi?**

Katika karne ya tano, Anicia Faltonia Proba, mwanamke aliyepewa heshima ya juu wa Kirumi aliomba ushauri kuhusiana na maombi. Proba alitaka kujua jinsi ya kuwa mtu wa maombi. Augustine aliandika barua ndefu ikiwa na ushauri wa hekima kuhusu maombi.[68] Katika sehemu hii, tutaichunguza kanuni ya Augustine kuhusu maombi.

***Ni aina gani ya mtu anayeweza kuwa mtu wa maombi?***

Kwanza, Augustine anasema kwamba mtu wa maombi ni lazima awe mtu asiyekuwa na vianzo vingine. Mtu mwombaji ni mtu anayetumainia maombi peke yake.

Proba alikuwa mjane wa mmoja wa wanaume matajiri na wenye nguvu sana wa Roma. Wanawe watatu wa kiume walitumika kama Mabalozi wadogo wa Kirumi. Augustine alianza kwa kumwambia Proba kwamba "ni lazima ajihesabu mwenyewe kama aliyejitenga na ulimwengu." Haijalishi sisi ni matajiri, au wenye nguvu au tuliofanikiwa kwa kiasi gani, ni lazima tujitambue kwamba sisi tutambue kutokuwa na uwezo wowote mbele za Mungu. Vinginevyo, maombi yetu yatakuwa kama maombi ya Mfarisayo badala ya maombi ya Mtoza Ushuru.

***Mambo gani tunapaswa kuombea?***

Augustine anatoa jibulakushangaza kwa Proba. Anasema, " Omba kwa ajili ya maisha ya furaha." Hii inawezekana kuonekana kama ni ubinafsi, lakini Augustine anaelezea kwamba furaha ya kweli inatoka kwa Mungu peke yake. Mtu "ana furaha ya kweli ambayo ana yote anayotamani kuwa nayo, na hataki kuwa na kitu ambacho haipaswi kukitaka."

Mkristo ana furaha kwa sababu anaye Mungu, na anataka asiwe na kitu ambacho Mungu hangetaka awe nacho. Kama mtunga Zaburi, tunaridhika na uwepo wa Mungu.

---

[68] Philip Schaff, ed. *The Confessions and Letters of St. Augustine: Nicene and Post-Nicene Fathers, First Series, Volume 1.* (Buffalo, New York: Christian Literature Publishing Company, 1886)

> Neno Moja nimelitaka kwa Bwana, Nalo ndilo nitakalolitafuta, Nikae nyumbani mwa Bwana Siku zote za maisha yangu, Niutazame uzuri wa Bwana, Na kutafakari hekaluni mwake.[69]

Kama kweli tunatamani uwepo wa Mungu juu ya mambo yote, tunaweza tukaomba kwa ajili ya furaha tukijua kwamba Mungu atatosheleza matamanio yetu ya ndani kwa kujitoa mwenyewe kwetu!

### *Tunapaswa kuombaje katika nyakati za shida?*

Augustine anamkumbusha Proba kwamba Paulo alitambua kuna nyakati zitakazokuwepo ambazo "hatujui kuomba jinsi itupasavyo."[70] Tunapaswa kuombaje tunapofikia hatua ya kutokuwa na msaada?

Augustine anaangalia katika Maandiko matatu. Kwanza, anaelezea mfano wa Paulo wakati alipoomba kwa ajili ya ukombozi wa "kutokwa na mwiba katika mwili wake." Badala ya ukombozi, Mungu akamwahidi, "Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu." Paulo akashuhudia, "Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu… Maana niwapo dhaifu ndipo nilipo na nguvu."[71]

Pili, Augustine anaangalia mfano wa Yesu pale Getsemane. Yesu alikabidhi haja zake zote kwa Mungu. Yesu aliomba kwa ajili ya ukombozi: "Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke." Lakini akahitimisha, "Walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe."[72]

Mwisho, Augustine anaangalia kutoka katika Warumi 8:26. Tunapokuwa hatujui jinsi ya kuomba, Roho Mtakatifu huongoza roho zetu. Roho "hutusaidia katika madhaifu yetu" na "hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa." Wakati tunapokuwa tumekosa maneno ya zaidi ya kuomba, Roho Mtakatifu huyapeleka maombi yetu kwa Baba, ambaye anayapokea na "katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake."[73]

## Hitimisho: Unapojitambua kwamba hujui jinsi ya kuomba

Mara nyingine ukimya ndio jambo bora unaloweza kufanya.[74] Unataka kuomba, lakini hujui ni kwa jinsi gani; maombi hayatakuja. Katika hili ufanyeje? Siri moja ni kuelewa kwamba Kristo ndiye Kuhani wetu Mkuu.

---

[69] Zaburi 27:4
[70] Warumi 8:26
[71] 2 Wakorintho 12:8-10
[72] Mathayo 26:39
[73] Warumi 8:26-28
[74] Sehemu hii imenukuliwa kutoka kwa Marc Cortez, *Everyday Theology*.

Kama Wakristo wa kiinjili, tunaamini katika ukuhani wa waamini wote. Mafundisho haya makuu ya marekebisho yanafundisha kwamba kila mmoja wetu ana uwezo na njia ya kufika kwa Baba. Hata hivyo, kama haieleweki, mafundisho haya yanaweza kusababisha matatizo ya kiroho. Ninaweza nikashikwa na fadhaa: Je! Niliomba yakutosha? Je! Nilitimiza kwa uhakika sehemu yangu?"

Kwenye kongamano la mwaka 2013, Profesa Alan Torrance alitoa ushuhuda huu kuhusu matatizo aliyokumbana nayo katika maswali haya.

> Mnamo Januari 2008, mke wangu Jane alikufa kwa ugonjwa wa Saratani. Alikuwa mwanamke Mkristo wa ajabu sana, mke na mama. Nilipokuwa nikimwangalia akifa kwa maumivu ya saratani iliyoenea katika mwili wake wote, ilikuwa hali ngumu sana na nikiwaangalia watoto wetu wakishuhudia mateso yake ilikuwa ni hali ngumu sana. Kulikuwa na nyakati nyingine, katika huzuni yangu, nilitatizika kujua niombe kwa namna gani na niombe nini. Sikujua jinsi ya kuomba.
>
> Kwa wakati ule, ukuhani wa Kristo ulikuwa ni wa maana zaidi kuliko ninavyoweza kuanza kuelezea. Nilipokuwa nimemshikilia Jane kwenye mikono yangu, kuhani aliyepaa juu (Yesu Kristo) alikuwa akiomba kwa niaba yangu. Tulijisikia tumepumzika kwenye uwepo wake.
>
> Maombi niliyokuwa nikishikilia na kuomba hadi wakati ule ilikuwa ni Sala ya Bwana. Sikuachwa niombe peke yangu. "Baba **yangu** uliye mbinguni –nimeondolewa mbali na mahali nilipo." Badala yake kupitia Roho Mtakatifu, Niliomba, "Baba **yetu**, uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe."
>
> Kugundua umuhimu wa ukuhani endelevu wa Kristo nikugundua ijnjili katika njia inayobadilisha kila sehemu ya maisha yetu na kuabudu.

Tunashindwa kuelewa ukuhani wa waumini wote tunapofikiri ina maana kwamba nilazima tumwendee Baba kupitia nguvu zetu wenyewe za kiroho. Hili ni kosa. Ukuhani wa waumini wote unasisitiza kwamba hatuhitaji mpatanishi mwingine *zaidi ya Yesu.* Yeye ndiye anayetuombea, akikubaliana na majaribio yetu yaliyovunjika katika sala, na kuyawakilisha kwa Baba kama dhabihu ya kukubalika. Maombi yetu yanawezeshwa na Roho Mtakatifu na kupatanishwa na Kuhani wetu Mkuu, Yesu Kristo

Wakati unapokuwa hujui jinsi ya kuomba, usikate tamaa. Tunaye mmoja aliye mwombezi wetu, akipiga magoti pembeni mwetu, akituombea kwa Baba, akisema yale ambayo hatuwezi kuyasma.

**Kazi za kufanya Somo la 2**

(1) Kwa kutumia kitabu cha mpangilio wa maneno cha upatano au programu ya kupekua Biblia, pata mifano mitatu ya maombi katika Biblia. Linganisha kila ombi na Sala ya Bwana, Kuna vipengele gani vya Sala ya Bwana vinavyopatikana katika maombi yaliyoko katika maeneo mengine ya Biblia? Tumia jedwali lifuatalo hapa chini kuweka kumbukumbu za yale utakayoyaona.

(2) Weka jarida la maombi yako kwa mwezi mmoja. Weka taarifa za maumivu yako katika maombi, ushindi wako katika maombi, na majibu ya Mungu kutokana na maombi yako. Tumia jarida hili kuimarisha ukuaji wako katika maisha ya maombi.

| Maombi katika Biblia | Maandiko | Vipengele vya Maombi |
| --- | --- | --- |
| Maombi ya Nehemia | Nehemia 1:5-11 | • Uhusiano: “kutunza agano”<br>• Heshima: “Mungu Mkuu na wa kushangaza”<br>• Kujitoa: “maombi ya mtumishi wako”<br>• Utoaji: “toa mafanikio kwa mtumishi wako”<br>• Ukiri: “Kukiri dhambi za Wana wa Israeli” |
| | | |
| | | |
| | | |

# Somo la 3
# Kuongoza kama Yesu

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi atapaswa:

(1) Kutambua sifa zilizomfanya Yesu akawa kiongozi mashuhuri.

(2) Kuruhusu kusudio na wito uliopewa na Mungu kupima mambo yako muhimu ya kila siku.

(3) Kuanzisha utaratibu wa kufundisha viongozi wajao na kujenga timu ya huduma.

(4) Kukubaliana na jukumu lako kama mtumishi wa watu unaowaongoza.

## Kanuni ya Huduma

Viongozi ni kama Yesu wanapokuwa wanahudumia watu wengine.

## Utangulizi

"Uongozi" ni neno linalochochea hisia nzito. Wakati watu wenye mawazo ya ulimwengu wanapofikiria kuhusu uongozi, wanazingatia katika nguvu na nafasi. Kuwa kiongozi ni kuwa "bosi". Viongozi wenye tamaa wanachotaka ni "kupanda ngazi" na kupata cheo kikubwa. Hata wachungaji wanaweza wakachukua mawzo haya. Wanaweza kuzingatia katika mawazo yao jinsi ya kupata makanisa makubwa, nafasi za juu za uongozi na heshima kubwa.

Kwa kukabiliana na mawazo haya ya kidunia, baadhi ya Wakristo huonyesha hisia tofauti na neno hili "uongozi." Wakati mmoja mchungaji aliniambia. "Sitaki kuwa kiongozi katika kanisa langu. Ninachotaka ni kuwa mtumishi tu." Hata hivyo, ingawaje kauli hii inaonyesha hali ya unyenyekevu, unaliacha kanisa lake katika kutopambanua mwelekeo au kusudi. Mashirika yote, yakiwemo makanisa, yanahitaji viongozi.

Wachungaji wanapaswa kukumbuka kwamba chimbuko kubwa la neno "mchungaji" ni "mchungaji wa kondoo." Mchungaji wa kondoo hana kazi inayoonekana kwamba ni ya maana sana! Mchungaji wa kondoo hukamilisha kila siku akiwa na kondoo wanaonuka shombo ya kondoo. Kazi yake ni pamoja na majukumu yanayokinaisha – kutafuta chakula na maji, kufukuzana na wana kondoo wanaotangatanga huku na kule bila mpangilio wake, na kuwahudumia kondoo walioumia.

Mchungaji wa kondoo analo jukumu moja muhimu sana. Mchungaji wa kondoo anafanya kazi zinazoonekana ni za chini sana., mchungaji huyo huyo anabeba jukumu kubwa la

kuwaongoza kondoo wake kwenye usalama. Kondoo wanamtegemea mchungaji aliye kiongozi wao.

Yesu hutoa mfano bora wa kuigwa wa kiongozi wa kweli. Alikuwa ni kiongozi wa kondoo aliyetumika kwa unyenyekevu lakini akiwa na fasili ya dhana akilini ya mwelekeo mkubwa na kusudi. Alikuwa na nguvu lakini aliyejaa huruma. Hakutafuta nafasi ya madaraka, lakini alikuwa na uhakika na utume wake. Yesu alifanyika mfano wa kuigwa wa watumishi – viongozi.

► Fikiri juu ya kiongozi mmoja aliyefanikiwa sana ambaye ulimjua au unamjua binafsi. Orodhesha tabia tatu au nne ambazo zilimfanya huyu mtu akawa kiongozi mzuri. Je tabia hizi zinaonekana katika huduma ya Yesu? Je, tabia hizi zinaonekana kwenye huduma yako?

Yesu anaonyesha kwamba uongozi wa kweli unahusisha huduma ya unyenyekevu. Unyenyekevu hauna maana ya kuwa mdhaifu au kukosa maamuzi; Yesu alikuwa mwenye nguvu. Vitabu vya injili kwa kurudia mara nyingi zinaonyesha mamlaka ya Yesu.[75] Hata hivyo, alipata mamlaka hayo siyo kwa kudai heshima, bali kwa kuhudumu. Wakati wanafunzi wake walipouliza kuhusu nafasi za uongozi katka ufalme wa mbinguni, Yesu alijibu:

> Wafalme wa Mataifa huwatawala, na wenye mamlaka juu yao huitwa Wenye fadhili; lakini kwenu ninyi sivyo; bali aliye mkubwa kwenu na awe kama aliye mdogo; na mwenye kuongoza kama yule atumikaye. Maana aliye mkubwa ni yupi? Yeye aketiye chakulani, au yule atumikaye? Siye yule aketiye chakulani? Lakini mimi kati yenu ni kama atumikaye.[76]

Katika somo hili, tutaangalia tabia zilizomfanya Yesu akawa kiongozi mashuhuri. Tutajifunza jinsi ya kuwa viongozi wenye ufanisi kwa kufuata mfano wa Yesu.

### Kiongozi wa Kikristo mwenye Ufanisi anajua kuhusu Utume wake

Kiongozi mkuu na mashuhuri ana utume ulio wazi na anazingatia kwa nia moja uzito wa utume alioubeba. Yesu alijua kusudio la utume wake. Utume wa Yesu umejumlishwa kwa pamoja katika Marko 10:45: "Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi."

Katika hotuba yake ya kwanza ya hadharani, Yesu aliwaambia wasikilizaji wake kwamba alikuaja ili kukamilisha ujumbe uliokuwa umetabiriwa na Isaya, kwamba:

> Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu

[75] Mathayo 7:28-29; Marko 1:22-28; Luka 4:32-36; Luka 20:1-8
[76] Luka 22:25-27

> kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa, Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa.[77]

Utume wa Yesu uliongoza maamuzi yake ya kila siku. Alipokuwa akisafiri kutoka Yudea hadi Galilaya, utume wake uliongoza njia yake ya kupitia. Marabi wa Kiyahudi mara nyingi walisafiri kupitia upande wa Mashsriki wa mto Jordani ili kuepuka kukutana na kunajisiwa na Wasamaria. Njia ya Yesu, hata hivyo, iliongozwa na utume wake wa "kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa" Kwa mwanamke Msamaria. Kwa sababu ya hiyo, "ilibidi ni lazima apitie katika nchi ya Samaria."[78] Kama kiongozi wa Kikristo, utume wako ni lazima ukuongoze katika maamuzi yako ya kila siku.

Kama kiongozi, kuna mambo ya ziada ya kufanya kuliko yale unayoweza kukamilisha. Ni kwa jinsi gani unaweza kupima vipaumbele vyako? Huwezi ukafanya kila kitu, na *hutakiwi* ufanye kila kitu. Ni lazima ufanye mchanganuo wa nafasi zilizopo katika huduma yako ya umisheni/utume. Kila kiongozi anapaswa awe na orodha mbili: orodha ya "Mambo ya kufanya" na nyingine ya "Mambo yasiyotakiwa kufanyika," Orodha "Mambo ya kufanya" inakuwa pamoja na mambo yale ambayo unapaswa uyakamilishe. Orodha ya "Mambo yasiyotakiwa kufanywa" inakuwa na mambo yote ambayo yanakukengeusha katika utume au umisheni wako. Mtu fulani anaweza akaitwa kutumika katika mambo kadhaa, lakini wewe usiitwe kwa mambo hayo. Utume wako ni lazima ukuongoze katika vipaumbele vyako vya kila siku.

Mtume Paulo ni mfano wa kiongozi aliyejua kusudi la utume wake. Paulo aliitwa kupanda makanisa katika miji mikubwa ya Dola ya Kirumi. Hakutaka "kujenga juu ya msingi wa mtu mwingine," lakini alikuwa na wajibu wa kuipeleka injili kwa watu wote ambao walikuwa hawajabahatika kuisikia. [79] Utume huu uliweza kumwongoza Paulo mahali pa kwenda, akae mahali pamoja kwa muda gani, na hata ujumbe aliopaswa kuhubiri.. Utume wa Paulo uliongoza maamuzi yote.

► Jadili maswali haya:

- Mungu amekupa wewe utume wa aina gani? Fupisha maelezo ya utume wako kwa maneno machache.
- Je, umeshawashirikisha utume wako watu wengine wanaojiunga nawe katika huduma yako?
- Je, utume wako unaongoza maamuzi yako ya kila siku?

[77] Luka 4:18-19, akinukuu Isaya 61:1-3
[78] Yohana 4:4, msisitizo umeongezwa.
[79] Warumi 15:20

## Kiongozi wa Kikristo mwenye Ufanisi Anafundisha Viongozi Wengine.

Tangu mwanzo wa huduma yake, kwa uangalifu mkubwa Yesu alichagua na kufundisha kikundi cha wanafunzi ambao wangeendeleza huduma yake baada ya kuwa ameondoka kurejea kwa Baba yake. Wanafunzi hawa walijifunza kutoka kwake, walichukua muda mrefu kukaa naye, walitumika pamoja naye, na walisambaza ujumbe wake wa injili kwa dunia nzima. Yesu aliwatia muhuri hawa wanafunzi katika mfano wake, kasha akawatumia katika kulijenga kanisa lake.

Luka aliandika kuhusu shinikizo la huduma. "Wakati huo, makutano walipokutanika elfu elfu, hata wakakanyagana, alianza kuwaambia wanafunzi wake kwanza."[80] Yesu hangeweza kuingiliwa na wasiwasi kutokana na huduma yake hadi kwenye wanafunzi wake,ingawaje hudumakwa maelfu ya watu walio wengi ingekuwa ni ya kushangaza. Alijua kwamba, ili kuujenga ufalme, ni lazima awafundishe wanafunzi wake jinsi ya kuongoza kanisa. Kwa kuwafundisha wanafunzi, tunawaanda viongozi wa kizazi kijacho.

> "Yesu kamwe hakuwahi kuandika vitabu. Badala yake, aliandika ujumbe wake juu ya wanadamu, mitume."
> - William Barclay

Paulo alifuata mfumo huu wa Yesu. Aliwahubiri makutano, lakini alikazia mawazo yake yote katika kufundisha wanafunzi wachache katika kila mji. Hii inatoa mfano wa viongozi tunaotakiwa tuwe kwa wakati wa sasa. Paulo aliwataka wachungaji "kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke."[81] Mchungaji hahitajiki kufanya kazi zote za kanisa; mchungaji anapaswa kuwafundisha na kuwawezesha wafuasi kufanya kazi kwa ajili ya kanisa. Viongozi wenye ufanisi huwafundisha viongozi wengine.

## Mfano wa Yesu wa kuwashauri Wanafunzi

### Mshauri ni lazima Achague Wanafunzi kwa Umakini[82]

► Soma Yohana 1:35-51, Yohana 2:1-11, Mathayo 4:18-22, Luka 5:1-11, Luka 6:12-16.

Unaposoma aya hizi, je, unaona mchakato unaotumika? Wakati wa wiki ya kwanza ya huduma yake hadharani, Yesu aliwakaribisha Andrea na Yohana wamfuate. Andrea alimleta Simoni Petro kwa Yesu. Yesu akamwalika Filipo ambaye alimletea Nathanaeli.[83] Hii ilikuwa ni hatua ya kwanza katika wito wao. Walimkubali Yesu, lakini bado hawakufanyika wafuasi wa kudumu. Huu ulikuwa ni wito wa kumfuata Yesu. Baadaye, Yesu atawaalika kwenye uanafunzi wa kudumu.

---

[80] Luka 12:1
[81] Waefeso 4:12
[82] Nukuu kutoka kwa Robert Coleman, *The Master Plan of Evangelism.* (Grand Rapids: Baker Book House, 1963)
[83] Yohana 1:35-51

Yohana 2, ni hatua muhimu katika mchakato huu. Kwenye ndoa ya Kana, Yesu "aliudhihirisha utukufu wake" kwa wanafunzi wake. Wageni wengine hawakujua kuhusu mmjiza alioufanya; muujiza ulikuwa ni kwa ajili ya wanafunzi. Yesu alijidhihirisha mwenyewe kwa wafuasi wake ili waweze kuweka tumaini lao kwake. "Na wanafunzi waliamini katika yeye."[84]

Mathayo 4:18-22 inatokea baada ya Yesu kuondoka Nazarethi kwenda Kapernaumu na kuanza kuhubiri.[85] Akiwa anatembea kandokando ya Ziwa la Galilaya, Yesu alimwita Simoni, Andra, Yakobo na Yohana wamfuate. Mara hiyo hiyo waliacha nyavu zao wakamfuata yeye."[86] Baada ya wito wa kwanza katika Yohana 1, wanafunzi hawa waliendelea na kazi zao kama wavuvi. Sas, Yesu anawaita katika kutumika: "Tangu sasa utakuwa ukivua watu."[87]

Hatua nyingine iliyofuata katika mchakato huu ulikuwa ni Yesu kufanya uteuzi wa wanafunzi kumi na wawili. Miongoni mwa wafuasi wengi (walioitwa "wanafunzi" katika Yohana 6), Yesu alichagua hapo wanafunzi kumi na wawili ambao wangekuwa ni washirika wake wa karibu sana na yeye.

Yesu hakuharakisha katika kuwachagua wanafunzi wake. Inaonekana kama mchakato huu ulichukua miezi kadhaa. Hatua hii ilimpa Yesu nafasi ya kukaa na kila mwanafunzi katika wanafunzi wake Kumi na Wawili. Mara nyingi, kiongozi huwa mwepesi kuharakisha kuchagua mrithi wake bila ya kuchukua muda wa kumjua huyo mtu. Kiongozi mwenye busara hugawa majukumu yanayotoa nafasi ya kumfanyia mtu tathmini kuhusu uwezo wake wa kuwa kiongozi.

**Mshauri ni lazima Achukue Muda wa kukaa pamoja na Wanafunzi Wake**

► Ni lipi la kusisimua zaidi, kuwafikia wengi au kuwashauri wachache? Ni jambo gani lililo muhimu kwa ajili ya kipindi kirefu? Kwa nini Yesu aliwekeza nguvu zake nyingi sana kwa ajili ya hawa watu kumi na wawili?

Yesu aliutumia muda wake mwingi akiwa na hawa wanafunzi kumi na wawili. "Alichagua Kumi na Wawili (ambao aliwaita Mitume) **ili waweze kuwa pamoja naye** na ili aweze kuwatuma kuhubiri pamoja na kuondoa mapepo."[88] Kwanza, wangetumia muda wao kukaa pamoja na yeye ili wajifunze mbinu zake. Kuanzia hapo ndiyo sasa wangekuwa tayari kutumwa nje kwa ajili ya huduma.

---

[84] Yohana 2:11
[85] Matthew 4:12-17
[86] Matthew 4:20
[87] Luke 5:10
[88] Mark 3:14-15

Marko alichukua kumbukumbu mojawapo ya safari za Yesu katikati ya Galilaya: "Naye hakutaka mtu kujua, kwa sababu alikuwa akiwafundisha wanafunzi wake."[89] Lengo kubwa na la msingi la Yesu halikuwa kuanzisha utaratibu wa kuwafikia watu kwa makundi mengi, bali kuwaandaa watu ambao wangeongoza kanisa.

Yesu alihubiri kwa maelfu ya watu, lakini umuhimu wake mkuu ulikuwa katika kuwafundisha watu wachache kwa ajili ya huduma ya baadaye. Yesu alitambua kwamba kufundisha kunaleta matokeo bora zaidi kama mkazo utawekezwa kwenye kikundi kidogo. Robert Coleman anaonya, "Kwa jinsi huduma yako inavyokua, itakuwa ni **vigumu** zaidi kufanikiwa kupata muda wa kuwahudumia wanafunzi kibinafsi. Lakini jinsi huduma yako inayokua, itakuwa ni **muhimu** zaidi kufanikiwa kupata muda wa kuwahudumia wanafunzi kibinafsi."

Unapokuwa unapitia kusoma Vitabu vya Injili, utaona kwamba siyo mara nyingi utaweza kumwona Yesu akihudumu bila ya kuwepo angalao wanafunzi watatu pamoja naye. Mara nyingi, Yesu na wanafunzi wake walijiondoa kwa muda kwenda kwenye maeneo yasiyokuwa na watu kwa ajili ya vipindi vya mafunzo. Kukaribia mwishoni mwa huduma ya Yesu ulimwenguni, aliweza kutumia muda mwingi zaidi kwa ajili ya kukaa na wanafunzi wake. Katika wiki yake ya mwisho Yerusalemu, Yesu hakuwaacha wanafunzi wake wakae mbali na uwepo wake. Kuwafundisha watu hawa lilikuwa ni mojawapo ya majukumu yake muhimu sana.

Mithali ya Kiyahudi inasema, "Mwanafunzi ni mtu anayekula mavumbi ya bwana wake." Mwanafunzi alitembea karibu sana na bwana wake kiasi kwamba alimeza mavumbi yaliyotifuliwa na mguu wa bwana wake. Mwanafunzi alikula kile alichokula bwana wake; mwanafunzi alikwenda kila alipokwenda bwana wake; mwanafunzi aliwajibika kwa bwana wake kwa mafundisho na kuwa mfano wake. Wafuasi wa Yesu walitumia muda wao na yeye hadi walipochukuana na tabia ya mwalimu wao. Baadaye, wakaja kujulikana kama "Wakristo"; wamekuja kufanana na mwalimu wao.

Kwa njia hiyo hiyo, Paulo alikuwa na wafuasi wake kama Timotheo, Tito, Luka, au Tychicus pamoja naye. Paulo aliwafundisha kuhusu huduma kwa kuchukua muda wa kukaa nao.

Pia, njia hii inatupa mfano wa kuiga sisi wa leo. Unapofanya huduma yako, unaweza kuwatia moyo wafuasi wachanga ya timu yako wakufuate wewe, ili waweze kujifunza jinsi ya kuhudumu. Kiongozi mmoja wa kanisa aliyefanikiwa alisema, "Kamwe sifanyi safari ya huduma bila ya kufuatana na mhudumu mchanga pamoja nami. Kuwafundisha viongozi wa kanisa la baadaye ni muhimu kwangu kama ilivyo huduma ninayoitumikia." Mchungaji huyu anaelewa kwamba viongozi wenye ufanisi huwafundisha viongozi wengine.

---

[89] Mark 9:30-31

**Mshauri ni lazima afanye Huduma kwa Wanafunzi wake**

Baada ya kuwaosha miguu wanafunzi wake, Yesu alisema, "Nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo."[90] Yesu alifundisha kwa kuwa mfano. Alijua kwamba haitoshi tu kusema, "Fanya jambo hili." Ni lazima tuonyeshe kwa vitendo *namna* ya kufanya. Yrsu hakuwaelekeza wanafunzi wake kufanya jambo lolote hadi yeye mwenyewe awe ameshalifanya ili kuwaonyesha.

Wanafunzi walimwona Yesu akiomba kisha wakamwambia, "Bwana tufundishe jinsi ya kuomba."[91] Akaomba. Walipokuwa wakimwangalia jinsi anavyoomba, wanafunzi walipatwa na njaa ya kutaka kuelewa maombi. Wakati wanafunzi wanapokuwa na njaa ya kujifunza, wanajifunza vizuri sana!

Wanafunzi walimsikia Yesu akitumia maandiko katika mahubiri yake. Yesu alirejea kwenye Maandiko ya Agano la Kale zaidi ya mara sitini. Aliielezea Biblia jinsi inavyoweza kutumika kimantiki katika kuhubiri na kuandaa mahubiri kutokana na Maandiko yaliyomo. Je, wanafunzi walijifunza somo hili? Kwa hakika ndiyo! Wakati Petro alipohubiri kutoka katika Matendo 2, alirejea katika Yoeli, Zaburi 16, na Zaburi 116. Petro alijifunza kutoka kwa Yesu kuyajenga mahubiri yake kutoka katika Maandiko. Kila andiko la mahubiri katika Matendo linarejea kwenya Agano la Kale.

Paulo alifuata njia hiyo hiyo. Kwa kurudiarudia aliandika, "Mmeona mfano kutoka kwangu. Fuateni mfano wangu."[92] Paulo alifundisha kwa vitendo. Wanafunzi kama Tito na Timotheo walijifunza uchungaji kwa kufuata mfano wa mshauri wao, Paulo.

Wakati wa leo, tunapaswa kuwa mfano wa huduma kwa wale tunaowafundisha. Katika hili inatupasa sisi tuwe watu tunaoonekana wakati wote. Watayaona yale tunayoshindwa, lakini watatuona tukiyakiri madhaifu yetu. Watatuona kama tunaoyumba, lakini watatuona sisi tukikataa kuacha kusonga mbele. Wanafunzi hujifunza uhalisia wa huduma kwa kuangalia mifano kutoka kwetu.

**Mshauri ni lazima Akaimu Majukumu kwa Wanafunzi wake**

► Soma Mathayo 10:5-11:1.

Tangu mwanzo, kusudi la Yesu lilikuwa ni kuwaandaa wanafunzi kwa ajili ya huduma. Aliwaita wamfuate ili aweze kuwanya wawe "wavuvi wa watu."[93]

Muda mwingi wa wakati wao wa mwaka wa kwanza na Yesu, wanafunzi walikuwa wakiichunguza huduma yake. Walijifunza kutokana na mfano wake. Baada ya kuwa

[90] Yohana 13:15
[91] Luka 11:1
[92] Mifano ni pamoja na 1 Wakorintho 11:1; Wafilipi 3:17; Wafilipi 4:9.
[93] Mathayo 4:19

wameshachunguza, Yesu aliwatuma wanafunzi watoke nje kwa ajili ya kwenda kuhudumu. Mathayo 10 anaonyesha jinsi Yesu alivyokaimu majukumu kwa wanafunzi.

***Aliwapa Mamlaka (Mathayo 10:1).***

> Majukumu bila kuwa na mamlaka kunawalemaza wale unaowafundisha.

Kabla ya kuwatuma nje kwa huduma, Yesu aliwapa mamlaka ya kufanya kazi aliyokuwa awapangie kuifanya. Mara nyingine viongozi wana mashaka ya kuwaamini wale wanaowasaidia kwa mamlaka. Hata hivyo, *majukumu bila kuwa na mamlaka kunawalemaza wale uanaowafundisha.* Hatupaswi kuwapa wasaidizi wetu majukumu isipokuwa wamepewa mamlaka kamili ya kutimiza majukumu hayo.

***Aliwapa maelekezo yaliyo wazi (Mathayo 10:5-42).***

Yesu aliwapa wanafunzi wake ujumbe ulio wazi: hubiri kuhusu ufalme. Wajibu wao ulikuwa wazi. Walijua kwa uhakika ni nini Yesu alikuwa anawategemea wafanye.

Yesu aliwaambia wanafunzi wake ni mahali gani waende kuhudumu: "kwa kondoo waliopotea wa Israeli." Kisha, hawa mitume waende kuhubiri kwa Mataifa, lakini wakati walipokuwa wanajifunza kuhudumu, Yesu aliwataka waanzie karibu na nyumbani. Tunapaswa tufanye kila linalowezekana tuwasaidie wanafunzi wetu wafaulu. Anza na wajibu mdogo ambao ni wepesi kuumaliza. Yesu aliweka malengo yanayoeleweka na yenye maana.

Yesu aliwapa maelekezo wanafunzi wake kuhusiana na mateso. Mateso hayangekujakwa sababu wanafunzi wameshindwa katika huduma yao, bali kwa sababu Yesu mwenyewe huleta utengano kati ya wafuasi wake na wale wanaomkataa yeye.

***Aliwatuma wakiwa katika vikundi (Marko 6:7).***

Yesu alionyesha umuhimu wa kuwa kwenye vikundi katika huduma. Aliwatuma wanafunzi wake kwa vikundi vya watu wawili wawili. Miezi michache baadaye, Yesu aliwatuma wengine Sabini katika vikundi vya watu wawili wawili. Huu ukafanyika ndio mfumo wa huduma katika kanisa la mwanzo. Petro na Yohana walihudumu pamoja. Barnaba na Sauli walisafiri pamoja. Paulo na Sila walihudumu pamoja.

**Mshauri ni lazima Awasimamie Wanafunzi wake**

Baada ya wanafunzi kurejea kutoka katika huduma, walitoa taarifa kwa Yesu.[94] Ufuatiliaji ulikuwa ni sehemu muhimu katika mafunzo ya Yesu kwa wanafunzi wake. Haitoshi tu kukaimu majukumu; kiongozi mwenye ufanisi atatathmini utendaji wa wanafunzi. Kukaimu wajibu bila kuyafanyia tathmini kunasababisha matokeo hafifu.

► Soma Mathayo 17:14-21.

---

[94] Marko 6:30

Howard Hendricks alifundisha kwamba kushindwa ni sehemu sana katika mwendelezo wa hatua za mafunzo. Wanafunzi waliuliza, "Kwa nini sisi tulishindwa kumtoa pepo kutoka kwa huyu kijana?" Yesu aliwajibu kwa kuwafundisha kuhusu imani. Ilikuwa ni vyema sana kushindwa katika hatua za mwanzo za huduma kuliko ingekuwa baada ya Yesu kurejea kwake mbinguni!

Ukaguzi wnye ufanisi wa wanafunzi na lazima uambatane na tathmini. Wakati mwanafunzi anaposhindwa kutimiza wajibu, hatimuliwi "kutoka kwenye kikundi." Badala yake ni lazima tutafute sababu za kushindwa na tupange tena upya kwa ajili ya maboresho ya baadaye.

Yesu anaonyesha mpangilio huu katika Luka 9:

- Luka 9:1-6, Yesu anawatuma nje wanafunzi kumi na wawili.
- Luka 9:10, Walitoa taarifa kwake kuhusiana na safari yao.
- Luka 9:37-43, Wanafunzi walishindwa kutoa pepo.
- Luka 9:46-48, Yesu aliwafundisha kuhusu ukuu katika ufalme.
- Luka 9:49-50, Yesu alimkemea Yohana kwa maamuzu mabaya katika huduma.
- Luka 9:52, Yesu aliwatuma nje wanafunzi nje kwa ajli ya maandalizi ya kukitembelea kijiji katika Samaria.
- Luka 9:54-55, Yesu alimkemea Yakobo na Yohana kwa ajiliya tukio jingine la maamuzi mabaya katika huduma.
- Luka 10:1, Yesu alituma kundi kubwa zaidi la watu (Sabini) kwenda kuhudumu.

Yesu alibadilika kati ya mafundisho, kutuma wajumbe, na kufanya tathmini. Hakutaka kuwaacha wanafunzi wake hata pale ilipotokea kwamba wameshindwa. Badala yake alitumia kushindwa kwao huko kama nafasi ya kufundisha.

Paulo alifautilia mapangilio huo huo. Alimchagua Tito kuongoza kanisa katika visiwa vya Krete, na Timotheo kuwa mchungaji katika Efeso. Kisha aliandika nyaraka nyingi kwa ajili ya kuwapa mafunzo zaidi. Baada ya kupanda makanisa kwenye safari yake ya kwanza ya umishenari, Paulo alirudi tena kwenye safari ya pili kwa ajili ya kutoa miongozo kwa makanisa.[95]

Mfumo huu wa mafunzo ni wa ufanisi hata leo. Viongozi wengi wanatuma mhudumu mchanga bila ya usimamizi ulio endelevu au uwajibikaji – na wanashangaa wakati mhudumu anapokuwa ameshindwa. Hatupaswi kufikiri kwamba, "Nimefundisha somo,

---

[95] Matendo 15:36

kwa hiyo watafanya vizuri." Badala yake, usimamaizi ni mchakato ulio endelevu. Kama unataka kufundisha viongozi, ni lazima uwekeze muda wako katika kusimamia.

Howard Hendricks aliorodhesha hatua nne katika kufundisha wafanyakazi wapya

1. *Kuelezea*: Wafundishe maudhui. Yesu alifundisha ujumbe wa ufalme kwa wanafunzi wake.

2. *Kuonyesha*: Onyesha mfano wa huduma. Yesu alionyesha huduma kwa wanafunzi wake.

3. *Kufanya majaribio:* Huduma chini ya uangalizi wa moja kwa moja. Yesu aliwatuma wanafunzi kwena nje kwa ajili ya huduma kasha akatathmini uzoefu wao.

4. *Kutenda*: Huduma bila ya uangalizi wa moja kwa moja. Baada ya Pentekoste, wanafunzi walihudumu bila ya uangalizi wa Yesu.

► Unafanya nini katika kuwafundisha wanafunzi kwa ajili ya kuwa viongozi? Kwenye hatua ambazo tumeshajifunza, ni ipi unayoifanya kwa ufanisi? Ni hatua zipi zinahitaji kuboreshwa? Kama kikundi, jadili ni kwa jinsi mnaweza kuwa na ufanisi zaidi katika kuwa washauri wa viongozi wa baadaye. Majadiliano haya yanapaswa yaendelee hadi utakapopata mpango kazi wa kuwaendeleza viongozi katika mpangilio wa huduma yako.

### Wanafunzi wetu ni Lazima Wazalishe Wanafunzi wengine

Yesu alisema kwa wanafunzi wake, "Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa."[96] Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuzalisha wanafunzi wengine zaidi.

► Soma Mathayo 13:31-32.

Mfano wa Yesu wa punje ya haradali unaonyesha kwamba ufalme wa Mungu utakua kupita kiwango chake cha awali. Kama ambavyo mbegu ndogo sana ya haradali inavyoweza kuchipua na kuwa mti mkubwa kupita kiwango kilichotarajiwa, kanisa litaongezeka kupita kiwango ambacho mtu yeyote anaweza kutegemea. Kwenye Agano la Kale, ndege waliofanya makao yao kwenye mti huwakilisha ufalme mkuu yakiwemo mataifa.[97] Yesu aliahidi kwamba kwa jinsi ambavyo wanafunzi watazalisha, kanisa litaongezeka kupita viwango vyake vya mwanzo na litayafikia mataifa yote.

Dr. Robert Coleman aliandika kwamba tathmini ya mwisho ya huduma yetu inaonyesha kwamba huduma yetu inaendelea kuzalisha. "Mwisho wake hapa, sisi sote ni lazima tutathmini ni kwa jinsi gani maisha yetu yanaongezeka. Je, wale watu waliokabidhiwa dhamana kwa ajili yetu wanaweza wakachukuana na maono ya Agizo kuu la Mungu, na je,

---

[96] Yohana 15:16
[97] Danieli 4:12 na Ezekieli 31:6

kwa upande mwingine wanaweza kuliambukiza kwa wanafunzi waaminifu ambao nao pia watawafundisha wanafunzi wengine? Muda unawadia mapema sana ambapo huduma yetu itakuwa mikononi mwao."[98]

**Angalia kwa kuzingatia: Maombi ya Kuhani Mkuu Yesu**

Sehemu ya katikati ya maombi ya Kuhani mkuu Yesu yanaelekezwa kwa wanafunzi wake.[99] Maombi yake yanafundisha masomo ya thamani sana kuhusiana na njia ya Yesu ya kuwashauri wanafunzi.[100]

**(1) Mwanzo kabisa, tunawalinda wale tunaowashauri.**

Yesu aliomba, "Nilipokuwapo pamoja nao, mimi naliwalinda." Mara ishirini katika vitabu vya Injili, Yesu anawaambia wanafunzi wake kwamba "wajihadhari" na hatari. Aliwalinda na makosa. Tunapokuwa tunawafundisha wanafunzi, ni lazima tuwalinde kutokana na hatari za ulimwengu wao. Mafunzo yetu ni lazima yawe ya vitendo

► Ni hatari gani wanazopitia wanafunzi wa huduma wachanga katika mila yako? Kama mshauri, utawaandaje watoke katika hizi hatari?

**(2) Wanapoendelea kukomaa, tunawaamini wale tunaowashauri.**

Yesu aliomba, "Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu." Yesu alijua kwamba wanafunzi watakutana na majaribu, lakini alikuwa na matumaini kwa wale aliokuwa amewafundisha. Ni lazima tujifunze kuwaamini viongozi wadogo tunaowafundisha. Hii inatuhitaji sisi kusalimisha mbinu ya "mamlaka ya kimabavu" ya uongozi na kuwaamini wengine wenye maamuzi muhimu.

Ajith Fernando anaandika kwamba kuna njia mbili ambazo viongozi wanaweza kuwaona wafuasi wao.

- Viongozi wadhaifu wanaangalia madhaifu ya wafuasi wao.
- Viongozi wenye ufanisi wanaangalia uwezo wa wafuasi wao wakati wakiendelea kufanyia kazi madhaifu yaliyopo. Viongozi wenye ufanisi huwaangalia wengine "kupitia macho ya matumaini."

**(3) Baada ya kuwa wameshafundishwa, tunawatuma wanafunzi wetu nje kwenda kuuhudumia ulimwengu.**

Yesu aliomba, "Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami vivyo hivyo naliwatuma hao ulimwenguni." Baada ya Pentekoste, wanafunzi walianzisha huduma ya umisheni

---

[98] Robert Coleman, "The Jesus Way to Win the World: Living the Great Commission Every Day." Evangelical Theological Society, 2003.
[99] Yohana 17:6-19
[100] Nukuu kutoka kwa Ajith Fernando, *Jesus Driven Ministry* (Wheaton, Illinois: Crossway Books, 2002), 172-173

mkubwa ambao yesu alikuwa amewaandaa. Tunawashauri wanafunzi, ili nao baada ya hapo, wakaipeleke injili kwa ulimwengu wenye kuhitaji.

Yesu aliandika, “Mimi nimetukuzwa ndani yao.” Tunapokuwa tunawatuma nje wale tuliowafundisha, ni lazima tuhakikishe kwamba Yesu anapokea utukufu. Tunaweza kushawishika kujipatia utukufu kutoka kwa wale tuliowafundisha. Tuaweza kushawishika kuupokea utukufu kutoka na uwezo wetu wa kuwafundisha wanafunzi wengine. Badalayake, ni lazima tuhakikishe kwamba utukufu unamrudia Mungu mwenyewe.

## Kutumika: Thamani ya Timu za Huduma

Mfano wa Yesu unaonyesha umuhimu wa timu za huduma. Timu ya huduma kwa pamoja inahuska na kuwashauri watendakazi wasaidizi wadogo na kujenga mahusiano na wachungaji wengine. Tuliumbwa kwa ajili ya kuwa na ahusiano na watu wengine. Kwa nini timu za huduma ni muhimu sana?

### Timu zinaleta Uwiano

Yesu alichagua watu kutoka katika kaida tofauti za maisha. Petro na Yohana walikuwa wapinzani wa mara kwa mara. Mathayo alikuwa akifanyia kazi zake Roma, Simoni aitwaye Zelote alitaka kuwafurumisha Wayahudi watoke Yudea. Watu hwah walikuwa wanatofautiana. Katika kuchagua wanafunzi wake, Yesu alichagua kundi la watu waliokuwa na tabia na mitazamo tofauti.

Ingawaje mara kwa mara tunaona matatizo ya kuwa na watu wanaopingana na watu wengine katika timu, hatupaswi kudharau faida za tabia na mitazamo hiyo inayotofautiana na wengine. Petro kama Mtume alikuwa mwepesi kufanya matangazo makubwa. Aliwekwa kwenye usawaziko na mitume waangalifu kama Thomasi na Andrea. Kanisa la mwanzo lilifaidika kutokana na kuwa na watu waliokuwa na tabia na mitazamo tofauti katika uongozi.

Viongozi wenye hekima hutafuta watu watakaounda timu kutoka katika kaida tofauti za maisha. Timu yenye nguvu inaleta watu wenye uwezo unaotofautiana kwenye uongozi wa kanisa. Mwanachama mmoja kwenye timu anaweza kuwa na ufahamu mzuri katika mambo ya fedha, mwingine anaweza kuwa na nguvu kwenye mambo ya mahusiano, mwingine anaweza kuwa na ufahamu wa kina wa kibiblia. Wote wakija kwa pamoja wanaleta uwiano wa uongozi kwa ajili ya kanisa.

### Timu zinatoa Ushauri wenye Hekima

Alipokuwa akifundisha wanafunzi wake, Yesu alijua kwamba anajenga msingi kwa ajili ya kanisa.Baada ya Pentekoste, kutakuwepo na maamuzi mengi magumu yatakayolikumba kanisa la mwanzo. Yesu alijua kwamba wanafunzi watahitajiana kila mmoja na mwenzake wakati wa kufanya maamuzi haya.

Moja ya maamuzi ya mwanzo kabisa yaliyolikumba kanisa, “Ni kwa jinsi gani Mataifa watakaoamini watafanyika kuwa sehemu ya kanisa? Je, wanatakiwa kufuata vipengele

vyote vya sheria ya Kiyahudi? Ingawaje hili linaweza kuonekana ni jambo rahisi kwetu, lilikuwa ni uamuzi mgumu. Hili halikuwa suala la upendeleo wa binafsi; sheria za chakula na kutahiriwa, pamoja na kutahiriwa kwenyewe viliwekwa kwenye msingi wa Agano la Kale. Maamuzi yalikuwa yawe na matokeo yenye madhara ya muda mrefu. Kwa leo, wewe na mimi tunaguswa na uamuzi huu; kama Baraza la Yerusalemu lingeamua vinginevyo, watu wa Mataifa wanaogeukia katika Ukristo wangepaswa wakubaliane na Sheria za Kiyahudi.

Matendo 15 iaonyesha jinsi kanisa la mwanzo lilivyotatua suala hili muhimu. Baada ya kusikia maoni mbalimbali, walifikia kwenye maamuzi. Kwenye barua yao kwenda kwa kanisa la Mataifa, mitume walitumia kauli nzuri ya hekima katika kuelezea maamuzi yaliyoanyika, "Kwa maana ilimpendeza Roho Mtakatifu na sisi."[101] Roho Mtakatifu aliongoza katika kuwaleta viongozi wa kanisa mahali pamoja, akiruhusu washirikishane maoni yao, na kasha waliongoze kundi kwenye maamuzi sahihi.

Mwandishi wa Mithali anasisitiza thamani ya mchanganyiko wa mawazo wakati wa kufanya maamuzi.

- Njia ya mpumbavu imenyoka machoni pake mwenyewe; Bali yeye aliye na hekima husikiliza shauri.[102]
- Kwa wingi wa washauri huja wokovu.[103]
- Maana kwa mashauri ya akili utafanya vita; Na kwa wingi wa washauri huja wokovu.[104]

Hii ni kanuni muhimu sana kwa viongozi wa kanisa. Kama hauko tayari kuwasikiliza wengine, kwenye Mitahali anasema wewe ni mpumbavu. Mpumbavu siku zote hujifikiria kwamba yeye yuko sahihi, lakini mtu mwenye hekima yuko tayari kuwasikiliza wengine.

Kama kusudi la timu ni kutoa ushauri wa busara, tnahitaji watu wenye kufikiria mawazo tofauti kuliko tunavyofikiria sisi. Ni lazima tuhakikishe kwamba katika kuchagua timu hatuangalii wale wenye kufanana na sisi tu. Hatuhitaji watu wa "Ndio tu."

### Timu zinaleta Kutiwa Moyo

Mhubiri anaelezea faida za timu. "Afadhali kuwa wawili kuliko mmoja; Maana wapata ijara njema kwa kazi yao. Kwa maana wakianguka, mmoja wao atamwinua mwenzake; lakini ole wake aliye peke yake aangukapo, wala hana mwingine wa kumwinua!"[105]

---

[101] Matendo 15:28
[102] Mithali 12:15
[103] Mithali 11:14
[104] Mithali 24:6
[105] Mhubiri 4:9-10

Wakati kanisa lilipokuwa linapitia katika kipindi cha mateso, mitume walitiana moyo wenyewe kwa wenyewe. Luka analitumia neno "kwa umoja" kuelezea msaada wa pamoja miongoni mwa washiriki wa kanisa la mwanzo.

Mmishenari maarufu Hudson Taylor anaelezea hii kanuni. Taylor alikwenda China kwa shauku ya huduma, lakini katika muda mfupi sana alijikuta amekata tamaa. Hata baadhi ya wafadhili wake walisitisha kupeleka misaada ya kifedha. Wamishenari waliokuwa wameshajijenga vizuri kihuduma walikuwa wakimkosoa yeye. Hata serikali ya Uingereza ilipinga huduma yake. Mchumba wake alimwandikia akiwa akiwa Uingereza kwamba alikuwa hana uhakika kama anaweza kuolewa na mmishenari. Taylor alikuwa amekatishwa tamaa sana na alikuwa yuko tayari kurejea nyumbani.

Kwenye kipindi hicho, mmishenari mmoja mzee Mskoti aitwaye William Burns alikaa na Hudson Taylor miezi saba katika safari ya uinjilisti maeneo ya ndani ya China. Hawa watu wawili walisafiri pamoja, waliomba pamoja, na walihubiri pamoja. Wakati huo wa safari, Taylor aliingiwa tena na maono mapya kwa ajili ya China. John Pollock aliandika, "William Burns alimwokoa Hudson Taylor kutoka kwake mwenyewe."

Hudson Taylor baadaye alianzisha shirika la kimisheni la China Inland Mission na alijulikana kama mmishenari maarufu sana wa kizazi cha sasa; William Burns ni kama hajulikani kabisa. Hata hivyo, William Burns anastahiki kupokea sehemu ya pongezi kwa ajili ya maelfu ya watu waliookoka kupitia shirika la China Inland Mission. Burns alimtia moyo Hudson Taylor wakati akiwa katika mazingira magumu sana. Timu zinaleta kutiwa moyo.

**Timu zinaleta Uwajibikaji**

Kila mmoja wetu ana kasoro. Tunaleta kwenye huduma zetu madhaifu yanayotokana na kaida za maisha ya familia zetu, yanayotokana na maisha yetu kabla ya kuwa Wakristo, na kutoka katika haiba zetu binafsi. Mambo haya yote huathiri huduma zetu.

Hatuwezi kuziona kasoro hizi ndani yetu sisi wenyewe, lakini wengine walioko kwenye timu wanaweza kutuonya katika maeneo haya ambayo yanaweza kuharibu huduma zetu. Mwandishi wa Kitabu cha Waebrania aliwataka Wakristo "Kuhimizana katika kazi nzuri."[106] Neno *kuhimizana* lina wazo la kuchochea au kuleta msukumo kwa mtu. Wakati mwingine, hili halikubaliki. Hakuna hata mmoja wetu anayetaka kuchochewa au kusukumwa, uwajibikaji ni muhimu. Kila kiongozi wa Kikristo angalao mtu mmoja anayeweza kumwambia, "Kitendo hiki siyo cha hekima. Unapaswa ufikirie tena upya,"

Kutokea majumba makubwa ya utawa ya Zama za Kati na mikusanyiko ya madarasi ya Wesley hadi kwenye vikundi vya kisasa kama vile Watunza Ahadi, viongozi wa Kikristo wana msururu mrefu wa uwajibikaji wa mapokeo. Viongozi wa makanisa wa leo

[106] Waebrania 10:24

wanafaidika na uwajibikaji wa kila wiki. Hii inaweza kufanyika kati ya mtu mmoja na mwingine, kwenye vikundi vidogo, au kwa njia ya simu. Uwajibikaji huu unaweza kutuonya hatari ya kiroho kabla hatujaenda mbali sana.

Uwajibikaji mzuri unahitaji uaminifu kabisa kutoka kwa kila mhusika, na siri kabisa miongoni mwa wahusika. Unaweza ukapata mifano mingi ya maswali ya uwajibikaji. Orodha mojawapo ni hii inayohusisha maswali haya:

- Katika wiki hili, je, umeutumia muda wako na Mungu mara kwa mara?
- Katika wiki hili, je, umelegeza masharti ya uadilifu wako kwa njia yeyote?
- Katika wiki hili, je, mawazo ya maisha yako yamekuwa masafi kabisa?
- Katika wiki hili, je, umefanya dhambi yeyote ya uzinifu?
- Katika wiki hili, je, umefanya jambo gani la maana kwa mke wako?
- Katika wiki hili, je, umeishirikisha imani yako kwa mtu asiyeamini?
- Je, umekuwa mwaminifu kwa kila jibu lililotolewa hapa?

Kuwajibika kwa timu ni muhimu katika nyakati za majaribu. Akimwandikia mchungaji kijana, Paulo anampa ushauri wa jinsi ya kujenga huduma ya kudumu. Paulo anamwonya Timotheo, "zikimbie tamaa za ujanani; ukafuate haki, na imani, na upendo, na amani, pamoja na wale wamwitao Bwana kwa moyo safi."[107] Paulo alielewa kwamba maisha ya kiroho ya Timotheo yatakuwa na faida kama ataungana na watu wengi wanaomfuata Mungu ambao "wanamwita Bwana kutoka ndani ya mioyo iliyo safi."

► Kama wewe ni mmojawapo katika timu ya huduma, shirikisha baadhi ya faida unazozipata kutoka katika timu yako. Kuna changamoto gani zinazopatikana kwa kuwa mmojawapo katika timu ya huduma?

### Kufanya kazi na Timu

Yesu alitengeneza kikundi cha watu wenye sifa zinzotofautiana kabisa kwenye timu yenye umoja.. Yesu alichukuliana na zile tofauti zao na kuunda timu ambayo ingeweza kuongoza kanisa la mwanzo. Kanisa lilihitaji uongozi wa ujasiri wa Petro, na lilihitaji utulivu wa roho wa Filipo. Mojawapo ya changamoto kubwa za kiongozi ni kutengeneza kikundi cha wafuasi ili kuwa timu ya huduma.

Ajith Fernando, kiongozi wa kanisa kutoka Sri Lanka, anaelewa vizuri changamoto za kuijenga timu. Anaandika:

> Labda masikitiko makubwa ya kanisa la kiinjili ni kwamba mara kwa mara hisia zinakuwa juu ya theolojia katika kupima jinsi tunavyoamua na kutenda. Mkristo anayeiamini Biblia husema, "Hata kama kuna hisia zozote kuhusiana na mtu huyu. nitamkubalii kwa sababu Mungu ananitaka nifanye hivyo. Na nitamwomba Mungu

---

[107] 2 Timotheo 2:22

anipe neema ya kufanya kazi kwa kupatanishwa pamoja naye." Theolojia yetu inasema kwamba jitihada hii ya kufanya kazi na mtu huyuitafanikiwa, ingawaje hisia zetu zinaweza zikatupa ujumbe mwingine. Theolojia yetu inatutuma kufanya kazi kwa bidii katika mahusuiano haya. Tunaomba kwa ajili ya mtu huo na kuhusu mahusiano yetu na yeye. Tutakutana naye mara kwa mara. Tutatafuta kumwonyesha upendo wa Kristo na kufanya yale yote tunayoweza kwa ajili ya ustawi wake wa binafsi. Tunatengeneza ndoto za kile ambacho mtu huyu anaweza kukifanikisha kupitia katika timu.[108]

1 Wakorintho inafundisha kwamba ndani ya mwili wa Kristo, hatuna haki ya kuwakataa watu kisa tu kwamba hatuwataki. Kama ukijenga kanisa, utakuwa na washirika ambao hutaweza kuwafurahia. Kama kiongozi wa Kikristo, ni lazima useme. "Hata niwe na hisia za aina gani, nitamkubali mtu huyu kwa sababu Mungu amemweka chini ya usimamizi wangu. Nitamwomba Mungu anipe neema ya kufanya kazi pamoja naye, na nitamwomba Mungu ambariki na kumpa mafanikio katika huduma."

## Kiongozi wa Kikristo mwenye ufanisi ni Mtumishi

Wakati mmoja nilimwuliza mchungaji mtarajiwa, "Kwa nini unataka kuwa mchungaji?" Kijana huyu akajibu, "Nilipokuwa kwenye uwanja wa ndege nilimwona mtu mmoja akiwa amebeba mkoba wa mchungaji wake. Nami ninataka mtu wa kubeba mkoba wangu!"

Mtazamo wa Yesu ulikuwa tofauti kabisa! Huyu rafiki yangu alikuwa anataka ahudumiwe; Yesu alitaka ahudumie. "Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi."[109] Yesu anatuonyesha sis kwamba uongozi wa kweli unahusisha huduma. Yesu alijinyenyekesha mwenyewe, "akatwaa namna ya mtumwa."[110]

► Soma Yohana 13:1-20.

Kuna maeneo mengi kutoka katika Vitabu vya Injili ambako tunaweza kujifunza aina ya kiongozi mtumishi, lakini moja ya mfano wenye nguvu sana ni maelezo yanayohusiana na Yesu kuwaosha miguu wanafunzi wake. Katika tukio hili, Yesu anaonyesha inamaanisha nini kuwa mtumishi.

Baadhi ya makanisa yanashikilia huduma ya "kuosha-miguu" kama tendo la kuigiza matendo ya Yesu wakati wa Chakula cha Mwisho. Hii inaweza ikawa ni huduma nzuri sana, lakini itakuwa na nguvu zaidi tukitambua kwamba Yesu hakufanya sherehe maalumu. Badala yake, alitimiza wajibu ambao ulipaswa ufanyike.

---

[108] Ajith Fernando, *Jesus Driven Ministry* (Wheaton, Illinois: Crossway Books, 2002), 133
[109] Marko 10:45
[110] Wafiipi 2:7

Kwa sababu mavumbi mengi kwenye barabara za Yerusalemu, ilikuwa ni kawaida kwa mtumishi aliyeajiriwa kuosha miguu ya wageni kwenye chakula rasmi cha jioni. Huu ulikuwa ni wajibu wa unyenyekevu waliokuwa wamepewa watumishi wa hadhi ya chini. Wakati Yesu alipojiunga na wanafunzi wake kwa ajili ya sherehe za Pasaka, hakukuwa na mtimishi katika kile chumba. Hakuna mwanafunzi hata mmoja ambaye angeweza kujitolea kuifanya kazi ya kuosha miguu; walikuwa wanategemea kupata vyeo vikubwa katika ufalme wa Yesu. Yesu akainama akaanza kuifanya kazi iliyokuwa ifanywe na mtumishi wa hadhi ya chini kabisa.

Tukio hili linaonyesha uelewa wa Yesu wa uongozi. Watu wengine huutafuta uongozi kwa ajili ya kupata madaraka na nguvu. Kusudi lao lilikuwa ni kuwa pale juu ya shirika. Yesu tayari alikuwa pale juu; alikuwa Mkuu wa wanafunzi. Lakini kwa hiari yake mwenyewe akajishusha hadi kwenye nafasi ya chini kabisa.

Hii ndiyo inayomaanisha kuwa kiongozi anayemfanania Kristo. Kiongozi anayemfanania Kristo anabeba wajibu ambazo wengine hawazipendi. Kiongozi anayemfanania Kristo huwahamasisha wengine siyo kwa kupitia uwezo wake wa kutoa maamrisho, lakini kupitia mfano wa huduma yake ya unyenyekevu.

> "Meza kuu za watu wa heshima imekuwa ni alama mbadala wa taulo na karai la kunawia kama ishara ya uongozi miongoni mwa watu wa Mungu. Ni wakati wa kurejesha upya utumishi wetu."
> - C. Gene Wilkes

Mtu mmoja siku moja akasema, "Kipimo cha roho ya mtumishi ni 'Ninafanyaje ninapokuwa nimetendewa kama mtumishi?'" Kiongozi anayefuata mfano wa Yesu hakwaziki anapotendewa kama mtumishi wa hadhi ya chini. Katika maisha yake yote, Yesu alitendewa kama mtumishi wa hadhi ya chini, lakini hakutaka kufanya mashambulizi kwa ajili ya hali hiyo. Ususahau kwamba Yesu aliiosha miguu ya Yuda pamoja na wanafunzi wengine. Je, unaweza kufikiria kumwosha mtu kwa unyenyekevu ambaye tayari ameshadhamiria kukusaliti?

Baada ya kuwa amemaliza kuosha miguu ya wanafunzi wake, Yesu aliwaambia hawa watu wanaotafuta nafasi za madaraka, "Nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo."[111] Miaka thelathini baadaye, Simoni Petro atakuwa amekumbuka unyenyekevu wa Yesu alipoandika, "Jifungeni unyenyekevu, mpate kuhudumiana."[112] Kwa jinsi ile ile ambayo Yesu alijizungushia toweli ili awahudumie wanafunzi wake, sisi nasi tunapaswa tujizungushie unyenyekevu kwa ajili ya kuwahudumia watu wengine.

Kama viongozi wa Kikristo, tunaweza tukashawishika kutafuta madaraka kuliko kutafuta nafasi za kuwahudumia watu wengine. Yesu alionyesha kwamba uongozi ni huduma.

---

[111] Yohana 13:15
[112] 1 Petro 5:5

## Hitimisho: Umuhimu wa kuwashauri Wahudumu wengine wa Kikristo

Mwishoni mwa maisha yako, athari yako kama mshauri wa wahudumu wengine wa Kikristo inaweza kuwa urithi mkubwa wa huduma yako. Kama utakuwa mshauri wa wahudumu kumi na mbili tu wa Kikristo wakati wa huduma yako, matokeo ya utumishi wako itazidishwa na wale kumi na mbili pamoja na wale ambao wanashauriwa.

Kwa masikitiko, ingawaje viongozi wengi wa Kikristo wanajua umuhimu wa kushauri, viongozi wachache wanatumia muda wao kushauri wengine. Kwa nini tunapuuzia kipengele hiki cha huduma?

Sababu mojawapo ni **gharama** za kufanya ushauri. Kufanya ushauri kunachukua muda muhimu sana. Mara nyingi tunaamini kwamba muda unaotumika katika ushauri kwa viongozi vijana ungeweza kutumika vizuri zaidi kuhudumia vikundi vikubwa.

Sababu nyingine ni **kukatishwa tamaa** kunakoambatana na kushauri. Inaonekana kama inaleta mvuto kusema, "Ninafundisha kizazi kingine kijacho cha viongozi." Ukweli halisi mara nyingi msisimko ni mdogo.

Mara nyingi, yumkini Yesu alikuwa anafikia mahali pa kukata tamaa kutokana na hatua za kuendelea polepole kwa wanafunzi wake. Baada ya miaka mitatu na Yesu, , Filipo aliuliza, "Bwana, utuonyeshe Baba, yatutosha."[113] Majuma kadhaa baadaye Yesu akawalisha chakula watu elfu tano, wanafunzi walikabiliana na mkutano wa watu elfu nne. Wakaambizana, "Je! Ataweza wapi mtu kuwashibisha hawa mikate hapa nyikani?"[114]

Mtume Paulo alikutana na hali ya kupita kiasi inayofanana na hii ya kukataa tamaa. Yohana Marko aliachana naye kwenye safari yake ya kwanza ya umishenari.[115] Baada ya miezi kadhaa ya kumfundisha Dema, Paulo anaandika akiwa peke yake katika chumba cha gereza, "Dema aliniacha, akiupenda ulimwengu huu wa sasa."[116]

Kushauri kuna gharama na kunaweza kukatisha tama, lakini ni sehemu muhimu sana ya kazi ya kiongozi.. Kila kiongozi wa Kikristo aliyekomaa anapaswa aweze kufanya ushauri kwa kutengeneza viongozi wa baadaye. Wakati huo huo, kila kiongozi wa Kikristo anahitaji awe na mshauri atakayetoa msaada nyakati za mapambano.

Howard Hendricks alisema kwamba kila mtu anahitaji watu watatu kwenye maisha yake:

1. Kila mtu anamhitaji Paulo, mshauri anayekupa changamoto ya kuendelea kukua.
2. Kila mtu anamhitaji Barnaba, rafiki anayekupenda vya kutosha atakayekuwa mkweli na wewe katika madhaifu yako.

---

[113] Yohana 14:8
[114] Marko 8:4
[115] Matendo 13:13
[116] 2 Timotheo 4:10

3. Kila mtu anamhitaji Timotheo, kijana mdogo wa kumhudumia kama mwanafunzi na ushauri katika huduma.

► Malizia somo hili kwa kujiuliza:

- "Paulo wangu ni nani?"
- "Barnaba wangu ni nani?"
- "Timotheo wangu ni nani?"

**Kazi za Kufanya Somo la 3**

(1) Orodhesha mifano minne ya wakati ambapo wanafunzi waliweza kushuhudia huduma ya Yesu. Angalia ni nini wanafunzi walijifunza kutokana na kumwangalia Yesu.

| Mfano | Andiko | Fundisho kwa wanafunzi |
|---|---|---|
| Yesu akimponya kijana aliyepagawa na mapepo | Mathayo 17:14-21 | Nguvu ya imani |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |

(2) Orodhesha watu wawili au watatu unaoweza kuwa mshauri kwa kuwaanda kwa ajili ya huduma ya baadaye. Andika ibara fupi ambayo utajibu maswali mawili yafuatayo:

- Ni sifa gani ninazozitaka kuona kwa mtu ambaye namshauri?
- Ninataka kuona Mungu akikamilisha nini kwa mtu ambaye namshauri? (Kuwa maalumu)

Anza kuchukua hatua za ushauri kwa watu uliowataja kwa majina. Mwombe Mungu akuonyeshe jinsi ya kuwaandaa kwa ajili nafasi za huduma.

# Somo la 4
# Kufundisha kama Yesu

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi atapaswa:
(1) Kutambua sifa ambazo zilimfanya Yesu akawa mwalimu mashuhuri.
(2) Kujifunza njia za vitendo kwa ajili ya kuboresha huduma yake kama mwalimu.
(3) Kupanga kazi ambazo zitaboresha utayari wa wanafunzi kwa ajili ya darasa.

## Kanuni ya Huduma

Watakapokuwa tayari wamekamilika kabisa kwa mafunzo, wanafunzi wetu watamfanania mwalimu wao.

## Utangulizi

*Somo hili halina kazi za kufanya pale mwishoni. Badala yake, kazi ndogo ndogo za kufanya zimewekwa kwa mfululizo katika somo hili chini ya kichwa cha habari, "Liweke Somo katika Mazoezi." Baadhi ya haya, yatahitaji kuandika au shughuli za vitendo. Mengine yatahitaji tu kufikiri au kujadiliana. Kamilisha kila kazi kama utakavyokuwa unapitia maelezo ya mafundisho.*

Moja ya taarifa za maana sana ambazo hazikuwahi kutolewa kuhusu nguvu ya ualimu zilitoka kwa Yesu. "Mwanafunzi hawi mkuu kuliko mwalimu wake, lakini kila mtu ambaye amehitimu hulingana na mwalimu wake."[117] Yesu alijua kwamba baada ya kuwa ameshawafundisha wanafunzi wake, watashabihiana na tabia yake mwenyewe. Kwa sababu hiyo, Yesu alituma nguvu zake nyingi katika kuwafundisha wanafunzi wake Kumi na mbili.

Kwenye baadhi ya makanisa, jukumu la kufundisha kwa kiwango kikubwa limepuuzwa. Shule za jumapili zilizo na waalimu wasiokuwa na ujuzi wanapewa elimu ndogo sana na wakati mwingine hawapewi kabisa. Juhudi ndogo sana zinachukuliwa katika kuwafundisha waongofu wapya au watoto wadogo.

Kama viongozi wa makanisa, tunapaswa kutoa umuhimu katika kufundisha kama vile Yesu alipotoa umuhimu katika kufundisha. Kama wanafunzi "watafanana na mwalimu wao," jukumu la kufundisha ni la muhimu sana. Tunapaswa kufundisha waalimu wafuate mfano wa Yesu, Mwalimu Mkuu.

---

[117] Luka 6:40

► Fikiri kile unachokijua kuhusiana na mtindo wa Yesu wa ufundishaji. Orodhesha tabia tatu au nne zilizomfanya akawa mwalimu mkuu. Sasa fikiria kuhusu mwalimu mzuri sana ambaye umewahi kujifunza kutoka kwake. Orodhesha tabia tatu au nne ambazo zilimfanya huyu mtu akawa mwalimu mashuhuri. Ni tabia gani katika hizi orodha mbili zinahusiana?

## Moyo wa Mwalimu Mkuu: Tabia

Maudhui ya mafundisho ya Yesu yalikuwa katika msingi wa **tabia** ya Mwalimu. Moyo wa Yesu ulitoa msingi wa mafundisho yake. Msingi wa moyo wa mwalimu mkuu ni nini?

### Yesu, Mwalimu Mkuu alielewa Mahitaji ya Wanafunzi wake

► Soma Luka 4:16-21.

Waalimu wa shule huandaa "andalio la somo" kwa kila siku ya darasa. Andalio la somo linaonyesha ni kitu gani mwalimu anataka kukamilisha katika kila kipindi cha darasa. Andalio la somo linahusisha mambo kama:

- Lengo: Wanafunzi watajifunza kuongeza sehemu ndogo.
- Shughuli: Wanafunzi watajibu maswali 1-20 katika ukurasa wa 89 kwenye daftari la darasani.

Nilipoanza kuandaa kozi hii ya Shepherds Global Classroom, niliandaa andalio la somo lilitoa muhatasari wa kile nilichokuwa nataka kukamilisha katika kila somo. Yesu alikuwa na "andalio la somo" kwa ajili ya huduma yake, lakini andalio lakela somo halikuorodhesha kurasa katika daftari la kazi. Badala yake, andalio la somo la Yesu lililenga katika mahitaji ya wanafunzi wake. Yesu aliwaambia wasikilizaji wake kile ambacho alikuja kukikamilisha:

- Kuwahubiri maskini habari njema.
- Kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao.
- Kuwafanya vipofu kupata kuona tena.
- Kuwaacha huru waliosetwa,
- Kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa.[118]

Malengo ya Yesu yalikidhi mahitaji ya wanafunzi wake, Wanafunzi wa Yesu hawakuwa matajiri kama Masadukayo na ndiyo walioliendesha sinagogi la Yerusalemu na pia kushikilia vyeo vya juu vya kisiasa katika baraza la utawala la Sanhedrin. Wanafunzi wake walikuwa ni Wayahudi wa kawaida ambao walikuwa wakigandamizwa na utawala wa Kirumi. Baadhi yao walikuwa vipofu au viguru. Wengi wao walikuwa watu maskini walioteseka kutokana na kodi kubwa.

[118] Luka 4:18-19

Andalio la somo la Yesu lilikuwa rahisi; atashughulikia mahitaji ya wanafunzi wake. Atawafungua waliofungwa katika vifungo. Atawaponya vipofu. Kwenye kalenda ya Kiyahudi, "Mwaka wa Jubilii" ulikuwa ni mwaka wa kusherehekea. Madeni yalifutwa, ardhi zilizochukuliwa zinarejeshwa kwa familia husika zilizokuwa wamepokonywa; watumwa waliachiwa huru. Yesu alitangaza kwamba alikuja kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa kwa wale wote waliokuwa wamegandamizwa.

Kwa kipindi chote cha utumishi wake hapa duniani, Yesu alizungumzia mahitaji ya wanafunzi wake. Mara zote Yesu hakuwapa watu mahitaji waliyokuwa wanayataka, bali aliwapa mahitaji yaliyokuwa yanahitajika. Mwanamke Msamaria alitaka apewe maji; alihitaji ukombozi.[119] Petro alitaka avue samaki; alihitaji umisheni.[120] Kwa kila kipengele, Yesu alikutana na mahitaji mazito ya wanafunzi wake.

Hivi karibuni nilikuwa nahitaji kununua gari. Wauzaji wengi wakaanza kusema, "Hili ni gari kubwa. Hapa kuna sababu za wewe kuweza kununua gari hili." Nilikutana na mwuzaji mmoja aliyekuwa tofauti sana. Alianza kwa kuuliza maswali. Aliuliza, "Unaendesha gari kwa muda gani kila siku? Una uwezo gani wa kifedha wa kuweza kulipia gari?" Ni kipi unachoona ni muhimu kwako – gari ya starehe au gari inayotumia mafuta vizuri kwa maili? Nilipomaliza kujibu maswali yake, mwuzaji akaniambia, "Hili hapa gari nzuri kwako kulingana na mahitaji yako." Nilipokuwa ninasikiliza, nilitambua kwamba, "Hivi ndivyo Yesu alivyofanya wakati alipokuwa akifundisha. Alianza kwa kusikiliza mahitaji ya wanafunzi wake."

► Soma Marko 10:17-22.

Katika maelezo haya ya kijana tajiri aliyekuja kwa Yesu, mwelezeaji anasema, "Yesu akamkazia macho, akampenda." Neno akamkazia macho" katika mstari huu na zaidi ya kutizama kulikokwa kawaida. Inamaanisha "kuangalia kwa makini na kutambua kwa uwazi. Yesu aliuona moyo wa huyu kijana. Watu wengine walikuwa wamemwona tu kijana mdogo tajiri; Yesu aliona moyo uliokuwa na njaa.

► Soma Marko 16:1-8.

Fikiria aibu ya Petro baada ya kuwa amemkana Yesu. Hata ile furaha ya kufufuka iliharibiwa na aibu yake mwenyewe alipokumbuka jogoo akiwika. Katika hali hii, Malaika alimwambia Mariamu, "Lakini enendeni zenu, mkawaambie wanafunzi wake, **na Petro,** ya kwamba awatangulia kwenda Galilaya; huko mtamwona, kama alivyowaambia." Yesu alijua kwamba kati ya wanafunzi wake wote, aliyekuwa anataka awe na uhakika zaidi ni Petro. Wenzake walimwona kama ni mtu mmoja mwoga aliyemkana Bwana wake; Yesu alimwona kama mwanafunzi aliyeanguka ambaye alihitaji urejesho.

[119] Yohana 4:7-42
[120] Mathayo 4:18-22

Yesu alijua kwamba hatuwezi kufundisha wanafunzi kama hatutaweza kuwafahamu vizuri. Wavuvi wakasema, "Kama unataka kumkamata samaki, ni lazima ufikiri kama samaki." Kama unataka uupate moyo wa mwanafunzi, ni lazima ufikiri kama mwanafunzi. Ni lazima uelewe moyo wa wale unaowafundisha. Kama mwalimu, ni lazima ujifunze somo, lakini zaidi pia, ni lazima ujifunze kuhusu wanafunzi wako. Ni lazima uyaelewe mahitaji ya wanafunzi wako.

**Liweke Somo katika Mazoezi**

► Fikiria kuhusu wale unaowafundisha (aidha iwe rasmi au isiwe rasmi). Zingatia juu ya mwanafunzi ambaye anajitahidi. Andaa orodha ya mambo ambayo unaweza kuyafanya ili kukidhi mahitaji ya huyu mwanafunzi.

**Yesu, Mwalimu Mkuu, alikuwa na Subira.**

***Yesu alikuwa mwenye subira kwa wale waliokengeuka dhidi yake.***

► Soma Yohana 6:41-71.

Tukio hili linafanyika katika wakati mmoja wa mabadiliko ya mpito ya huduma ya Yesu. Kipindi cha mwaka uliokuwa umepita, Yesu alikuwa amefurahia sana umaarufu usikuwa na kifani. Watu walikuwa wamestahi sana miujiza yake na walifurahia mikate na samaki. Sasa Yesu akatangaza, "Mimi ndimi chakula cha uzima." Haya maneno aliyoyasema yaliwasumbua wasikilizaji wake. "Amin, amin, nawaambieni, Msipoula mwili wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima ndani yenu." "Kwa ajili ya hayo wengi miongoni mwa wanafunzi wake wakarejea nyuma, wasiandamane naye tena."

Yesu alifundisha watu kwa maelfu, akijua kwamba wengi hawangekubaliana na mafundisho yake. Aliwafundisha wale wanafunzi Kumi na mbili, akijua kwamba "mmoja wenu ni shetani." Alikuwa mwalimu mwenye subira.

***Ysu alikuwa mwenye subira kwa wale ambao hawakumwelewa.***

► Soma Marko 8:27-33.

Yesu alikuwa na subira kwa wale wanafunzi waliokuwa wazito katika kujifunza. Angalia ni mara ngapi Yesu anataja kuhusu upofu na mashaka ya wanafunzi. Hata wakati Petro alipokiri kwamba "Wewe ni Kristo" alikuwa haelewi kwa ukweli ilikuwa na maana gani. Ni katika aya chache baadaye, Yesu anamkemea Petro kwa mawazo yake potofu.

► Soma Yohana 3:1-21.

Yesu alikuwa na subira na yule Mfarisayo ambaye hakuyaelewa mafundisho yake. Wakati Nikodemo alipokuwa amechanganyikiwa, Yesu alimwuliza kwa mshangao, "Je! Wewe u mwalimu wa Israeli, na mambo haya huyafahamu?" Nikodemo alipaswa awe anajua

kwamba Ezekieli alishatabiri siku ambayo Israeli ingezaliwa kwa maji na kwa Roho. Lakini badala ya kuachana na hilo, Yesu akachukua nafasi kumfundisha Nikodemo somo.[121]

Hapa ndipo palipo na kipimo changu kama mwalimu. Ni mara ngapi nimekuwa tayari kufundisha somo kabla ya kukata tamaa? Kwa uvumilivu, Yesu alifundisha na kufundisha tena wanafunzi wake. Hakuwahi kusema, "Tayari nimeshafundisha somo hilo. Kama hukulipata, umechelewa." Alikuwa akikuta kwamba kama mwanafunzi wake amekuwa mwepesi kufundishika na mafundisho yake, Yesu aliendelea kufundisha. Yesu, Mwalimu Mkuu, alikuwa na subira.

**Liweke Somo katika Mazoezi**

► Je, unashawishika kuachana na wanafunzi wazito kufundishika? Je, unafadhaika wanapokuwa hawapokei mafundisho yako? Ni kwa jinsi gani unaonyesha subira kama Mwalimu Mkuu kwa wale unaowafundisha?

**Yesu, Mwalimu Mkuu, Aliwapenda Wanafunzi wake.**

► Soma Marko 6:30-34.

Yesu aliwachukua wanafunzi wake kupitia ziwa la Galilaya kwa ajili ya kutafuta eneo la kujitenga ili waweze kupumzika kutokana na msongo wa mara kwa mara kutoka kwa makutano na huduma. Maelfu ya watu waliona alikokuwa akienda wakakimbilia huko kupitia ufukweni ili wakakutane na Yesu. Yesu alipofika pwani alikutana na umati mkubwa wa watu wa wanaume elfu tano, wanawake na watoto. Alipouona mkutano ule mkubwa wa watu, "akawahurumia; kwa sababu walikuwa kama kondoo wasio na mchungaji; akaanza kuwafundisha mambo mengi."[122] Yesu, Mwalimu Mkuu, alifundisha kwa sababu aliwapenda wanafunzi wake.

Mapema katika somo hili, tulisoma maelezo ya kijana mmoja tajiri ambaye "alikwenda zake kwa huzuni" kwa sababu hakuweza kulipa gharama za kumfuata Yesu.[123] "Yesu alipokuwa anamwangalia, **alimpenda**."[124] Mwalimu Mkuu alimpenda mwanafunzi wake, hata yule ambaye anataka kuachana naye.

Yesu aliuangalia ule umati mkubwa wa watu akauonea huruma, watu binafsi pamoja na wale ambao walimkataa. Mhubiri mmoja alihubiri somo lililosema, "Yuda, Mwanafunzi aliyependwa na Yesu." Mhubiri huyu alitambua kwamba Yesu alionyesha upendo hata kwa Yuda. Huku akijua kabisa kwamba Yuda atamsaliti, Yesu, Mwalimu Mkuu, alimpenda mwanafunzi wake hadi mwisho.

---

[121] Yohana 3:5 anaonyesha ahadi ya Ezekieli 36:25-27. Ezekieli aliiona siku ambayo watu wa Mungu watanyunyiziwa maji safi, (maji haya yatatakasa kutoka katika uchafu na vinyago) na kutiwa Roho mpya (itakayoleta kuzishika sheria na hukumu ya Mungu).
[122] Marko 6:34
[123] Marko 10:17-22
[124] Marko 10:21

Ni rahisi kumpenda mwanafunzi anayekuja darasani mapema, ambaye amefanya kazi zote alizoachiwa, na anayeonyesha nia ya kujifunza. Lakini inakuwa ni vigumu kumpenda Yuda anayetusaliti, kijana tajiri anayetuacha na kuondoka, na Petro ambaye mara kwa mara anashindwa kuelewa. Yesu, Mwalimu Mkuu, anaonyesha kwamba ni lazima tuwapende hata wale wanafunzi ambao wanaonekana ni tatizo.

**Liweke Somo katika Mazoezi**

► Fikiri kuhusu mwanafunzi ambaye ana matatizo ya kupenda. Labda ni mtumishi wako wanayepingana na uongozi wako. Labda ni mfuasi wa kanisa lako anayekushutumu. Anza kwa kuomba, "Mungu, ninajitahidi kumpenda mtu huyu, lakini ninajua wewe unawapenda.. Naomba unisaidie kuwaona kupitia macho yako. Nisaidie kuwapenda kama Yesu alivyowapenda wanafunzi wake."

## Mikono ya Mwalimu Mkuu: Mbinu

Katika "Moyo wa Mwalimu Mkuu, "tunaniona tabia ya Yesu. Kila jambo alilofundisha Yesu lilikuwa ni kulingana na tabia yake. "Katika Mikono ya Mwalimu Mkuu," tunaona mbinu alizotumia Yesu. Kama tunataka tufundishe kama Yesu, ni lazima tufuate mitindo yake.

**Yesu, Mwalimu Mkuu, Aliwasilisha Malengo yake.**

► Soma Luka 5:1-11.

Wakati Yesu alipokuwa akihubiri kando ya Ziwa la Galilaya, makutano walimsonga hadi ikabidi apande kwenye chombo kimoja cha kuvulia mali yake na Simoni Petro.[125] Baada ya kufundisha, Yesu alimgeukia Simoni akamwambia, "Tweka mpaka kilindini, mkashushe nyavu zenu mvue samaki."

Simoni alikuwa mvuvi mzoefu aliyetumika usiku kucha kuvua samaki bila mafanikio. Alijua kwamba ilikuwa ni kazi bure kujaribu tna kuvua chochote, lakini alifanya kama Yesu alivyomwagiza. Kwa mshangao wa Petro, wavuvi walirudi na idadi kubwa ya samaki ya kushangaza. Yesu akamwambia Simoni, "Kuanzia leo utakuwa mvuvi wa watu."

Yesu, kama waalimu wengine wote wazuri, aliwakilisha kwa uwazi malengo yake kwa wanafunzi wake. Kwenye siku ya Pentekoste, Petro alionyesha kwamba alikuwa tayari kukamilisha malengo ya Yesu aliyoyaweka kwake.

Waalimu wenye ufanisi huwakilisha malengo yao. Wanawaambia wanafunzi wao, "hiki ndicho mtakachojifunza leo." Mwisho wa somo hili, uliza, "umejifunza nini leo?" Wanahakikisha wanafunzi wanaona kwamba lengo la somo lililowekwa limekamilika.

---

[125] Neno la Luka "Ziwa la Geneserati," au la Yohan "Ziwa la Tiberia," Mathayo na Marko "Ziwa la Galilaya," na Musa' "bahari ya Kinerethi" (Hesabu 34:11) yote yanarejea ziwa moja tu kubwa na muhimu wakati wa huduma ya Yesu. Baadhi ya wanafunzi wa Yesu walikuwa ni wavuvi katika ziwa hili, na huduma zake nyingi alifanyia kwenye ufukwe wa Ziwa la Galilaya.

**Liweke Somo katika Mazoezi**

► Kwenye nafasi yako ifuatayo ya kufundisha, andika kusudi lako la somo kwenye ubao mahali ambapo wanafunzi wanaweza wakaona.. Hakikisha kwamba kusudi lako liko wazi na rahisi kuleweka. Toa utambulisho wa somo lako mwanzoni mwa kipindi. Mwishoni mwa somo, waulize wanafunzi, "Je, tumefanikisha kusudi letu?"

**Yesu, Mwalimu Mkuu, alitoa fursa kwa Mazoezi ya Kuongozwa.**

Ufundishaji wenye ufanisi ni zaidi ya hotuba. Mafunzo ya kweli yanahitaji mazoezi.

► Soma Luka 10:1-24.

Wanafunzi hawa walikuwa bado hawajafundishika kwa ukamilifu, lakini Yesu aliwaachia wayafanyie mazoezi masomo aliyokuwa anawafundisha. Wanafunzi walipokuwa wakirejea kwanya safari hii ya mazoezi, walitoa taarifa kwa Yesu. Aliona kwamba bado hawakuwa wameelewa masomo, hivyo aliendelea kuwapa maelekezo. Pia aliwatia moyo akiwaambia, "Heri macho yaonayo mnayoyaona ninyi!" Yesu aliongoza mazoezi yao.

Haitoshi tu kutoa fursa kwa ajili ya mazoezi; mazoezi ni lazima yafanyiwe tathmini kisha yafuatiwe na mafunzo zaidi. Mithali ya kawaida inasema, "Mazoezi husababisha ukamilifu." Hii siyo moja kwa moja kweli. Mazoezi yasiyokuwa kamilifu hayawezi kuleta utendaji bora. Ni vizuri kusema, "**Mazoezi yaliyoongozwa** yanaleta ukamilifu." Mwalimu mwenye ufanisi atawapa wanafunzi wake furrsa ya kufanya mazoezi, kutathmini mazoezi pamoja na wanafunzi, kisha awatie moyo na kuwaongoza hao wanafunzi.

Wakati fulani nilijaribu kujifunza mchezo wa gofu. Nilipiga ile mipira ya gofu na kufanya mazoezi kwa masaa mengi, lakini haikutokea nikawa mzuri kwenye mchezo. Kwa nini? Nilikuwa peke yangu kwenye eneo la kupigia mpira bila kuwepo na mtu wa kuniongoza. Wakati mpira ulipokwenda upande usiotakiwa, hakuwepo mtu wa kunieleza kwamba, "Hapa ndipo ulipofanya vibaya." Wakati mpira ulipobiringika fiti chache mbele yangu kutoka nilipokuwa mimi, hakuna mtu aliyeniambia, "shikilia klabu ya kupigia mpira namna hii…" Nilifanya mazoezi, lakini mazoezi yangu yalikuwa hayana manufaa.

Paulo alijua thamani ya mazoezi ya kuongozwa. Alimfundisha Timotheo na Tito, kisha akawapa nafasi kwenye huduma. Katika Nyaraka za Kichungaji, Paulo aliwaandikia Timotheo na Tito akiwapa maelekezo ya ziada. Aliwaongoza wanafunzi wake kila walipokuwa wakifanyia mazoezi kanuni za huduma alizokuwa amewafundisha.

Wakati fulani nilitembelea shule ya Wakristo nchini Afrika ya Kusini. Kila mwanafunzi alikariri na kusoma bila kuangalia 1 Wakorintho 13 ndani ya darasa. Mwanafunzi mmoja alijitahidi kwa majuma kadhaa na zoezi hili. Hakuwa amekariri vizuri na alikuwa na aibu sana mbele ya wanafunzi wenzake. Siku hiyo nilipoitembelea shule, mwanafunzi huyu mwishowe alifanikiwa kuisoma kwa kukariri sura nzima mbele ya darasa.

Alipomaliza, wanafunzi wengine walisimama na kumshangilia huyu kijana mdogo. Kwa nini? Sura hii inahusaina na upendo, na mwalimu wao alikuwa amewafundisha kwamba

upendo huwatia moyo watu wengine. Walipokuwa wakimshangilia mwanafunzi mwenzao, wanafunzi hawa walikuwa wanaliweka kwenye mazoezi somo hili la 1 Wakorintho 13. Waalimu wenye ufanisi watawatia moyo wanafunzi wao kufanyia mazoezi kanuni ambazo wanajifunza.

**Liweke Somo katika Mazoezi**

► Wape wanafunzi wako fursa ya kufanyia mazoezi yale wanayojifunza. Kama unawafundisha wachungaji wako vijana, wape nafasi ya kuhubiri, kutembelea wagonjwa, au kushirikisha injili kwa mtu asiyeamini. Baada ya kumaliza, fanya tathmini ya huduma yao, toa maoni yako ya kuboresha vizuri zaidi, na watie moyo kwa kuangalia maeneo ambayo wamefanya vizuri.

**Yesu, Mwalimu Mkuu, alikuwa mwepesi wa kubadilika.**

Fikiria kuhusu maeneo na mazingira mbalimbali ambayo Yesu aliyatumia wakati wa kufundishia:

- Ufukweni mwa bahari (Luka 5)
- Wakati wa mawimbi (Luka 8:22-25)
- Kwa kuruhusu mwanafunzi apambane (Mathayo 14:25-33)
- Wakati somo lake lilipoingiliwa na wageni (Mathayo 12:46-50)
- Wakati wa kutembelea sinagogi (Mathayo 24)
- Wakati mtu aliporarua bati la darasa lake (Luka 5:18-26)

Fikiria "wanafunzi" ambao walirudi nyumbani baada ya muujiza katika Luka 5:18-26. Kamwe hawakusahau somo walilojifunza kuhusiana na uwezo wa Yesu. Luka anaandika kwamba, "Ushangao ukawashika wote, wakamtukuza Mungu; wakajaa hofu, wakisema, Leo tumeona mambo ya ajabu."[126]

Yesu alikuwa mwepesi wa kubadilika kwa ukamilifu katika kujua kwamba mwalimu mkuu hutafuta nyakati za kufanya mafunzo wakati wanafunzi wakiwa wako tayari kujifunza. Luka anatoa mfano wa kanuni hii. "Ikawa alipokuwa mahali fulani akiomba, alipokwisha, mmoja katika wanafunzi wake alimwambia, Bwana, tufundishe sisi kusali."[127] Yesu aliutumia muda huu kufundisha kuhusu maombi.

Sabrina, msichana wa miaka minane aliingia kwenye somo lake la kupiga piano akaanza kulia, "Paka wangu amekufa leo asubuhi!" Sabrina hakuwa na nia ya kujifunza kucheza mizani au mbinu za piano. Hata hivyo, nilipomkabidhi kipande cha wimbo uitwao "Paka wangu nimpendaye," Sabrina aliamua, "Nataka nijifunze huu wimbo kwa kumbukumbu ya paka wangu!"

[126] Luka 5:26
[127] Luka 11:1

Kama waalimu, ni lazima tuwasikilize wanafunzi wetu na tuwe na majibu ya mazingira yao. Kama Yesu Mwalimu Mkuu, ni lazima tuwe wepesi kubadilika katika kufundisha kwetu. Ni lazima tuwe tayari kurekebisha somo ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wetu.

**Liweke Somo katika Mazoezi**

► Je, wewe ni mwepesi wa kubadilika katika kufundisha kwako? Panga angalao njia mbili za kufundisha somo. Kama una kawaida ya kutoa hotuba, panga somo ambalo halitakuwa na hotuba. Kama una kawaida ya kutumia vyombo vya umeme au teknolojia nyingne, panga somo ambalo halitatumia nguvu ya umeme. Kama unafundisha darasani, panga somo la nje na uhusishe mazingira ya asili kwenye somo lako.

**Yesu, Mwalimu Mkuu, aliwasiliana kwa Ubunifu.**

Yesu hakukaa chini na kusema, “Leo tutasoma ukurasa wa 212 kutoka kwenye kitabu chetu. Petro, unasoma aya ya kwanza kwa ajili yetu.” Badala yake, Yesu alitafuta njia mpya za kuwasiliana kwa ubunifu.

► Soma mifano hii ya ubunifu wa Yesu katika ufundishaji.

- *Luka 6:39-42.* Fikiria juu ya kisa cha kipofu kumwongoza kipofu mwingine. Fikiria kuhusu mtu mwenye kibanzi jichoni mwake akijaribu kuondoa boriti lililo ndani ya jicho la mtu mwingine.
- *Lukea 18:18-30.* Je, inawezekana kutumia utajiri wa dunia ili kuurithi uzima wa milele? Fikiria ni kwa jinsi gani ngamia anaweza kupita kwenye tundu la sindano!
- *Luka 9:46-48.* Yesu alimtumia mtoto mdogo kama somo linalohusiana na kuishi kwa unyenyekevu
- *Luka 15:1-7*. Ni kwa jinsi gani Mungu hushughulika na nafsi ya mwenye dhambi aliyepotea anaporejea tena nyumbani? Yesu aliwaweka wakulima kwenye kuthaminiwa na Mungu kama vile kondoo aonekanavyo wa thamani kwa wakulima.
- *Luka 15:11-32*. Kuwafundisha watu katika jamii inayoheshimika ambayo mamlaka yote yako chini ya baba, Yesu alisimulia mfano ambao baba aliwashangaza watu wote waliokuwa wanamwangalia kwa kumkimbilia na kumpokea mwanaye ambaye alikuwa amemwasi.

Mara chache sana Yesu alijibu swali kwa njia ya moja kwa moja. Badala yake, alijibu kwa kutoa kisa, au kwa kutumia swali lingine. Katika Luka 10, mwana-sheria alimwuliza Yesu, “Mwalimu, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?” Yesu alimjibu kwa kutumia kisa cha Msamaria mwema.[128]

[128] Luka 10:25-37

Yesu alijua jinsi ya kuuliza maswali magumu. Mara chache sana aliuliza maswali ambayo yangeruhusu majibu mepesi ya "Ndiyo" au "Hapana." Badala yake, aliuliza maswali ambayo yalimlazimisha anayeulizwa kufungua macho yake kwenye mambo mengine mapya yanayowezekana.

► Soma mifano hii:

- *Luka 7:36-50*. Mtu mmoja katika Mafarisayo aliyemshutumu, Yesu alimwuliza, "Unampenda nani zaidi, aliyesamehewa kabisa au aliyesamehewa kidogo?"
- *Marko 8:36*. Akifundisha kuhusu uanafunzi, Yesu aliuliza, "Kwa kuwa itamfaidia mtu nini kuupata ulimwengu wote, akipata hasara ya nafsi yake?"
- *Luka 6:46*. Kwa wale waliokataa kutii, Yesu aliuliza, "Na kwa nini mnaniita, Bwana, Bwana, walakini hamyatendi nisemayo?"

Hakuna swali hata moja katika haya linaloruhusu jibu jepesi. Kila moja linatufanya tufikirie kwa kina kuhusu ufundishaji wa Yesu.

Kuna njia mbili ambazo waalimu hushindwa kutumia maswali inavyopaswa:

1. Tunauliza maswali ambayo ni mepesi sana. Tunaweka maswali ya "Ndiyo" au "Hapana." Kama tunataka wanafunzi wetu wafikiri kwa kina, tunatakiwa tuulize maswali ambayo yataenda mbali zaidi ya majibu ya vitabuni.
2. Hatusubiri kwa muda mrefu wa kutosha ili kupewajibu. Watafiti wanasemakwamba waalimu wengi wanasubiri chini ya sekunde kabla hajjachana na wanafunzi mmoja kwenda kwa mwingine kwa ajili ya kupewa jibu. Inachukua takribani sekunde tatu kwa mwanafunzi kuweza kulielewa swali na kisha kuanza kutengeneza jibu. Kuongeza kiwango chako cha kutumia maswali, siku zote hesabu hadi saba kabla hujaachana na mwanafunzi mmoja kwenda kwa mwingine.

**Liweke Somo katika Mazoezi**

► Je, wewe ni mbunifu katika kufundisha kwako? Andaa somo kutoka katika Wagalatia 6:7-8. Andaa maswali ambayo yatasaidia wanafunzi kufikiri kwa kina kuhusiana na kanuni ya kupanda na kuvuna. Baada ya kuwa umeshaandaa masomo yako, angalia kwenye tanbihi chini ya ukurasa kwa maswali ya nyongeza ambayo unaweza ukauliza.[129]

---

[129] Maswali kuhusiana na kanuni ya kupanda na kuvuna katika Wagalatia 6:7-8:
+ Kuna mifano gani kutoka katika mazingira ya asili au kijamii yanayoelezea kanuni ya kupanda na kuvuna?
+ Kuna aina gani ya watu katika Biblia wanaotumika kuelezea kanuni hii?
+ Je, unajua mfano wowote wa binafsi unaohusiana na kanuni hii?
+ Je, katika maisha yako ya binafsi, unapanda mbegu ambazo hutaki kuvuna?

**Angalia kwa Karibu: Kufasiri mafumbo.**

Mafumbo yalikuwa ni moja ya aina za kufundishia alizokuwa amezipenda sana Yesu. Wakati fulani mtu mmoja alifafanua fumbo kama "hadithi ya kidunia iliyosheheni somo la mbinguni." Mafumbo ya Yesu yalitumia mipangilio ya kawaida ya vijijini kama (wakulima, wachungaji wa wanyama na kondoo), watu waliozoeleka kama (Wasamaria, wachungaji, watoza ushuru, na Mafarisayo), na mazingirira ya kawaida kama (kondoo aliyepotea, fedha iliyopotea, na mtoto mpotevu) ili kuunganisha shauku na moyo wa kutaka kujua wa wanafunzi wake.

Kozi ya Shepherds Global Classroom inayohusiana na Kanuni za Kuitafsiri Biblia inahusisha na kipengele kinachohusu kutafsiri mafumbo. Huu hapa ni muhtasari wa kanuni zinazofundishwa kwenye kozi hiyo. Tunapojifunza kuhusu fumbo, tunapaswa tuulize:

**(1) Ni swali gani au mazingira gani yaliyoshawishi kuwepo kwa hili fumbo?**

Fumbo la Msamaria Mwema linajibu swali lililoulizwa na mwana-sheria, "Jirani yangu ni nani?" Maelezo ya Yesu anajibu, "Mtu yeyote aliye mhitaji katika njia yangu ni jirani yangu na wajibu wangu."[130]

Yesu alielezea fumbo la mtoto mpotevu kwa viongozi wa dini ambao walimnung'unikia kwa kuwa na mahusiano na wenye dhambi. "Basi watoza ushuru wote na wenye dhambi walikuwa wakimkaribia wamsikilize. Mafarisayo na waandishi wakanung'unika, wakisema, Mtu huyu huwakaribisha wenye dhambi, tena hula nao." Ndipo ilipobidi awaeleze fumbo hili."[131]

- Mchungaji alipoteza kondoo. Alifurahia alipokuwa amempata tena kondoo wake!
- Mwanamke alipoteza shilingi yake. Alifurahia alipokuwa ameipata tena shilingi yake!
- Baba alimpoteza mtoto wake. Alifurahia mtoto wake aliporudi tena!

Yesu alimaanisha kwamba, "Hupaswi kushtuka unaponiona ninakula na wenye dhambi. Mbinguni hufurahia wakati mwenye dhambi mmoja akitubu!"

Kama fasiri yetu haina majibu ya swali au hailengi katika mazingira ambayo yalisababisha kuwepo msukumo wa maelezo ya Yesu, tutakuwa tumekosa kipengele muhimu cha fumbo.

**(2) Ni nini msingi mkuu (au misingi) katika fumbo?**

Mara nyingi fumbo litakuwa na msingi mkuu mmoja kwa kila mhusika mkuu katika kisa kinachozungumziwa. Msingi mkuu wa fumbo utahusishwa moja kwa moja na swali au mazingira yaliyosababisha kuwepo na msukumo wa fumbo hilo. Masomo mengine hutokana na wahusika waliotumiwa katika kisa husika.

---

[130] Luka 10:36-37
[131] Luka 15:1-3

Kisa cha mwana mpotevu kinahusisha wahusika watatu wakuu. Tayari tumeshaona kwamba msingi mkuu wa kisa ni furaha kuu mbinguni kwa mwenye dhambi mmoja anayetubu. Somo hili linajibu mazingira yaliyosababisha kuwepo na msukumo wa kisa hiki kutoka kwa Yesu. Kila mhusika katika fumbo hili anaweza kufundisha masomo yanayohusiana na msingi mkuu wa ujumbe ulioko katika kisa hicho. Baba anafundisha upendo wa ajabu wa Baba yetu wa mbinguni. Mtoto mpotevu kwa pamoja anafundisha gharama ya dhambi na uwezekano wa kutubu tena. Kaka mkubwa anatuonya kwamba tunaweza tukakosa fadhila za upendo wa Baba hata pale tunapoonekana kuwa ni "mtoto mzuri."

### (3) Maelezo gani ya kitamaduni ni muhimu katika fumbo?

Mara nyingi mafumbo ya Yesu yalikwenda kinyume na kanuni za utamaduni wake. Hii ndiyo iliyofanya mafumbo yake yawe ya kukumbukwa: Baba anakimbia kwenda kumlaki mtoto aliyeasi; Msamaria ni shujaa; mjane asiyekuwa na chochote anamshinda jaji mwenye nguvu. Kwa jinsi tutakavyokuwa tunaelewa vizuri muundo wa kitamaduni katika fumbo, ni kwa jinsi hiyo hiyo tutaelewa vizuri ujumbe wa Yesu.

## Matumizi: Sheria Saba za Mwalimu

Dr. Howard Hendricks[132] alifundisha katika Seminari ya Theolojia ya Dallas kwa zaidi ya miaka sitini. Wakati wa kazi yake, alifundisha zaidi ya wanafunzi 10,000. Mojawapo ya kitabu chake kilichokuwa na ushawishi sana ni kitabu kidogo kinachoelezea kwa muhtasari "sheria saba za mwalimu." Sheria hizi zinajitegemeza kwenye aina ya ufundishaji wa Yesu. Jinsi utakavyokuwa anazitumia kanuni hizi, utakuwa mwalimu mwenye ufanisi zaidi.

### Sheria ya Mwalimu.

*Sheria ya Mwalimu*: Kama utasimamisha kukua leo, utasimamisha kufundisha kesho.

Dr. Hendricks aliuliza, "Je, ungependa kunywa maji kutoka katika bwawa lenye maji yaliyochina au kwenye maji yanayotiririka kutoka katika kijito? Maji safi yanayotiririka kutoka katika kijito ni mazuri kuliko maji yaliyotuama mahali pamoja na yasiyofaa kwa ajili ya kuchacha.

Baadhi ya waalimu wanaenda mbali hata zaidi ya miaka bila ya kusoma kitabu kipya kinachohusiana na somo lake au bila ya kupata mawazo mapya. Ufundishaji wao unakuwa kama bwawa lililoachwa, limetuama mahali pamoja tu, na maji yamechina. Kama waalimu, tunapaswa kukua katika eneo letu la ualimu kama ambavyo wachungaji wanavyotafuta kujifunza bila kukoma ili kuinua upeo mpya katika Neno la Mungu.

---

[132] Taarifa inayotumiwa kuandikia maandiko haya imenukuliwa kutoka kwa Howard Hendricks, *Teaching to Change Lives* (Colorado Springs: Multnomah Books, 1987).

**Liweke Somo katika Mazoezi**

► Fikiria kwamba mwanafunzi anakuuliza, "Mwalimu, Umejifunza nini kutoka kwenye Biblia kwenye siku za karibuni? Je, jibu lako litatokana na wiki hili, mwezi huu, mwaka huu au muda mefu uliopita? Je, unakua kila siku katika ufahamu wako wa Neno la Mungu?

**Sheria ya Elimu**

*Sheria ya Elimu*: Jinsi watu wanavyojifunza ni kipimo chako cha jinsi unavyofundisha.

> "Jaribio la msingi la kufundisha siyo kile unachofanya au ni kwa jinsi gani unafanya vizuri, bali ni kwa namna na jinsi gani mwanafunzi atafanya vizuri."
> - Dr. Howard Hendricks

Yesu aliwafundisha wachungaji wa kondoo kwa kuwaelezea visa vinavyohusiana na kondoo; aliwafundisha wavuvi wa samaki kwa kuzungumzia kuhusu "uvuvi wa watu"; aliwafundisha wale wanawake pale kisimani kwa kuzungumzia kuhusu maji. Yesu alijua kwamba mwalimu mwenye ufanisi anajiambatisha na mahitaji ya kila mwanafunzi.

Dr. Hendricks analinganisha kufundisha na kazi ya kocha wa mpira. Kocha siyo mchezaji katika mchezo wa mpira. Kocha huleta msisimko na kutoa maelekezo kwa wachezaji. Kwa njia hiyo hiyo, mwalimu mzuri hafanyi kazi zote kupitia mafundisho ya hotuba. Mwalimu mzuri humhamasisha kila mwanafunzi kujifunza katika njia ambayo ni ya ufanisi kwa yule mwanafunzi.

Morris alikuwa mwanafunzi atika darasa langu a Biblia. Ninategemea wanafunzi wangu wawe waangalifu kuandika yale yanayofundishwa kwa ajiliya kujiandaa kwa mtihani. Morris hakutaka kuandika kwa ajili ya kumbukumbu yale niliyokuwa ninayasema. Badala yake, wakati nikiwa natoa hotuba ya somo, yeye anachora picha kwenye daftari lake. Kama mwalimu, nilikuwa na mashaka kwamba Morris alikuwa hanisikilizi. Mara kadhaa, nilisema, "Morris, tafadhali usichore picha. Andika kile ninachofundisha." Alijaribu kufanya kile nilichomwelekeza, lakini Morris akawa amechanganyikiwa sana.

Kisha nikakumbuka Sheria ya Elimu ya Dr. Hndrics. Nikasema, "Morris, acha tufanye jaribio. Unaweza kuchora *kama* utanionyesha kwamba unakumbuka yale niliyokuwa nafundisha darasani. Jaribio lilifanikiwa. Morris alikuwa anajifunza kwa kubadilisha maneno kwenye mfumo wa picha. Nikajifunza kubadilisha mategemeo yangu kwa sababu "jinsi watu wanavyojifunza ni kipimo cha namna unavyofundisha."

**Liweke Somo katika Mazoezi**

► Je, unaye mwanafunzi ambaye ana njia yake ya kujifunza tofauti na wanafunzi wengine katika darasa lako? Unafanya nini kumsaidia huyu mwanafunzi aweze kujifunza kwa ufanisi zaidi?

**Sheria ya kushughulika**

*Sheria ya kushughulika*: Kuwajibikia kwa kiwango cha juu kunaleta kujifunza kwa kiwango cha juu.

> "Ninasikia… na ninasahau.
> Ninaona…na ninakumbuka.
> Ninafanya… na ninaelewa."
> - Mithali ya Kichina

Yesu alielewa kwamba wanafunzi wake ni lazima wafanye mazoezi katika yale aliyokuwa akiwafundisha. Aliwatuma kwenda katika safari za huduma; aliwafanya waweze ugawa mikate na samaki kwa umati wa watu; aliwapeleka jangwani kuomba; aliwapa fursa ya kuyafanyia kazi yale waliyojifunza. Matokeo yake yalikuwa nini? Mitume walijulikana kama watu "walioupindua ulimwengu chini."[133]

Wanasaikolojia wanasema kwamba tunakumbuka chini ya asilimia 10% vile tunavyovisikia, tunakumbuka chini ya asilimia 50% ya vile *tunavyoona na kusikia*, lakini tunakumbuka kwa zaidi ya asilimia 90% ya vile tunavyoona, *kusikia na kufanya.* Kuhusika kikamilifu kunaongeza kwa kiasi kikubwa kujifunza.

**Liweke Somo katika Mazoezi**

► Unapojiandaa kwa somo lako lijalo, andaa shughuli ambayo itawaruhusu wanafunzi wako kufanyia kazi kanuni uliyofundisha.

**Sheria ya Mawasiliano**

*Sheria ya Mawasiliano*: Kufundisha kwa ukweli, ni lazima tujenge madaraja na mwanafunzi.

Kama waalimu na wachungaji, tuko kwenye biashara ya mawasiliano. Kazi yetu ni kubwa kuliko kutoa taarifa; kazi yetu ni kuwasilisha ukweli kwa wasikilizaji wetu. Wetu. "Mawasiliano" ni neno linatokana na neno la Kiyunani, *communis,* likimaanisha "kawaida." Mawasiliano yanahitaji kupata msingi wa kawaida. Mawasiliano yanahitaji kujenga daraja kwa ajili ya wasikilizaji wetu.

Yesu alitoa mfano wa kujenga madaraja kwa ajili ya wasikilizaji. Kulikuwa na vizuizi kati ya Yesu na mwanamke Msamaria: vya ubaguzi wa rangi, dini na vikwazo vya kijamii. Yesu alikuwa Myahudi; yeye alikuwa Msamaria. Yesu alikuwa mwanaume; yeye alikuwa mwanamke. Yesu alikuwa mwalimu aliyeheshimika; yeye alikuwa mwanamke wa maadili ya zamani ya uasherati. Yesu angewezaje kujenga daraja kupitia vizuizi hivi? Alitafuta kigezo cha kufanana; wote walisikia kiu. Hitaji la kimwili lilijenga daraja la kufikia badiliko la maisha.[134]

Dr. Hendricks aliandika kwamba mawasiliano ni lazima yahusishe ngazi tatu:

---

[133] Matendo 17:6
[134] Yohana 4:1-42

1. *Maarifa* – Kitu ninachokijua. Hii ni hatua rahisi ya mawasiliano.
2. *Shauku* – Kitu ninachokuwa na hisia nacho. Hii ni hatua ya kiwango cha juu zaidi ya mawasiliano.
3. *Kitendo* – Kitu ninachokifanya. Kiwango hiki cha mawasiliano kinaleta mabadiliko kwa wanafunzi wetu.

Nilisikiliza wakati mtawala mmoja wa seminari moja katika Afrika alipokuwa akiwakilisha maono yake kwa mfadhili mmoja tajiri. Alimwomba yule mfadhili fedha za zaidi kuliko nilivyoweza kufikiria! Kwa mshangao wangu, mfadhili alitoa kwa ukarimu. Kwa nini? Mtawala wa seminari aliwasiliana naye katika njia tatu:

1. *Maarifa* - Alijua hitaji la mafunzo ya seminari katika Afrika.
2. *Shauku* – Alikuwa ameshikwa na hisia kali kuhusiana na mafunzo ya viongozi wa kanisa katika Afrika.
3. *Kitendo* – Ametumia muda wa maisha yake yote katika Afrika na ametoa dhabihu nyingi kwa ajili kufundisha viongozi wa kanisa. Yule mtawala aliwasilisha kile alichokuwa anakifanya katika Afrika.

Ili kufundisha kwa ukamilifu, ni lazima tuwe na shauku katika somo letu. Tafakari mazungumzo haya katika madarasa mengi ya Shule za Jumapili:

> Mwalimu: "Leo tutajifnza kuhusukuhusu kulishwa chakula kwa watu 5000 katika Yohana 6."
>
> Mwanafunzi: "Nina swali. Biblia inasema kwamba walihesabu wanaume tu. Kwa nini?"
>
> Mwalimu: "Sielewi. Hilo siyo muhimu. Wewe zingatia kwenye somo tu."

Ghafla, hadithi ya kusisimua sana katika Biblia unakuta inachosha. Wanfunzi *wangependa* kujua ni kwa jinsi gani Yesu aliweza kulisha chakula watu 20,000 kwa mikate michache na samaki. Tunawezaje kuifanya hiyo ikawa ya kuchosha? Huyu mwalimu hawasilishi maarifa; hajajifunza historia na kuelewa ni kwa nini waandishi wa Kiyahudi walihesabu wanaume tu. Mwalimu hajisikii kuwa na shauku ya somo hili. Kuna uwezekano mdogo kwamba maisha ya mwalimu huyu yamebadilishwa na somo hili katika njia ambayo ingemruhusu na yeye aweze kubadilisha maisha ya wanafunzi.

**Liweke Somo katika Mazoezi**

► Unapokuwa unaanda somo, fikiri kuhusu umbali ulioko kutoka ulimwengu wako na ulimwengu wa wanafunzi wako. Chukua muda kujenga daraja kwa ajili ya wanafunzi wako. Tafuta njia ya kuunganisha somo na mahitaji ya wanafunzi wako.

### Sheria ya Moyo

*Sheria ya Moyo*: Ufanisi wa kufundisha ni zaidi ya kichwa – kwenda - kichwa; ni moyo – kwenda - moyo.

Wakati Yesu alipomaliza Hotuba ya Mlimani, "Makutano walishangaa mno kwa mafundisho yake; kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi wao."[135] Mafundisho ya Yesu yalitoka ndani ya moyo wake na yakagusa mioyo ya wasikilizaji wake.

Kwa kurudiarudia, Vitabu vya Injili vinaelezea kuhusu huruma ya Yesu. Watu waliguswa na huruma yake. Moyo wake uligusa mioyo yao. Howard Hendricks anaonyesha vipengele vya kufundisha kwa ufanisi.

***Tabia* ya mwalimu inahamasisha mwanafunzi kujiamini.**

Kama mwanafunzi anaamini tabia ya mwalimu, huwa na kujiamini katika kile anachofundishwa. Kama wachungaji na waalimu, hatutakiwi kabisa kuuharibu uaminifu huo. Kiti kigumu kuliko vyote ni kuujenga upya uaminifu.. Viongozi wa Kikristo wenye hekima hujitenga na jambo lolote ambalo linaweza kupelekea kushindwa katika uadilifu au maadili. Tabia yako ni lazima ihamasishe kujiamini ndani ya wanafunzi wako.

***Huruma* ya mwalimu huzalisha motisha ndani ya mwanafunzi.**

Mwanafunzi anapojisikia kuwa na huruma ya mwalimu, anakuwa na motisha wa kujifunza. Wanafunzi walimfuata Yesu kwa sababu walijua anawapenda. Kama huwezi kuwapenda wanafunzi wako, watakuwa na motisha mdogo sana wa kujifunza kutoka kwako.

Akiongea na waalimu wanaohusika na watoto wadogo, Dr. Hendricks anasema, "Kama Dorini ana viatu vipya, unapaswa uvitambue viatu vyake vipya, vinginevyo hatasikiliza kabisa somo lako jipya!" Baada ya kuonyesha kuvutiwa na mwanafunzi (kwa sababu ya upendo), wako tayari kusikiliza somo unalofundisha

***Maudhui* ya mwalimu huleta kuelewana na mwanafunzi. .**

Ni baada tu ya mwanafunzi kuwa na motisha wa kujifunza ndipo utakapokuwa tayari kufundisha kuhusu maudhui. Baada ya kuwa umepata matumaini yao, unaweza kuzungumza kutoka ndani ya moyo wako kwenda kwa moyo wa mwanafunzi wako.

### Liweke Somo katika Mazoezi

► Je, unawapenda wanafunzi wako? Kwa umuhimu wake, je, **wanajua** kwamba unawapenda? Unawezaje kuunganisha kwa njia iliyo bora zaidi moyo wako na mioyo ya wanafunzi Mungu anaowaleta kwako?

---

[135] Mathayo 7:28-29

**Sheria ya Kutia Moyo**

*Sheria ya Kutia Moyo*: Kufundisha kunakuwa na ufanisi mkubwa wakati mwanafunzi anapokuwa amehamasika vya kutosha.

Wanaposikia neno "hamasa," waalimu wengi hufikiria kuhusu pipi, vyeti, kupewa wadhifa au njia nyingine za kuhamasisha wanafunzi. Hivi ni vitu vya nje tu au "visivyokuwa na maana" vya kuhamasisha. Vinatoka nje ya mwanafunzi. Wahamasishaji wanaotumia vitu vya nje hutumia zawadi ("kariri aya 100, na tutakupa kikombe") na utakuwa na hatia ("kama hutakariri aya za Biblia, wewe siyo Mkristo mzuri"). Waalimu wengi wanategemea kabisa kwenye uhamasishaji wa vitu vya nje visivyokuwa na maana.

Uhamasishaji wa vitu vya nje visivyokuwa na maana unaweza kufanya kazi kwa kitambo kidogo, lakini matokeo yake ni ya muda tu. Kama mwanafunzi atafanya kukariri aya za Biblia kwa ajili ya kupata cheti tu, siku moja ataacha kukua katika hamasa hiyo. Cheti hakitakuwa tena kivutio cha maana cha kuhamasisha kufanya kazi kwa bidii. Kama mwanafunzi atakuwa akikariri aya ili asionekane na makosa, hiyo hali kwa hakika itapoteza nguvu yake. Wataamua kwamba, "Nafikiri ninaweza kuwa Mkristo bila ya kufanya hii kazi ya ziada!"

Uhamasishaji wa ndani ni wa kina zaidi. Unatoka ndani ya mwanafunzi. Dr. Hendricks anaorodhesha hapa mambo yanayohusiana na uhamasishaji wa ndani:

- *Umiliki*. "Hili ni kanisa langu. Ili kusaidia liweze kukua, nitaalika wageni."
- *Hitaji*. "Ninahitaji Neno la Mungu kushinda majaribu, kwa hiyo nitakariri maandiko."
- *Uthibitisho*. "Ninampenda mwalimu wangu na ninataka nimfurahishe. Kwa hiyo nitajifunza somo lake."

Mambo haya ya uhamasishaji yanadumu kwa muda mrefu kuliko pipi au nyadhifa.. Kwa jinsi tutakavyokuwa tunatumia nyenzo hizi za uhamasishaji, tunawatia moyo wanafunzi wetu waendelea kujifunza kwa muda mrefu zaidi.

**Liweke Somo katika Mazoezi**

► Andaa orodha ya mambo ya uhamasishaji unayotumia kwa wanafunzi wako. Yapi ni ya nje, na yapi ni ya ndani?

**Sheria ya Utayari**

*Sheria ya Utayari*: Kufundisha huwa ni kwa ufanisi zaidi wakati mwanafunzi na mwalimu kwa pamoja wamejiandaa vya kutosha.

Je, hili linaonekana kama ni somo la kawaida la Shule ya Jumapili kwenye kanisa lako?

> Mwalimu: "Leo tutajifunza kutoka katika Waefeso 5. Tafadhali fungueni Biblia zenu."
>
> Wanafunzi wanafikiria: "Kwa nini tujifunze kutoka katika Waefeso 5?

Mwalimu anatumia saa moja nzima akifundisha Waefeso 5. Ni mwalimu mzuri. Baada ya saa moj y a kufundisha, wanafunzi wanahamasika na ujumbe wa Paulo. Somo linamalizika, na wanafunzi wanaondoka kwenda nyumbani. Wiki moja baadaye, tukasikia tena haya:

> Mwalimu: "Leo, tutajifunza kutoka katika Waefeso 6. Tafadhali fungueni Biblia zenu."
>
> Wanafunzi wanafikiri: "Kwa nini tunapaswa kujifunza kutoka katika Waefeso 6?"

Ni kwa kiasi gani ingekuwa vizuri kama wanafunzi wangejifunza kutoka katika Waefeso 6 kabla ya darasa kuanza! Je. somo halingekuwa kumilifu zaidi kama wanafunzi wangekuja darasani na lundo la maswali? Hakika! Utawezaj kukamilisha hili? Profesa Hendricks anashauri utoaji wa kazi za kufanya ili kuwaandaa wanafunzi kwa ajili ya somo. Kwa mfano:

- Toa kazi za kufanya ambazo zitawafanya wanafunzi waafikiri kuhusu somo hilo watakaloenda kujifunza wiki ijayo. "Kabla ya Jumapili, soma Matendo 19 ili kujifunza jinsi Paulo alivyoanzisha kanisa katika Efeso."
- Toa kazi zinazotoa msingi wa nyuma wa somo. Kabla ya Jumapili, soma kutoka katika kamusi ya Bibilia kuhusiana na sinagogi la Atemi kataka Efeso. Hi itasaidai kuelezea msisitizo wa Paulo kuhusiana na vita vya kiroho katika Waefeso 6:10-20."
- Toa kazi ambazo zitainua uwezo wa mwanafunzi wa kujifunza akiwa mwenyewe. Soma Waefeso 6 mara moja kila siku kwa wiki hii yote. Utakapokuwa unasoma, andika swalimja utakaloliona kutokana na ibara hii. Jumapili ijayo, tutayajadili maswali yenu."

### Liweke Somo katika Mazoezi

► Kwenye darasa lifuatalo utakalofundisha, wape wanafunzi kazi ya kufanya ili kuwaandaa kwa ajili ya somo linalofuata. Hakikisha kazi hiyo inawaanda wanafunzi kwa ajili ya ufahamu bora zaidi wa somo watakalojifunza.

## Hitimisho: Umuhimu wa Tabia ya Mwalimu.

Yesu alijua kwamba "kila mmoja atakapokuwa amefundishika na kufuzu kikamilifu hulingana na mwalimu wake."[136] Wanafunzi wake wanadhihirisha kanuni hii. Kwa kuwa alikuwa amefundishwa kwa mfano wa upendo mkamilifu, Yohana aitwaye "Mwana wa Radi" alikuja kuwa Yohana "Mtume wa Upendo." Kwa kuwa alikuwa amefundishika kwa mfano wa imani, "Thomaso aliyekuwa mtu wa mashaka" alikuja kuwa "Thomaso, Mtume

[136] Luka 6:40

katika India." Wakati wakiwa wamefundishika kwa ukamilifu, mitume walimfanania mwalimu wao.

Hatua ya kwanza kwa mwalimu ni *kufanana na jinsi ambavyo unataka wanafunzi wako waje wakawe.* Yesu hangeweza kumgeuza Petro kuwa "Mwamba" kama yeye hangekuwa mfano wa utulivu. Tunapaswa tuwe kama tunavyotaka wanafunzi wetu waje wakawe.

Paulo aliielewa kanuni hii. Aliwaambia Wakorintho, "Mnifuate mimi kama mimi ninavyomfuata Kristo."[137] Hii ni kanuni ya ujasiri sana. Paulo anaelezea, "Kama unataka kuishi aina ya maisha yaliyo sahihi, mniige mimi." Kwa kuwa Paulo alikuwa anamfuata Kristo, ilikuwa ni salama zaidi kwa Wakorintho kumfuata Paulo.

Kama wanafunzi watafanana na mimi, ni lazima nijiulize, "Je, ninaonyesha sifa na tabia chafu ambazo zitakuwa ni aibu kwangu kama wanafunzi wangu wataziiga? Kama ninawajibu wanafunzi wangu kwa hasira na kukosa uvumilivu, sitashangaa kama wanafunzi wangu "baada ya kuwa wamemaliza mafunzo kwa ukamilifu" wataonyesha hasira na kukosa uvumilivu kwa watu wengine.

Tabia ni muhimu sana kwamwalimu. Huwezi ukakuza viwango vya tabia za wanafunzi wako ambavyo wewe hukuonyesha mfano wake katika maisha yako. Ni muhimu zaidi kabisa kwamba mwalimu aonyeshe tabia ya kimungu kuliko aonyeshe uwezo wake mkubwa wa elimu. Ni lazima tutake kuwa kama vile tunavyotaka wanafunzi wetu wawe.

### Liweke Somo katika Mazoezi

► Tunapofikia mwisho wa somo hili kuhusiana na kufundisha kama Yesu, omba Mungu akuonyeshe kama unazo sifa na tabia mbovu ambazo hungetaka wanafunzi wako waziige. Mwombe Mungu akupe neema ya kufanya mabadiliko yanayohitajika ili kwamba wakati wanafunzi wako "watakapokuwa tayari wamekamilika kwa mafunzo," ukaone tabia za kimungu zikionekana katika maisha yao.

## Kazi za kufanya Somo la 4

Kazi za kufanya kwa ajili ya somo hili zimefanyika moja kwa moja kwenye mfululizo wa somo hili katika maeneo yote. Kama utakuwa umemaliza kila kazi iliyoonyeshwa katika mfululizo wa somo hili, hakuna tena kazi za ziada za kufanya kwa ajili ya Somo la 4.

[137] 1 Wakorintho 11:1

# Somo la 5
# Kuhubiri kama Yesu

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi atapaswa:
(1) Kutambua sifa ambazo zilimfanya Yesu akawa mhubiri mwenye ufanisi.
(2) Kukubaliana na utendaji wa Roho Mtakatifu katika kuhubiri kwa ufanisi
(3) Kujitoa kwa upendo kama mchungaji wa kondoo.
(4) Kuandaa somo la mahubiri ambalo linafuata mfano wa Yesu kwa ajili ya kuhubiri.

## Kanuni ya Huduma

Kuhubiri kwa ufanisi siyo matokeo ya jitihada za mwanadamu peke yake; kuhubiri kwa ufanisi kunawezeshwa na Roho Mtakatifu.

## Utangulizi

Sikiliza majibu ya umati wa watu uliokusanyika kwa ajili ya mafundisho ya Yesu.

- "Ikawa, Yesu alipoyamaliza maneno hayo, makutano walishangaa mno kwa mafundisho yake."[138]
- "Mkutano wote walishangaa kwa mafundisho yake."[139]
- "Na mkutano mkubwa walikuwa wakimsikiliza kwa furaha."[140] Mahubiri ya Yesu yalikuwa na nguvu sana.

Maelfu walikusanyika kumsikiliza alipokuwa akihubiri. Kwa hakika, aina yake ya kuhubiri inapaswa iwe mfano kwa ajili yetu sisi wa leo. Kumbuka kwamba, Yesu alipokuwa angali duniani alihudumu akiwa katika ubinadamu wake. Usifikirie kwamba, "Bila shaka yesu alikuwa mhubiri mwenye nguvu; alikuwa Mungu." Badala yake, fikiri kwamba, "Yesu – kama – mwanadamu alihubiri katika njia ambayo iliunganisha nguvu na mamlaka. Kuhubiri kwake kuliwavutia makutano wengi kwenye ukweli. Ni kitu gani ninachoweza kujifunza kutoka kwa Yesu kitakachoweza kunifanya mimi niwe mhubiri mwenye ufanisi zaidi wa injili?"

► Fikiria kwamba uliishi kwenye miaka ya 30 B.K. na ulimsikia Yesu akihubiri. Ni nini unachotegemea kukiona na kusikia?

---

[138] Mathayo 7:28
[139] Marko 11:18
[140] Marko 12:37

## Yasu Alihubiri kwa Mamlaka

► Soma 2 Wakorintho 4:1-6.

Wakati Yesu alipohubiri Kaperinaumu, makutano walishangaa mno kwa mafundisho yake, kwa kuwa neno lake lilikuwa na mamlaka."[141] Baada ya hotuba ya mlimani, "makutano walishangaa mno kwa mafundisho yake; kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi wao."[142] Waandishi walinukuu kutoka kwa rabi wengine ili kusaidia nadharia zao, lakini Yesu alihubiri kwa mamlaka.

Kama wachungaji, tunapaswa tuhubiri kwa mamlaka. Mamlaka yetu ni tofauti na mamlaka ya Yesu. Mamlaka yake yalikuwa yanatoka ndani ya asili yake mwenyewe; mamlaka yetu sisi tumepewa kama wawakilishi wa Yesu Kristo; mamlaka yetu yanatokana na ujumbe tunaouhubiri.

### Tunahubiri kwa Mamlaka kama Wawakilishi wa Yesu Kristo

Yesu akawaambia, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Katika aya iliyofuata anawaagiza wafuasi wake, "Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi…Na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."[143] Tunayo mamlaka kwa sababu tumepewa maagizo kama wawakilishi wa Yesu.

Mwaka 1783, wawakilishi wa Marekani na wawakilishi wa Mfalme George wa III walikutana kuweka saini kwenye Mkataba wa Paris wa kumaliza Vita vya Mapinduzi vya Marekani. Mfalme George wa III hakusafiri kwenda Paris kusaini mkataba huo. George Washington hakuusaini mkataba huo. Wawakilishi kutoka katika kila nchi walikuwa na mamlaka ya kuusaini makataba huo kwa mamlaka ya wakuu wa nchi zao.

Kwa hali hiyo hiyo, tunahubiri kama wawakilishi wa Yesu Kristo. Paulo anaandika, "Kwa maana hatujihubiri wenyewe, bali Kristo Yesu ya kuwa ni Bwana; na sisi wenyewe kuwa tu watumishi wenu kwa ajili ya Yesu."[144] Mamlaka ya Paulo hayakuwa ya kwake mwenyewe. Alikuwa "mtumishi," lakini alikuwa mwakilishi wa "Yesu Kristo kama Bwana."

### Tunahubiri kwa Mamlaka kwa sababu ya Ujumbe Tuliopewa

Mamlaka yetu yanatokana na Maandiko tunayohubiri. Paulo aliandika, "Lakini tumekataa mambo ya aibu yaliyositirika, wala hatuenendi kwa hila, wala kulichanganya neno la Mungu na uongo; bali kwa kuidhihirisha iliyo kweli twajionyesha kuwa na haki, dhamiri za

---

[141] Luka 4:32
[142] Mathayo 7:28
[143] Mathayo 28:18-20
[144] 2 Wakorintho 4:5

watu zikitushuhudia mbele za Mungu."[145] Paulo anakataa kufanya jambo lolote la hila au kitu chochote ambacho kitadhoofisha ujumbe wake unaohusiana na Neno la Mungu.

Marekani, wachungaji wengi wameachana na kutegemea mamlaka ya Maandiko. Baadhi yao wamechukua mafunzo yao kutoka katika vyuo vikuu vya wanazuoni wenye uwezo mzuri, lakini kwa sasa hawahubiri tena kwa mamlaka. Badala yake, wamejawa na mashaka. Kwa nini? Wana mashaka na uhalali wa mamlaka ya Biblia; wanategemea hakima za mwanadamu peke yake. Kama watumishi wa Mungu, mamlaka yetu ni lazima itokane na Neno la Mungu.

Wakati fulani nilisikia mchungaji wa mawazo mapya akilezea kisa cha Yesu cha kutembea juu ya maji.[146] Marko anasema kwamba wanafunzi walipigwa na mashangao! Huyu mchungaji hakuwa na imani kwamba Yesu alitembea juu ya maji. Alisema kwamba Yesu alikuwa anatembea kwenye maji machache kando kando ya ufukwe wa bahari.

Mchungaji alisema, "Marko 6 siyo kisa cha muujiza; ni kisa cha kusisimua tu kinachoonyesha jinsi mitume walivyokuwa wamevutiwa na Yesu." Baada ya ibada, nikamsikia mtu mmoja akisema, "Kwa nini watu walishangazwa? Yesu alitembea tu ufukweni mwa bahari! Hilo siyo jambo la kushangaza."

Mchungaji huyu hakuiamini Biblia yake; hakuwa na tegemeo au tumaini na mamlaka ya Maandiko. Hakuna sababu ya kuhubiri Neno la Mungu kama huamini ujumbe wake uliopo. Tunaweza tu kuhubiri kwa mamlaka tunapoamini ujumbe uliopo katika Neno la Mungu.

Kuelewa kwamba mamlaka yetu yanatokana na Yesu na katika ujumbe wa Neno la Mungu tunalohubiri kunatusaidia sisi kuepukana na hatari mbili za wachungaji.

**(1) Hatari ya kwanza ni kiburi** kinachosema kwamba, "Mimi ni mchungaji. Mimi ndiye kiongozi. Hakuna mtu anayeweza kunihoji."

Kiburi hiki kinawaondoa watu kutoka kwenye ujumbe wa injili. Paulo anasema, "Tunachokihubiri siyo chetu wenyewe, bali kinatokana na Yesu Kristo." Mamlaka yetu yanatoka kwa Yesu na Neno la Mungu.

Ni lazima tuwe na unyenyekevu wa kukiri tunapojikuta tuna makosa. Wakati mmoja mchungaji aliniambia, "Kamwe siliambii kanisa kama nikifanya kosa. Watapoteza matumaini nami katika mamlaka yangu." Huyu mchungaji alijisahau kwamba mamlaka yetu hayatokani na sisi kuwa wakamilifu bila ya kufanya makosa; mamlaka yetu yanatokana na Neno la Mungu. Tunapaswa kuelekeza kutaniko letu kwenye mamlaka ya mwisho ya Neno la Mungu. Maneno yangu siyo muhimu; Maneno ya Mungu ni ya umuhimu wa mwisho.

---

[145] 2 Wakorintho 4:2
[146] Marko 6:45-52

**(2) Hatari ya Pili ni Unyenyekevu wa Uongo** unaosema kwamba, "Mimi ni mchungaji. Sina mamlaka. Mabingwa wa ushauri wanajua zaidi kuhusiana na saikolojia; wanasayansi wanajua zaidi kuhusiana na asili ya dunia; wanasaikolojia wanajua zaidi kuhusiana na matamanio ya mwanadamu ya ngono. Siwezi nikazungumzia kuhusu mahitaji ya mihemuko, uumbaji au maadili kwa sababu mimi siyo mtaalamu mbobezi."

Paulo akasema, "Sisi ni watumishi *lakini* tulio na mamlaka kama wawakilishi wa Yesu Kristo. Kama watumishi, tunapaswa tuishi kwa unyenyekevu. Lakini kama wawakilishi wa Yesu Kristo, tunapaswa tuhubiri kwa ujasiri. Tunatumika kwa mamlaka ya Mfalme wa ulimwengu.

### Hotuba za Yesu zilileta "Habari Njema" kwa Watu wote Wahitaji.

Yesu alizungumzia kuhusu mahitaji ya wasikilizaji wake. Yesu alipokuwa akisafiri kupitia Galilaya "akihubiri injili ya ufalme, alikuwa na huruma kwa umati wa watu "kwa sababu walikuwa wamechoka na kutawanyika."[147] Wayahudi walikuwa kama watumwa kwa Warumi; masikini walikuwa na matumaini haba ya kuondoka na umaskini wao; wakoma walitengwa na jamii; watoza ushuru walikataliwa na jamii. Kwa wote hawa, Yesu alileta matumaini mapya.

Unapokuwa unazungumzia mahitaji ya watu, unakamata mawzo yao. Kama ninaishi jangwani, na wewe ukasema, "Leo nitahubiri kuhusu maji ya uzima," nitakusikiliza kwa makini sana! Kama mimi ni mzee na mdhaifu, na unasema, "Leo nitahubiri kuhusu Mungu anayekupa nguvu kama tai," nitakusikiliza!

Yesu siku zote alikumbuka kwamba "Injili" maana yake ni "habari njema." Alikuja kuleta habari njema kwa wale wote ambao walihitaji matumaini. Kuhubiri kwa ufanisi ni lazima kulete matumaini kwa wasikilizaji wanaoutusikiliza. Kama Yesu, ni lazima tuulize, Ninamhubiria nani? Mahitaji yao ni nini?"

Jaribu kufikiria kana kwamba uko kwenye gari iliyofikwa na ajali na kwamba uko kwenye hatari ya damu kukutoka na kusababisha kifo. Pake hospitalini daktari anakuonyesha chati kamilifu ya rangi yenye takwimu za ajali za magari. Anakueleza historia ya maendeleo ya stetoskopu, (yaani chombo cha kusikilizia mapafu au mapigo ya moyo). Mwishowe, anakuonya kuhusu hatari ya kuendesha gari bila uangalifu.

Kila kitu anachosema daktari ni cha kweli, lakini bado maelezo yake hayajakidhi haja ya kile unachohitaji. Unahitaji mtu wa kukufunga majeraha yako na kukupa dawa ya kuzuia maumivu yako. Kuhubiri kunapaswa kuwe ni zaidi ya kuelezea ukweli; kuhubiri kunahitaji kukutana na mahitaji ya wasikilizaji wetu.

> Wahubiri ni lazima wakune mahali ambapo watu wanahitaji wakunwe.

[147] Mathayo 9:36

Ni rahisi kuona "habari mbaya" za dunia yetu iliyoanguka. Injili inaenda mbali zaidi ya hapo; inaleta matumaini kwa dunia iliyoanguka. Siku zote Yesu alileta matumaini kwa wasikilizaji wake. Yesu kamwe hakulegeza msimamo wako kuhusu ukweli, na kamwe hatupaswi kulegeza msimamo wetu kuhusu ukweli. Lakini Yesu aliijua kweli, akahubiri kwa usahihi, akalete matumaini. Mhubiri wa zamani alisema, "Ni lazima ukune mahali ambapo watu wanhitaji wakunwe." Ni lazima uzungumzie mahitaji ya wale unaojaribu kuwafikia.

## Mahubiri ya Yesu yalikuwa Yanaleta hukumu Ndani ya Mtu

Yesu alianza na mahitaji ya wasikilizaji wake, lakini kusudi lake lilikuwa la ndani zaidi kuliko tu kuweka bendeji ya muda kwenye vidonda vyao. Kuhubiri kwa Yesu kuliweza kuleta hukumu ndani ya dhamira zao na hivyo kuleta mabadiliko ya maisha yao.

Yesu alikuwa hana hofu ya kukabiliana na wasikilizaji wake kwa ujumbe wa hukumu kuhusiana na dhambi zao. Yesu alimwambia yule mwanamke aliyekamatwa kwenye tendo la uzinzi, "Wala mimi sikuhukumu," lakini pia akamwambia, "Enenda zako; wala usitende dhambi tena."[148]

Moja ya maelezo ninayoyapenda sana katika huduma ya Yesu ni kuhusu kisa cha mtu aliyekuwa amepooza katika birika la Bethzatha. Baada ya kumponya, Yesu alisema, "Angalia, umekuwa mzima; usitende dhambi tena, lisije likakupata jambo lililo baya Zaidi."[149] Yesu hakuwa mwoga kukabiliana na dhambi.

Wakati Yesu akihubiri, wasikilizaji wake walihukumiwa ndani yao. Tofauti na wahubiri wengine wa siku hizi, Yesu alihubiri umuhimu wa maisha ya haki. Hakuna mahali popote ambapo Yesu alisema, "Baba yangu hategemei wewe kuzishika amri zake." Badala yake Yesu alisema, "Haki yenu isipozidi hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni."[150] Yesu alihitaji zaidi ya viongozi wa kidini wa wakati wake. Kuhubiri kwa Yesu kulileta kuhukumiwa ndani kwa kila mtu aliyemsikiliza.

## Mahubiri ya Yesu Yalileta Mabadiliko ya Maisha

> "Biblia hakuletwa kwa ajili tu ya sisi kuongeza ujuzi wetu bali kubadilisha maisha yetu."
> - Imenukuliwa kutoka D.L. Moody

Wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe vya Wamarekani, Raisi Abraham Lincoln alihudhuria ibada katika kanisa ambalo lilikuwa linahudumiwa na Dr. Phineas Gurley. Baada ya ibada moja, rafiki mmoja aliuliza, "Unafikiriaje kuhusu mahubiri?" Lincoln akasema, "Yaliwakilishwa vizuri na yameleta mawazo mazuri sana."

[148] Yohana 8:11
[149] Yohana 5:14
[150] Mathayo 5:20

Yule rafiki akamjibu, “Kwa hiyo umeyapenda?” Bwana Lincoln alisita kisha akasema, “Hapana. Ninaamini Mchungaji Gurley leo amepotoka. Rafiki yake alitaharuki. “Kwa nini unasema hivyo?” Lincoln alijibu, “Hakututaka sisi tufanye jambo lolote la muhimu.” Raisi Lincoln aliamini kwamba mahubiri ni lazima yalete wito wa kuwajibika. Aliamini kwamba mahubiri ni lazima yalete mabadiliko ya maisha.

► Soma Mathayo 18.

Yesu alihubiri ili kuleta mabadiliko ya maisha. Mahubiri yake yalikuwa ni ya vitendo. Mathayo 18 ina kumbukumbu za mahubiri ya Yesu kuhusu “Mahusiano katika Ufalme wa Mbinguni.” Yesu anafundisha kuhusu:

- Umuhimu wa unyenyekevu (18:2-6)
- Kujibu kwa majaribu (18:7-9)
- Kujibu kwa waliopotea (18:10-14)
- Kujibu kwa wale wanaokukosea (18:15-20)
- Umuhiu wa kusamehe (18:21-35)

Haya ni masuala ya vitendo ya kila siku. Yesu alizungumzia mahitaji halisi ya wasikilizaji wake. Alihubiri ili kuleta mabadiliko ya maisha.

Kuhusu mwanamume aliyekuwa amezaliwa kipofu Yesu alifanya uponyaji – kasha akampa ujumbe ambao ungebadilisha maisha yake kwa ajili ya maisha ya milele.

> Yesu akasikia kwamba wamemtoa nje; naye alipomwona alisema, Wewe wamwamini Mwana wa Mungu? Naye akajibu akasema, Ni nani, Bwana, nipate kumwamini? Yesu akamwambia, Umemwona, naye anayesema nawe ndiye. Akasema, Naamini, Bwana. Akamsujudia..[151]

Kwa watu waliokuwa na njaa, Yesu alitoa mkate – kisha akahubiri ukweli ambao ungebadilisha maisha yao kwa ajili ya umilele. “Mimi ndimi chakula cha uzima; yeye ajaye kwangu hataona njaa kabisa, naye aniaminiye hataona kiu kamwe.”[152]

Mahubiri yanayoleta mabadiliko yanaleta kwa pamoja ukweli wa Neno la Mungu na mahitaji ya watu. Kuhubiri kwnye ufanisi kunazungumzia ukweli wa Mungu kuhusiana na mahitaji ya watu.

Wakati Yesu alipohubiri, alizungumza na akili, mihemuko na utashi. Yote matatu kwa pamoja yanahusika katika mabadiliko ya kweli.

---

[151] Yohana 9:35-38
[152] Yohana 6:35

**Yesu alizungumza na Akili**

Yohana alitumia istihali "Neno" kumwelezea Yesu. "Neno" lilikuwa ni istihali ya Kiyunani ikiwa na maana ya hekima na ufahamu. Unaposoma mahubiri ya Yesu katika Mathayo 18, utakuwa unasoma mafundisho ya hekima sana kuhusu mahusiano ambayo yalishatolewa kwa wakati wote. Fikiria jamii ambayo watu wake wanachukuliana kwa unyenyekevu. Fikiria jamii ambayo kwayo msamaha ni jambo la kawaida. Yesu alizungumzia hekima kwenye akili za wasikilizaji wake.

**Yesu alizungumza na Mihemuko**

Mara thelathini na nne Injili zinazungumzia kuhusu, "mshangao," "maajabu" na "mfano mzuri," miongoni mwa wasikiizaji wa Yesu. Wanafunzi walipokuwa wakienda Emau, walisema, "Je! Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na kutufunulia maandiko?"[153] Wale waliomsikia Yesu walifurahia kwa maneno yake ya neema, majuto kwa ajili ya dhambi zao, na juu ya hayo yote, matumaini kwa wakati ujao.

**Yesu alisema na Utashi**

Yesu hakuridhishwa kirahisi hivyo kuwa na wasikilizaji; aliwaita wafuasi. Yesu hakuwa anaridhishwa na matokeo ya nje peke yake; aliwataka watu kubadili mioyo yao na maisha yao. Aidha kama alikuwa ni mwanamke Msamaria wa dhambi zilizopita au kijana mdogo tajiri ambaye alikuwa mwangalifu sana kuzishika sheria, Yesu aliwaita wasikilizaji wake kusalimisha kwa hiari utashi wao kwa Mungu. Tunapokuwa tunahubiri kama Yesu, tutakuwa tunawaita wasikilizaji wetu kwenye mfumo mwingine mpya wa maisha.

**Angalia kwa kuzingatia: Je, Unaihubiri Injili?**

Mchungaji mmoja alihubiri kutoka Warumi 1 kuhusiana na dhambi ya ushoga. Lakini jambo moja lilikuwa limekosekana…Jirani karibu nami alikuwa amekaa kijana mmoja aliye na tatizo la kuvutiwa kufanya mapenzi ya jinsia moja. Kijana huyu anajua kwamba ushoga ni dhambi na alikuwa ameanza kuomba kwa ajili ya ukombozi wake. Anajua ukweli kuhusiana na dhambi yake; anahitaji kusikia habari njema (za injili) kwamba Mungu anao uwezo wa kuleta ushindi katika kila jaribu.

Mchungaji akanukuu onyo la Yesu kuhusiana na talaka. Alilaumu sheria zinazoruhusu kirahisi kuwepo na talaka. Alihubiri ukweli. Lakini jambo mojalilikuwa limekosekana…Wiki hiyo, wanandoa wawili na watoto wao wawili walikuwa wamemtembelea mwanasheria anayehusika na mambo ya talaka kwa sababu walishindwa kufikia maridhiano kuhusiana na mgogoro uliokuwa unapelekea ndoa yao kuvunjika.Wanajua kwamba kuachana ni dhambi; wanahitaji kusikia habari njema (za injili) kwamba Yesu ana uwezo wa kuleta uponyaji kwenye ndoa zenye maumivu.

[153] Luka 24:32

Mchungaji mmoja alikuwa anapaaza sauti kwamba, "Kutoa mimba kunaua mtoto asiyekuwa na hatia." Alihubiri ukweli. Lakini jambo moja lilikuwa limekosekana…Katika kusanyiko lake kulikuwa na msichana wa umri wa kati aliyekuwa akilia kila anapokumbuka siku alipojiingiza kwenye kliniki ya kutoa mimba kwa kijana ambaye bado hajaolewa. Miaka ishirini baadaye, bado ana mashaka kama Mungu anaweza kusamehe dhambi yake. Anajua kwamba kutoa mimba ni dhambi; anahitaji kusikia habari njema (za injili) kwamba Mungu anatoa msamaha kwa matendo yake ya dhambi yaliyopita.

Yesu kamwe hakuwahi kuubadili ukweli kwa ajiliya kitu kingine, lakini kamwe hakusahau kuleta matumaini. Alijua kwamba injili inaleta mabadiliko. Kwa kijana aliyekuwa anasumbuliwa na matamanio ya ushoga, Yesu angesema, "Neema yangu yakutosha katika kukupa wewe ushindi dhidi ya jaribu lako." Kwa wanandoa waliokuwa wanakabiliana na tatizo la kuvunjika kwa ndoa yao, Yesu angesema, "Ninaweza kurejesha moyo wa upendo hata kwa yule mwanandoa anayeonekana kwamba upendo kwake umetoweka." Kwa msichana ambaye alimtendea dhambi mtoto wake aliyekuwa bado hajazaliwa, Yesu angesema, "Nitasamehe dhambi ya kutoa mimba sawa na ninavyosamehe dhambi nyingine. Enenda zako lakini usitende dhambi tena."

Injili inahusisha ujumbe wenye hukumu juu ya dhambi. Tunapaswa tuhubiri hukumu kwa mamlaka. Lakini kuhubiri kama Yesu, tunapaswa tusisahau nguvu ya neema yenye kubadilisha maisha. Ni lazimatulete habari njema za neema ya Mungu kwa ulimwengu uliopasuka.

Injili siku zote inahusisha aina mbili za habari njema. Kwanza, Injili inatueleza kile ambacho Mungu amefanya kwa ajili yetu. Inaleta matumaini kwa ulimwengu ulioharibika.

Kisha jambo la pili, injili inatueleza kile ambacho tunaweza kuwa kupitia uwezo wa Roho Mtakatifu. Injili kamwe hatuachi pale tulipokuwa; inatubadilisha tuingie kwenye kina cha ndani cha kutembea na Mungu.

### Mahubiri ya Yesu yalikuwa marahisi na ya Kukumbukwa.

Yesu hakuwachosha watu na ukweli. Alijua jinsi ya kuhubiri kwa njia rahisi na iliyo ya wazi. Mahubiri yake yalikuwa ya kina sana, lakini yalikuwa yanaweza kueleweka na kila msikilizaji. Alizungumzia mambo ya ukweli kwa undani sana, lakini hata watu waliokuwa hawana elimu walikuwa wamejielekeza kwenye yale mambo aliyokuwa akizungumza Yesu, kwa sababu yalikuwa ni ya kuvutia sana.

Lengo la mhubiri mwenye ufanisi siyo kuwavutia wasikilizaji kwa kiwango cha juu cha elimu yake. Lengo la mhubiri linapaswa liwe ni kuwasilisha ujumbe wa Neno la Mungu kwa njia rahisi na yenye nguvu – na kumruhusu Roho Mtakatifu kuwagusa wasikilizaji kwa ukweli wa Neno la Mungu.

Ni kwa jinsi gani Yesu aliyafanya mahubiri yake yawe marahisi na yenye kuvutia?

**Yesu Alisimulia Hadithi**

Watu wute waliosikia mahubiri ya Yesu mara nyingi walisikia maneno haya, "Acheni niwaeleze hadithi." Hadithi zake ziliwahamasisha wasikilizaji wake na zikafungua masikio yao katika kusikiliza ujumbe wake.

Wengi wetutunakuwa na kumbukumbu ya hadthi kuliko tunavyoweza kukumbuka muhtasari wa vipengele vitatu. Hadithi nzuri zinaelezea mahubiri kwa njia ambayo inatusaidia sisi kukumbuka jambo la msingi katika mahubiri. Hadithi yenye nguvu inatoa muhtasari kwa ujumbe ambao mhubiri anatarajia kuwasilisha.

► Jadili hadithi uliyoisikia mara ya mwisho kwenye mahubiri. Je, iliwakilisha kwa ukamilifu ujumbe wa mhubiri? Je, unakumbuka kusudi lililokuwa limekusudiwa katika hadithi hiyo? Je, hayo mahubiri yangeweza kuwa ya ufanisi nay a kukumbukwa bila hadithi hiyo?

**Yesu alitumia Lugha Rahisi**

Mimi ninafudisha darasa la waalimu wa piano. Kama sehemu ya darasa, ninatoa dhana ya kufanya na kumtaka kila mwalimu akafafanue kwa mpiga piano mwanafunzi. Kwa kiwango kile ambacho mwalimu atakakuwa ameelewa dhana ya kufanya, zaidi tu ni kwa kiwango hicho hicho atakachoweza kumwelezea mwanafunzi wake. Mwalimu anayetumia maneno magumu yenye kuchanganya katika kufundisha dhana ya kile kinachotakiwa mara nyingi huwa anaficha upungufu wa uwezo wake mdogo wa ufahamu. Jinsi unavyoelewa jambo kwa uzuri zaidi, ndivyo hivyo unapokuwa na urahisi zaidi wa kuliwakilisha.

Yesu alikuwa anajua jinsi ya kutafsiri ukweli kwenye lugha inayoelewka ya wasikilizaji wake. Alihubiri kwa wakulima kuhusu kupanda mbegu. Alihubiri kwa wachungaji wa kondoo kuhusu kondoo. Alihubiri kwa wavuvi kuhusu uvuaji. Watu wengi waliukataa ujumbe wa Yesu, lakini hakuna hata mmoja aliyechoshwa na mahubiri yake.

Ujumbe wa Yesu uliweza kueleweka wa wavuvi, wakulima, na wanawake wa majumbani. Lakini yaliweza kuwaudhi wasomi, viongozi wa dini, na maafisa wa kisiasa. Mafundisho yake yalizungumza na kila kada ya jamii. Kuwa rahisi haimaanishi kwamba kuna mapungufu. Mahubiri yetu ni lazima yabebe kweli kuu za injili kwa uwazi na kwa urahisi.

**Yesu alitumia Njia ya Kurudiarudia**

Wakati fulani nilimtembelea mchungaji ambaye alikuwa amefadhaishwa sana na kongamano lake. Alisema, "Walipaswa wawe wameshajua hili; nililihubiri miaka miwili iliyopita." Nilimkumbusha kwamba Yesu alihubiri ujumbe huo mara nyingi kabla wanafunzi wake hawajamwelewa.

> Nilimwuliza huyu mchungaji, "Unadhani mahubiri yako ni mazuri kulikoya Yesu?"
>
> "Bila shaka sivyo!"
>
> "Unadhani waumini wa kanisa lako wana hekima kuliko wanafunzi wa Yesu?"

“Hapana!”

“Kwa hiyo itakubidi uwe unarudiarudia hizo kweli kama Yesu alivyofanya.”

Yesu alihubiri mahubiri kwa kurudiarudia kweli zile zile. Mara kwa mar, aliwafundisha wanafunzi wake kifo chake na kufufuka kwake. Alifundisha mara nyingi ujumbe kuhusiana na ufalme. Yesu alijua kwamba kweli zilikuwa muhimu, kwa hiyo alihubiri ujumbe mara nyingi ilivyowezekana kwa umuhimu wake ili ziwafikie wasikilizaji wake.

**Angalia kwa kuzingatia: Je, Wasikilizaji wako wanauelewa Ujumbe wako?**

Soma mahubiri haya:

Увидев народ, Он взошел на гору; и, когда сел, приступили к Нему
ученики Его. И Он, отверзши уста Свои, учил их, говоря:
Блаженны нищие духом, ибо их есть Царство Небесное.
Блаженны плачущие, ибо они утешатся.
Блаженны кроткие, ибо они наследуют землю.
Блаженны алчущие и жаждущие правды, ибо они насытятся.
Блаженны милостивые, ибо они помилованы будут.
Блаженны чистые сердцем, ибо они Бога узрят.
Блаженны миротворцы, ибо они будут наречены сынами Божиими.
Блаженны изгнанные за правду, ибо их есть Царство Небесное.
Блаженны вы, когда будут поносить вас и гнать и всячески
неправедно злословить за Меня.
Радуйтесь и веселитесь, ибо велика ваша награда на небесах: так
гнали [и] пророков, бывших прежде вас.

Hizi ni aya kumi na mbili za mwanzo za Mahubiri ya Yesu Mlimani. Ni mahubiri yenye nguvu sana, lakini kama hutasoma kwa Kirusi, hutapata faida yeyote katika mahubiri haya. Kwa nini? Hayajatfsiriwa katika lugha yako. Inawezekana kuhubiri ukweli bila ya kutafsiri kwa lugha rahisi ambayo inaeleweka kwa wasikilizaji wetu. Ili kuhubiri kama Yesu, ni lazima tuhubiri kwa lugha rahisi na kwa njia ya kukumbuka.

**Mahubiri ya Yesu yalikuwa ya Kweli**

Mafundisho ya Yesu yalikuwa ya kweli. Maisha yake yalifanana na mahubiri yake. Yesu siyo tu kwamba alihubiri kuhusu kuishi maisha ya kimungu yaliyotakaswa; aliyaishi maisha ya kimungu ya kutakaswa. Hakuna hata mtu mmoja ambaye angeweza kumnyooshea Yesu kidole kwamba mahubiri yake yanapingana na maisha yake. Yesu aliishi sawasawa na kile alichokuwa akihubiri.

Fikiria kwamba unataka kujifunza kuendesha gari. Unakutana na waalimu wawili wanaotoa mafunzo ya kuendesha gari. Mwalimu moja kamwe hajawahi kuendesha gari lakini amesoma vitabu vingi kuhusiana na udereva. Mwalimu mwingine anayo kumbukumbu ya usalama wa kuendesha gari kwa miaka mingi. Je, utamchagua mwalimu gani?

Sasa fikiria kwamba unataka kujifunza jinsi ya kuishi maisha ya Kikristo. Unakutana na wachungaji wawili. Mchungaji mmoja naishi maisha ya dhambi, lakini ana mahubiri mazuri. Mchungaji mwingine anaishi maisha ambayo unaona yuko kwenye ushirika wa karibu na Mungu. Je, utachagua kuwa na mchungaji gani?

> "Yesu kamwe hajasema, 'Mtawajua kwa ukubwa wa huduma zao.' Alisema, 'Mtawajua kwa matunda yao' – kwa kutii kwao mapenzi ya Baba."
> - Craig Keener

Mahubiri yetu ni lazima yawe ya kweli. Ni lazima tuyaishi maisha tunayohubiri. Wahubiri wengi wamejikuta kwamba inawezekana wakawa waaminifu bandia kwa muda. Watu wanaweza kudanganywa na mhubiri anayehubiri uaminifu wakati yeye anaiba fedha za matoleo. Wanaweza kupotoshwa na mhubiri ambaye anahubiri kuhusu uadilifu huku wakiwa na uhusiano usio na maadili. Wanaweza kupumbazwa na mchungaji anayehubiri upendo wakati yeye anampiga mke wake. Lakini hatimaye, ukweli utajidhihirisha. Moyo mtupu usio na kitu utasababisha kuwa nanhuduma tupu isiyokuwa na nguvu za kiroho. Mungu anafanya kazi *kupitia sisi* tunapomruhusu afanye kazi *ndani yetu*.

Kamwe usiruhusu uzuri wa kuhubiri ufiche maisha ya dhambi. Ufanisi wa kufundisha unaanza na moyo unaomjua Mungu.

### Matumizi: Mchungaji kama Mchungaji wa KondooThe Pastor as Shepherd

► Soma Marko 6:30-34.

Moja ya sura nzuri ya mchungaji ni ile ya mchungaji wa kondoo. Yesu "akaona mkutano mkuu, akawahurumia; kwa sababu walikuwa kama kondoo wasio na mchungaji; akaanza kuwafundisha mambo mengi." Yesu aliuangalia umati wa watu akaona kondoo waliohitaji kuwa na mchungaji.

► Jaribu kufikiria ni nani waliokuwa kwenye kundi la watu 5,000 katika Marko 6. Tengeneza orodha.

- Je, orodha yako inaorodhesha pamoja na wakusanyaji wa kodi waliokuwa wakiwadanganya watu? Walikuwepo pale. Ilikuwa kazi rahisi kupiga kelele za kuwashutumu hawa watoza ushuru wasiokuwa waaminifu, lakini Yesu aliona kondoo aliyepotea aliyehitaji kuokolewa.
- Je, orodha yako inaorodhesha pamoja na wanasheria wa Kifarisayo waliokuwa wanategemea kumwekea Yesu mtego ili wamkamate? Walikuwepo. Ingewezekana

kuwa rahisi kwa Yesu kuwanyanyasa mbele ya umati wa watu, lakini Yesu aliwaona kondoo wasumbufu waliokuwa wanahitaji kuonyeshwa njia iliyo sahihi.

- Je, orodha yako inaorodhesha pamoja na mume asiyekuwa mwaminifu ambaye moyono mwake anahukumiwa kwa uzinzi wake? Alikuwepo pale. Yesu aliona kondoo aliyepotea anayehitaji kufanyiwa marekebisho na kisha uponyaji.
- Je, orodha yako inaorodhesha pamoja na vijana walioasi nyumbani na kukimbia shule ili kujiunga na umati usiojulikana? Walikuwepo pale. Yesu aliona kondoo waliokuwa wakitangatanga waliohitaji kurudishwa kwenye njia sahihi kabla hawajaendelea kutawanyika zaidi.

Ni nani unayemwona unapokuwa unahubiri? Je, unaona tu makosa ya kusanyiko lako, au unaona mahitaji ya ndani sana ya kondoo wako? Je, unaona tu hasira ya mjumbe wa baraza lako, au unaona jinsi kondoo mtaabishaji anavyowataabisha wengine? Unamwona tu mtu aliyerudi nyuma, au unamwona na kondoo anayetaabika kwa ajili ya dhambi? Yesu aliwaona kondoo wenye uhitaji.

► Soma Yohana 10:1-18.

Kama wachungaji, tumeitwa ili tuwe wachungaji wa kondoo. Ni kwa jinsi gani mchungaji wa kondoo hutumikia kondoo wake? Yohana 10 inatoa mfano.

### Mchungaji wa Kondoo huwaongoza Kondoo

Ukimchunguza mchungaji wa kondoo, hutamwona akiwa na rungu la kuwaongoza kondoo. Badala yake, mchungaji wa kondoo huwatangulia kondoo wake ili kuwapitisha katika njia sahihi. Yesu alisema, "Kondoo humsikia sauti yake; naye huwaita kondoo wake kwa majina yao, na kuwapeleka nje. Naye awatoapo nje kondoo wake wote, huwatangulia; na wale kondoo humfuata, kwa maana waijua sauti yake."[154]

Tunapokuwa tunasoma Vitabu vya Injili, kuna mara nyingi tunategemea Yesu amgonge Petro, Yohana au Thomaso kwa rungu! Mara kwa mara walijikuta wakirudiarudia kwenye matatizo. Lakini badala ya kuwagonga, Yesu alitumia fimbo ya mchungaji kuwainua hawa wanafunzi wadhaifu waliokuwa wakijitahidi na kuwaweka kwenye njia sahihi.

Kama mchungaji wa kondoo, je, unawaongoza kondoo ambao Mungu amewaweka katika kanisa lako au unawaendesha? Je, wewe ni mchungaji **unayeongoza** kondoo au ni meneja **unayeamuru** kondoo kutii?

### Mchungaji wa Kondoo Huwajali Kondoo wake

Je, upo wakati mara nyingine unafikiri, "Ningependa niwe na kazi inayoanzia saa 3 asubuhi hadi saa 11 jioni pamoja na wikiendi bila kazi na kusiwepo na simu baada ya saa

[154] Yohana 10:3-4

11 jioni?” Hili linaweza likaonekana ni zuri sana! Lakini hayo siyo maisha ya mchungaji wa kondoo.

Mchungaji wa kondoo huwajali kondoo wake wanapohitaji msaada, siyo tu “wakati wa saa za ofisi.” Mchungaji wa kondoo hawezi kumwambia kondoo aliyejeruhiwa kwamba, “Ngojea hapo hadi saa 3 kesho asubuhi nitakapoingia kazini.” Mchungaji wa kondoo hutoka hata usiku kwenda kumwokoa mwana kondoo.

Ni kwa njia hiyo hiyo, mchungaji hujali kondoo wake wanapokuwa wanahitaji msaada. Kuwajali kondoo wa kiroho ni zaidiya kuhubiri. Inahusisha kuhubiri, lakini pia ni pamoja na ushauri, kuwatembelea, kuwasikiliza, kuwaombea na mara nyingine kukaa tu na kondoo aliyejeruhiwa.

Ndiyo, wachungaji, lazima ujijali mwenyewe. Huwezi kuwa mchungaji wa kondoo mwenye ufanisi kama utajikinai mwenyewe kimwili, kimhemuko na kiroho. Mara nyingine Yesu aliutumia muda wake akiwa peke yake, na wewe ni lazima uwe na muda wako wa kuwa peke yako. Lakini kulikuwa na nyakati nyingine ambazo Yesu alijua kwamba ni lazima aitoe dhabihu faraja yake kwa ajili ya kuwaangalia kondoo.

Uwiano huu wa huduma na kupumzika unaweza ukawa mgumu. Kama mchungaji na – mchungaji wa kondoo mwenye hekima, unapaswa uwe makini sana kusikia uongozi wa Roho Mtakatifu na ushauri wa hekima kutoka kwa wale wanaokuzunguka. Sikiliza sauti ya Roho Mtakatifu inaposema, “Ni muda wa kwenda kwa mapumziko na kujiboresha upya tena.” Sikiliza sauti ya mke wako au mtumishi mwenzako wanaosema, “Unahitajika ukae nje ya kazi kwa muda.” Rudi kutoka nyakati za kujiboresha kwa upya na shauku mpya ya kutunza kondoo wa Mungu walioaminiwa kwako.

### Mchungaji wa Kondoo Huwalinda Kondoo wake

Yesu alilinganisha mchungaji wa mshahara hukimbia anapoona hali ya hatari na mchungaji mwema huwalinda kondoo wake hata ikibidi iwe ni kuhatarisha uhai wake. Mchungaji wa mshahara “hukimbia kwa kuwa mambo ya kondoo si kitu kwake” lakini mchungaji wa kondoo “huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo.”[155]

Hata kwenye kipindi cha saa zake za mwisho, Yesu aliwachunga wanafunzi wake. Kwenye Chakula cha Mwisho cha jioni, aliwaandaa kwa ajili ya jaribu ambalo si muda mrefu wangekutana nalo. Akiwa Bustanini, aliendelea kumfundisha Petro, Yakobo naYohana. Akiwa msalabani, Alimweka Mariamu mikononi mwa Yohana. Hadi muda wa mwisho, Mchungaji Mwema alikuwa akiwachunga kondoo wake.

Paulo aliwaingiza kaziniwazee wa kanisa la Efeso kuhudumu kama wachungaji wa kondoo. Walitakiwa walichunge kundi la kondoo ambalo limenunuliwa kwa damu ya Yesu. Kwenye

[155] Yohana 10:13, 15

aya ya mwisho, Paulo anaonya kuhusu "mbwa wakali" ambao watawapiga kondoo. Wachungaji wa kondoo wana wajibu wa kulilinda kundi.[156]

Je, kama mchungaji na – mchungaji wa kondoo, unawlinda kondoo wako ambao Mungu amewaweka kwenye kanisalako? Je, unawalinda dhidi ya imani potofu, au kutokana na mashambulizi ya ndoa, au kutokana na mashambulizi ya kiroho? Wewe ni mchungaji wa kondoo au ni mchungaji wa mshahara?

Kabla hujaenda kuhubiri Jumapili ijayo, mwombe Mungu akuonyeshe mahitaji ya kondoo wako. Mwombe Mungu akuonyeshe mioyo iliyovunjika katika kundi lako. Unapokuwa unahubiri, waone kondoo ambao "wamenyanyasika na hawawezi kujisaidia" na ambao wanahitaji upendo wa mchungaji wa kondoo wa kimungu.

**Angalia kwa kuzingatia: "Ole!"**

► Soma Mathayo 23:1-39.

Yesu alitumia neno "Ole wenu" alipokuwa akizungumza kwenye miji iliyokuwa imemkataa[157], kwa Mafarisayo na waandishi ambao waliwapotosha watu[158], na kuhusu Yuda ambaye atamsaliti.[159] Mara nyingine tunazisoma hizi "Ole" kwa sauti ya hasira ambayo inasahau upendo wa Yesu, hata kwa wale ambao wamemkataa yeye.

Kuna hukumu katika neno "ole" lakini pia kuna huzuni. "Ole" inajumuisha kwa pamoja hukumu na "huzuni na huruma" kwa wale wanaohukumiwa. Inaonyesha "huzuni ya Yesu juu ya wale wote wanaoshindwa kutambua ukweli wa taabu ya kweli ya hali zao."[160] "Ole" inaonyesha huzuni kubwa pamoja na onyo.

Yesu alihitimisha tangazo lake la hukumu juu ya viongozi wa kidini kwa kulilia hatima ya jiji alilolipenda. "Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka!" Yesu alilia juu ya jiji ambalo siku siyo nyingi litamsulubisha.[161]

Huu unatakiwa uwe mfano wetu kuhubiri kuhusu hukumu. Kuhubiri kwetu ni lazima kuhusishe maonyo dhidi ya dhambi na ujumbe wa hukumu dhidi ya wale wanaokataa kutubu. Lakini ujumbe wetu ni lazima uonyeshe huzuni dhidi ya dhambi na siyo kupandisha hasira kwa mwenye dhambi.

---

[156] Matendo 20:28-31
[157] Mathayo 11:21
[158] Mathayo 23:13-29
[159] Marko 14:21
[160] Martin H. Manser, *Dictionary of Bible Themes.* (London: Martin Manser, 2009). Ona pia, Joel B. Green and Scot McKnight, *Dictionary of Jesus and the Gospels.* (Westmont, Illinois: InterVarsity Press, 1992).
[161] Mathayo 23:37 na Luka 19:41

Kijana aliyeasi alirejea nyumbani baada ya ujumbe kuhusu jahanamu kuhubiriwa. Baba yake akamwuliza, "Mwanangu, unafikiriaje kuhusiana na ule ujumbe? Kijana akajibu, "Sikuupenda. Ulinifanya nipandishe hasira!" Wiki iliyofuata, kijana akamsikia mhubiri mwingine akihubiri kuhusu kuzimu. Baba yake akamwuliza tena, "Unafikiriaje kuhusiana na ule ujumbe?" Kijana akamjibu, "Ni lazima nimtumikie Yesu. Sitaki kabisa kwenda mahali pa kutisha kama hapo!"

Baba alishangazwa. "Wiki jana, mahubiri kuhusu jahanamu yalikupandisha hasira. Wiki hii, mahubiri kuhusu jahanamu yamekufanya ukatubu. Kuna tofauti gani?" Kijana akajibu, "Mhubiri huyu wa mwisho alitokwa na machozi aliponionya mimi kuhusu jahanamu."

Je, huwa unajisikia kulia tunapohubiri kuhusu hukumu? Je, unajisikia kulia unapokuwa unaandaa mahubiri kuhusu jahanamu? Je, wewe ni mchungaji unayewapenda kondoo wako – hata inapokubidi kuwa ni lazima uwaonye kuhusiana na jahanamu?

### Hitimisho: Wajibu wa Roho Mtakatifu katika Kuhubiri

Kama wahubiri, ni lazima tutegemee uwezo wa Roho Mtakatifu katika kuleta mguso kwa wasikilizaji wetu. Kama tuutatumia mbinu za kibinadamu peke yake ili kuzalisha rufaa za hisia zetu, tunaweza tukapata majibu ya haraka, lakini majibu ya kiroho yatakuwa yamekosekana. Roho Mtakatifu peke yake anaweza kuleta mabadiliko ya kudumu kwa wasikilizaji wetu.

► Soma 1 Wakorintho 2:1-16.

Paulo alielewa kwamba mabadiliko ya kiroho hupatikana peke yake kupitia uwezo wa Roho Mtakatifu. Baada ya kuondoka Athene alipokuwa akijadiliana na wana falsafa huko Areopago, alirejea Korintho.[162] "Akiwa Korintho, aliamua asitumie "ufasaha wa maneno au hekima yake" bali "naliazimu nisijue neno lo lote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulibiwa." Alihubiri "kwa dalili za Roho na za nguvu."[163]

Paulo alijua kwamba Roho hufasiri "Mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni."[164] Paulo alithamini elimu; alikuwa mwanazuoni wa kiwango kikubwa. Alielewa mahubiri ya viwanjani yenye ufanisi; alijifunza kutoka kwa Wagiriki kuhutubu kwa ufasaha. Alijua jinsi ya kujenga hoja yenye maana; Warumi ni bora sana katika muundo wa mantiki. Lakini juu ya hayo, Paulo alithamini uwezo wa Roho Mtakatifu. Alijua kwamba kusadiki kwa ukweli kunapatikana tu kupitia kazi ya Roho Mtakatifu.

Paulo aliwakumbusha Wakorintho kwamba, "tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu."[165] Chombo cha kubebea siyo

---

[162] Matendo 17:16-18:1
[163] 1 Wakorintho 2:1-5
[164] 1 Wakorintho 2:13
[165] 2 Wakorintho 4:7

hazina! Sisi kama viongozi wa huduma ni vyungu vilivyopasuka, vilivyotengenezwa kwa udongo. Lakini tunayo fursa nzuri ya ajabu sana ya kubeba hazina, ambayo ni injili, kwa wale tunaowahudumia.

Hili ni angalizo la nguvu sana kwa viongozi wa huduma. Ni rahisi kuangalia kwenye "jagi" badala ya "hazina" iliyoko kwenye jagi. Tunaweza kujikuta tunachukua umakini zaidi katika muonekano wetu kuliko ujumbe; tunaweza kujikuta tunachukua umakini zaidi kwenye jagi kuliko hazina iliyomo ndani yake. Paulo anatukumbusha kwamba Mungu kwa makusudi anatumia jagi za udongo kudhihirisha kwamba "uwezo ni wa Mungu na siyo wetu." Hatupaswi kuingilia njia ya Mungu ya uwezo wake. Hatupaswi kuuchukua utukufu ambao ni wa Mungu peke yake. Ni lazima tuhubiri tukiwa ndani ya uwezo wa Roho Mtakatifu.

**Kazi za kufanya Somo la 5**

(1) Injili ya Mathayo inajumuisha mahubiri makuu matano. Soma kila andiko la mahubiri na ainisha tabia moja katika kila andiko la mahubiri hayo inayofanya yawe ya ufanisi. Katika kazi hii, hakuna majibu ya ndio au hapana. Jiulize, "Ni kwa jinsi gani Yesu ananisaidia kusadiki, kunitia moyo, au kunisaidia kukumbuka na kuyafanyia kazi yanayotokana na ujumbe wake?"

| Mahubiri | Tabia |
|---|---|
| Mahubiri ya Mlimani (Mathayo 5-7) | |
| Kuwatuma wanafunzi (Mathayo 10) | |
| Mifano ya ufalme (Mathayo 13) | |
| Maisha kwenye ufalme (Mathayo 18) | |
| Mhadhara (Mathayo 24-25) | |

(2) Unapokuwa unaandaa mahubiri yako yanayofuata, rejea tabia ulizozikuta ndani ya mahubiri ya Yesu. Tumia mahubiri yake kama mfano wa kuwasilisha ujumbe wako kwa ufanisi. Shirikisha andiko hili la mahubiri kwa wengine ulioko nao darasani. Fanya tathmini ya mahubiri yako na swali hili, "Je, nilipangilia mahubiri yangu kuambatana na mfano wa Yesu?"

# Somo la 6
# Yesu na Ufalme wa Mungu

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi atapaswa:

(1) Aelewe maana ya ufalme wa Mungu katika Vitabu vya Injili.

(2) Kutambua kwa pamoja vipengele vya wakati huu na wakati ujao vya ufalme wa Mungu.

(3) Kufuata kanuni za Yesu za maisha katika ufalme kutokana na Mahubiri ya Mlimani.

(4) Kufasiri kwa ukamilifu mifano ya Yesu kuhusiana na ufalme.

(5) Kujikabidhi kwenye masharti ya Yesu kuhusiana na uanafunzi.

## Kanuni ya Huduma

Sisi tunahudumu kama mabalozi wanaouwakilisha Ufalme wa Mungu katika ulimwengu wetu.

## Utangulizi

Ufalme wa Mungu ndiyo dhamira kuu ya msingi katika Agano Jipya. [166] Neno "ufalme" linaonekana mara hamsini na nne katika Mathayo, mara kumi na nne katika Marko, mara thelathini na tisa katika Luka na mara tano katika Yohana. [167]

Karibia nusu ya mifano ya Yesu inafundisha kuhusu ufalme wa Mungu. Anahubiri kuhusu ufalme. Anaponya na kutoa mapepo kudhihirisha uwezo wa ufalme. Baada ya kupaa, kanisa la mwanzo liliendelea kuhubiri ujumbe wa ufalme.[168]

---

[166] Vianzo vilivyotumika katika sura hii ni pamoja na:
+ D. Matthew Allen, "The Kingdom in Matthew." (1999). Kinapatikana kutoka https://bible.org/article/kingdom-matthew March 22, 2021.
+ Darrell L. Bock, *Luke*: *Baker Exegetical Commentary on the New Testament*. (Grand Rapids: Baker Books, 1994-1996)
+ J. Dwight Pentecost, *The Words and Works of Jesus Christ.* (Grand Rapids: Zondervan, 1981)
+ Martyn Lloyd-Jones, *Studies in the Sermon on the Mount.* (Grand Rapids: Eerdmans, 1959)

[167] Mathayo kwa kawaida alirejea "ufalme wa mbinguni," Luka alirejea kama "ufalme wa Mungu." Wasikilizaji wa kwanza wa Mathayo walikuwa Wayahudi; Wayahudi walikwepa kutumia
Jina la Mungu na mara nyingi wakitumia "mbinguni" kama tasifida ya Mungu. Inaonekana kwamba Mathayo alibadili "Ufalme wa Mungu" kuwa "Ufalme wa Mbinguni" kwa namna nyingi. Katika somo hili, nitatumia "Ufalme wa Mungu" isipokuwa pale ninapokuwa nanukuu kwa Mathayo.

[168] Matendo 8:12; 28:23

Katika somo hili, tutajifunza kuhusu ufalme wa Mungu katika huduma ya Yesu na matokeo ya ufalme katika huduma leo. Mwisho wa somo hili, nimeweka mahubiri yaliyohubiriwa Nigeria kuhusu ufalme wa Mungu. Mahubiri haya yanaonyesha jinsi ujumbe wa ufalme ulivyo na matokeo kwenye huduma katika dunia yetu.

## Ufalme wa Mungu

Kuna maswali mawili yanayotambulisha fundisho hili kuhusu ufalme wa Mungu.[169]

1. Je, Ufalme wa Mungu ni nini?
2. Je, Ni lini ufalme wa Mungu utaanzishwa?

### Je, Ufalme wa Mungu ni nini?

► Soma Matendo 1:1-8.

Siku arobaini baada ya kufufuka, Yesu alikuwa na wanafunzi wake "akizungumzia juu ya ufalme wa Mungu." Muda mfupi kabla ya kupaa, wanafunzi wake walimwuliza, "Je! Bwana, wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme?" Wanafunzi walitegemea yafuatayo:

1. *Ufalme wa haraka*: "wakati huu." Walitegemea Yesu angeanzisha ufalme kwa haraka.

2. *Ufalme wa kisiasa na kijiografia*: "unapowarudishia." Walitegemea kwamba Yesu angeuangusha utawala wa Rumi na kuwarudishia mamlaka ya kisiasa ya Israeli.

3. *Ufalme wa Kitaifa* : "ufalme wa Israeli." Walitegemea Yesu angetawala taifa lao kama ufalme wa wakati wa Daudi kwenye Agano la Kale.[170]

Yesu alijibu," Si kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba aliyoyaweka katika mamlaka yake mwenyewe. Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi."

Jibu la Yesu lilionyesha yafuatayo kuhusu ufalme wake:

1. *Ufalme usio na wakati*: "nyakati wala majira Baba aliyoyaweka." Ufalme wa Yesu siyo wa kutegemea nyakati wala majira ya kibinadamu bali wakati wa Baba.

2. *Ufalme usiokuwa wa ulimwengu huu*: "nguvu, Roho Mtakatifu akiisha kuwajilia juu yenu." Ufalme wa Yesu ulijengwa kwenye msingi wa uwezo wa Roho Mtakatifu, na siyo kwenye mamlaka ya kisiasa.

---

[169] Kwa ajili ya hotuba za kupitia video kuhusiana na Ufalme wa Mungu, unaweza ukaangalia Scot McKnight, "What and Where is the Kingdom of God?" katika http://www.seedbed.com/where-is-the-kingdom-of-god/ (Iliyopatikana Marchi 22, 2021.)

[170] John Stott, *The Message of Acts* (Westmont, Illinois: InterVarsity Press, 1990), 41

3. *Ufalme wa ulimwwengu wote*: "hata mwisho wa nchi." Ufalme wa Yesu uliwafikia mataifa yote. Haukuwa maalumu kwa ajili ya Iraeli tu.

Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba hawahitaji kujua mambo ya nyakati wala majira. Badala yake, wanapaswa wawajibike na mambo mawili: kupokea Roho Mtakatifu na kuwa mashahidi wake "hata mwisho wa nchi."

**Ufalme wa Mungu utaanzishwa lini?**

> "Ufalme ulishakuja;
> Ufalme unakuja;
> Ufalme bado haujaja."
> - Martyn Lloyd-Jones

Miongoni mwa wanazuoni wa theolojia, kuna mitazamo mitatu ya msingi kuhusiana na ufalme wa Mungu.

***Ufalme wa Mungu Utakuja.***

Baadhi ya wanazuoni wa theolojia wanauona ufalme wa mwisho ukianzishwa na Yesu atakapokuja kuitawala dunia wakati wa miaka elfu moja. Waandishi hawa huangalia maandiko kama Mathayo 24-25 penye msisitizo wa vipengele vya kisiasa na mipaka vya ufalme.

***Ufalme Ulishakuja.***

Wanazuoni wengine wa theolojia wanafundisha kwamba ufalme wa Yesu ulianzishwa wakati akiwa bado hapa duniani. Wanaweka msisitizo wa maandiko kama ile kauli ya Yesu kwamba "ufalme wa mbinguni umekaribia" na "ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia."[171] Mtizamo huu wa ufalme unazingatia asili ya kiroho ya ufalme na utawala wa Mungu ndani ya mioyo ya waumini.

***Ufalme tayari ulishakuja, lakini bado haujatambulishwa kikamilifu.***

Wanazuoni wa theolojia wengi wanasema kwamba ufalme unahusisha kwa pamoja vipengele vya wakati uliopo na ujao. Mtizamo huu unafundisha kwamba ufalme wa Mungu ulizinduliwa wakati wa huduma ya Yesu hapa duniani; unaendelea kuenea kupitia kazi ya kanisa; utatambulishwa kwa utimilifu wakati Yesu atakaporudi duniani kuja kutawala.[172] Wakati wa kuja kwa Yesu, "Hapo ndipo mwisho, atakapompa Mungu Baba ufalme wake; atakapobatilisha utawala wote, na mamlaka yote, na nguvu."[173] Huu ndio utimilifu wa ufalme wa Mungu.

► Katika mitazamo hii mitatu wewe unashikilia mtazamo upi? Je, kuna matokeo gani ya kivitendo kwenye huduma kutoka katika kila mtazamo?

---

[171] Mathayo 4:17 na Luka 11:20

[172] Watoa maoni hutumia maneno "kuzinduliwa kwa ufalme" wakimaanisha kuanza kwa ufalme wakati wa huduma ya Yesu hapa duniani. "Utimilifu wa ufalme" ni ukamilishwaji wa mwisho wa ahadi za ufalme wakati wa kuja tena kwa Yesu Kristo duniani.

[173] 1 Wakorintho 15:24

Katika somo hili, tutaona vipengele vya ufalme ambavyo tayari vinaonekana na vipengele ambavyo bado vimebakia kutimizwa. Ufalme unahusisha mambo yafuatayo:

- **Mfalme**: Kuanzia kwa Mamajusi wakati wa kuzaliwa kwake hadi kubandikwa kwa tangazo la "Mfalme wa Wayahudi" juu ya msalaba, Yesu alikuja kama mfalme.
- **Mamlaka**: Yesu alidhihirisha mamlaka yake kupitia miujiza yake na ushindi dhidi ya kaburi.
- **Sheria**: Yesu alitoa muhtasari wa sheria za ufalme kwenye Hotuba ya Mlimani.
- **Eneo la nchi**: Yesu alifundisha kwamba ufalme wake umeenea hadi miisho yote ya nchi za dunia ikiwa ni pamoja na lugha zote na watu wote.
- **Watu**: Watu wote waliokombolewa na Mfalme na wanatawaliwa na yeye ni raia wa ufalme wa Yesu

### Ahadi ya Ufalme

► Soma Mathayo 3:1-12.

Marejeo ya kwanza ya ufalme wa Mungu katika Agano Jipya yanapatikana katika mahubiri ya Yohana Mbatizaji. Akiwa ninabii wa mwisho wa katika Manabii wa Kale wa Agano, Yohana alishutumu unafiki wa viongozi wa dini ya Kiyahudi. Akiwa mjumbe wa kwanza wa Agano Jipya, aliandaa njia kwa ajili ya ujio wa mfalme mpya. "Tubuni, kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia."[174] Neno "umekaribia" linaashiria kwamba ufalmeunakaribia kwa haraka. Haujafika bado, lakini uko karibu sana. Yohana alihubiri kuwaandaa Wana wa Israeli katika ujio wa Masihi ambaye ataongoza katika ufalme mpya.

Kitambo kidogo baada ya Yohana kukamatwa, Yesu alianza huduma yake ya hadharani. Alisafiri kupitia Galilaya "akitangaza injili ya ufalme." Kama ilivykuwa kwa Yohana Mbatizaji, Yesu naye alitangaza, "Tubuni, kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia."[175]

► Soma Mathayo 10:5-42.

Yesu aliwatuma wanafunzi kumi na mbili kuhubiri ujumbe wa ufalme kwa "kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli." Kama ilivyokuwa kwa Yohana Mbatizaji na Yesu, walihubiri wakisema, "Ufalme wa mbinguni umekaribia."[176]

Huduma ya wanafunzi ilikuwa imekaa katika mpangilio sawa na huduma ya Bwana wao. Kama Yesu, walikuwa watangaze kuhusu ufalme na wahudumie mahitaji ya kimwili ya watu. Kama Yesu, waliponya wagonjwa na kutoa mapepo kama ishara kwamba ufalme wa

[174] Mathayo 3:2
[175] Mathayo 4:17
[176] Mathayo 10:5-7

Mungu sasa umeingia kusambaratisha kwenye mamlaka za Shetani. Yesu aliwatuma wawakilishi wake, "Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo."[177]

## Kuzinduliwa kwa Ufalme

► Soma Mathayo 12:22-32.

Ahadi ya ufalme haikuwa mpya. Manabii wa Agano la Kale walikuwa wametabiri kuhusu ujio wa ufalme wa baadaye. Hata hivyo, Yesu alitangaza kwamba ufalme haukuwa tu kwa ajili ya matumaini ya baadaye, lakini ni ukweli wa mara moja. Yesu alitangaza kuzinduliwa kwa ufalmewa Mungu. Ufalme wa Mungu ulikuwepo mahali popote ambapo Yesu alikuwa yupo.

Akiwa na uwezo dhidi ya mapepo, Yesu alidhirisha mamlaka ya mfalme ambaye ameushinda ufalme wa Shetani. Baada ya kumponya mtu aliyekuwa amegandamizwa na pepo, Mafarisayo walidai kwamba Yesu "anatoa pepo" kwa nguvu za "Beelzebuli, mkuu wa pepo." Yesu alijibu kwamba alikuwa anaushinda ufalme wa Shetani kupitia nguvu za Mungu: "Mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia."[178] Yesu alikuwa amevamia ufalme wa Shetani.

► Soma Mathayo 11:1-24.

Miujiza ya Yesu ilikuwa ni ishara ya uzinduzi wa ufalme wake.Injili ya Yohana inatumia neno "ishara" kwa ajili ya miujiza ya Yesu. Miujiza ilikuwa ni ishara ya utambulisho wa Yesu na ushahidi wa ufalme mpya.

Yohana Mbatizaji alitangaza kwamba "ufalme wa mbinguni umekaribia." Alikuwa ametegemea ufalme wa kisiasa utakaoleta ukombozi kwa Israeli.. Badala yake, Yohana akajikuta yuko gerezani akikabiliwa na kifo!. Aliwatuma wanafunzi wake kuuliza, "Wewe ndiwe yule ajaye, au tumtazamie mwingine?" Huduma ya Yesu haikuendana na mategemeo ya Yohana Mbatizaji ya Masihi wa kisiasa ambaye angeanzisha ufalme wa kidunia.

Yesu alimjibu kwa kuelezea kazi zake kama Masihi.

> Nendeni mkamweleze Yohana mnayoyasikia na kuyaona; Vipofu wanapata kuona, viwete wanakwenda, wenye ukoma wanatakaswa, viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa, na maskini wanahubiriwa habari njema. Naye heri awaye yote asiyechukizwa nami.

Yesu alimfundisha Yohana kuwa mtu wa subira kwa ajili ya mpango wa Mungu unaoonekana.

---

[177] Mathayo 10:8
[178] Mathayo 12:24, 28

Ingawaje Yesu alimpongeza Yohana kwa nguvu na ujasiri, alitangaza kwamba "aliye mdogo katika ufalme wa mbinguni ni mkuu" kuliko Yohana. Kwa nini? Yesu alikuwa amekuja kuanzisha agano jipya pamoja na mafao yote yaliyoko kwenye ufalme. Mwamini wa mwisho wa Agano Jipya ana faida kubwa kuliko mtakatifu maarufu sana wa Agano la Kale ambayo hakuwahi kuipata. Waamini wa Agani Jipya wameshuhudia utimilifu wa utabiri wa Agano la Kale. Ufalme uliokuwa umetabiriwa umeshazinduliwa.

## Maisha katika Ufalme: Hotuba ya Mlimani

Mahubiri marefu ya wakati mmoja yaliyokwisha rekodiwa katika Vitabu vya Injili ni Hotuba ya Yesu Mlimani. Ufalme wa Mungu ndio dhamira kuu iliyoko katika mahubiri haya. Hii inaonekana kwa njia mbalimbali:

- Hali ya heri ya kwanza inafundisha kwamba ufalme wa Mbinguni ni "kwa walio maskini wa roho. Hali ya heri ya mwisho inafundisha kwamba ufalme wa Mbinguni ni kwa ajili ya wale "wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki." Heri hizi mbili zinaifunga bahasha yenye hali zote za Heri zikionyesha kwamba msingi mkuu wa dhamira ya Hali za Heri ni ufalme wa Mbinguni.
- Yesu anadai mamlaka ya kufasiri sheria.[179] Hiki ni kitendo cha mfalme ambaye ana mamlaka ya kufasiri na kutumia sheria za ufalme wake.
- Yesu aliwafundisha wanafunzi wake jinsi ya kuomba, "Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni."[180] Tumeitwa kuomba kwa ajili ya kuendelea kwa ufalme wa Mungu hapa duniani. Watu wa Mungu wanapoishi sawasawa na Hotuba ya Mlimani, ufalme unapanuka na mamlaka ya Mungu yanapanuka kwenda kwa raia wapya wa ufalme.
- Mwisho wa mahubiri yake, Yesu alifundisha kwamba "matendo mema" peke yake hayatoshi kwa mtu "kuingia kwenye ufalme wa mbinguni." Ni wale tu "wafanyayo mapenzi ya Baba yangu" ndio watakaoingia kwenye ufalme huo.

### Kanuni za Kusoma Mahubiri ya Mlimani

Inatupasa tukumbuke kanuni tatu jinsi tunavyoendelea kusoma Mahubiri ya Mlimani.

### (1) Kutii maamrisho ya Hotuba ya Mlimani hakuleti kupewa "uraia" kwenye ufalme wa mbinguni.

Hatupaswi kufikiri, "Ishi kwa njia hii na utakuwa Mkristo." Badala yake, tunapaswa tuisome hii Hotuba ya Mlimani kama mwongozo wa maisha kama raia wa ufalme: Ishi kwa njia hii kwa sababu wewe ni Mkristo." Tumeokolewa kwa neema peke yake; kasha, kama raia wa ufalme wa Mungu, tunatii maagizo yake.

---

[179] Mathayo 5:21-48
[180] Mathayo 6:9-13

**(2) Hotuba ya Mlimani ni kwa Wanafunzi tu na siyo kwa watu wasioamini.**

Hii siyo katiba ya nchi ya kidunia. Usishangae wakati majirani zako ambao hawajaamini wakikataa kuishi sawasawa na kanuni hizi! Huu ni ufafanuziwa maisha katika ufalme wa Mungu, na siyo maisha katika falme za mwanadamu.

**(3) Hotuba ya Mlimani ni kwa ajili ya kila Mwamini.**

Watu wengi wamejitahidi kuepuka kuendana na madai yaliyopo kwenye haya Mahubiri wakidai kwamba kanuni hizi hazifai kwa waamini wa kawaida. Wengine wamesema, "Sheria hizi ni za baadaye kwa ajili ya ule ufalme ujao wa miaka elfu moja. Wengine wamesema, "Hizi sheria ziko kwa ajili ya watakatifu wachache. Wakristo wengi hawana uwezo wa kuzifuata hizi sheria. Wengine wamesema, "Mahubiri haya yanaashiria kwamba kamwe hatuwezi tukazitimiza sheria za Mungu. Tunapojikuta kwamba kamwe hatuwezi tukazitimiza sheria za Mungu, tutategemea neema ya Mungu peke yake."

Hata hivyo, kanisa la mwanzo liliyasoma Mahubiri haya kama mwongozo kwa kila mwamini. Barua za Yakobo na 1 Petro zina marejeo mengi ya sheria zinazotokana na haya Mahubiri. Yesu alikataa kudhoofisha hadhi ya kiwango cha utakatifu wa Mungu. Badala ya hadhi ya kiwango cha chini kuliko Mafarisayo, Yesu aliwaweka wafuasi wake kwenye hadhi ya kiwango *cha juu*: "Haki yenu isipozidi hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni."[181]

**Maisha kwenye Ufalme wa Mungu**

► Soma Mathayo 5-7.

Kama Ysu alizindua ufalme wakati wahuduma yake hapa duniani, sasa tunaishi kweye ufalme wa Mungu. Hotuba ya Mlimani inafafanua tabia za raia wa ufalme wa mbinguni. Hapa kuna mtazamo mfupi wa dhamira ya haya Mahubiri.

**(1) Maadili ya ufalme wa Mungu ni kinyume kabisa na maadili ya ulimwengu huu.**

Hakuna mtawala katika ulimwengu huu anayesema kuwa maskini ni kubarikiwa, kuomboleza, kusalimisha haki zetu, au kuteswa. Haki ya Heri zinaelezea kinyume kabisa cha maadili ya Utawala wa Rumi wakati wa Yesu, na ulimwengu wetu wa leo. Ufalme wa Mungu ni tofauti na ufalme wa mwanadamu.

**(2) Raia wa ufalme wa Mungu wanapaswa walete mabadiliko kwenye ulimwengu wao**.

Kundi la Waesene la wakati wa Yesu lilisema kwamba wenye haki wanapaswa kujiondoa katika jamii na kuanzisha ufalme wa Mungu wakiwa wamejitenga. Yesu alisema, "Hapana!

---

[181] Mathayo 5:20

Ninyi ni chumvi ya dunia; ambayo inahifadhi na kuikoleza dunia yenu. Ninyi ni nuru ya ulimwengu inayoleta utukufu kwa 'Baba yeu aliye mbinguni'" Wakati ufalme wa Mngu kimsingi ni wa kiroho, dunia yetu inatakiwa ifaidike kisiasa, kiuchumi, na kijamii kutokana na uwepo wa raia wa ufalme.

> "Mwenye moyo safi siyo tu kwamba atamwona Mungu lakini atakuwa barua ambayo jamii itamwona Yeye."
> - Leon Hynson

Tunaweza tukaorodhesha mifano mingi ya Wakristo waliokuwa chumvi na nuru katika jamii ya kidunia. William Wilberforce aliongoza Bunge katika kukomesha biashara ya watumwa katika iliyokuwa Dola ya Uingereza. Uamsho wa Wamethodisti ulileta mabadiliko ya kijamii katika ngazi zote za jamii ya Waingereza. Kuua watoto na kuwachoma wajane pamoja na maiti za waume zao ilikuwa halali nchini India. William Carey alipigana kukomesha uovu huu. Wakristo wameeneza kusoma na kuandika ili kuondoa ujinga, wameanzisha mahosipitali na vituo vya kutunzia watoto yatima na wasoijiweza, na wamesaidia maskini na wahitaji katika mataifa mengi.

**(3) Raia katika ufalme wa Mungu wanaenda hata zaidi ya mahitaji ya chini ya Sheria ili kuonyesha upendo wa Baba**

Yesu hakuja duniani ili kuitangua Sheria, bali "kuitimiza" Sheria. "Sikuja kutangua, bali kutimiliza." Kutimiliza kitu ni "kuleta kwenye kukamilika" au "kuhitimisha." Yesu hakuja kwa ajili ya kuitangua Sheria bali kuidhihirisha roho nyuma ya Sheria. Katika mfululizo wa mifano sita, Yesu anaonyesha kwamba haki ya raia wa ufalme ni lazima "izidi haki ya waandishi na Mafarisayo."

| Sheria | Raia wa Ufalme |
|---|---|
| Sheria inakataza mauaji. | Raia wa ufalme wanashughulikia chanzo cha uhamasishaji wa chuki. |
| Sheria inakataza uzinzi. | Raia wa ufalme “hawaangalii kwa nia ya kumtamani mwanamke.” |
| Sheria inahitaji “cheti cha talaka.” | Raia wa ufalme wanatafuta njia za kuidumisha ndoa, kuliko kutoa sababu za kutaka kuachana. |
| Sheria inakataza viapo vya uongo. | “Ndio” au “Hapana” kwa raia wa ufalme inatosha. |
| Sheria inaweka mipaka ya kulipiza kisasi ("jicho kwa jicho"). | Raia wa ufalme wanachukua hatua za upendo, na siyo kulipiza kisasi aact from love, not revenge. |
| Sheria inataka upendo kwa jirani yako. | Raia wa ufalme wanawapenda hata maadui wao.[182] Wanadhihirisha upendo na huruma za Baba yao wa mbinguni.[183] |

**(4) Raia wa ufalme wanajali zaidi kumpendeza Mungu kuliko kuwapendeza watu wengine.**

Mafarisayo walitaka watu waone ukarimu wao; raia wa ufalme wanaweka siri. Wanafiki waantaka watu wengine wasikie sala zao znyekuvutia; raia wa ufalme wanaomba kwa wepesi na kwa kumaanisha. Mafarisayo walitaka watu wengine wawaheshimu kwa ajili ya kufunga kwao kwa muda mrefu; raia wa mbinguni wanafunga tu kwa ajili ya kupata thawabu ya Mungu.

**(5) Raia wa mbinguni hawategemei utajiri wao au kuwa na mashaka kuhusu mahitaji yao.**

Badala yake, wana imani ya utoaji kutoka kwa Baba yao wa mbinguni.

**(6) Raia wa ufalme hawana hukumu dhidi ya watu wengine.**

Hata hivyo, ni waangalifu kugundua tunda la uovu la waalimu wa uongo.

**(7) Raia wa ufalme wanajiamini katika maombi yao.**

Raia wa ufalme wanajiamini katika maombi yao kwa sababu wanajua kwamba “Baba yao aliye mbinguni anatoa yaliyo mema kwa ajili ya wale wamwombao!”

---

[182] Agano la Kale *halijaamuru* Israeli “mchukie adui yako.“ Hii ilikuwa ni kueleweka visivyo kwa Agano la Kale.
[183] Luka 6:36

**(8) Raia wa ufalme wanaelewa kwamba kuna njia mbili tu.**

Wanaelewa kwamba kuna lango pana na lango jembamba. Kuna mti wa mema na mti wa maovu. Kuna mjenzi mwenye hekima na mjenzi mpumbavu. Raia wa ufalme wanatambua hayo.

**Kuishi kwa kanuni za ufalme.**

Tunawezaje kuishi kwa kanuni za Hotuba ya Mlimani? Msingi ni katika Mathayo 5:48. Raia wa ufalme tumeitwa tumfananie Baba yetu wa mbinguni. Mahubiri ya Yesu ni mepesi – na ni magumu. Ni neema ya Mungu tu inayotuwezesha tuishi sawa na mafundishoya Yesu. Kwa uwezo wetu wenyewe, kamwe hatuwezi kuishi kulingana na mahitaji ya Hotuba. Ni Roho Mtakatifu peke yake anayefanya maisha ya ufalme yawezekane.

> "Hotuba ya Mlimani ni onyo dhidi ya kupenda kukiwa na masharti yaliyoambatanishwa, kupenda kwa ajili ya kujpatia faida binafsi, au kukataa wito wa haki ya kweli. Kwa hakika, hotuba hii ni wito wa kuonyesha aina za misamaha, utoaji, upendo wa kushukuru na rehema ambao unamfanania Mungu."
> - Darrell Bock

Ni lazima tuelewe kanuni hii tunapokuwa tunahubiri Hotuba ya Mlimani. Kama tutahubiri Hotuba hii kama sheria peke yake, tutawaacha watu wakiwa wamechanganyikiwa na kukataa tamaa. Ni pale tu tutakapohubiri hii Hotuba kama mfano wa maisha ya ufalme – yaliyowezeshwa kwa neema ya Mungu, yaliyonunuliwa kwa dhabihu ya Mwanae, na kuwezeshwa na Roho Mtakatifu – kwamba Hotuba ya Mlimani kweli imekuwa injili, "habari njema."

► Baada ya kusoma Hotuba ya Mlimani na kutafakari muhtasari huu, jadili:

- Ni mafundisho gani kutoka katika Hotuba hiyo yanaonekana kuwa magumu kwa Wakristo katika jamii yako?
- Ni mafundisho gani kutoka katika Hotuba hiyo yanaonekana kuwa magumu sana kwako kama kiongozi wa Kikristo?

## Siri ya Ufalme: Mifano ya Ufalme

Waalimu wa Kiyahudi walijua kwamba tunakumbuka hadithi zaidi kuliko tunavyokumbuka taarifa za kupendeza. Kwa sababu hiyo, mifano ilikuwa ni aina maarufu ya kufundishia iliyotumiwa na rabi wa Kiyahudi. Yesu alitumia mifano ili kuunganisha kweli za ufalme wa Mungu.

Mapema kwenye huduma yake, matumizi ya mifano ilimruhusu Yesu kufundisha wanafunzi akiwa anakwepa mgogoro wa moja kwa moja na maadui zake. Baadaye, Yesu angekabiliana moja kwa moja na viongozi wa dini Yerusalemu; lakini katika miaka ya mwanzo, fokasi yake ilikuwa ni kufundisha wanafunzi.

Watu wengi waliisikia ile mifano lakini hawakuelewa. "Wanasikia lakini kamwe hawaelewi"; "wanaona lakini kamwe hawajui." Kwa nini? Kwa sababu wameifanya migumu mioyo yao. Isaya alitabiri:

> Mioyo ya watu hawa imekuwa mizito, Na kwa masikio yao hawasikii vema, Na macho yao wameyafumba; Wasije wakaona kwa macho yao, Wakasikia kwa masikio yao, Wakaelewa kwa mioyo yao, Wakaongoka, nikawaponya.[184]

Kupitia mifano, Yesu aliweza kufundisha wale ambao masikio yao yalikuwa tayari kusikia

Mathayo 13 inawakilisha mfululizo wa mifano kuhusu "siri za ufalme."[185] Mifano hii inafichua asili ya ufalme wa Mungu kwa wafuasi wa Yesu, huku ikificha mengi ya mafundisho yake kutoka kwa viongozi wasioamini.

► Kabla ya kuendelea, simama na usome Mathayo 13:1-52. Utakapokuwa unasoma kila mfano, andaa muhtasari wa dhamira ya msingi ya kila mfano kwa mistari miwili au mitatu katika jedwali lililoko katika ukurasa unaofuata. Kwa kila mfano, tafuta matumizi yake kwenye huduma leo. Nimekamilisha mfano wa kwanza kama kielelezo.

---

[184] Mathayo 13:15, akinukuu Isaya 6:9

[185] Mathayo 13:11

| **Mifano ya Ufalme** | | |
|---|---|---|
| **Mfano** | **Dhamira** | **Somo la kujifunza kwa huduma leo** |
| **Mpanzi** | Kinachotegemewa kutoka kwa msikilizaji ni kipimo cha utoaji wa matunda | Ninapokuwa ninahubiri au kufundisha, ni lazima nimwamini Mungu kwa matunda. Siwajibiki katika mavuno; ninawajibika katika kupanda mbegu kwa uaminifu |
| **Magugu** | | |
| **Mbegu ya haradali** | | |
| **Chachu** | | |
| **Hazina iliyositirika** | | |
| **Lulu ya thamani kubwa** | | |
| **Wavu (juya)** | | |
| **Bwana wa nyumba** | | |
| **Watumwa kumi** (Luka 19:11-27) | | |

**Mfano wa Mpanzi (Mathayo 13:3-9, 18-23; Luka 8:5-18)**

Mfano wa kwanza katika mfululizo huu wa mifano kuhusiana na ufalme unafundisha kwamba kinachotegemewa kwetu katika mbegu kinapimwa kutokana na kuzaa kwa matunda yake. Kwenye ufalme wa mbinguni, baadhi ya watu wataamini na kuzaa matunda hali wengine watakataa kuamini au watakengeuka baada ya kuwa wamekuwa tegemeo la kwanza.

Mfano huu unaweza kuitwa kuitwa mfano wa udongo kwa sababu ni hadithi kuhusiana na aina mbali mbali za udongo, na siyo wapandaji tofauti. Katika kila mfano, mbegu ni ile ile moja, na mpandaji alikuwa ni yule Yule; tofauti ni udongo tofauti. Tunapokuwa tunatangaza ujumbe wa ufalme, hatupaswi kushtuka wakati tunapoona watu wengine wanakuwa wagumu kupokea kuliko wengine. Hatupaswi kukataa tama. Yesu alifundisha kwamba baadhi ya wasikilizaji watakuwa udongo mzuri unaozaa matunda wakati watu wengine watakuwa wagumu dhidi ya Neno.

Uamuzi wa mwisho wa Luka kuhusiana na mfano huu wa mpanzi unaonyesha kwamba huu ni mfano kuhusiana na kusikiliza ukweli. "Jiangalieni basi jinsi msikiavyo; kwa kuwa mwenye kitu atapewa, na yule asiye na kitu atanyang'anywa hata kile ambacho anadhaniwa kuwa nacho."[186] Wakati mtu anapokuwa na mwitikio chanya wa ukweli, anapokea ukweli wa ziada. Kabla ya kutoa mifano mingine katika hotuba yake, Yesu alifundisha wasikilizaji wake jinsi ya kusikiliza kama udongo wenye kuzaa matunda.

**Mfano wa Magugu (Mathayo 13:24-30, 36-43)**

Wayahudi walitegemea ufalme wa Mungu ulete hukumu ya haraka dhidi ya wenye dhambi. Yesu aliwaandaa wanafunzi wake kwa ajili ya kipindi cha mpito ambacho kwa pamoja watu walioamini na ambao hawajaamini wataishi kwa pamoja katika dunia. Katika hadithi hii, "lile konde ni ulimwengu."[187] Ni katika "mwisho wa dunia tu" malaika watayakusanya magugu na kuyachoma motoni. Ufalme wa Mungu utakuwa katika wakati wa Bwana na siyo katika wakati wa mwanadamu.

**Mfano wa Mbegu ya Haradali (Mathayo 13:31-32)**

Hakuna hata mtu mmoja aliyeangalia huduma ya Yesu hapa duniani angeweza kubaini usambaaji wa kanisa katika ulimwengu wote. Wanafunzi hawakuwa na elimu, walikuwa masikini,na wenye hofu. Walikosa haiba kubwa, hadhi katika jamii na nguvu ya kisiasa. Walikuwa kama "punje ndogo ya haradali." Lakini kama vile punje ndogo ya haradali inavyokua na kuwa mti mkubwa au msitu, ufalme wa Mungu ndivyo hivyo utakavyoifikia dunia yote.

---

[186] Luka 8:18
[187] Mathayo 13:38

Wasikilizaji wa Yesu wangeshituka kumsikia Yesu akilinganisha ufalme wa Mungu na punje ndogo ya haradali. Rabi wa Kiyahudi walitegemea ufalme wa Mungu uje kwa nguvu na utukufu. Walitegemea zitolewe hukumu dhidi ya watenda dhambi; walitegemeamapinduzi ya kijeshi dhidi ya utawala wa Rumi; walitegemea mapinduzi ya hali ya kijamii wakati ufalme mpya wa Kiyahudi utakapokuwa umeanzishwa. Badala yake, Yesu aliwaandaa wanafunzi wake kwa mwanzo usiovutia wa ufalme.

Tunaposoma katika Agano Jipya, tunaweza tukasahau umuhimu wa nchi ya Yudea katika karne ya kwanza. Yudea ndio kitovu cha Agano Jipya, lakini ilikuwa mbali sana na katikati ya karne ya kwanza ya dunia. Fikiria kuhusu mji mkuu wa nchi yako. Hili halikuwa jukumu la Yudea katika karne ya kwanza; jukumu hilo lilikuwa la Rumi. Fikiria kuhusu jiji lililo na vyuo vikuu vingi na mfumo mzuri wa elimu. Hili halikuwa jukumu la Yudea katika karne ya kwanza; jukumu hilo lilikuwa la Athene au Alexandria.

Yudea haikuwa muhimu kisiasa; haikuwa muhimu kuichumi; haikuwa muhimu kijamii. Fikiria kuhusu miji isiyokuwa na muhimu wowote katika nchi yako; hiyo ndiyo ilikuwa nafasi ya Yudea wakati wa utawala wa Dola ya Kirumi

Mfano wa punje ya haradali unaonyesha kukua kwa ufalme wa Mungu kutokea kikundi kidogo cha watu kutokea nyuma pembezoni mwa Dola ya Kirumi kuwa mti mkubwa uliofikia mataifa yote.[188] Rabi wa Kiyahudi walifundisha kwamba ufalme wa Mungu utakuwa ni kwa wana wa Israeli tu; Yesu anafundisha kwamba ufalme wa Mungu utafika hadi miisho ya nchi.

**Mfano wa Chachu (Mathayo 13:31-32)**

Mfano wa chachu unaonyesha pia ukuaji wa muujiza wa ufalme Ingawaje chachu kwa kawaida imekuwa na mtazamo hasi katika Maandiko, [189] Yesu alitumia chachu kama alama ya kusambaa kwa ufalme. Vipimo vitatu vya shayiri vinatosha kutengeneza mikate ya kutumiwa na watu mia moja. Pamoja na mwanzo wake kutokuwa muhimu, ufalme utakua kwenye kiwango cha nguvu kubwa sana.

Mfano wa chachu unaonyesha kukua kwa kasi kwa ufalme. Chachu siyo kitu cha kuvutia; hailipuki kama baruti kali; inafanya kazi polepole kwenye mkate. Rabi wa Kiyahudi walifundisha kwamba ufalme wa Mungu utatambulishwa kwa ishara mbalimbali duniani; Yesu alionyesha kwamba ufalme utakua polepole, lakini ukiongezeka kwa kasi hadi utakapoifikia dunia nzima.

---

[188] Katika Danieli 4:12 na Ezekieli 31:6, ndege waliojenga viota kwenye mti kunawakilisha ufalme mkuu ukiyafikia mataifa mengi.
[189] Mathayo 16:6; 1 Wakorintho 5:6-7

**Mifano ya Hazina Iliyofichwa na Lulu ya Thamani Kubwa (Mathayo 13:44-46)**

Mifano hii miwili ni juu ya furaha ya ufalme. Kwa pamoja, mtu alipata kitu cha thamani kubwa kiasi kwamba ilbmbdi "auze vyote alivyokuwa navyo ili akinunue." Mtizamo wa hii mifano siyo ntu kujitoa mhanga, bali ni furaha yake kwa kupata kitu cha thamani sana, "kwa furaha yake huenda akauza vitu vyote." Wanafunzi *walifurahia* kuachana na kila kitu ili wamfuate Kristo.

Mifano hii inaonyesha thamani ya juu sana ya ufalme. Ufalme waMungu unagusa tabia zetu zinazohusiana na maisha yetu yote. Kwenye maeneo mengine, Yesu anasema kwamba "Na jicho lako likikukosesha, ling'oe, ulitupe; ni afadhali kuingia katika ufalme wa Mungu, una chongo, kuliko kuwa na macho mawili, na kutupwa katika jehanum."[190] Kuingia kwenye ufalme wa mbinguni ni kwa thamani kubwa kuliko dhabihu yeyote ya ulimwengu huu.

**Mfano wa wavu (juya) (Mathayo 13:47-50)**

Boti za kuvua katika Ziwa la Galilaya hushusha nyavu kwenye Ziwa nyavu (juya) kubwa, wakikamata samaki wanaolika na visivyolika. Baada ya kurejea ufukweni, wavuvi watatenganisha samaki wazuri kutoka katika vitu vibaya vilivyovuliwa.

Kama ilivyo kwa mfano wa mpanzi, mfano huu uliwakumbusha wanafunzi kuhusu hukumu itakayokuja "wakati wa mwisho wa dunia." Badala ya kutegemea hukumu ya haraka, ni lazima wahubiri habari za ufalme wakijua kwamba mungu, kwa wakati wake mwenyewe, atahukumu wenye dhambi na wenye haki.Kutakuwa na hukumu ya mwisho ambayo itatenganisha mema kutokana na maovu, lakini tunapaswa tuuache wakati huo kwa Mungu mwenyewe.

**Mfano wa Bwana wa Nyumba (Mathayo 13:51-52)**

Yesu alianza mfululizo wa mifano hii kwa kuwafundisha wanafunzi wake kwamba ni lazima wawe udongo mzuri unaozaa matunda. Alimalizia mifano yake kwa kuwafundisha kuwashirikisha na wengine. "Kila mwanafunzi aliyefundishwa" ni lazima atoe katika hazina yake chochote alicho nacho ili kufundisha wengine. Hatujifunzi kwa ajili ya faida yetu sisi peke yake. Wanafunzi walifundishwa ili waweze kuwafundisha na wanafunzi wengine.

**Mfano wa watumwa Kumi (Luka 19:11-27)**

► Soma Luka 19:11-27.

Mfano huu unatoka kwa Luka, lakini Mathayo 24 anajumuisha mfano unaofanana uliopatikana kutokana na mhadhara wao na Yesu. Yesu aliutoa mfano huu wa watu kumi

[190] Marko 9:47

waliotoka miongoni mwa watumwa alipokuwa karibu na Yerusalemu, “kwa sababu walikuwa wakidhania kwamba ufalme wa Mungu ungekuja kwa haraka.”

Yesu alipokuwa akikaribia Yerusalemu, watu waliongeza hamu yao kubwa katika matazamio yao ya Masihi wa kisiasa. Yesu alitoa mfano huu ili kuwafundisha wanafunzi wake waendelee kuwa waaminifu wakati wakiwa wanaungojea ufalme. Hawakutakiwa kuficha kwa tahadhari yale ambayo Bwana wao aliwapa; badala yake walitakiwa watumie rasilimali zao zote walizokuwa nazo kwa ajili ya maendeleo ya ufalme.

## Kilele cha Ufalme

► Soma Mathayo 24-25.

Mengi ya mafundisho ya mwanzo ya Yesu yalielekezwa kwenye kuzinduliwa kwa ufalme. Alipokuwa anakaribia mwisho wa huduma yake hapa duniani, Yesu alizungumzia zaidi kuhusu wakati wa mwisho wa kilele cha ufalme. Mhadhara ulioko katika Mathayo 24 na 25 ni mwendelezo muhimu sana wa mafundisho ya Yesu kuhusiana na ahadi za ukamilishwaji wa mwisho wa ufalme.

### Angalia kwa kuzingatia: Hekalu la Herode

Mwaka wa 19 K.K. Herode Mkuu alianza matengenezo makubwa ya Hekalu. [191] Hekalu hili, lililomalizwa matengenezo na Zerubabeli mwaka wa 516 K.K., lilikuwa ndogo na lililokuwa la kawaida zaidi kuliko Hekalu la mwanzo la Sulemani. Herode alikuwa amekusudia kulirudisha Hekalu kwenye uzuri wake wa mwanzo. Alianza mradi wa ujenzi uliochukua takribani miaka themanini. Herode alichagua watendakazi wenye uzoefu mkubwa 10,000 kwa ajili ya ujenzi, na akawafundisha Walawi 1,000 kuhudumia idara mbalimbali za Hekalu hilo ambazo zilikuwa hazitakiwi zifanywe na watu wa kawaida.

Herode alitegemea abaki akikumbukwa kama mjenzi wa Hekalu kubwa duniani. Wakati Yesu akiwa bado kwenye huduma yake hapa duniani, kazi ya ujenzi ilikuwa kwenye miaka arobaini na sita ikiwa bado inaendelea. [192] Ujenzi wa Hekalu na maeneo yake yote yanayohusika katika ujenzi huo ulimalizika mwaka 63 B.K. – lakini miaka saba baadaye likabomolewa kutokana na kupigwa na kutekwa kwa Yerusalemu na jenerali Tito wa Kirumi mwaka wa 70 B.K.

Katika muda ambao “Hekalu la Herode” lilikuwa limekamilika, lilikuwa takribani mara mbili kwa ukubwa ukilinganisha na Hekalu la Sulemani likiwa na nafasi ya kuenea maelfu ya mahojaji wa Kiyahudi waliokuwa wanakuja Yerusalemu kwa ajili ya sikukuu. Hii ilikuwa ni moja ya maajabu makubwa ya Dola ya Kirumi.

---

[191] "Ulinganifu wa Hekalu," Haki miliki ya michoro, Faithlife / Logos Bible Software (www.logos.com). Imetumiwa kwa kibali.

[192] Yohana 2:20

Kwenye wiki ya mwisho ya Yesu kuwa Yerusalemu, "Wanafunzi wake walimwendea ili kumwonyesha majengo ya hekalu hilo." Kwa kuwa ujenzi wa hekalu hilo ulikuwa bado unaendelea, yumkini walikuwa wanaelezea kuhusu ujenzi uliobadilishwa kwa kipindi tokea walipokuwa wamelitembelea mara ya mwisho hekalu hilo.

Yesu aliwajibu kwa unabii kuhusu kubomolewa kwa hekalu hilo akawaambia. "Hamyaoni haya yote? Amin, nawaambieni, Halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomoshwa." Kisha wanafunzi wakamwuliza, "Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?"

Maswali ya wanafunzi yalikuwa katika sehemu mbili; Majibu ya Yesu pia yalikuwa katika sehemu mbili. Kama ilivyo kwa unabii wa Agano la Kale ukihusisha kwa pamoja vipengele vya karibu na vya mbali, unabii wa Yesu pia ulihusisha baadhi ya matukio ambayo yangetokea kwa wakati uliopo na mengine yatatokea wakati wa "mwisho wa dunia."

- Wanafunzi waliuliza, "Mambo hayo yatakuwa lini?" "Mambo hayo" (ubomoaji wa hekalu, "Halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomoshwa) ilitokea mwaka wa 70 B.K.

- Wanafunzi waliuliza,, "Nayo ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?" Yesu alizungumzia mambo ya baadaye ya kurudi kwake, "Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake."[193]


Yesu alionyesha kwamba ufalme utahusisha watu kutoka kwa mataifa yote, Wayahudi na Mataifa. Alionyesha kwamba kuwepo kwa Mataifa katika ufalme ulikuwa ni mpango wa Mungu, "tangu kuumbwa ulimwengu."[194] Ufalme wa Mungu ulikuwa mpango wa Mungu wa milele kwa ajili ya watu wake.

Mifano miwili katika hotuba ya mhadhara (wa Olivet) unafundisha kwambani lazima tuwe waaminifu wakati tukiwa tunaungojea ufalme. Wanawali watano wapumbavu walingojea – lakini bila maandalizi kamili. Mtumwa aliyekuwa na talanta moja alingojea - lakini bila uwakili mzuri. Kama raia wa ufalme, tunaitwa tuwe waaminifu na tunaostahimili katika kumhudumia Mfalme.

Katika hukumu ya mwisho, kutenganishwa kwa wema na wabaya kama ilivyoahidiwa katika Mathayo 13 kutafanyika. Somo kuu la msingi hapa siyo kuhusu ni lini na ni kwa namna gani hukumu hiyo itakavyofanyika. Badala yake, fundisho la Yesu ni jinsi ambavyo raia wa ufalme watakavyoishi *sasa* kwa ajili ya maandalizi ya hukumu ya mwisho. Siku hiyo, Mfalme atasema, "Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi." Tunapaswa tuishi katika utayari endelevu kwa ajili ya ujio wa Mfame. Ni lazima tukutwe tukiwa waaminifu wakati atakaporudi.

---

[193] Mathayo 25:31
[194] Mathayo 25:34




# Temple Comparison

Solomon's Temple, finished in 957 BC, was less than one-half the size of Herod the Great's expanded Second Temple in Jerusalem, built in 20–19 BC.

GRAPHIC BY KARBEL MULTIMEDIA, COPYRIGHT 2008 LOGOS BIBLE SOFTWARE

| Kiingereza | Kiswahili |
|---|---|
| Temple Comparison | Ulinganifu wa Hekalu |
| Solomon's Temple | Hekalu la Sulemani |
| Herod's Temple | Hekalu la Herode |
| American Football Field | Uwanja wa Soka wa Marekani |

## Matumizi: Gharama ya Uanafunzi

► Soma Luka 9:21-27.

Uraia katika ufalme wa Mungu unapatikana kwa neema peke yake. Hatufanyiki kuwa raia wa ufalme kwa ajili ya kazi njema. Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba hakuna gharama katika maisha ya uanafunzi. Katika Luka 9, Yesu alifundisha wafuasi wake kuhusu gharama za uanafunzi.

Dallas Willard aliandika, "neema haipingwi na jitihada; neema inapingana na kupata."[195] Jitihada tunazofanya kama wanafunzi hazipingani na neema. Kwa kweli, njia pekee tuliyo nayo sisi ya nguvu za kufanya uanafunzi ni *kwa sababu* ya neema ya Mungu.

Tafadhali angalia mfumo wa Yesu wa kufundisha: **Msalaba na kisha utukufu.**

- Yesu alitabiri kuhusu kifo chake na kufufuka. (Luka 9:21-22). Hii ilkuwa gharama Yesu aliyolipa ili kutupatia uraia katika ufalme.
- Yesu aliwaambia wafusi wake gharama itakayokuwepo katika kuwa wanafunzi wake (Luka 9:23-25). "Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate." Yesu alikabiliana na msalaba ili kuanzisha ufalme; ni lazima tuubebe msalaba kama tunataka tuishi kwenye huo ufalme.
- Yesu alizungumzia kuhusu ufalme wa Mungu (Luka 9:26-27). "Kwa sababu kila atakayenionea haya mimi na maneno yangu, Mwana wa Adamu atamwonea haya mtu huyo, atakapokuja katika utukufu wake na wa Baba na wa malaika watakatifu."

Hatuwezi kushiriki utukufu wa Mungu bila ya kushiriki msalaba. Yesu "alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, … mauti ya msalaba. **Kwa hiyo,** tena Mungu alimwadhimisha mno…."[196]

Kama watoto wa Mungu, tunafuata mfumo unaofanana. "Na baada ya kuwa mmeteswa kwa muda kidogo, Mungu wa neema yote, aliyewaita kuingia katika **utukufu wake wa milele** katika Kristo…."[197] Hii ndiyo sura ya maisha katika ufalme. Kristo aliteseka na msalaba kabla ya kuadhimishwa kkwenye utukufu. Wafuasi wake ni lazima "waubebe msalaba" kabla ya kuufurahia "utukufu wake wa milele."

Yesu alitafuta wanafunzi wenye msimamo. Hakuhitaji wanafunzi wake wawe wenye elimu sana, bali aliwataka wawe na mioyo ya uaminifu. Inagharimu nini kuwa mwanafunzi? "Mtu

---

[195] Dallas Willard, *The Great Omission: Reclaiming Jesus's Essential Teachings on Discipleship.* (New York: HarperOne, 2006)

[196] Wafilipi 2:8-9, mkazo umeongezwa

[197] 1 Petro 5:10, mkazo umeongezwa

ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate."

1. **Mwanafunzi ni lazima ajikane mwenyewe.** Kusema "Hapana" kwa ajili ya nafsi ni jambo gumu sana kufanya.
2. **Mwanafunzi ni lazima ajitwike msalaba wake mwenyewe.** Wafuasi wa Yesu walielewa kwamba msalaba ulikuwa unamaanisha kifo. Msalaba huwakilisha mateso na fedheha. Lakini wakristo wa mwanzo walielewa kwamba uanafunzi unahitaji msalaba. Wakati Ignatusi aliposafiri kwenda Romakwenda kufa kama mfia dini, alisma, "Ninaanza kuwa mwanafunzi." Uanafunzi unahitaji msalaba.
3. **Mwanafunzi ni lazima aendelee kumfuata Yesu katika mwenendo na tabia.** Kitenzi "kumfuata" ni wakati wa sasa.

Je, faida ya kuwa mfuasi ni zaidi ya gharama ya kuwa mfuasi? Yesu alitoa sababu tatu za kuwa mwanafunzi. Kwa kushangaza, hizi ndizo sababu hasa ambazo watu wengi *wanakwepa* uanafunzi. Kwa nini tulipe gharama kwa ajili ya uanafunzi?

1. *Usalama*. Mtu anayejaribu kuokoa maisha yake kwa kukwepa kwamba msalaba utapita. (Luka 9:24).
2. *Utajiri wa kweli*. Mtu anayekataa utambulisho na Kristo atapoteza kila kitu. (Luka 9:25).
3. *Tuzo*. Ni watu wale tu watakaomfuata Kristo watakaokaribishwa kwenye ule ufalme. (Luka 9:26-27).

► Soma Luka 14:25-33.

Yesu baadaye alipanua mafundisho yake juu ya uanafunzi. Maelekezo yake yanagawanyika katika sehemu tatu:

1. Gharama za uanafunzi (Luka 14:26-27)
2. Upumbavu wa kuwa mwanafunzi bila ya kuhesabu hasara. (Luka 14:28-32)
3. Ukumbusho wa gharama za uanafunzi (Luka 14:33)

Kama ukienda kununua gari, muuzaji mara nyingine atajaribu kuficha bei yake ya mwisho. Atasema, "Angalia gari hili lilivyo zuri!" Sikiliza nguvu ya gari hili." Ni pale tu utakapokuwa umeridhika na gari hilo anapoweza kukuambia bei halisi ya hiyo gari.

Yesu kamwe hakuwapa wanafunzi wake njia rahisi ya kwenda ufalme. Alianza kwa kuelezea gharama zake:

> Kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake, na mama yake, na mke wake, na wanawe, na ndugu zake waume na wake; naam, na hata nafsi yake mwenyewe,

> hawezi kuwa mwanafunzi wangu. Mtu yeyote asiyeuchukua msalaba wake na kuja nyuma yangu, hawezi kuwa mwanafunzi wangu.

Neno "kuchukia" ni dhana ya Kiyahudi ambayo ni tofauti kabisa na dhana yetu ya Kiswahili. "Kuchukia" kitu inamaanisha ni kupenda kitu siyo zaidi kuliko kitu kingine. Yesu anasema. "huwezi kuwa mwanafunzi wangu kama huwezi kunipenda mimi kuliko baba yako, mama, mke, watoto, kaka, dada, na hata wewe mwenyewe!"

Inagharimu nini kuwa mwanafunzi? Kila kitu! Kuwa mwanafunzi wa Kristo ni zaidi ya kushiriki furaha ya ahadi za kimasihi; kunahitaji kuushiriki msalaba.

► Injili ya Yohana inatoa maelekezo mengine matatu kwa ajili ya uanafunzi. Soma Yohana 8:31; 13:35; na 15:8. Kwa kuzingatia maelekezo ya uanafunzi yaliyoko katika Luka na Yohana, je, unatengeneza wanafunzi katika huduma yako?

## Hitimisho: Ufalme wa Mungu ni nini?

Hadi hapo Kristo atakaporudi, hatutaelewa undani wote wa mahubiri yake kuhusu ufalme. Hata hivyo,Vitabu vya Injili vinaonyesha tabia nyingi za ufalme wa Mungu:

- Ufalme wa Mungu ni ufalme wa kiroho. "Maana ufalme wa Mungu si kula wala kunywa, bali ni haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu."[198] Kuzaliwa upya kunatuondoa katika nguvu za giza na kutufanya tuwe sehemu ya ufalme wa Mungu.
- Ufalme wa Mungu utajumuisha utawala wa kimwili na kisiasa katika nyakati za mwisho.
- Ufalme wa Mungu ni wa ulimwengu wote. Haujakusudiwauwe kwa ajiliya Taifa la Israeli tu.
- Ufalme wa Mungu ni "wenye nguvu," na siyo wa kijiografia. Ni nguvu ya Mungu itendayo kazi katika ulimwengu huu, na siyo eneo maalumu lililo mahali fulani. Katika mfano wa watumwa kumi, ufalme ndio ulikuwa wenye mamlaka ya utawala, na sio eneo la kijiografia.[199]
- Ufalme wa Mungu ni wa kiroho usio wa kawaida. Mwanadamu anaotesha mbegu; hana uwezo wa kuifanya iote. Ufalme wa Mungu unakua kupitia uwezo wa Mungu.
- Ufalme wa Mungu ni zaidi ya tumaini la baadaye lisilokuwa na uhakika. Ni ukweli wa sasa uliopo unaodai jibu la haraka.
- Ufalme wa Mungu ulizinduliwa kupitia huduma ya Yesu hapa duniani. Uwezo wake dhidi ya mapepo ulionyesha ushindi wa ufalme wa Mungu dhidi ya ufalme wa Shetani.

---

[198] Warumi 14:17
[199] Luka 19:11. "fungu" lilikuwa ni kiasi cha fedha. Lilikuwa ni sawa na mshahara wa miezi mitatu wa mfanyakazi.

- Ufalme wa Mungu unazidi kusonga mbele kupitia kazi ya kanisa. Hotuba ya Mlimani inaonyeaha jinsi ambavyo waamini walivyoitwa kuishi katika wakati huu wa sasa.
- Ufalme wa Mungu utakuwa umekamilika wakati Kristo atakaporudi mara ya mwisho kuja kutawala kwa utukufu wake. Mamlaka ya Shetani itasambaratishwa na Mungu atatawala milele.

*Katika kiambatisho kuna mahubiri yenye kichwa cha habari "Injili ya Ufalme." Soma haya mahubiri kabla hujaendelea na Somo la 7.*

### Kazi ya kufanya Somo la 6

Andaa mfululizo wa masomo matatu kutoka kwenye msingi wa Hotuba ya Mlimani ya Yesu. Dhamira ya mahubiri yako iwe "Maisha kwenye Ufalme wa Mungu." Onyesha ni kwa jinsi gani tuishi kwa sasa kama raia wa ufalme wa Mungu. Hakikisha unahubiri mahubiri hayo kama "habari njema." Onyesha ni kwa jinsi gani neema ya Mungu inatuwezesha sisi kuishi kama raia kwenye ufalme wa Mungu.

# Somo la 7
# Kuwa na Upendo kama Yesu

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi atapaswa:

(1) Kutambua undani wa upendo katika maisha na huduma ya Yesu.

(2) Kuelewa kwamba upendo kwa ajili ya Mungu unahusisha mahusiano na Mungu, Ufahamu wa Neno la Mungu, na kuamini katika mapenzi ya Mungu.

(3) Kufuatisha upendo wa Yesu kwa watu wengine katika huduma.

(4) Akubaliane na umuhimu wa kuendelea kujisalimisha kwa Mugu Appreciate the importance of ongoing surrender to God.

(5) Aonyeshe mwenendo unaomfanania Yesu katika maisha ya kila siku.

## Kanuni ya Huduma

Upendo unaomfanania Kristo ni hamasa kwa huduma inayomfanania Kristo.

## Utangulizi

Maisha yote ya Yesu na huduma yake vilihamasishwa na upendo. Mara kwa mara alionyesha kwamba upendo kwa Mungu na upendo kwa watu wengine vilikuwa katika kina cha ndani cha maisha na huduma yake. Kama tutafuatilia mfano wa Yesu, upendo ni lazima uwe katika kina cha ndani cha maisha yetu na huduma. Hakuna mahali palipowekwa wazi kuhusu hili zaidi ya kwenye mfano wa Msamaria Mwema.

► Soma Luka 10:25-37.

Kabla tu ya kutoa mfano huu, Yesu alikuwa ameshasema kwamba "mambo haya umewaficha wenye hekima na akili; umewafunulia watoto wachanga."[200] Hii inafundisha somo la msingi kuhusu uelewa wa mambo ya kiroho. Kuelewa ukweli wa kiroho kunahitaji jambo lililo zaidi ya utafiti wa akili; kunahitaji ufunuo wa kiroho.Ukweli wa Mngu ni rahisi mno kiasi cha mtoto kuelewa, lakini ni zitosana kwa mwanazuoni.

Hii inatokeaje? Je, Mungu huficha ukweli kwa wale wanaouhitaji? Jibu linahusisha kanuni mbili.

[200] Luka 10:21

1. **Ukweli wa kiroho unafunuliwa tu kupitia Roho mtakatifu.** Paulo aliandika kwamba "mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye ila Roho wa Mungu." Kwa sababu hiyo, ni lazima tufundishwe na Roho, tukiyafasiri mambo ya kweli ya rohoni kwa maneno ya rohoni kwa watu ambao ni wa kiroho."[201]

2. **Ukweli wa Kiroho hufunuliwa tu kwa wasikilizaji walio tayari kupokea.** Paulo aliendelea kuandika, "Mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni."[202]

Mfano wa mpanzi unaonyesha kwamba mtazamo wa msikilizaji unategemea na matunda yatokanayo na hiyo mbegu.[203] Ni wale tu walio tayari kupokea ukweli watakaoweza kuelewa ukweli wanaousikia.

Mwanasheria katika Luka 10:25 ni mfano halisi wa maisha kwenye hii kanuni ya pili. Swalila mwansheria halikutoka kwa mtu mwenye kiu ya kujua ukweli, bali kwenye matamanio ya kumtega Yesu; alitaka "kumweka kwenye jaribu." Baada ya kusikia jibu la Yesu, jibu la mwanasheria halikuwa jibu la udongo wenye kuzaa matunda. Badala yake, aliuliza tena swali lingine "akitaka kujidai haki."

Mwanasheria alikuwa tayari ameshapata jibu la swali lake alilouliza, "Nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?" Jibu lilikuwa limeandikwa kwenye sheria, "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako.

Huu ni mfano wa moyowa Yesu kwa ajili yetu. Kuishi na kuhudumu kama Yesu alivyofanya, ni lazima tumpende Mungu, na tumpende jirani yetu kama Yesu alivyopenda. Bila ya kuwa na upendo unaomfanania Kristo, masomo mengine yote katika kozi hii hayatakuwa na maana yeyote. Maombi, uongozi, kufundisha, na kuhubiri – bila kuwa na upendo, hakuna jambo lolote hata moja la ukweli.

Inawezekana hili likaonekana ni rahisi sana. Unaweza ukasema, "Bila shaka, tunapaswa tumpende Mungu na tuwapende watu wengine. Tayari ninalijua hilo! Lakini katika mzigo wa siku hadi siku wa huduma, tunaweza tukapoteza moyo wa upendo. Inawezekana kuhudumia washirika wa kanisa bila kuwapenda. Inawezekana kuhudumia familia zetu bila kuwapenda. Inawezekana kufanya wajibu wa Kikristo bila kumpenda Mungu. Hamasa yetu kwenye huduma ya Kikristo ni lazima pawepo upendo unaomfanania Kristo.

---

[201] 1 Wakorintho 2:11, 13
[202] 1 Wakorintho 2:14
[203] Mathayo 13:1-23. Hasa zaidi angalia katika 13:12. Mtu anayekubali ukweli huupata ukweli zaidi. "Kwa maana ye yote mwenye kitu atapewa." Mtu anayekataa ukweli ni kipofu hata kwa ule ukweli ambao tayari anao: "lakini ye yote asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang'anywa."

**Kumpenda Mungu kama Yesu alivyompenda.**

Huduma ya Yesu kwa wanadamu ilihamasishwa na upendo wake kwa Baba. Ili kukwepa kuchoka sana na kuchangayikiwa katika huduma, kuwajibika kwetu kwa watu ni lazima kuwe na msukumo wa upendo wa Mungu. Huduma bila ya upendo kwa Mungu muda si mrefu inakuwa tupu na isiyoweza kuzaa matunda.

Vipengele vitatu vya upendo wa Yesu kwa Baba vitasaidia kuwa mfano kwetu: mahusiano, ufahamu na uaminifu.

**Yesu alidumisha Uhusiano wake wa Ndani na Baba yake.**

Mara kwa mara, Vitabu vya Injili vinaonyesha uhusiano wa karibu wa Yesu na Baba yake. Hii inaonekana katika:

- Tamko la Yesu kwa wazazi wake, "Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu?"[204]
- Maombi ya ndani sana ya Yesu katika Yohana 17.
- Kilio cha Yesu cha uchungu juu ya msalaba, "Eloi, Eloi, lama sabakthani? Yaani, Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?"[205]

Katika Bustani ya Gethsemane, Yesu alimwita Mungu akimwita lugha ya ndani ya kifamilia, *"Aba, Baba*."[206] Hii ni lugha ya mtoto aliyekuwa salama katika mahusiano na Baba yake.

Maombi ya Kiyahudi ya jadi yalitumia majina mengi ya Mungu: Mungu wa Abrahamu, Isaka na Yakobo; Mungu wa Baba zetu; Mungu Mbarikiwa; Mungu mmoja Mwenyezi; Mkombozi wa Israeli. Yesu alitumia jina la ndani zaidi la mahusiano *Aba.* Yesu aliishi katika mahusiano ya ndani na Baba yake.

Kenneth E. Bailey alitumia miaka mingi akifundisha katika Mashariki ya Kati. Anaandika kwamba *Aba* ni jina la kwanza la mtoto katika nchi za Mashsriki ya Kati. *Aba* ni jiananalotumia mtoto kwa ajili ya baba yake.

Paulo anatueleza sisi kama watoto wa Mungu kwamba, hata sisi tunayo fursa ya "kulia, '*Aba*! Baba!'" [207] Hatumwabudu Mungu ambaye anakaa mbali. Badala yake, kama Yesu tunaishi kwa usalama na raha ndani ya upendo wa Baba.

Kama wachungaji, tunaweza tukashawishika kujipima wenyewe kwa mafanikio ya huduma zetu. Kama thamani yetu inatoka katika ukubwa wa kanisa, kukubalika kwa kusanyiko

---

[204] Luka 2:49
[205] Mathayo 27:46
[206] Marko 14:36
[207] Warumi 8:15; Wagalatia 4:6

letu, au kutambuliwa na wenzetu, tutashawishika kujitoa dhabihu kwa ajili ya uaminifu kwa mafanikio. Tutakuwa tumekatishwa tamaa juhudi zetu zinapokuwa zimeshindwa. Hata hivyo, kama tuna uhakika kwamba *Aba* wetu anantupenda hata bila ya kujali mafanikio yetu, tunaweza tukayaacha matokeo kwake. Upendo wake hautegemei utendaji wetu.

**Yesu aliyajua Mapenzi ya Baba yake.**

Mwishoni mwa huduma yake hapa duniani, Yesu alishuhudia, "Nimeimaliza kazi ile uliyonipa niifanye. "[208] Yesu alijuani nini baba yake alichomtuma akamilishe na alijitolea maisha yake kwa ajili ya kukamilisha misheni hiyo.

Katika hali ya ubinadamu, Yesu alijifunza mapenzi ya Baba kupitia maombi na kupitia Neno. Kupitia maombi, Yesu aliyapata mapenzi ya Baba.

Yesu pia alijifunza mapenzi ya Baba kupitia Neno. Akiwa Kaperinaumu, Yesu alitoa muhtasari wa umisheni wake kama kukamilishwa kwa unabii za Isaya. [209] Wakati alipowajibu wajumbe waliokuwa wametumwa kwake na Yohana Mbatizaji, Yesu alitumia maneno ya Yesaya kama ushahidi wa huduma yake ya Kimasihi. [210] Yesu alilijua Neno.

Katika Agano Jipya yote, tunawakuta Wakristo wakirejea kwenye Maandiko kama jawabu kwa matatizo yao. Akiwa anakabiliwa na kifo cha mfia dini, hotuba ya mwisho ya Stefano ilikuwa imesheheni sana Maandiko kutoka katika Agano la Kale na utimilifu wake kwa Yesu Kristo. [211] Wakati viongozi wa kidini wa Kiyahudi walipowaamuru waachane kabisa na kuhubiri ujumbe wa Yesu, kanisa lilikutanika pamoja kwa ajili ya maombi. Maombi yao yalikuwa na nukuu ndefu ya Zaburi ya 2. [212] Waamini wa mwanzo waliyajua Maandiko. Ilikuwa ni katika lugha yao ya asili katika kuhubiri na kuomba.

"Kamwe usiruhusu vitabu vizuri vikachukua nafasi ya Biblia. Kunywa kutoka kwenye kisima!"
- Amy Carmichael

Kupitia historia yote ya kanisa, wahubiri ambao waliweza kuibadilisha dunia ni wale waliokuwa wanaume wa Neno. Martin Luther alishuhudia kwenye kongamano la Chakula cha Minyoo, "Nimefungamanishwa na Maandiko na dhamira yangu ni kuwa mateka wa Neno la Mungu." John Wesley alijifafanua mwenyewe kama "Mtu wa Kitabu Kimoja." Charles Spurgeon alisema kwamba wahubiri wanapaswa wajilishe kwa Neno hadi "harufu ya Biblia itoke ndani yako." Hudson Taylor alitumia muda wake mwingi sana katika Biblia hadi mwandishi mmoja akaandika, "Biblia ni anga ambalo Hudson Taylor aliishi." Watu hawa waliibadilisha dunia yao kwa sababu walilihubiri Neno kwa mamlaka.

[208] Yohana 17:4
[209] Luka 4:18-19
[210] Mathayo 11:4-5
[211] Matendo 7:1-53
[212] Matendo 4:24-30; Zaburi 2:1-2

Kama tunapaswa tuhubiri kama Yesu, au kama Wakristo wa mwanzo, au kama wahubiri maarufu katika historia, sisi pia ni lazima tuwe tumefurika Neno la Mungu. Maandiko yalikuwa ndio mamlaka iliyokuwa kuu kwenye huduma ya Paulo. [213] Yesu aliomba kwamba wanafunzi wake waweze kutakaswa, na kutengwa, kwa ajili ya huduma. Hili linaenda kukamilishwa kupitia Neno: "Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli."[214] Neno liliwafanya wanafunzi wakawa wa ufanisi mkubwa katika huduma; Neno linatufanya sisi tuwe na ufanisi katika huduma.

Ajith Fernando ametumia maisha yake kwa ajili ya huduma katika nchi ya Sri Lanka. Anaadika kwamba amefanya mazoea kwamba kamwe hakuna kutoa tamko zito katika mahubiri bila kuwa na msingi wake kutoka katika Maandiko. Hali hii ilimwezesha kuhubiri kwake kuwe kwenye msingi wa Neno. Kama Wakristo, tunamjua Mungu kupitia Neno lake, tunajenga makanisa yenye nguvu kupitia huduma zenye msingi wa Neno la Mungu.

**Yesu alimwamini Baba yake**

Uhusiano wa Yesu na Baba yake wakati wa huduma yake hapa duniani unaweza kujumuishwa pamoja katika maneno ya maombi yake kwenye Bustani ya Getsemani, "Walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe. "[215] Hii ni lugha yenye kuonyesha uaminifu wa kutosha na kujikabidhi kabisa.

Ni vigumu sana kujikabidhi kabisa kwenye mapenzi ya mtu ambaye hatumwamini. Tunaweza kwa nje kulazimishwa kumtii, lakini mioyo yetu inapinga kusalimisha uthibiti wetu kwa mtu tusiyemwamini. Yesu alijikabidhi kwenye mapenzi ya Baba kwa sababu alimwamini kabisa Baba yake katika upendo na uzuri wake.

► Soma Yohana 5:1-47.

Huduma yote ya Yesu inaonyesha tabia hii ya kumtegemea Mungu kwa kila kitu. Wakati viongozi wa Kiyahudi walipomwudhi Yesu kwa kumponya mtu aliyekuwa amepooza siku ya Sabato, aliwajibu:

> Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo yeye, ndiyo ayatendayo Mwana vile vile.…Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe; kama nisikiavyo ndivyo nihukumuvyo; na hukumu yangu ni ya haki, kwa sababu siyatafuti mapenzi yangu mimi, bali mapenzi yake aliyenipeleka.

Yesu alishajinasibu mapema kwamba yeye ni wa kiungu: "Baba yangu anatenda kazi hata sasa, nami ninatenda kazi." Lakini ingawaje alikuwa ni wa kiungu kwa ukamilifu wote,

---

[213] 2 Timotheo 3:16-17
[214] Yohana 17:17
[215] Mathayo 26:39

Yesu alijikabidhi kwa hiari yake mwenyewe jukumu la chini la misheni ya kidunia. Yeye na Baba wako sawa, lakini alijikabidhi kwenye mapenzi ya Baba.

Wakati waandishi na Mafarisayo walipompinga Yesu miezi michache baadaye, aliweza pia kutetea vitendo vyake kwa kuelekeza maelezo yake kwenye mamlaka ya Baba yake: "sifanyi neno kwa nafsi yangu, ila kama Baba alivyonifundisha ndivyo ninenavyo."[216] Kwa kuwa alikuwa ameweka tumaini lake lote kwa Baba, Yesu aliweza kujitoa kwa hiari yake mwenyewe kwa ajili ya mapenzi ya Baba.

Uongozi wa kanisa unahitaji uwiano mgumu. Wachungaji wengi na viongozi wa makanisa wana ujuzi wa uongozi wenye nguvu. Kama viongozi, wana maoni mazito na haiba. Hivi vinaweza kuwa ni nguvu yenye thamani sana kwa kiongozi. Hata hivyo, nguvu hii ni lazima iwe na uwiano na kujitoa kwa hiari kwa Mungu. Isipokuwa iwe tumejitoa kwa Mungu kwa uaminifu, tutaweza kulazimisha njia yetu wenyewe badala ya kujitoa kwa ajili ya njia ya Bwana.

Labda mfano bora wa kibiblia ni Musa. Musa alikuwa "Mpole sana zaidi ya wanadamu wote waliokuwa juu ya uso wa nchi."[217] Musa alikuwa na nguvu, lakini pia alikuwa mpole. Alikabiliana na Farao, mtu aliyekuwa na nguvu sana katika Misri. Aliwaongoza watu wa Israeli waliokuwa na usumbufu mkubwa jangwani. Musa alikuwa kiongozi mwenye nguvu. Lakini kwa wakati huo, alikuwa amejitoa kwa ajili ya Mungu. Uongozi wa kanisa ulio na ufanisi unahitaji kwamba tuzitoe nguvu zetu za asili kwa ajili ya Mungu. Hii inawezekana tu tunapokuwa tunatembea na Mungu katika maisha ya imani na uaminifu.

► Katika vipengele hivi vitatu vya upendo kwa ajili ya Baba (mahusiano, ufahamu wa Neno lake, na kujitoa kunakoendana na uaminifu, ni changamoto gani unayokutana nayo wewe binafsi?

## Angalia kwa kuzingatia: Je, Yesu alijinasibu kuwa ni Mungu?

Dini za uongo kama vile Mormoni na Mashahidi wa Yehova, pamoja na dini myingine zisizo za Kikristo kama vile Uislamu zinakataa kabisa kwamba Yesu alikuwa Mungu wa kweli. Wanamtambua Yesu kama mwalimu wa kiwango cha juu, au mtume, kama kiumbe wa kwanza kuumbwa, na kama Masihi. Lakini wanakataa kabisa kwamba alikuwa Mungu wa kweli.[218]

Wafuasi wa dini hizi maramaranyingi hudai kwamba, "Yesu kamwe hakuwahi kudai kwamba yeye ni Mungu. Alisema yeye alikuwa ni mwana wa Mungu katika njia ile ile ambayo kila mmoja wetu ni wana wa Mungu."

---

[216] Yohana 8:28
[217] Hesabu 12:3
[218] Ili kujifunza mafundisho kuhusiana na dini za uongo, tafadhali soma kozi ya Shepherds Global Classroom, *Dini za Ulimwengu na Ibada.*

Je, Yesu alidai kwamba yeye ni Mungu? Ndiyo. Watu waliomsikia Yesu walielewa madai yake. Wakati Yesu aliporejea Mungu kama "Baba yangu," Wayahudi walijaribu kumwuwa. Kwanini? "Kwa sababu hiyo Wayahudi walizidi kutaka kumwua, kwa kuwa hakuivunja sabato tu, bali pamoja na hayo alimwita Mungu Baba yake, akijifanya sawa na Mungu."[219]

Katika moja ya madai ya Yesu ya wazi kabisa ya kuwa Mungu, aliwaambia viongozi wa Kiyahudi, "Amin, amin, nawaambia, Yeye Ibrahimu asijakuwako, mimi niko."[220] Haya ni maneno ambayo Mungu aliyatumia kujidhirisha mwenyewe kwa Musa kwenye kichaka kilichokuwa kinawaka moto: "Ndivyo utakavyowaambia wana wa Israeli; MIMI NIKO amenituma kwenu."[221] Kwa maneno haya, Yesu alikuwa anajinasibu kwamba alikuwa ni Mungu ambaye alimtokea Musa. Viongozi wa Kiyahudi walijua wazi kwamba Yesu huwa anamaanisha katika maneno yake. Kwa kujibu, 'walichukua mawe" wakitaka kumwua. Hii ndiyo ilikuwa adhabu sahihi kwa mtu yeyote anayekufuru – kutoa madai ya uongo ya kuwa Mungu.[222]

Kwenye kesi ya Yesu, Kayafa aliuliza, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wake Mtukufu?" Jibu la yesu lilikuwa la uhakika, "Mimi ndiye, nanyi mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija na mawingu ya mbinguni." Kwa jibu hili, Yesu alijinasibu kuwa mmoja anayeketi mkono wa kuume wa Mungu na Mwana wa Adamu aliyetabiriwa na Danieli ambaye atakuja kuuhukumu ulimwengu.[223] Kayafa alijua kwamba Yesu alikuwa anajinasibu kwamba yeye ni Mungu. Akararua nguo zake akasema, "Mmesikia kufuru yake."[224]

Unaweza kukataa kuyaamini madai ya Yesu, lakini huwezi ukawa unasoma kwa uangalifu katika Vitabu vya Injili bila ya kukiri kwamba Yesu mwenyewe alijinasibu kuwa Mwana wa Mungu. Wasikilizaji wake waliyasikia madai yake na walilazimika aidha kumkubali yeye kama Mungu au kumwua kama nabii wa uongo na mwenye kukufuru.

### Kuwapenda jirani zetu kama Yesu alivyopenda

Yesu alipokuwa anafundisha, mara nyingi alivuta umati wa "watoza ushuru na wenye dhambi." Siyo kwamba Yesu aliwafundisha hawa watu tu, bali alikula pamoja nao. Wakati Mafarisayo walipomwona Yesu kwa hiari yake akila pamoja na wenye dhambi, walianza kumshutumu.Yesu aliwajibu kwa hadirhi tatu. Utakapokuwa umezisoma hadithi hizi, utagundua sehemu mbili muhimu za historia ya nyuma.

---

219 Yohana 5:18
220 Yohana 8:58
221 Kutoka 3:14
222 Mambo ya Walawi 24:16
223 Zaburi 110:1 na Danieli 7:13-14
224 Marko 14:61-64

1. Wakati wa siku za Yesu, kula kwa pamoja na mtu mwingine kulimaanisha unataka kuanzisha mahusiano.[225] Wakati Yesu alipokula na wenye dhambi, alimaanisha kwamba kwa makusudi anaunganishwa nao. Yesu alionyesha kwamba Mungu hangojei watu waende kwake, badala yake, Mungu huwatafuta kwa bidii sana wale waliopotea.

2. Wayahudi wa wakati wa Yesu walitegemea mtu mwenye haki kujizuia kukutana na watu wenye dhambi. Rabi wa Kiyahudi walifundisha kwamba wakati Masihi atakapokuja, ataepukana na mchanganyiko wowote wa watu wenye dhambi na atakula tu na wenye haki.

► Soma Luka 15:1-32.

Huu ni mfanommoja mkubwa katika sehemu tatu: kondoo aliyepotea, shilingi iliyopota, na mtoto mpotevu. Katika kila kipengele, msingi wa mfano ni furaha ya mtu aliyepata tena kile ambacho kilikuwa kimepotea. Yesu anaonyesha furaha ya mbinguni wakati wenye dhambi wanaporejeshwa kutubu.

Rabi wa Kiyahudi walikuwa na methali yao iliyozoeleka: Kuna furaha mbinguni wakati mwenye dhambi mmoja anapoharibiwa mbele za Mungu.” Yesu akabadilisha huu msemo kuwa kinyume chake, ‘Kuna furaha mbinguni wakatimwenye dhambi mmoja anapotubu.” Kulikuwa na tofauti gani kati ya Yesu na hawa Rabi wengine? Upendo. Yesu alionyesha kile kilichomaanisha kuhudumu kutoka ndani ya moyo wa upendo.

> "Mifano hii inaonyesha kwamba injili siyo kwa wale wenye kila kitu kilicho sahihi. Injili ni kwa ajili ya wale wanaojua kwamba hawana kila kitu kilicho usahihi."
> - Samuel Lamerson

Tunapohudumu bila upendo hadhi na nafasi zetu huwa ni muhimu zaidi kuliko watu. Hata hivyo, tunapohudumu kutoka katika moyo wenye upendo, tuko tayari kuweka kando hadhi zetu kwa ajiliya wanaopotea. Yesu alikuwa tayari kuteswa kutokana na shutuma za viongozi wa dini kwa ajili ya kuonyesha upendo kwa wale ambao walihitaji upendo sana.

► Kama tutauliza, “Utaonyesha upendo kwa Mtoto Mpotevu?’ Sisi wote tutajibu, “Ndio.” Tunajua jibu sahihi. Badala yake, uliza, “Ni nani mpotevu ambaye mara ya mwisho nilikutana naye? Ni kwa jinsi gani nilionyesha upendokwa mtu huyo?

### Yesu alionyesha Upendo kupitia Huruma yake kwa Waliojeruhiwa

Wakati wa kusoma Vitabu vya Injili, je, umeshagundua kwamba wenye dhambi waliokimbia *kutoka* kwa viongozi wa dini walikimbia *kuja* kwa Yesu? Ni nini kilichowafanya wenye dhambi kutafuta uwepo wa Yesu?

---

[225] Hii inaonyeshwa katika kitabu cha Mithali. Mama Hekima anamkaribisha “mtu mjinga” ale pamoja naye mezani pake. (Mithali 9:1-6). Kupitia mahusiano haya na Mama Hekima, huyu mtu mjinga atajeuka kuwa na Hekima

Siyo kwamba Yesu alipuuza dhambi zao; alitaka haki iliyozidi viwango vya Mafarisayo.[226] Wenye dhambi walikimbilia kwa Yesu kwa sababu alikuwa mtu wa huruma. Hakuwa na huruma dhidi ya dhambi, lakini alikuwa na huruma kwa mtu aliyekuwa mateka wa dhambi.

Tunaliona hili kutoka kwa mwanamke aliyekamatwa kwenye tendo la uzinzi. Baada ya waliomtuhumu kuondoka, Yesu alimwambia, "Wala mimi sikuhukumu. Enenda zako; wala usitende dhambi tena."[227] Yesu hakusamehe dhambi; alimtaka huyu mwanamke kuachana na maisha ya dhambi. Lakini alionyesha kumhurumia kuliko kumhukumu.

Injili ya Luka inatoa kipaumbele maalumu kwa huruma ya Yesu. Luka anaelezea taarifa inayomhusu Zakayo, mtoza ushuru ambaye angeweza kunyanyaswa na viongozi wa dini. Kwa mshangao wa watazamaji wengi, Yesu alijikaribisha mwenyewe "kuwa mgeni wa mtu ambaye ni mtenda dhambi."[228]

► Soma Luka 5:12-16.

Akitoa taarifa ya uponyaji huu, Luka anatoa maelezo ya kina ambayo yangeweza kuushangaza umati. Yesu "akaunyosha mkono wake, akamgusa." Hakuna hata mtu mmoja katika ulimwengu wa zamani aliyegusana na mwenye ukoma! Ilikuwa ni hatari kiafya kwa sababu ya uwezekano wa kuambukizwa. Na kwa Myahudi, ilimfanya mtu atambulike rasmi kwamba siyo mwenye haki.

Kwa nini Yesu alimgusa mwenye ukoma? Alijawa na huruma. "Naye akamhurumia, akanyosha mkono wake, akamgusa."[229] Mtu huyu aliyekuwa na ukoma alihitaji uponyaji wa kimwili, lakini pia alihitaji kuponywa kihisia. Watu waliokuwa na ukoma walihitajika kukaa mbali kabisa na watu wengine. Baada ya kuambukizwa na ukoma, mtu huyu alikuwa hajawahi kuguswa tena na mwanadamu yeyote. Yesu alikuwa na uwezo wa kuuponya huu ugonjwa bila ya kumgusa mwathirika, lakini alijua kwamba mwenye ukoma alihitaji mguso wa mtu mwingine. Yesu alisikia huruma.

> Watu hawajali ni kwa jinsi gani unajua hadi pale watakapojua ni kwa jinsi gani wewe unajali.

Kama tunataka tuhudumu kama Yesu, ni lazima tuwe na mioyo ya huruma kama Yesu. Watu wenye dhambi walipomtizama Yesu kwenye macho yake, waliona upendo wa huruma. Wakati watu wenye dhambi wanapokutizama wewe kwenye macho yako, wanaona nini?

---

[226] Mathayo 5:20
[227] Yohana 8:11
[228] Luka 19:7
[229] Marko 1:41

**Yesu alionyesha Upendo wake Kupitia Huduma yake kwa Wahitaji**

Ni rahisi kusema, "Ninajisikia kuwa na huruma kwa ajili ya wahitaji"; ni vigumu zaidi kushughulikia mahitaji yao. Yesu alionyesha upendo wake kwa kuhudumia mahitaji ya wale waliokuwa pamoja naye. Huduma yote ya Yesu ilikuwa ni kwa ajili ya kuhudumia wengine. Paulo aliandika kwamba Yesu "alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa."[230] Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi."[231]

Miujiza aliyoifanya Yesu inaonyesha huduma yake kwa watu wengine. Miujiza ilikuwa alama yake ya umisheni wa kimasihi, lakini *pia* ilikuwa ni namna ya kukutana na kuhudumia mahitaji ya watu. Mara nyingine miujiza iifanyika kwa ajili ya kikundi kidogo tu cha watu. Mara nyingine waliwafaidisha watu ambao hawakuwa na nguvu au ushawishi wowote. Mara nyingine, miujiza yake (ya wakati wa Sabato) ilimsababishia kukataliwa zaidi.

Yesu hakufanya miujiza ili kupata kibali kwa watu wenye nguvu; alifanya miujiza kuwahudumia wenye mahitaji. Kulikuwa na matukio mawili tu ambayo Yesu alikataa kufanya miujiza. Mafarisayo walipohojiana naye, "wakitafuta kwake ishara itokayo mbinguni; wakimjaribu."[232] Yesu alikataa kutoa ishara hiyo. Kisha kwenye kesi ya Yesu, Herode "akataraji kuona ishara iliyofanywa na yeye. "[233] Yesu alikataa hata kumjibu Herode. Yesu hakuwa wa kufanya miujiza "kwa shinikizo" au kwa ajili ya kuwavutia wasikilizaji waliokuwa na mashaka naye.

Ingawaje Yesu alikataa kufanya muujiza kwa Herode Antipasi, lakini alimponya mkwe wa mvuvi, wenye ukoma, waombaji vipofu, na waliopagawa na mapepo ambao hawakuwa na chochote cha kuweza kumlipa. Aliwalisha watu elfu tano ambao walionyesha ukosefu wa shukrani kwa kumwacha yeye na alimponya mjakazi wa kuhani mkuu aliyekuwa ameenda kumkamata yeye. Yesu alihudumia wahitaji kupitia miujiza yake.

Kama wachungaji na viongozi wa makanisa, ni rahisi kujipa moyo katika maamuzi yetu ya kuwasaidia wale ambao wanaweza kutusaidia sisi. Tunapotumiamuda wtu mwingi na watu wenye uwezo kuliko watumaskini, tunaweza kusema, "Wafanyabiashara wanaweza kusaidia huduma ya kanisa." Tunapoahirisha safari ya kumtembeleeamjane ili kumtembelea afisa mwenye ushawishi mkubwa, tunaweza kutoa udhuru, "Ana ushawishi mkubwa na anaweza kusaidia katika kazi ya Mungu." Yesu kamwe hakufanya hivyo. Kama

[230] Wafilipi 2:7
[231] Marko 10:45
[232] Marko 8:11
[233] Luka 23:8

tunataka tuwe wahudumu tunaomfanania Yesu, ni lazima tuwe watumishi kama Yesu. Kama yeye alivyokuwa, ni lazima tutafute "siyo kutumikiwa, bali kutumika."[234]

Paulo aliandika, "Kwa maana hatujihubiri wenyewe, bali Kristo Yesu ya kuwa ni Bwana; na sisi wenyewe kuwa tu watumishi wenu kwa ajili ya Yesu."[235] Neno mtumishi linaweza pia likatafsiriwa kama "mtumwa." Watumwa wengi wakati wa Dola ya Kirumi walikuwa wameelimika, wengine walikuwa madaktari na waalimu. Hata kama mtumwa alikuwa na elimu sana kuliko bwana wake, bado alikuwa ni mtumwa tu. Hawezi kuwa na kiburi na kusema, "Sitakutumikia! Mimi ni mkubwa kuliko wewe."

Baadhi ya wachungaji wanajisikia kwamba, "Nina elimu nzuri. Mimi siyo mtumishi wa mkulima katika kanisa langu!" Paulo kamwe kakusikia hivyo. Paulo alikuwa msomi sana wa elimu ya juu, lakini alifanyika mtumwa kwa Wakorintho "kwa ajiliya Yesu." Angeweza kusema, "Angalia elimu yangu; Nimefundishwa fasihi ya Kiyahudi, filosofia ya Kigiriki, na theolojia ya Kikristo. Ninaweza kuzungumza kwenye baraza la Kiyahudi la Sanhedrini, la Kigiriki Aeropagi, na baraza la Seneti la Kirumi." Badala yake alisema, "Mimi ni mtumishi wa watu wa chini sana katika Korintho - kwa ajili ya Bwana wangu, Yesu."

Kama tunataka tuhudumu kama Yesu, ni lazima tuwe na unyenyekevu wa kuishi kama mtumishi. Kama watumishi, aina ya maisha yetu siyo aina ya maisha ya hali ya juu ya gavana. Kama tunataka tuwe na upendo kama Yesu, ni lazima tuwe watumishi wanyenyekevu.

### Yesu alionyesha Upendo kwa kuwa na Rehema kwa Maadui zake

► Soma Mathayo 5:43-48.

Yesu aliwafundisha wafuasi wake kwamba, "Ninyi mtakuwa wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu." ikiwa na maana ya kuwa na upendo kama Baba wa mbinguni alivyo na upendo. Inamaanisha zaidi kwamba, "kuwapenda adui zako na kuwaombea wale wanaokutesa." Unapoonyesha aina hiyo ya upendo, dunia itajua kwamba ninyi ni "watoto wa Baba yenu aliye mbinguni."

Takribani miaka 200 kabla ya Yesu hajahubiri Hotuba ya Mlimani, mwandishi wa kiyahudi aliandika mkusanyiko wa mafundisho yaliyoitwa *Hekaya za Bin Sira*. Sikiliza jinsi alivyowafundisha wafuasi wake jinsi ya kushughulika na maadui zao:[236]

- Unapofanya jambo jema, hakikisha ni nani anayefaidika kutokana na hilo; kisha utakalolifanya halitapotea bure.

---

[234] Marko 10:45
[235] 2 Wakorintho 4:5
[236] Hekaya za Bin Sira 12:1-7, *Toleo la tafsiri ya Habari Njema*

- Fanya mambo mema kwa watu wanyenyekevu, lakini usiwape kitu chochote watu ambao siyo wacha Mungu.
- Usiwape chakula, vinginevyo watautumia wema wako kinyume chako. Kila jambo zuri unalofanya kwa ajili ya watu hao litakuletea badala yake matatizo mara mbili.
- Yeye mwenyewe Aliye Juu sana anachukia watenda dhambi, na atawaadhibu.
- Toa kwa ajili ya watu wema, lakini usiwasaidie wenye dhambi.

Maandishi ya Bin Sira yalichukuliwa na Wayahudi kama ni Maandiko wakati wa Yesu. Wakati Yesu aliposema, "Mmesikia kwamba imenenwa, Umpende jirani yako, na, Umchukie adui yako," hili ndilo andiko ambalo yawezekana alilirejea. Sira alisema, "Tenda wema kwa wenye haki tu." Usipoteze mambo yako mema kwa watenda dhambi." Sasa soma kwa mara nyingine tena Mathayo 5:43-48. Je, unaweza kuona ni kwa nini mafundisho ya Yesu yalileta mshtuko kwa wasikilizaji wake?

Katika Agano la Kale, Mungu alifundisha watu wake kuwapenda adui zao. Hili halikuwa jambo jipya. Kwenye masomo yangu ya Agano la Kale, mara nyingine huwapa "Jaribio" hili kwa wanafunzi wangu.

*Jirani yako ni adui wa kanisa. Unapokuwa unapita, anakulaani. Anajaribu kukudanga na hata kukuibia wanyama wako. Siuku moja wakati wa mvua za radi, unamwona ng'ombe wa jirani yako amevunja boma na anakimbia zake. Je, jukumu lako ni nini kwa huyu jirani yako?*

*(1) Je, unachukua fimbo na kumchapa ili apotelee mbali zaidi?*

Wanafunzi wangu wanajua kwamba hili siyo jibu sahihi!

*(2) Je, unapuuzia na kusema, "Hili siyo tatizo langu"?*

Wanafunzi wengi hufanya chaguo hili. Wanasema, "Ni ng'ombe wa jirani yangu na siyo ng'mbe wangu. Nitajali shughuli zangu peke yake. Mbali na hilo, jirani yangu hanipendi; hatakubaliana na msaada wangu."

*(3) Je, unatii andiko la Kutoka 23:4? "Ukimwona ng'ombe wa adui wako, au punda wake, amepotea, sharti umrudishie mwenyewe tena."*

Hata katika Agano la Kale, watu wa Mungu waliitwa kuwapenda jirani zao. Lakini wakati wa Yesu, watu walikuwa hawanukuu sana katika Kutoka 23 bali *Hekaya za Bin Sira*. Walipenda mafundisho yaliyowaruhusu wawapende jirani zao na wawachukie maadui zao! Yesu alisema, "Wapendeni maadui zenu kwa sababu Baba yenu wa mbinguni anawapenda watu wote waovu na wema."

Hii inaonekanaje katika "maisha halisa?" Jaribu kufikiria kisa hiki katika huduma yako:

*Kundi la watu ambao wamekuwa wakishiriki pamoja nawe katika mambo ya imani mara kwa mara wanakupinga hadharani. Wanakuuliza maswali yenye lengo la kukutega wewe; wanawaeleza wafuasi wakokwamba wewe ni mwalimu wa uongo; wanategemea utafanya jambo lolote litakalosababisha uingie kwnye mgogoro na wafuasi wako. Je, utawafanyiaje?*

*(1) Kuwafukuzia mbali na kuwaagiza kwamba kamwe msirejee tena?*

*(2) Kuwatendea kama wanavyokutendea wewe?*

*(3) Kuwa mkweli kuhusu makosa yao, lakini uwajibu kwa upendo?*

Mafarisayo walitumia kila njia ili kumpinga Yesu. Alikuwa mkweli kuhusiana na makosa yao; alijitahidi kuwafundisha ukweli; lakini siku zote aliwachukulia kwa upendo.

Kama tunataka tuhudumu kama Yesu, ni azima tuwapende maadui zetu. Hilo ni mojawapo ya mafundisho ya Yesu magumu sana. Kwa mtu yeyote anayetusaliti, kwa mtu yeyote anayekataa ujumbe wetu, kwa mtu yeyote anayetutesa, ni lazima tumwonyeshe upendo wa Yesu wa *agape*. [237] Hiyo ndiyo gharama ya kuwa na upendo kama Yesu.

**Matumizi: Tabia ya Yesu katika Maisha ya Mkristo**

Ni rahisi sana kuandika kuhusu kumpenda Mungu na kumpenda jirani yetu. Ni vigumu sana kuuonyesha upendo huo katika maisha ya kila siku. Ni pale tu tutakapokuwa tunaipalilia tabia ya Yesu ndani ya maisha yetu tutakapokuwa katika utayari wa kumshirikisha na ulimwengu wetu.

Je, inawezekana sisi kuwa na tabia ya Yesu? Maandiko yanafundisha kwamba Mungu ana uwezo wa kuwawezesha watu wake kufikiri kama eye anavyofikiri. Anataka awape watu wake roho mpya ambayo itatusababisha sisi tupende kile ambacho Mungu naye anakipenda, na tuishi kwa hiari ile anayotuitia tuishi nayo. [238] Mungu anataka akuze ndani yetu tabia ya Mwanae.

Sikiliza kile ambacho Oswald Chambers alizungumzia kuhusu uaminifu katika huduma ya kila siku:

> Unapokuwa huna maono kutoka kwa Mungu, hakuna shauku iliyoachwa ndani ya maisha yako, na hakuna anayekuangalia au kukutia moyo wewe, inahitaji neema ya Mwenyezi Mungu kuweza kuchukua hatua inayofuata katika kujitolea kwako kwa ajili yake…Inachukua zaidi ya neema ya Mungu, na uangalifu wa ziada wa kumsogelea yeye, ili kuweza kuchukua hatua inayofuata, kuliko ilivyo katika kuhubiri injili.

---

[237] *Agape* ni neno la Kigiriki lenye maana ya upendo usiokuwa na masharti unaotumika katika Agano Jipya. Ni neno lililotumika katika 1 Yohana na 1 Wakorintho 13.
[238] Ezekieli 36:26-27

> Kitu ambacho kwa uhakika huthibitisha kwa Mungu na kwa watu wa Mungu baada ya hapo ni uvumilivu thabiti, hata pale ambapo kazi haiwezi kuonekana kwa watu wengine. Na njia pekee ya kuishi maisha ya kutoshindwa ni kuendelea kumwangalia Mungu. Mwombe Mungu ayaweke macho yako ya kiroho yawe wazi kwa yeye Kristo aliyefufuka….[239]

Tunawezaje kuimarisha uaminifu huu katika huduma? Tunawezaje kuendelea kumpenda Mungu na jirani yetu wiki hadi wiki, mwaka hata mwaka? Ni lazima tupalilie tabia ya Yesu ndani ya maisha yetu ya kila siku. Hii inatuhitaji kwamba tuwe na ufahamu wa Kristo.

**Maelezo kuhusu Ufahamu wa Kristo**

► Soma Wafilipi 2:1-16.

Maelekezo ya Paulo kwa kanisa la Filipi ni mwongozo wenye nguvu wa kile kinachomaanisha kuwa na tabia ya Yesu Kristo. Kwa kanisa lililogawanyika kutokana na migogoro, Paulo aliandika, "Msitende neno lo lote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake. Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine."

Wangewezaje kufikia hili? Wangeweza tu kama wangetii maelekezo ya Paulo, "Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu;

Paulo aliorodhesha tabia nne zisizopatana na maisha ya Kikristo. [240] Tabia hizi zinaharibu ushuhuda wa Kikristo na ufanisi wa mhudumu wa Kikristo. Paulo alisema:

**(1) Msitende neno lo lote kwa kushindana (Wafilipi 2:3).**

Tamaa ya ubinafsi inauliza, "Kuna nini ndani yake kwa ajili yangu? Nitafaidikaje katika hili? Je, unaweza kufikiria Yesu akiuliza, "nitafaidikaje?" kabla ya kumponya yule aliyepooza au wakati anakabiliana na msalaba? Kwa hakika hapana!

Paulo anasema, "Tukiwa na ufahamu wa Kristo – kama tutafikiri kama Kristo alivyofanya – hatutafanya jambo lolote linalohusiana na kushindana kwa ajili ya tamaa binafsi. Tabia yetu ya ndani itakuwa tabia ya mtumishi. Tutauliza, "Nitawezaje kutumika?' na siyo "Nitawezaje kutumikiwa?"

**(2) Msitende neno lolote kwa majivuno (Wafilipi 2:3).**

Majivuno huuliza, "Je, hii inanifanya nionekaneje? Je, watu watavutiwa?" Pia katika hili, jaribu kufikiria Yesu akiuliza, "Watu watavutiwa?" kabla hajamtembelea mwanamke Msamaria kisimani? Kwa hakika hapana!

---

[239] Oswald Chambers, *My Utmost for His Highest* (March 6 entry). Yamepatikana kutoka https://utmost.org/taking-the-next-step/ tarehe ya March 22, 2021.
[240] Sehemu hii imenukuliwa kutoka kwa Dennis F. Kinlaw, *The Mind of Christ* (Anderson, Indiana: Warner Press, 1988), 101-107.

Paulo anasema, “Tukiwa na ufahamu wa Kristo – kama tutafikiri kama Kristo alivyofanya – hatutafanya jambo lolote linalohusiana na majivuno. Tutatafuta nafasi za kumdhihirisha Kristo, na siyo nafasi kwa ajili ya kujijengea hadhi zetu.

**(3) Fanya mambo yote bila manung’uniko (Wafilipi 2:14).**

Manung’uniko husema, “Mimi ninastahili zaidi kuliko hiki!” Je, unaweza kufikiria Yesu akisema, “Sikutakiwa niwaoshe wanafunzi miguu yao. Mimi ni mwalimu wao. Ninastahili zaidi. Kwa hakika hapana!

Paulo anasema, ““Tukiwa na ufahamu wa Kristo – kama tutafikiri kama Kristo alivyofanya – tutahudumu bila manung’uniko, hata katika nyakati ngumu sana.” Hapo tutatambua kwamba “hatustahili” chochote. Wakati tunapokumbuka kwamba kila kitu tulicho nacho ni zawadi ipatikanayo kwa neema ya Mungu, inabadilisha mtazamo wetu wa changamoto za huduma.

Helen Roseveare alikuwa ni mmoja wa wamishenari wakuu sana wa karne ya ishirini. Alikuwa daktari wa matibabualiyefundishwa katika Chuo Kikuu Cha Cambridge. Wakati akiwa anatumika kama mmishenari na daktari nchini Zaire, alitaka kujenga hospitali. Kwa sababu kulikuwa hakuna vifaa vya kujengea, hatua ya kwanza aliyochukua ni kutengeneza matofali. Dr. Roseveare alifanya kazi ya kutengeneza matofali ya kuchoma sambamba na wafanyakazi wa Kiafrika.

Alipokuwa anafanya kazi ya kutengeneza hayo matofali, mikono yake iliyokuwa milaini ilianza kububujikwa na damu. Alianza kunung’unika, “Mungu, nilikuja Afrika kama mtaalamu wa upasuaji, na siyo kutengeneza matofali! Bila shaka kuna watu wengine wa kufanya hii kazi ya watu wa chini.”

Wiki chache baadaye, mmoja wa wafanyakazi wa Kiafrika akamwambia, “Daktari, unapokuwa kwenye chumba cha upasuaji unatuogofya sisi kama daktari. Lakini unapokuwa unafanya kazi ya matofali na vidole vyako vinabubujika damu kama vidole vyetu, wewe ni dada yetu na tunakupnda.” Dr. Roseveare ghafla akatambua kwamba, “Mungu hakunituma mimi Afrika kuja kuwa daktari wa upasuaji tu; Alinituma pia kuonyesha upendo wa Kristo.”

**(4) Fanya mambo yote pasipo kuwepo na Mashindano (Wafilipi 2:14).**

Mashindano yanasema, “Ndiyo, Bwana, lakini…. Niko tayari kutii, lakini….” Pia katika hili, je, unaweza kufikiria Yesu akisema, “Baba, niko hapa kukutumikia; kwanini unafanya kukutumikia kwangu kuwe kugumu kiasi hicho? Haitatokea sisi kufikiria kwamba Yesu anaweza akawa na mashindano na Baba yake.

Paulo anasema, “Tukiwa na ufahamu wa Kristo – kama tutafikiri kama Kristo alivyofanya – hatutashindana kwa jambo lolote katika kutafuta njia rahisi ya kupita.” Hatutaweza kuridhia mapenzi ya Mungu katika maisha yetu kwa ajili ya kujadiliana katika mambo

tofauti na yale Mungu aliyokusudia kwetu. Jibu letu kwa Mungu litakuwa, "Ndiyo Bwana." Kwa njia hii tutakuwa na ufahamu wa Kristo.

Tangu Paulo alipowataka Wafilipi kuwa na ufahamu wa Kristo, aliamini wazi kwamba ingewezekana. Alijua kwamba wangeweza kuwa na roho ya unyenyekevu na utii ambavyo vilikuwa ni alama ya kuonekana katika maisha ya Yesu. Ni kwa jinsi gani tunaupata huu ufahamu wa Yesu?

**Fahamu zetu Zinabadilishwa kupitia Maandiko**

Mapema katika somo hili, tuliona ni kwa jinsi gani Maandiko hutufundisha kuhusiana na mapenziya Mungu. Yesu alikuwa analifahamu Neno la Mungu. Mitume walilijua Neno la Mungu. Kila uamsho wa kudumu katika historia ya kanisa ulianza kwa kujifunza Neno la Mungu.

Paulo aliwapa changamoto waamini wa Filipi, "kulishika vyema neno la uzima." [241] Ujasiri wao na msimamo wao kwa ajili ya injili kungewafanya wawe nuru ya ulimwengu wao.

Ni kupitia kwenye mafunzo ya kina ya Neno la Mungu kunakotuwezesha tuanze kufikiri kama Yesu, na kuwa na ufahamu wa Kristo. "Kupitia kwenye mafunzo ya kina," simaanishi kwamba ni lazima ujue Kigiriki na Kiyunani ili kuyaelewa maandiko; simaanishi kwamba ni lazima uwe na maktaba kubwa ya vitabu vya kusherehesha Biblia; kwa wepesi ninamaanisha kwamba ni lazima kutumia muda wa kutosha kujifunza Neno la Mungu. Ni lazima iwe kama ni sehemu yako ya mlo wa kila siku.

Kama Wakristo, Neno la Mungu ni lazima mlo wetu wa kila siku. Itakuwa ni furaha, siyo tu kazi. Hakuna mtu anayeweza kumwambia kijana mwenye njaa kwamba, "Unatakiwa leo ule chakula! Endapo hutakula, hutakuwa na afya," Kinachotakiwa kufanywa hapa ni kutengeneza mlo mzuri utakaopatikana, na kijana atataka kula! Neno la Mungu linapaswa liwe mlo wa kila Mkristo mwenye njaa.

Tunapokuwa tunajilisha kwa Neno la Mungu, akili zetu zinabadilishwa kuwa kwenye ufahamu wa Kristo. Wakristo wengi wamezaliwa mara ya pili, lakini bado wanaendelea kufikiri kwenye njia ile ile waliyokuwa wakifikiri wakati wakiwa bado hawajaamini. Akili zao bado hazijabadilishwa kuwa kwenye ufahamu wa Kristo. Kwa nini?

Dr. Paul Brand mmishenari na daktari wa upasuaji nchini India. Aliwatibu wagonjwa wengi wa ukoma. Aliwafanyia upasuaji uliotengeneza sehemu za viungo vyao ambavyo vilikuwa vimeharibiwa na ugonjwa wa ukoma. Aliandika kwamba wagonjwa ni lazima wajifunze njia mpya ya kufikiri jinsi ya kujisimamia baada ya kufanyiwa matengenezo upya.

Kwa mfano, angeondoa kano yenye afya kutoka kwenye kidole cha pete ili kurekebisha kano iliyoharibiwa kwenye kidole gumba. Lakini atakaposema kwa mgonjwa, "chezesha

---

[241] Wafilipi 2:16

kidole gumba," hakuna kilichotokea. Kisha atasema, "chezesha kidole chako cha pete," haraka watachezesha kidole gumba! Wanapaswa "kupangilia upya" ubongo wao. Watalazimika kujifunza jinsi ya kukifanyia kazi kidole gumba kwa njia mpya. [242]

Kama waamini wapya, tunapaswa "kupangilia upya" ufahamu wetu ili tuweze kufikiri kama Kristo. Kabla hujawa Mkristo, ulifikiria kwanza kuhusu mahitaji yako mwenyewe. Labda ulimwona mtu maskini, lakini ukafikiria kwamba "mimi mwenyewe ninahitaji fedha. Siwezi nikatoa fedha yangu kumpa mtu Yule." Kama Mkristo, uliwahi kusoma Neno la Mungu kwamba, "Mwenye kuwagawia maskini hatahitaji kitu"[243] Unasikia Neno la Mungu, "Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa."[244] Unaanza kufikiri mambo ya fedha kama Kristo naye alivyofikiri kuhusu fedha. Unaupata ufahamu wa Kristo kupitia Neno la Mngu.

Kabla hatujawa Wakristo, tulijaribu kuwaumiza wale waliotujeruhi sisi. Mtu alipokuwa mkali kwetu, tulighadhabika kwa hasira. Lakini kama Wakristo, tunasoma, "jivikeni moyo wa rehema."[245] Tunasoma tuwe, "watu wasiolipa baya kwa baya, au laumu kwa laumu; bali wenye kubariki; kwa sababu hayo ndiyo mliyoitiwa ili mrithi baraka. "[246] Tunaanza kuwajibu watu wengine kama Kristo alivyokuwa akiwajibu wale waliokuwa wakimuumiza. Tunaupata ufahamu wa Kristo kupitia Neno la Mungu.

**Fahamu zetu Zinabadilishwa kupitia Kujisalimisha kila siku.**

Paulo aliwataka Wafilipi wawe na ufahamu ambao ulikuwa ndani ya Yesu Kristo. Aliufafanua ufahamu huu kisha akawaeleza jinsi ambavyo hili litawezekana katika maisha yao. Ni lazima waendelee "kuufanyia kazi" wokovu wao kwa utii wa uaminifu na siyo kupata wokovu wao tu – bali kwa sababu Mungu tayari alikuwa kazini kwa "kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema."[247] Walipojitoa kwa Mungu kwa unyenyekevu, aliwapa tamanio la ("kutimiza mapenzi") na nguvu ("ya kufanya kazi") ili kuishi maisha ya Kimungu.

Tunapoishi maisha ya kujisalimisha, Roho Mtakatifu hupalilia ndani yetu tabia zile zile tunazoziona ndani ya maisha na huduma ya Yesu. Hatuupati ufahamu wa Yesu kwa jitihada zetu wenyewe; tunapata ufahamu wa Yesu kwa kujisalimisha.

Kujisalimisha kunatakiwa kuwe ni kitendo cha kila siku. Paulo ametuambia "itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai. "[248] "Dhabihu iliyo hai" haijafa; inaendelea kuishi. Kuna

[242] Paul Brand na Philip Yancey, *In His Image* (Grand Rapids: Zondervan, 1984), 146
[243] Mithali 28:27
[244] Luka 6:38
[245] Wakolosai 3:12
[246] 1 Petro 3:9
[247] Wafilipi 2:12-13
[248] Warumi 12:1

**kujisalimisha** ambako tunasalimisha mapenzi yetu yote kwenye mapenzi ya Mungu, lakini pia kuna **kujisalimisha kwingi** ambako tunaendelea kila siku kujisalimisha kwenye mapenzi yake.

Nancy Leigh DeMoss anatoa picha ya maisha ya kujisalimisha. [249] Utakapokuwa unasoma maelezo aya, jiulize, "Je, ninaishi kwenye maisha ya kujisalimisha kila siku kwenye mazingira haya? Je, ninadhihirisha ufahamu wa Kristo kwenye mazingira haya?"

- Wakati mwili wako unapotaka urudie maneno ya kukosoa, Roho Mtakatifu anakuambia, "usimtukane mtu ye yote."[250] Moyo uliojisalimisha unasema, "Ndiyo."
- Wakati mwili wako unapotaka kulalamika kuhusu matatizo, Roho Mtakatifu anakuambia, "shukuruni kwa kila jambo."[251] Moyo uliojisalimisha unasema, "Ndiyo."
- Wakati mwili wako unapotaka kupingana na kiongozi asiyekuwa na busara, Roho Mtakatifuanakuambia, "Tiini kila kiamriwacho na watu, kwa ajili ya Bwana."[252] Moyo uliojisalimisha unasema, "Ndiyo."

Wakati tunapokuwa tumejisalimisha, Roho yule yule aliyekuwa anakaa ndani ya Kristo anakaa ndani yetu. Kupitia Roho Mtakatifu – siyo kupitia makusudi mazuri yetu wenyewe – tumepewa uwezo wa kuchukua hatua kama Kristo dhidi ya mambo ya kuvunja moyo ya kila siku, mambo ya kukatisha tamaa ya huduma, na majaribu ya Shetani.

> "Siri ya maisha ya utakatifu haiko katika kumuigiza Yesu, lakini iko katika kumruhusu Yesu ajidhihirishe Mwenyewe katika maisha yangu….Utakaso hauleti kutoka kwa Yesu uwezo wa kuwa mtakatifu; ni kuchukua kutoka kwa Yesu utakaso ule ambao ulikuwa umejidhirisha kwake."
> - Oswald Chambers

► Shirikisha muda wa hivi karibuni ambao matamanio ya mwili yaliingiliana na mapenzi ya Mungu. Uliishije katika kujisalimisha kila siku wakati wa kukabiliana na majaribu? Je, lipo jaribu la sasa hivi ambalo itakubidi ujisalimishe tena kwenye mapenzi ya Mungu? Kama darasa, kila mmoja amwombee mwenzake katika maeneo haya.

### Hitimisho: Mungu hufanya kazi kupitia Upendo unaomfanania Kristo

Nilipoanza kuandika somo hili, nilijisikia kusitasita. Ingawaje ninajua akilini kwamba tumeitwa kuwapenda adui zetu, ninajua pia kwamba tunaishi kwenye ulimwengu ambao umetatizika. Wengi waliosoma masomo haya, wanaishi kwenye mazingira ambayo kanisa linatishiwa na serikali, dini za uongo, au misongo ya kijamii. Nilipokuwa naandika kuhusu kumpenda adui yako, nilijiuliza mimi mwenyewe, "Je, ni busara kufikiri kwamba kweli

---

[249] Nukuu kutoka kwa Nancy Leigh DeMoss, *Surrender.* (Chicago: Moody Press, 2008), 223-224.
[250] Tito 3:2
[251] 1 Wathesalonike 5:18
[252] 1 Petro 2:13

tunaweza kuubadilisha ulimwengu wetu kwa kuwapenda adui zetu? Tutampendaje adui yetu wakati adui yetu anajaribu kutuua sisi?"

Wakati nikiwa nashughulka na kuandaa somo hili, nilisoma kipande cha habari kuhusiana na Mkristo mmoja wa Iraq anayeishi Baghdad. [253] Wakati mwandishi wa habari alipokuwa akihojiana naye, wanajeshi wa ISIS walikuwa wamebakiza dakika arobaini tu waingie nyumbani kwake. Mwandishi aliukiza, "Bado kanisa lako linakutana kwa ajili ya kuabudu?" Yule Mkristo akamjibu, "Ndiyo! Kwa kweli, tumeanzisha vikundi viwili vya maombi katika kanisa letu - Kundi mojakwa ajili ya kuombea ndugu zetu waliouawa kwa mateso upande wa kaskazini, na kikundi kingine kuwaombea adui zetu."

Washirika wa Kanisa la Mtakatifu George huko Baghdad huomba kwa ajili ya adui zao. Wanatoa vifurushi vya chakula kwa wajane wa Kiislamu. Wanawapenda adui zao kwa sababu wanaamini kwamba wameitwa kwa ajili ya kufuata mfano wa Yesu.

Makala hii ilinikumbusha mimi kuhusu ukweli unaoonekana muda wote katika historia ya kanisa. Njia za Mungu za kufanya kazi siku zote hazifanani na njia za wanadamu. Mwanadamu anafanya kazi kwa kupitia mikutano ya uamsho ya kijeshi dhidi ya Waislamu kwenye karne za kati; Mungu anafanya kazi kupitia Raymond Lull aliyekufa akiwa kwenye ziara zake za umisheni kwa ulimwengu wa Kiislamu akiwa na umri wa miaka themanini na mbili. Mwanadamu anafanya kazi kupitia nguvu za kijeshi; Mungu anafanya kazi kupitia Hudson Taylor aliyejitolea maisha yake kwa ajili ya kupeleka injili kwa watu wa katikati ya Uchina. Mwanadamu anafanya kazi kutumia nguvu zake; Mungu mara nyingi hufanya kazi kupitia udhaifu.

Njia za Mungu kamwe siyo njia za wanadamu. Lakini mwisho wa mambo yote, njia za Mungu siku zote ni lazima zishinde. Dunia yetu inabadilishwa ielekee kwenye umilele kufuatia jinsi ambavyo Wakristo wanavyokuwa na upendo kama Yesu. Mabadiliko yenyewe ni ya polepole lakini mara nyingi yameambatana na maumivu, Lakini hii ndio njia ya Mungu ya kufanya kazi yake katika ulimwengu wetu ulioanguka.

Kufanya huduma kama Yesu kunatuhitaji tuwe na upndo kama Yesu. Mwinjilisti mmoja aliyekuwa mzee aliulizwa kuhusu mafanikio ya huduma yake. Alisema, "Njia pekee ambayo watu watajua ni kwa jinsi gani Mungu anawapenda ni kukuona wewe unawapenda kwa kiasi gani." Huyu mwinjilisti alielewa kwamba kwa jinsi ile upendo wa Kristo utakavyokuwa unang'aa kupitia sisi, ndiyo hivyo tutakavyokuwa tunauvuta ulimwengu uje kwa Mungu. Hiyo ndiyo maana ya kupenda kama Yesu.

---

[253] Mindy Belz, "How Does the Church Move the World?" *World Magazine*, May 27, 2017

**Kazi ya kufanya Somo la 7**

Katika somo hili, tumeona ni kwa jinsi gani Yesu alikuwa na upendo. Kazi hii inakutaka wewe utafute njia ambazo unaweza kufuata mfano wa Yesu katikakumpenda jirani yako. Haitakiwi ichukue muda mrefu kuifanya kazi hii; Inaweza ikachukua muda mrefu kidogo katika kuiweka kwenye matendo! Usishinwe kuiweka kwenye vitendo. Tumeitwa tuwe na upendo kama Yesu alivyokuwa na upendo

Katika safu ya 1, toa mfano kamili kutoka katika Vitabu vya Injili unaohusiana na upendo wa Yesu kwa ajili ya watu.

Katika safu ya 2, elezea mfano kamili jinsi ulivyoutumia upendo katika maisha yako. Utafuataje mfano wa Yesu wa upendo? Hii kazi ya kufanya ni kwa ajili yako; kuwa mahiri sana kwa jinsi itakavyowezekana.

| Mfano wa Yesu | Nilivyoutumia |
|---|---|
| | |
| | |
| | |

# Somo la 8
# Msalaba na Kufufuka

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi atapaswa:
(1) Kutambua majibu tofauti ya huduma ya Yesu wakati wa Wiki ya Mateso
(2) Kuelewa kulaaniwa kwa mti wa mtini uliofanywa kuwa mfano.
(3) Kutambua madhaifu yaliyopelekea kushindwa kwa Paulo.
(4) Kuukubali msalaba na kufufuka kama msingi wa maisha ya Ukristo na huduma.

## Kanuni ya Huduma

Ufanisi wowote wa huduma unafanyika kwa nguvu ya masalaba na kufufuka.

## Utambulisho

Kilele cha Injili zote ni maelezo ya mateso ya Yesu. Sura thelathini kutoka katika sura themanini na tisa za Vitabu vya Injili zimejikita kati ya ile wiki ya kuingia Yerusalemu kwa shangwe hadi kufufuka. Takribani nusu ya kitabu cha Yohana imetumika kwa ajili ya wiki hii ya mateso. Hiki ndicho kilele ambacho maisha ya Yesu na huduma vililenga. Katika somo hili, tutajifunza wiki ya mwisho ya huduma ya Yesu hapa duniani ili kujifunza masomo yatakayohusiana na maisha yetu na huduma zetu.

► Kabla ya kuendelea na somo hili, jadili maswali mawili yafuatayo:

- Kusulubiwa msalabani kunamaanisha nini kwangu, kitheolojia na kibinafsi?
- Kufufuka kunamaanisha nini kwangu, kitheolojia na kibinafsi?

## Majibu kwa Yesu: Wiki ya mwisho ya huduma ya Yesu Hadharani.

Moja ya msisitizo mkubwa kutoka kwa wainjilisti ni majibu ya wale waliokuwa wanakutana na Yesu. Kwa mfano, kwenye mwanzo wa maisha ya Yesu, Mathayo analinganisha kuabudu kwa mamajusi na majibu ya Herode, aliyejaibu kumwangamiza huyu mfalme mpinzani. Yohana analinganisha jibu la swali la Nikodemo, Rabi wa Kiyahudi, na la mwanamke Msamaria asiyekuwa na elimu yeyote katika kisima.

► Soma Mathayo 10:32-39.

Hakuna hata mtu mmoja atakayeweza kubakia kwamba hana upande wowote wa kuegemea kwenye ujumbe wa Yesu; aidha tunakubaliana na maelezo yake au tunamkataa yeye. Yesu aliielezea huduma yake kama upanga unaogawa makundi haya mawili. Familia

ziligawanyika kwa majibu yao kwa Yesu; hata familia ya Yesu mwenyewe ilikutana na mtihani huu. [254] Hakuna hata mtu mmoja atakayeweza kubakia kwamba hana upande wowote wa kuegemea.

Hali hii ya ulinganifu wa majibu ya Yesu yanakuwa na mvuto wenye hisia zaidi katika wiki la mwisho la huduma yake hadharani. Ulinganifu huu unaendelea hadi kwenye msalaba wenyewe, kwa wezi wawili wakijibizana kwa njia mbili tofauti kabisa kuhusiana na Yesu.

**Majibu kwa kufufua Lazaro**

► Soma Yohana 11:1-57.

Hata kabla ya kufufuliwa kwa Lazaro. Viongozi wa kidini walikuwa wamempinga Yesu. Mapema kwenye majira ya baridi Yesu alipotembelea hekalu wakati wa Sikukuu ya Kutabaruku, viongozi wa Kiyahudi walimshutumu kwa kukufuru na wakajaribu kumpiga kwa mawe. Kwa kuwa muda wake wa kuwa dhabihu ulikuwa haujawadia, Yesu akatoka mikononi mwao. Akaenda zake tena ng'ambo ya Yordani mbali na mji wa kitovu cha dini wa Yerusalemu. [255]

Habari zilipotoka kuhusu kifo cha Lazaro, wanafunzi walijua ni hatari kwa Yesu kurejea Yudea. Wasomaji mara nyingi hufanyia dhihaka shaka na tabia ya kuona mambo yote ni mabaya aliyokuwa nayo Tomaso, lakini mimi ninavutiwa na uaminifu wake aliokuwa nao kwa Bwana wake. Ana hisia (sahihi) kwamba Yesu ataweza kuuawa huko Yudea, lakini Tomaso ni mwaminifu. Wakati Yesu alipokuwa akisisitiza kurudi Yudea, Tomaso anawaambia wanafunzi wenziwe, "Twendeni na sisi, ili tufe pamoja naye." Bila kujali mashaka ya baadaye ya Tomaso, tusisahau uaminifu wa huyu mwanafunzi aliyejazwa na mashaka. Haileti mshangao wowote kwamba baada ya Yesu kufufuka, Tomaso alikuja kufa kifo kibaya cha wafia dini akiwa anapeleka injili India?

Kwenye kijiji kidogokama Bethania, kufufuliwa kwa Lazaro hakungwezekana kuwe kwa kificho. Hakukuwa na jinsi yeyote ya viongozi wa dini kuficha tukio lenye kuleta msisimko kama hilo. Yohana anaonyesha majibu tofauti katika muujiza huu.

***Majibu ya Umati wa Watu***

Mara tu taarifa za kufufuka kwa Lazaro zilipoenea, wananchi walijawa na uhakika kwamba Yesu atakuja kuupindua utawala wa Kirumi na kuanzisha upya utawala wa Daudi katika Yerusalemu. Walikuwa na uhakika kwamba Yesu ndiye Yule Masihi aliyekuwa ameahidiwa. "Basi wengi katika Wayahudi waliokuja kwa Mariamu, na kuyaona yale aliyoyafanya, wakamwamini. "[256] "Maana kwa ajili yake wengi katika Wayahudi walijitenga,

[254] Mathayo 13:53-58
[255] Yohana 10:22-42
[256] Yohana 11:45 na 12:11

wakamwamini Yesu. "[257] Kwa hiyo watu wengi walimwamini Yesu ambaye Mafarisayo walisema, "tazameni, ulimwengu umekwenda nyuma yake. "[258] Hili liliongeza shauku ya umma wakati Yesu alipoingia Yerusalemu akiwa amempanda mwana punda.

### ***Majibu ya viongozi wa Dini***

Kufufuliwa kwa Lazaro kuliharibu nafasi zote za viongozi wa dini kuweza kukanusha madai ya Yesu kwamba ni Masihi. Wakati umati wa watu ukiwa unageuka kuja kwa Yesu, viongozi wa kidini walikuwa na chaguzi mbili tu:

1. Kukiri kwamba Yesu ni yeye kama alivyojinasibu kwamba ndiye. Pamoja na hayo, hii itawahitaji kusalimisha tamaa yao kwa ajili ya madaraka. Yesu tayari alishalaani tabia yao ya unafiki. Kama watakiri kwamba Yesu ni Masihi, watapoteza nafasi zao kama viongozi wa Wayahudi.

2. Kumkamata na kumwua Yesu. Kama wamekataa kumwamini Yesu kama Masihi, ni lazima watamwua.

Viongozi wa dini walitetea maamuzi yao ya kumwua Yesu kama yaliyokuwa bora sana kwa ajili ya taifa. Kama ilivyo kwa viongozi wote wadhaifu katika historia, walijitahidi kujiridhisha kuhusu uamuzi wao. "Tunafanya nini? Maana mtu huyu afanya ishara nyingi. Tukimwacha hivi, watu wote watamwamini; na Warumi watakuja, watatuondolea mahali petu na taifa letu."[259] Walikuwa na mashaka kwamba Yesu atakuja kuongoza maasi dhidi ya Warumi. Hawakuwa wanajua kwamba ufalme wake ni wa kiroho.

"Mahali petu" yawezekana inarejea kwenye hekalu na "taifa letu" inarejea kwenye uhuru wa aina mbalimbali ambazo Warumi walikuwa wametoa kwa Wayahudi. [260] Ingawa Yudea ilikuwa chini ya uthibiti wa Warumi, Wayahudi walikuwa wameruhusiwa kuabudu hekaluni, kusimamia sheria za dini, na kupitia baraza lao la Sanhedrini, wasimamie baadhi ya serikali za kiraia. Yote haya yangeondolewa kama Warumi watavunja hayo maasi.

Kayafa alilithibitishia baraza la Sanhedrini kwamba ilikuwa ni heri mtu mmoja afe kuliko taifa lote lisiangamie kwa mateso. [261] Kimsingi, Baada ya kumwua Yesu, mashaka yaliyokuwa yamelisibu baraza la Sanhedrini yalikuja kutoweka. Miaka arobaini baadaye baada ya kumwua Yesu, Warumi walilivunja jaribio la maasi lililofanywa na Wayahudi kwa kuvunja lile hekalu, kuwaondolea haki zao zote walizokuwa wamepewa na Warumi, na kufanya kila kitu walichoamriwa ambacho Kayafa alikuwa anajaribu kukikwepa hapo mwanzo.

---

[257] Yohana 12:19
[258] Yohana 12:19
[259] Yohana 11:47-48
[260] Ona Matendo 6:13 na 21:28.
[261] Yohana 11:49-50

Kwa kuwa hawakuwa na jinsi ya kuuficha muujiza bila ya kuharibu ushahidi wote, Baraza la Sanhedrini lilifanya shauri kumwua Yesu pamoja na Lazaro. Ili "kulinda taifa. "[262] Miujiza siyo lazima iwashawishi wasioamini. Mara nyingi tunafikiri kwamba, "Kama tu Mungu atajidhihirisha mwenyewe kwa muujiza, kila mtu ataamini." Hata hivyo, muujiza unaweza kuleta ugumu kwa mwenye kushuku katika hali yake ya kutoamini.

Kwenye hadithi ya Lazaro na maskii (siyo Lazaro aliyefufuliwa na Yesu), tajiri alimsihi Abrahamu amtume Lazaro aende kuwaonya ndugu zake. Abrahamu akamwambia, "Wasipowasikia Musa na manabii, hawatashawishwa hata mtu akifufuka katika wafu. "[263] Maandiko peke yake ni ushuhuda wa kweli unaotosha. Kama tutayakataa maandiko, ushahidi mwingine wowote hauwezi kutushawishi sisi.

**Majibu ya Yesu: Mariamu**

► Soma Mathayo 26:6-13 na Yohana 12:1-11.

Katika kipindi chote cha huduma ya Yesu duniani, Mariamu, dada wa Lazaro na Martha, walikuwa miongoni mwa wafuasi wake muhimu sana waliokuwa wamejitoa kwake. Katika hadithi ya mwanzo, Martha alilalamika kwa sababu Mariamu alikaa kumsikiliza tu Yesu wakati yeye akihangaika kuhudumia. Katika hadithi hiyo, Yesu alimpongeza Mariamu kwamba, "amelichagua fungu lililo jema, ambalo hataondolewa."[264]

Wiki moja kabla ya kifo chake, Yesu na wanafunzi wake walitembelea nyumbani kwa Simoni aliyekuwa anaugua ukoma. Lazaro na dada zake walikuwa wamealikwa kujiunga katika kundi hilo. Wakati wa chakula, Mariamu mwenye kibweta cha marhamu ya thamani kubwa alimkaribia Yesu akayamimina mafuta ya marhamu kichwani pake hadi miguuni. Marhamu hiyo ilikuwa inagh'arimu takribani dinari mia tatu, kiwango cha mshahara wa mtu kwa mwaka mmoja. Wakati huo ambao hakukuwepo na mabenki, hii inawezekana kwamba Mariamu alikuwa amejihifadhia mwenyewe fedha hizo.

Wanafunzi walikasirika kwa sababu Mariamu alikuwa amepoteza fedha nyingi, [265] lakini Mariamu alijali tu mawazo ya mtu mmoja, Yesu. Alifanya hayo yote kwa ajili ya upendo wake kwa Yesu uliomfanya kipofu wa kutoona mawazo ya mtu mwingine yeyote. Hakujali marhamu yale yaligharimu fedha kiasi gani na hakujali watu wengine watafikiria nini. Alikuwa anamwabudu Bwana wake, na hakuwa na shughuli na jambo lingine lolote.

Wakati wanafunzi walipopinga matendo ya Mariamu, Yesu aliwakaripia: "Mwacheni; mbona mnamtaabisha? Amenitendea kazi njema."[266] Huku akijua kwamba msalaba ulikuwa unamsubiri siku chache tu mbele, Yesu alitambua ishara iliyokuwemo kwenye

---

[262] Yohana 11:53 na 12:10
[263] Luka 16:31
[264] Luka 10:42
[265] Mathayo 26:8; Marko 14:5
[266] Marko 14:6

kitendo cha Mariamu: "ametangulia kuupaka mwili wangu marhamu kwa ajili ya maziko." Yesu alimheshimu huyu mwanamke aliyetoa kitu kizuri kuliko vyote alivyokwisha wahi kuwa navyo kwa tendo la kujitegemea la ibada ya upendo.

Tunaposoma taarifa ya Mariamu ya kumpaka Yesu marhamu, tunapaswa kujiuliza, "Je, ni kwa jinsi gani mimi ninampenda Yesu? Je, ninamjali zaidi yeye au ninajali mawazo ya watu wengine wanaonitazama? Hakika Mariamu alimpenda Yesu.

**Majibu ya Yesu: Kuingia kwa Shangwe**

► Soma Mathayo 21:1-11 na Yohana 12:12-19.

Ilikuwa siku ya Jumapili, Yesu aliingia Yerusalemu akiwa amepanda punda. Katika siku ya kawaida, hakungekuwa na kitu cha kushangaza katika tukio hili; mwalimu kutoka Galilaya akisindikizwa na kikundi kidogo cha wafuasi wakiingia Yerusalemu kwa ajili ya Sikukuu ya Pasaka. Lakini huu haukuwa muda wa kawaida. Kufufuliwa kwa Lazaro kulibadilisha kabisa hija ya Pasaka ijeuke kuwa ni tamko la kidini na kisiasa.

Mathayo anaakisi waziwazi madhara ya kidini yaliyopatikana kutokana na kuingia kwa Yesu Yerusalemu. Mathayo anaonyesha kwamba Kuingia kwa Yesu kulikamilisha unabii wa Zakaria. Maneno yaliyokuwa yakitamkwa na umati wa watu yalitoka katika Zaburi 118, Zaburi ya Pasaka inayoelezea kuingia kwa ushindi katika Yerusalemu.[267]

Kuingia kwa Yesu kwa ushindi kulionekana kama gwaride la kisiasa la mfalme:

- Umati wa watu ulitandaza nguo kwenye barabara zote ikiwa ni ishara ya kujisalimisha kwa mfalme. [268]
- Kuanzia kwenye kipindi cha Wamakabayo, matawi ya mitende yalikuwa ni ishara ya ushindi dhidi ya majeshi ya adui. [269]
- "Hosiana!" ilimaanisha "tuokoe sisi," kilio cha kutaka ukombozi,
- "Mwana wa Daudi" kilikuwa ni cheo cha kifalme na Masihi.

Watu waliamini kwamba Yesu alikuwa anaingia Yerusalemu kuuangusha utawala wa Kirumi na kuanzisha ufalme wake. Muda mrefu uliokuwa umesubiriwa wa utawala wa kifalme wa Daudi ulionekana sasa umemalizika. Ahadi zilizotolewa na manabii zinaenda kukamilika hivi karibuni.

Ni siku chache tu baada ya hapo, watu hawa - hawa watapiga kelele za kudai, 'Msulubishe!" Kwa nini? Kwa sababu walikuwa wanamshangilia Yesu kwa sababu potofu. Waliamini atauangusha utawala wa Kirumi, Lakini Yesu hakuwa na mpango wowote wa

---

[267] Mathayo 21:4-11; Zakaria 9:9; Zaburi 118:26
[268] Mathayo 21:8; 2 Wafalme 9:13
[269] Yohana 12:13; 1 Wamakabayo 13:51

kuongoza mapinduzi ya kijeshi. Walikuwa wanahitaji utawala wa kifalme wa kisiasa, lakini Yesu alikuwa analeta ufalme wa kiroho. Kwa kukatishwa kwao tamaa, umati wa watu baadaye unamgeuka na kumsaliti Yesu.

Wajumbe wenye uwezo na nguvu za kisiasa na kijamii kwenye baraza la Sanhedrini walishaamua Yesu auawe; wasiokuwa na uwezo au nguvu ghafla wanakuwa kinyume na Yesu na kumsaliti. Akijua yaliyokuwa mbele yake, Yesu akaulilia mji unaokwenda kumkataa. [270] Hapa tunasema, "kuingia kwa ushindi"; Yesu alijua kwamba hiyo ilikuwa ndiyo "njia ya kuuendea msalaba." Umati ulinukuu Zaburi 118:26, "Na abarikiwe yeye ajaye kwa jina la Bwana; Tumewabarikia toka nyumbani mwa Bwana!" Yesu aliijua aya nyingine iliyofuatia, "Bwana ndiye aliye Mungu, Naye ndiye aliyetupa nuru. Ifungeni dhabihu kwa kamba Pembeni mwa madhabahu!"[271] Yesu aliingia Yerusalemu kama dhabihu ambayo hivi karibuni itatundikwa kwenye "madhabahu," msalaba wa Kirumi.

**Angalia kwa kuzingatia: Yesu anaulaani Mti wa Mtini**

► Soma Marko 11:12-25.

Kwenye kila Kitabu cha Injili kinachochukua vidokezo, kinahusisha taarifa za Yesu akiulaani mti wa mtini ambao haukuwahi kuzaa kwenye wiki yake ya mwisho ya huduma ya hadharani. Yesu aliulaani huu mti wa mtini siku ya Jumatatu alipokuwa anarejea Yerusalemu baada ya kulala katika mji wa Bethania. Siku iliyofuata Jumanne, wanafunzi wakauona mti umeshanyauka kwa kipindi cha masaa ishirini na nne tu.

Ingawaje ulikuwa "siyo wakati wa tini" (Mark 11:13), ilimaanisha kwamba majani ya rangi ya kijani yalipaswa yawepo kwenye mti huo. Tunda la mtini hutokea muda mchache tu baada ya hayo majani. Wakati mti ukiwa na majani bila kuwepo na matunda machanga ya mtini, huo mti hautakuwa na matunda katika mwaka huo.

Maelezo haya ya mti wa mtini ni "mfano uliotolewa" kuhusiana na kushindwa kwa Israeli kuzaa matunda. [272] Israeli ilikuwa imechaguliwa na Mungu kuwa Baraka kwa mataifa yote.[273] Badala yake, Israeli imeliaibisha jina la Yehova.

Hekalu lilikuwa liwe mahali pa "watu wa aina zote" kwa ajili ya kumwabudu Mungu."[274] Badala yake, hakalu limekuwa "pango la wanyang'anyi," mahali ambapo makuhani waliokuwa na nguvu walipatumia kuwadanganya maskini.

Mti wa mtini haukuzaa matunda; Israeli haikuzaa matunda. Mti wa mtini ulikataliwa; Israeli hivi karibuni itakataliwa.

---

[270] Luka 19:41-44
[271] Zaburi 118:27, *Tafsiri mpya ya Kiingereza*
[272] Katika Agano la Kale, mara nyingi mti wa mtini huwakilisha Israeli (mfano: Yeremia 8:13; Hosea 9:10; Yoeli 1:7).
[273] Mwanzo 12:3
[274] Isaya 56:7

Kulaaniwa kwa mti wa mtini ni moja ya mfululizo wa ujumbe zenye laana za Yesu kwenye siku zake za mwisho za huduma ya hadharani:

1. Mfano ulioonekana wazi wa mti wa mtini usiozaa matunda (Marko 11:12-14, 20-25).
2. Kulisafisha hekalu (Marko 11:15-19).
3. Mfano wa wapangaji waovu wasiokuwa waaminifu (Marko 12:1-12).
4. Mabishano kati yake na viongozi wa kidini (Marko 12:13-40).
5. Yesu anatabiri kubomolewa kwa hekalu (Marko 13:1-37).

**Majibu ya Yesu: Viongozi wa Dini**

► Soma Mathayo 21:23-22:46.

Baada ya kufufuliwa kwa Lazaro, viongozi wa kidini walikusudia kumwua Yesu. Hata hivyo, umaarufu wake na watu wa kawaida ulisababisha mpango huo kuwa mgumu. Walikuwa wanatafuta njia yeyote ya kumshushia hadhi yake mbele ya macho ya umati wa watu. Kwenye siku kadhaa baada ya Yesu kuingia Yerusalemu kwa ushindi, viongozi wa kidini waliratibu msururu wa mahojiano ya kushindana naye ndani ya hekalu. Walikuwa wanajaribu kumtega Yesu, lakini kila wakati walishindwa. Badala yake, umati wa watu uliangalia kila siku Yesu akiwagalagaza kwa aibu kubwa viongozi wa kidini kwa hekima na kwa umahiri mkubwa.

Kwanza, "kuhani mkuu na wazee" walitaka sababu za kuthibitisha uhalali wake wa kulisafisha hekalu na kuhubiri hadharani. Yesu aliwajibu kwa kuwatega kwa swali lililohusiana na Yohana Mbatizaji.

Kisha Yesu akatoa mifano mitatu ambayo iliwashutumu viongozi wa kidini. Mfano wa watoto wawili unaonyesha kwamba utii, na siyo ujuzi, ndiyo uthibitisho wa mahusiano katika ufalme wa Mungu. Mfano wa wapangaji waovu unaonyesha madhara ya kumkataa Yesu kama Masihi. Mwisho, mfano wa sikukuu ya harusi unaonyesha kwamba viongozi wa kidini ambao walikuwa wamealikwa kwenye harusi sasa wamekataliwa na kwa upendeleo wamepewa wale wanaoonekana si chochote, lakini wameitikia mwito wa mwaliko waliopewa.

Wakiwa wamedhamiria kumdhalilisha Yesu, viongozi wa kidini walileta msururu wa maswali kwa ajili ya kutaka kumteka Yesu. Dhamira yao haikuwa katika kujifunza ukweli; dhamira yao ilikuwa ni ili kumsambaratisha Yesu. Yesu alijua kwamba hawakua na haja ya kujua ukweli, kwa hiyo kila swali alivutia upande wake.

Baada ya kushindwa kumtega Yesu, viongozi wa kidini waliachana naye. Mathayo anamalizia sehemu hii akionyesha kushindwa kwao: "Wala hakuweza mtu kumjibu neno; wala hakuthubutu mtu ye yote tangu siku ile kumwuliza neno tena."[275] Marko anamalizia kwa kugusia furaha ya watu wa kawaida waliyokuwa nayo wakati wamehudhuria kwenye majadiliano hayo. "Na mkutano mkubwa walikuwa wakimsikiliza kwa furaha."[276]

► Kama mchungaji na kiongozi wa Kikristo, mara kwa mara utakutana na maswali magumu. Je, ni kwa jinsi gani utaweza kutambua tofauti ya watu wanaouliza maswali ya kweli na wale ambao wanataka kukutega? Je, majibu yako kwa aina hizi mbili za watu yanatofautianaje? (Ona Mithali 26:4-5 kama mfano wa ulinganifu huu.)

## Mashtaka na Kusulubiwa

► Soma 1 Wakorintho 15:1-8.

Miaka ishirini baada ya Yesu kupaa mbinguni, Paulo alianzisha kanisa katika Korintho. Kanisa hili lilikuwa na watu wengi waliookoka kutoka kwenye mazingira mbalimbali ya historia. Kanisa ilihusisha pamoja na Wayahudi waliokuwa wanajua maandiko ya Kiyunani, na Mataifa ambao hawakuwahi kusikia jambo lolote linalohusiana na Mungu wa kweli.

Kanisa la Korintho lilikuwa limepasuka kwa ajili ya migogoro na tishio la mafundisho ya uongo. Akihusika kujibu matatizo haya, Paulo anakumbushia kuhusu ujumbe wake wa kwanza aliohubiri mahali hapo. Mafundisho ya kwanza ya Paulo kwenye jiji ambalo lilikuwa ni la wapagani, yalilenga kwenye matukio manne ya historia:

- Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu.
- Alizikwa.
- Alifufuka siku ya tatu.
- Alionekana hadharani – kwa Kefa, kwa wale Thenashara, kwa ndugu zaidi ya mia tano pamoja, kwa Yakobo, tena kwa mitume wote, na mwisho wa watu wote Paulo.

Sehemu ya kwanza ya ujumbe wa Paulo katika Korintho ilikuwa juu ya msalaba: "Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu." Ujumbe kuhusu msalaba ndio kiini kikuu katika imani ya Kikristo.

Kwenye Agano la Kale, mtu aliyeleta kondoo kwa ajili ya dhabihu huiweka mikono yake juu ya kichwa cha kondoo ili kujitambulisha na kifo cha dhabihu. Kwa kuweka mikono yake juu ya kichwa cha kondoo, anayeabudu husema, "Kondoo huyu anakufa kwa niaba yangu. Ninastahili kifo kwa ajii ya dhambi zangu." Kwa njia hiyo – hiyo, tulistahili kifo kwa ajili ya dhambi zetu, lakini Kristo akafa kwa niaba yetu. Tulistahili kifo; yeye akafa ili sisi tupate kuishi.

---

[275] Mathayo 22:46
[276] Marko 12:37

**Kukamatwa**

► Soma Mathayo 26:1-5, 14-56.

Siku ya Jumatano ya Mateso, Yesu alitabiri kifo chake "baada ya siku mbil." Baraza la Sanhedrini lilikuwa linapanga kumkamata Yesu baada ya umati wa hija ya Pasaka kuwa wamendoka katika jiji hilo, angalao siku tisa kutokea siku ya utabiri huu. Hata hivyo, wakati Yuda alipojitolea kumsaliti Bwana wake, waliamua kumkamata kwa ushirikiano na mfauasi wake mmoja.

Kwa nini makuhani wakuu walimhitaji Yuda? Walijua Yesu ni nani na wataweza kumpata mahali gani. Alikuwa akifundisha hekaluni kila siku. Viongozi wa Kidini walikuwa wanamhitaji Yuda aje atumike kama shahidi dhidi ya Yesu wakati wa kuendeshwa kwa mashtaka. Kwa kosa lolote kubwa lililohitaji hukumu ya kifo, sheria ya Kirumi inahitaji shahidi. Kwa kumsaliti Yesu, Yuda alikuwa anakubali kuwa shahidi wao. Baada ya kukamatwa, Yuda "alibadilisha mawazo yake" na viongozi wa Kiyahudi wakawa wamekosa shahidi wao nyota dhidi ya Yesu.[277]

Baada ya kushiriki chakula cha Pasaka na wanafunzi wake, Yesu alikwenda katika bustani ya Getsemani kuomba. Akifikiria jinsi ya kukabiliana na mateso ya mwilini katika msalaba na uchungu wa kutenganishwa kutoka kwa Baba yake, Yesu aliomba, "Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe." Hata katika mashtaka haya mazito, Yesu alijikabidhi kwenye mapenzi ya Baba yake.

> "Je alikuwa amepigwa?
> Ilikuwa kwamba kwa kupigwa kwake sisi tupate kupona.
>
> Je, alihukumiwa ingawaje hakuwa na hatia?
> Ilikuwa ni ili tufutiwe makosa yetu, ingawaje tulikuwa na makosa.
>
> Je, alivalishwa taji la miiba?
> Ilikuwa ni ili tuweze kuvaa taji la utukufu.
>
> Je, alivuliwa mavazi yake?
> Ilikuwa ni ili tuweze kuvalishwa haki ya milele.
>
> Je alichekwa na kukejeliwa?
> Ilikuwa ni ili tuweze kupewa heshima na kubarikiwa.
>
> Je, alitambuliwa kuwa mhalifu, na kuhesabiwa miongoni mwa wenye dhambi?
> Ilikuwa ni ili tusionekane wenye hatia, na kuhesabiwa haki kutoka katika dhambi zote.
>
> Je, alitangazwa kwamba hawezi kujiokoa mwenyewe?
> Ilikuwa ni ili aweze kuwaokoa wengine kwa kiwango cha mwisho kabisa.
>
> Je, mwishowe alikufa, na kwamba kilikuwa kifo cha maumivu makali na cha aibu sana miongoni mwa vifo vingine?
> Ilikuwa ni ili tuweze kuishi milele, na kuinuliwa kwenye kiwango cha utukufu wa juu sana."
>
> \- Askofu Ryle

Baadaye jioni ile ile, Yuda akaja na "kikosi kikubwa" ili kumkamata Yesu.[278] Baada ya Yuda kumtambuisha Yesu kwa njia ya kumbusu, Yesu alizungumza na wale askari. Wakati Yesu alipowaambia, "Ni mimi, walirudi nyuma, wakaanguka chini. "[279] Hili kundi kubwa la

[277] Mathayo 27:3-4, Marko 14:55-56
[278] Yohana 18:3 anatambulisha kikundi hiki kama "kikosi" au "divisheni" ya askari. Divisheni ya askari wa Kirumi kwa kawaida ilikuwa na wapiganaji 600.
[279] Yohana 18:6

askari lilikuwa na wasiwasi dhidi ya mtu aliyekuwa na uwezo juu ya kifo. Katika hili, Yesu ndiye aliyekuwa akisimamia mipango yote, na siyo wale maadui zake. Octavius Winslow, Mhubiri wa karne ya kumi na tisa aliandika, "Ni nani alimtoa Yesu ili afe? Siyo Yuda, kwa ajili ya fedha. Siyo Pilato, kwa ajiliyahofu. Siyo Wayahudi, kwa ajili ya wivu. Ni Baba aliyemtoa, kwa ajili ya upendo!"[280]

**Mashtaka**

► Soma Mathayo 26:57-27:26; Luka 22:54-23:25; Yohana 18:12-19:16.

"Yesu hakuomba unafuu katika Uungu wake kutokana na mateso ya wanadamu; alijikita kwenye maombi."
- Nukuu kutoka T.B. Kilpatrick

Kushtakiwa kwa Yesu kulihusisha kwa pamoja mashtaka ya Kiyahudi na mashtaka ya Kirumi. Sheria ya Kiyahudi ilikuwa inajali ubinadamu zaidi kuliko mifumo mingine yote ya kisheria ya zamani; sheria ya Kiyahudi ilitumia kila linalowezekana kuokoa uhai. Sheria ya Kirumi ilijulikana kwa kuwa na masharti magumu na akili ya kutambua mambo mengi. Hizi zilikua ni sheria kuu mbili za ulimwengu wa zamani, lakini hazikuweza kuwazuia watenda dhambi katika kumwua Mwana wa Mungu."

Masaa machache baada ya kukamatwa kwake, Yesu alikuwa na makesi ya kisheria sita ya kusikilizwa. Hii ni pamoja na mashtaka ya kidini ya Wayahudi, na mashtaka ya raia ya Kirumi. Wataalamu wa historia wanaelezea kwamba mashtaka ya kidini ya Kiyahudi yalikuwa siyo ya kisheria kwa mujibu wa sheria ya Kiyahudi.

Katika kuharakisha kwao kumhukumu Yesu, baraza la Sanhedrini:

- Liliendesha mashtaka usiku (kinyume cha sheria)
- Halikufuata taratibu za kawaida za mashtaka kabla ya kumkamta Yesu (kinyume cha sheria )
- Hawakuruhusu Yesu kuita mashahidi kwa ajili ya kujitetea (kinyume cha sheria )
- Waliharakisha mashtaka yafanyike kwa haraka sana kuliko sheria ya Kiyahudi ilivyokuwa inaruhusu. (kinyume cha sheria)

Kimsingi, haya yote yalifanyika ili Yesu asulubiwe msalabani na maiti yake iweze kuondolewa kabla ya Pasaka. Walimwua mwana kondoo wa Mungu ili kwamba waweze kula kondoo wa Pasaka katika utaratibu wao uliokuwa sahihi!

---

[280] Nukuu kutoka kwa John Stott, *The Message of Romans* (Westmont, Illinois: InterVarsity Press, 1994), 255.

***Mtiririko wa Mashtaka***

**(1) Kusikilizwa na Wayahudi mbele ya Anasi (Yohana 18:12-14, 19-23)**

Anasi alikuwa amechaguliwa kuwa kuhani mkuu wa maisha. Hata baada ya Warumi kumbadilisha Anasi na kumweka mkwewe Kayafa, Wayahudi wengi waliendelea kumwita Anasi kwa cheo chake cha zamani cha "Kuhani Mkuu." Huu usikilizwaji wa kwanza mbele ya Anasi haukuwa rasmi. Haukuwa na mashtaka au mashahidi.

**(2) Kusikilizwa na Wayahudi mbele ya baraza la Sanhedrini (Mathayo 26:57-68)**

Kusikilizwa kwa mara ya kwanza na zima la Sanhedrini litakuwa lilifanyika mapema ya saa 8:00 usiku. Ingawaje hawangeweza kuendesha mabhtaka halali ya kisheria kabla ya asubuhi, viongozi wa Kiyahudi walitaka jambo hili lifanyike kwa haraka. Ingawaje uendeshwaji wa mashtaka usiku haukuwa halali kisheria, Baraza la Sanhedrini lilifanya usikilizaji usiokuwa rasmi na likamwona Yesu kuwa na hatia ya kukufuru dini na wakaamua kwamba alistahili adhabu ya kifo.

**(3) Mashtaka rasmi ya Wayahudi mbele ya baraza la Sanhedrini (Luka 22:66-71)**

"Wakati siku ilipowadia," baraza la Sanhedrini lilisikiliza rasmi mashtaka kwa mujibu wa sheria, na likaamua rasmi kumhukumu Yesu kwa makosa ya kukufuru dini.

**(4) Kusikilizwa mara ya kwanza na Warumi mbele ya Pilato (Luka 23:1-5; Yohana 18:28-38)**

Warumi hawakuwa wametoa mamlaka kwa baraza la Sanhedrini kuwahukumu adhabu ya kifo wahalifu.[281] Ili wafanikiwe kupata hukumu ya kifo, viongozi wa Kiyahudi walibadilisha mashtaka yao kutoka kwenye kukufuru dini na kuwa mashtaka ya kisiasa ya kutaka kufanya mapinduzi. Walimshtaki Yesu wakisema, "Tumemwona huyu akipotosha taifa letu, na kuwazuia watu wasimpe Kaisari kodi, akisema kwamba yeye mwenyewe ni Kristo, mfalme."

Wakati wa msimu wa Pasaka, Wayahudi hawataweza kuingia kwenye majumba yeyote ya Warumi kwa hofu ya kunajisika, na kusababisha kuzuiwa kula Chakula cha Pasaka. Kwa kuwa watapaswa kuingia kwenye kasri la mfalme, Pilato aliendesha usikilizwaji wa mashitaka kwenye njia ya waenda kwa miguu nje ya lango la kasri ya mfalme.

**(5) Mashtaka kusikilizwa na Warumi mbele ya Herode Antipasi (Luka 23:6-12)**

Pilato alijua kwamba Yesu alikuwa hana hatia, lakini hakutaka kuwakasirisha viongozi wa Kiyahudi. Aliposikia kwamba Yesu "Huwataharakisha watu, akifundisha katika Uyahudi yote, tokea Galilaya mpaka huku," Pilato akaona amepata mahali pa kukwepea ili kutoka katika huu mtanziko. Wakati wa wiki la Pasaka, Herode Antipasi, mtawala wa Galilaya,

[281] Yohana 18:31

alikuwa Yerusalemu. [282] Kwa kuwa Yesu alikuwa mtu wa Galilaya, Pilato alitegemea kwamba Herode angetumika kama jaji katika shauri hili. Pilato akampeleka Yesu kwa Herode, lakini Herode alikataa kuingilia kati.

**(6) Hukumu ya mwisho ya Warumi mbele ya Pilato (Mathayo 27:15-26; Luka 23:13-25; Yohana 18:39-19:16)**

Wakati Yesu aliporejeshwa kwenye mahakama yake, Pilato alitafuta mbadala mwingine wa huo mtanziko. Pilato alijua kwamba Yesu alikuwa hana hatia: "Mtu huyu mmemleta kwangu kana kwamba anapotosha watu; nami, tazama, nimeamua mambo yake mbele yenu, ila sikuona kwake kosa lo lote katika mambo hayo mliyomshitaki."[283] Pilato hakuwa anataka amhukumu Yesu kifo, mtu aliyekuwa hana hatia.

Wakati viongozi walipomtishia kumpeleka Pilato kwa Kaisari kwa kukosa uaminifu, Pilato akahukumu kwamba haja yao ifanyike. Pilato alikuwa mtawala dhaifu. Katika mgogoro wa kwanza, Pilato aliruhusu askari kuingia Yerusalemu na sanamu ya mfalme mkuu. Kusanyiko kubwa la Wayahudi liliandamana mbele ya kasri la Pilato kwa siku tano. Alipotishia kuwauwa waandamanaji, walitangaza kwambawako tayari kufa kuliko kuiona sanamu ya Kaisari ndani ya Jiji Takatifu. Pilato alilazimika kusalimu kwa matakwa yao.

Kutokana na uzoefu huu, Pilato alikuwa na wasiwasi sana na Wayahudi. Zaidi ya hapo, mkubwa wake wa kazi kule Rumi, Sejani, hakuwa anaamini uwezo wa Pilato wa kuthibitiwatu katika nchi ya Yudea. Wakati viongozi walipotishia kumlalamikia Kaisari kama Pilato angemwachilia huru Yesu, "Basi ndipo alipomtia mikononi mwao ili asulibiwe."[284] Pilato akamhukumia Yesu adhabu ya kifo, siyo kwa sababu aliamini kwamba Yesu alikuwa na hatia, bali ni kwa sababu ya udhaifu wake mwenyewe.

***Wakati shauri likiwa linaendelea, Petro anamkana Yesu.***

Kwenye chakula cha Pasaka, Yesu alikuwa amemwonya Petro akimwambia, "Amin, amin, nakuambia, Jimbi hatawika hata wewe utakapokuwa umenikana mara tatu."[285] Sasa, wakati kesi ya Yesu lilipokuwa inaendelea kusikilizwa, Petro alimkana Yesu mara tatu.

Tunaposoma kuhusu anguko hili la aibu la Petro, tunapaswa tukumbuke kwamba Petro hakuwa peke yake aliyemkosea Yesu katika usiku ule. Ni Petro na Yohana peke yao waliohudhuria kwenye kesi ile usiku ule. Wanafunzi wengine wote walikuwa wamekimbia kwa ajili ya hofu.

---

[282] Wakati wa sikukuu ya Pasaka, kila afisa wa Kirumi katika Palestina alikuja Yerusalemu kutoa msaada endapo kungetokea machafuko.
[283] Luka 23:14
[284] Yohana 19:16
[285] Yohana 13:38

Ni wazi kabisa kwamba, Petro alikuwa anampenda Yesu. Lakini ni kwa nini alianguka? Awali, tulijifunza kuhusu kujaribiwa kwa Yesu ili kupata masomo ya kukabiliana na majaribu. Kutokana na anguko la Petro tunaweza kuona mambo ya kutuonya katika kutusaidia sisi kukabiliana na majaribu. Angalau sifa mbili zilichangia katika kuanguka kwa Petro:

**(1) Kujiamini kupita kiasi**

Wakati Yesu alipoonya kuhusu mashambulizi ya Shetani, Petro alijidai kwamba, "Wajapochukizwa wote kwa ajili yako, mimi sitachukizwa kamwe!"[286] Tunapojiamini kupita kiasi, tunakuwa kwenye hatari ya kuanguka. Tunaishi tu kwenye maisha ya ushindi ya Kikristo kupitia uweza wa Roho Mtakatifu. Kujiamini kupita kiasi ni hatua ya kwanza ya kushindwa kiroho.

**(2) Ukosefu wa maombi**

Akiwa Bustanini, Yesu aliwaonya wanafunzi wake, "Ombeni kwamba msiingie majaribuni."[287] Badala ya kuomba kwa ajili ya kupata nguvu za kukabiliana na jaribu lililokuwa linakuja mbele yake, Petro alilala.

Ukosefu wa maombi kwa vyovyote vile unapelekea anguko la kiroho. Haiwezekani kudumisha maisha endelevu ya ushindi wa Kikristo pasipokuwepo na umahiri wa maisha ya maombi. Shetani hujaribu kuwapata watumishi wa Kikristo wawajibike kwenye majukumu mbalimbali hadi kusiwepo na muda wa kuomba. Anajua kwamba kama tutakuwa hatuna muda wa kuomba kutokana na kuwajibikia majukumu yetu, haitatuchukua muda mrefu bila kuanguka.

► Rejea nyuma na uyaangalie tena maisha yako ya Kikristo na huduma. Fikiri maeneo ambayo ulianguka katika jaribu, au ni mahali gani ulipowahi kuwa karibu sana na kuanguka. Ni sababu zipi zilizokufanya uanguke au ukaribie kuanguka? Je, ulikuwa unakaribia kilele cha mafanikio katika huduma yako hata ukajiamini kupita kiasi? Je, ulikuwa unawajibika na majukumu mengi hata ukashindwa kuutumia muda wako kwa ajili ya maombi? Je, kuna mambo mengine ambayo yanaweza kutumika kama onyo katika dalili zinazoonekana kutuangusha baadaye?

***Wakati shauri likiendelea kusikilizwa, Yuda anajiua.***

Muda mfupi tu baada ya tukio la Petro kumkana Yesu, Mathayo anatoa maelezo ya kisa cha kujiua kwa Yuda. Alipoona matokeo ya yeye kumsaliti Yesu, Yuda aliamua kubadilisha mawazo yake akarejesha vile vipande vya fedha kwa makuhani wakuu na wazee, akisema. "Nalikosa nilipoisaliti damu isiyo na hatia."[288] Yuda akavitupa vile vipande vya

---

[286] Mathayo 26:35
[287] Luka 22:40
[288] Mathayo 27:3-4

fedha alivyokuwa amelipwa kwa ajili ya usaliti wake, kisha akaondoka; akaenda akajinyonga mwenyewe.[289] Yuda alichagua kujinyonga, kuliko akae na hatia katika maisha yake yote.

Maelezo ya Mathayo yanaweka toba ya Petro na majuto ya Yuda kama hali zinazokaribiana. Kaw pamojaPetro na Yuda walijutia matendo yao. Hata hivyo, Kwa ajili ya Yuda, Mathayo anatumia neno ambalo linaonyesha wazo la kubadilisha ufahamu wa mtu, na siyo la kawaida kwa ajili ya toba ya kweli. [290] Tofauti hii ni muhimu sana katika kuelewa jibu la watu wanapojisikia kwa ajili ya kutenda dhambi.

Paulo aliandika kuhusu tofauti ya majuto (huzuni inayoletwa kutokana na matokeo ya dhambi) na toba (huzuni kwa ajili ya dhambi yenyewe na badiliko la mwelekeo). Mtume Paulo aliandika, "Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti."[291]

"Huzuni ya kimungu" huleta toba ya kweli, ambayo mwisho wake ni wokovu na maisha. "Huzuni ya kidunia" huleta majuto, ambayo mwisho wake ni kujisikia mwenye hatia na kifo. Wote kwa pamoja Petro na Yuda walihuzunishwa na yale waliyotenda, lakini Petro peke yake alifanya toba ya kweli.

Yuda aliona matokeo ya usaliti wake akachagua kufa kuliko kuendelea kuishi kwa ajili ya aibu na kujisikia mwenye hatia; alikuwa na majuto, lakini hakutubu. Petro aliona matokeo ya kushindwa kwake akachagua kutubu kwa ukweli. Matokeo ya majuto ya Yuda yalikuwa ni kifo; matokeo ya toba ya Petro yalikuwa ni maisha yaliyoambatana na huduma iliyozaa matunda tele.

► Je, umeshawahi kuona watu waliojisikia kujuta kwa ajili ya dhambi, lakini hawakufanya toba ya kweli? Matokeo yake yalikuwaje? Katika mahubiri yetu, tunawezaje kuwaleta watu hadi wafikie kufanya toba ya kweli?

**Kusulubiwa**

► Soma Mathayo 27:27-54.

Yudea palikuwa mahali pa kusikitisha kwa askari wa Kirumi akipangiwa kazi huko. Watu waliwachukia askari wa Kirumi, na wakereketwa walipanga kuwauwa. Wakati wa Pasaka, jeshi lilikuwa likiwekwa kwenye tahadhari kubwa kwa ajili ya machafuko. Hakukuwa na kazi mbaya kwa askari. Wakati mfungwa wa Kiyahudi akiwa amehukumiwa kifo, wanajeshi huimwaga hasira yao dhidi ya mtu aliyehukumiwa kifo.

---

289 Mathayo 27:5
290 *metamelomai* badala ya *metanoia*
291 2 Wakorintho 7:10

Vitendo alivyofanyiwa Yesu – kupigwa, kudhihakiwa, kuvalishwa taji la miiba – kunadhihirisha ukatili wa askari walioichukia kazi yao, waliowachukia watu waliowazunguka, na waliokuwa wanafurahia wanapomwadhibu mtu ambaye hawezi kujitetea. Yesu alifikwa na mateso haya bila ya kutoa neno lolote la chuki kwa askari hawa waliomtesa.

Waandishi wengi wameitafakari taarifa ya kusulubiwa kwa kuangalia matamko saba ya Yesu akiwa pale msalabani. Maneno ya mwisho anayotoa mtu kabla hajafa huonyesha umuhimu wa huyo mtu. Akiwa anakabiliwa na kifo, Yesu alisema nini?

> "Ee upendo wa Mungu, umefanya nini! Mungu wa kuishi milele amekufa kwa ajili yangu! Mwana aishiye milele pamoja na Baba aliziweka dhambi zangu zote juu ya mti. Mungu aishie milele kwa ajili yangu amekufa: Bwana wangu, mpendwa wangu, amesulubiwa!
>
> Amesulubiwa kwa ajili yangu na yako, kuturudisha sisi waasi kwa Mungu. Amini, amini kumbukumbu ya kweli, wote mmenunuliwa kwa damu ya Yesu. Msamaha kwa mtiririko wote kutoka upande wake: Bwana wangu, mpendwa wangu, amesulubiwa!
>
> Mtazame, kila kitu kinampita, Mwana wa mfalme wa maisha na amani anatokwa na damu, njooni wenye dhambi, mwoneni mkombozi wenu akifa, na mseme, ‘kulishakuwepo na huzuni tena kama yake?’ Njooni, mjisikie pamoja nami damu yake imetumika: Bwana wangu, mpendwa wangu, amesulubiwa!”
>
> - Charles Wesley

***Maneno ya kusamehe***

Walipokuwa wakimpigilia kwa misumari msalabani, Yesu aliomba, “Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo.”[292] Alionyesha upendo na kusamehe hadi mwisho wake

Kwa yule mwizi aliyestahili adhabu ya kifo, Yesu alimwahidi, “Amin, nakuambia, leo hivi utakuwa pamoja nami peponi.”[293]

***Maneno ya Huruma***

Yesu alimwusia Yohana amwangalie mama yake wakati aliposema, “Mama, tazama, mwanao!” na kwa Yohana, “Tazama, mama yako!”[294] Mapema kabla ya hapo, Yesu alikuwa amefundisha kwamba uhusiano wa kina wa familia ni wa kiroho, “Tazama, Mama yangu na ndugu zangu! Kwa maana ye yote atakayeyafanya mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni, huyu ndiye ndugu yangu, na umbu langu, na mama yangu.”[295]

Wakati wa kifo chake, ndugu zake wa kimwili walikuwa bado hawajaamini; hawakuwa sehemu ya familia yake ya kiroho. Kwa hiyo, Yesu alimwacha mama yake chini ya uangalizi wa kaka yake wa kiroho, Yohana Mpendwa.

---

[292] Luka 23:34
[293] Luka 23:43
[294] Yohana 19:26-27
[295] Mathayo 12:49-50

***Maneno yaliyohusiana na kuteseka kwa mwili***

Kule kuwa Mwana wa Mungu hakukumwondolea Yesu maumivu ya kimwili ya msalaba. Aliteseka kwa maumivu yote ya kimwili ya mhalifu aliyehukumiwa kifo. Baada ya kukaa kwa masaa bila ya kunywa maji katika lile joto kali, Yesu akasema, "Naona kiu." [296]

***Maneno ya uchungu wa kiroho***

Mathayo na Marko wana kumbukumbu ya tamko moja tu, lakini haya maneno yumkini ndiyo yaliyokuwa ya kuumiza moyo zaidi kutokea pale msalabani: "Eloi, Eloi, lama sabakthani? Yaani, Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?"[297]

Kwa hakika uchungu mkubwa wa Yesu aliokuwa nao ni kutengwa na Baba yake. Baba na Mtoto waliishi kwenye ushirika ambao haujawahi kuvunjika tangu milele. Sasa kwa sababu alibeba dhambi zetu, Yesu alitengwa na Mungu.

Akiwa juu ya msalaba, Mungu "alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye."[298] Katika Isaya 53, nabii alizungumzia kuhusu "mtumishi anayeteseka" ambaye atazichukua dhambi zetu.[299] Paulo anaelezea kwamba huu mbadala wa upatanisho wa Mungu na binadamu kwa maisha na kifo cha Yesu ulikamilishwa pale juu ya msalaba.

Yesu alifanyika dhambi kwa ajili yetu "ili kwamba kwa kupitia kwake tufanyike wenye haki wa Mungu. Hatupo tena kwenye utumwa wa dhambi; kupitia kifo cha Yesu, tumefanywa wenye haki. Paulo hasemi tu kwamba "katika yeye" tunaitwa wenye haki. Badala yake alisema, "ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye." Kupitia kazi ya Yesu juu ya msalaba, mabadiliko ya kweli yanachukua nafasi. Yesu alifanyika kuwa dhambi kwa ajili yetu ili sisi tuweze kuwa wenye haki.

***Maneno ya kujiweka chini ya madaraka***

"Ee Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu!"[300] Katika maisha yake yote, Yesu aliishi kwenye mahusiano ya uaminifu na Baba yake. Akiwa anakabiliana na msalaba, aliomba, akasema, "walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe."[301] Wakati huu alitoa tamko hili la mwisho la kujisalimisha kabisa kwenye mapenzi ya Baba yake.

---

[296] Yohana 19:28
[297] Mathayo 27:46; Marko 15:34
[298] 2 Wakorintho 5:21
[299] Isaya 53:4-12
[300] Luka 23:46
[301] Mathayo 26:39

### *Maneno ya ushindi*

"Imekwisha."[302] Kwa kilio hiki cha ushindi, Yesu alitangaza kwamba amemaliza kazi ambayo Baba alimtuma kuifanya. Adhabu ya dhambi ililipwa; Shetani alishindwa. Upatanisho uliokuwa unafanywa kama kivuli cha upatanisho ujao kupitia kondoo katika Agano la Kale na kuahidiwa katika Isaya 53 ulikamilishwa.

### Mazishi

► Soma Mathayo 27:57-61.

Kwenye ujumbe Paulo kwa Wakorintho, alihubiri kwamba Yesu "alikufa kwa ajili dhambi zetu" na "kwamba alizikwa."[303] Kwa Paulo na kanisa la mwanzo mazishi yalikuwa ni jambo la muhimu sana.

Wachunguzi wengi wa Wiki la Mateso wametoka kwenye Ijumaa ya Pasaka hadi kwenye Jumapili ya Pasaka. Lakini zaidi kwa ajili ya historia ya kanisa, "Jumamosi ya Pasaka" ilitambuliwa kama sehemu muhimu ya Mkesha wa Pasaka. Kuna umuhimu gani katika haya mazishi?[304]

### *Umuhimu wa kihistoria*

Mazishi yanaonyesha kwamba Yesu ni kweli alikufa. Kinyume kabisa na madai ya dini ya Kiislamu kwamba Yesu alikuwa "amezimia" na baadaye akaamka, mazishi yanadhihirisha wazi kwamba Yesu ni kweli alikufa. Warumi walijua sana jinsi ya kumwua mfungwa aliyehukumiwa adhabu ya kifo. Hakuna uwezekano wowote kwamba wangeweza wakamchukua mtu kutoka kwenye mti aliosulubishwa kabla hajakata roho.

Zaidi ya hayo, jiwe kubwa lililokuwa langoni na walinzi wa kaburi ilikuwa ni uhakikisho kwamba hakuna mtu angeweza kutoroka kutoka kwenye kaburi. Hata kama kwa makosa Warumi watakuwa wamemzika Yesu kabla hajafa, ni jambo lisiloweza kufikirika kwamba mtu ambaye alikuwa ameumizwa na kuteseka kwa masaa ya maumivu juu ya msalaba angeweza akajifungua kutoka kwenye sanda, akasukuma jiwe kubwa lililokuwa limewekwa langoni, na kisha kukizidi nguvu na kukishinda kikosi cha walinzi waliopitia mafunzo. Mazishi yanathibitisha ukweli wa historia kwamba Yesu wa Nazarethi alikufa.

---

[302] Yohana 19:30
[303] 1 Wakorintho 15:3-4
[304] Nukuu kutoka kwa, "The Burial of Jesus." Inapatikana kutoka https://www.alliancenet.org/tab/the-burial-of-jesus-christ-part-one on March 22, 2021.

### *Umuhimu wa Kinabii*

Akiandika kuhusu kondoo anayepelekwa kwenda kuchinjwa, Isaya aliandika, "Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; Na pamoja na matajiri katika kufa kwake."[305] Mazishi ya Yesu yalihitimisha unabii wa Masihi.

Baada ya Yesu kufa, Yusufu wa Armathaya alikwenda kwa Piato akiomba kuuchukua mwili wa Yesu. Yusufu alikuwa mjumbe katika baraza la Sanhedrini, lakini hakukubaliana na maamuzi ya kumwua Yesu. Hata baada ya kuwa viongozi wengi walimjeuka Yesu wakaenda kinyume naye, "baadhi yao walikuwa "wakiutafuta ufalme wa Mungu." Yusufu alikuwa mmoja wa hawa wanafunzi wa siri. Yusufu na Nikodemo waliuzika mwili wa Yesu kwenye kaburi la Yusufu.[306]

Jaribu kufikiria ujasiri waliouchukua. Hata baada ya wanafunzi kuwa wamekimbia wakamwacha Yesu, Yusufu alisonga mbele kujitambulisha na mhalifu aliyehukumiwa kifo. Hii hali ya kujionyesha hivi hadharani kuliatarisha nafasi ya Yusufu kenye baraza la Sanhedrini na msimamo wake katika jamii. Kuna uwezekano mkubwa kwamba alikuja kuondolewa kwenye nafasi yake katika baraza la Sanhedrini kama gharama ya kujitambulisha hadharani na Yesu

Zaidi ya hapo, Yusufu alihatarisha hasira kutoka kwa Pilato. Maafisa wa Kirumi mara chache sana waliruhusu familia kufanya mazishi ya miili ya ndugu zao waliohukuiwa kifo kwa kusulubiwa. Miili yao ilitakiwa ibakie hapo kwa ajili wananchi wote kuona kama onyo kwa wahalifu wengine. Kibali cha Pilato ni ushahidi mwingine kwamba Pilato alijua Yesu hakuwa na hatia ya kosa lolote.

### *Umuhimu wa Kitheolojia*

Paulo alilinganisha ubatizo wetu na mazishi ya Yesu:

> Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.[307]

Mazishi yalikuwa ni uthibitisho kwa umma wa kifo cha Yesu. Kwa jinsi hiyo –hiyo, ubatizo ni uthibitisho kwa umma wa ushiriki wetu katika kifo cha Yesu. Katika ubatizo, tunatangaziwa mauti ya mfumo wetu wa maisha ya zamani.

> "Kurudia kwenye dhambi wakati umeshaunganishwa na Kristo ni sawa na kuchimbua mwili uliokufa."
> - James Boice

---

[305] Isaya 53:9
[306] Mathayo 27:57-60; Marko 15:42-46; Luka 23:50-54; Yohana 19:38-42
[307] Warumi 6:3-4

Mazishi ni hatua ya mwisho ya kutambua kifo cha mtu. Katika nchi za Magharibi, waombolezaji hutupa udongo juu jeneza lililoshushwa kaburini ikiwa ni mwisho wa kusema "kwaheri" katika dunia hii. Paulo anaweka mkazo wa kufikia mwisho wa kifo chetu kwa sababu ya dhambi. Kama Kristo alivyokuwa amekufa, na sisi tumekufa kwa dhambi. Kurudia kwenye dhambi baada ya kuwa tumeshazikwa pamoja na Kristo ni sawa na kuchimbua mwili uliokufa. Tumezikwa na Kristo; hatuko tena hai kwa dhambi.

## Kufufuka

Paulo alihubiri katika Korintho kuhusu msalaba; Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu na alizikwa. Kisha, Paulo akahubiri kuhusu kufufuka; Kristo alifufuka siku ya tatu na akawatokea mashuhuda wengi.[308] Kufufuka ndio msingi mkuu wa imani ya Kikristo.

► Soma Mathayo 27:62-28:15.

Mathayo 27:62-66 ni sehemu moja wapo ya matukio yangu ninayoyapenda katika maelezo ya Pasaka. Mapema, wakati viongozi wa kidini wa Kiyahudi walipomtaka Pilato abadilishe lile bango lililokuwa juu ya masalaba, aliwakatalia. Alimsulubisha Yesu chini ya bango lililosomeka, "Yesu Mnazareti, Mfalme Wa Wayahudi."[309] Kwa kutumia tangazo hili kwa mtu aliyehukumiwa kifo kwa uhalifu, Pilato alikuwa akiwadhihaki Wayahudi ambao aliwakasirikia.

Baada ya kusulubiwa msalabani, viongozi wa kidini wa Kiyahudi walirudi tena kwa Pilato wakiomba walinzi wa Kirumi kulilinda kaburi:

> Bwana, tumekumbuka kwamba yule mjanja alisema, alipokuwa akali hai, Baada ya siku tatu nitafufuka. Basi amuru kwamba kaburi lilindwe salama hata siku ya tatu; wasije wanafunzi wake wakamwiba, na kuwaambia watu, Amefufuka katika wafu; na udanganyifu wa mwisho utapita ule wa kwanza.

Charles Spurgeon alitoa maoni yake kwamba Pilato alikuwa akiwadhihaki tena viongozi wa kidini wa Kiyahudi wakati alipowajibu kwamba, '"Mna askari; nendeni mkalilinde salama kadiri mjuavyo.' *Lakini kama kweli ndiye yeye kama alivyosema ndiye, atatoka kaburini, hata ufanye nini!"*

Je, ni kweli viongozi walikuwa na mashaka kwamba wanafunzi watauiba mwili wa Yesu? Inawezekana sivyo. Waliwaona wanafunzi wakiwa wamekimbia kwa ajiliya hofu; walijua kwamba wanafunzi wake hawakuwa na ujasiri wa kuweza kuiba ule mwili. Kama huu ndio uliokuwa wasiwasi wao, baraza la Sanhedrini wangetoa amri ya kukamatwa kwa wale viongozi wa wanafunzi. Suala la wanafunzi kuwa tishio kwao halikuwepo.

---

[308] 1 Wakorintho 15:3-8
[309] Yohana 19:19

Sasa, ni kwa nini waliomba huyu mlinzi? Yesu alishatabiri kwamba atafufuka kutoka katika wafu. Walishaona uwezo wake juu ya kifo wakati alipomfufua Lazaro kutoka katika wafu. Je, inawezekanaje kwamba viongozi wa Kiyahudi walikuwa na mashaka kwamba Yesu atafanya lile ambalo alikuwa ameahidi atalifanya?

Kwa kibali cha Pilato, walilitia muhuri kaburi, na wakaweka walinzi kutoka katika kampuni iliyokuwa imetuma askari kwenda kumkamata Yesu bustanini. Ghafla:

> Palikuwa na tetemeko kubwa la nchi; kwa sababu malaika wa Bwana alishuka kutoka mbinguni, akaja akalivingirisha lile jiwe akalikalia. Na sura yake ilikuwa kama umeme, na mavazi yake meupe kama theluji. Na kwa kumwogopa, wale walinzi wakatetemeka, wakawa kama wafu.

Yesu alikuwa amefufuka!

► Soma Yohana 20:1-29.

Vitabu vya Injili vimeandika kumbukumbu ya kuonekana kwa Yesu baada ya kufufuka. Alionekana kwa watu wengi katika mazingira mengi tofauti.

Watu wenye kushuku mambo mara nyingine wanasema, "Wanawake waliokuwa pale kaburini walikuwa wanaota njozi. Waliona walichotegemea kukiona." Hata hivyo, mashuhuda hawa *hawakutegemea kumwona Yesu akiwa hai;* walijua alikuwa amekufa. Kwa maana hawajalifahamu bado andiko, ya kwamba imempasa kufufuka. [310] Hata pale mashuhuda wa kwanza waliposema kwamba walimwona Yes, wanafunzi wengine walitilia shaka taarifa hiyo. [311] Hawakumtegemea Yesu afufuke kutoka katika wafu.

Hatua kwa hatua, akajionyesha kwa Mariamu Magdalena, [312] kwa wanafunzi wawili waliokuwa wakielekea Emmau, [313] kwa Thenashara, [314] Ndugu zaidi ya mia tano pamoja, [315] wafuasi wa Yesu walitambua kwamba ni kweli Yesu amefufuka. Kanisa la mwanzo likaanza ibada za kusifu kwa maneno haya, "Amefufuka, Amefufuka kweli kweli!"

"Nendeni mkalilinde salama kadiri mjuavyo," yalikuwa maagizo ya Pilato. Kitambo siyo kirefu, Pilato anatambua kwamba hakuna mtawala yeyote wa dunia hii ambaye angeweza kushinda uwezo wa Yesu wa kufufuka. Amefufuka, Amefufuka kweli kweli!

### Matumizi: Huduma katika nguvu ya Msalaba na Kufufuka

Wengi wa wanatheolojia huru wamejaribu kupasisha kwamba ufufuo ni hadithi. Hata hivyo, imani ya wanafunzi ilikuwa haijajengwa kwenye "hadithi nzuri zenye mvuto wa

---

[310] Yohana 20:9
[311] Marko 16:13
[312] Yohana 20:11-18
[313] Luka 24:13-32
[314] Yohana 20:19-31
[315] 1 Wakorintho 15:6

kudumu wa maisha ya Yesu," bali katika kweli halisi za kifo chake na kufufuka. Mitume walijua kwamba Yesu alikufa na kwamba amefufuka kutoka kwa wafu. Hii iliwapa ujasiri wa kukabiliana na mateso ikibidi hata kama ni kufa. Je, ni kwa jinsi gani kifo na kufufuka kwa Yesu kunagusa huduma zetu leo?

**Kufanya Huduma ndani ya Nguvu ya Msalaba**

► Soma 1 Wakorintho 1:17-2:5.

Kwenye safari yake ya pili ya umishenari, Paulo alisafiri hado Korintho akitokea Athene alipokuwa amehubiri katika Aeropagi. Inaonekana kwamba Paulo alipata matokeo kidogo sana katika huduma yake pale Athene. [316] Hakuanzisha kanisa pale Athene, na wanafalsafa wa Athene walidhihaki ujumbe wake wa kufufuka. Kutoka Athene, Paulo alisafiri kilomita sabini na tano Magharibi mwa Korintho, kwenye mji uliokuwa na ushawishi sana katika jimbo la Akaya.

Paulo alikuja hadi Korintho baada ya upinzani wa mfululilizo wa majiji matatu: Thesalonike, Beroa na Athene. Labda ndiyo maana alisema, "Nami nalikuwako kwenu katika hali ya udhaifu na hofu na matetemeko mengi." Ingawaje wasikilizaji wa Kiyunani walikuwa wanahitaji lugha ya kushawishi na upeo wa akili inayong'ara, Paulo alikusudia kuhubiri habari za msalaba tu. Nguvu iliyokuwa katika ujumbe wake haikutokana na maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kutoka kwenye msalaba wenyewe. Paulo alihubiri "siyo kwa ufasaha wa maneno, wala kwa hekima, usije msalaba wa Kristo ukapunguzwa nguvu zake."

Akiwa Korintho, Paulo alisema, "naliazimu nisijue neno lo lote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulibiwa." Paulo alijua kwamba ujumbe wa Msalaba utawakera watu wengi.

> Kwa sababu Wayahudi wanataka ishara, na Wayunani wanatafuta hekima; bali sisi tunamhubiri Kristo, aliyesulibiwa; kwa Wayahudi ni kikwazo, na kwa Wayunani ni upuzi.

Ujumbe huu ulikuwa ni "kikwazo" au "kashfa" kwa Wayahudi. Walikuwa wanataka "ishara" ambazo zilimhalalisha Masihi. Kwa akili zao, wazo kwamba mtu ambaye amesulubishwa anaweza kuwa ndiye Masihi aliyechaguliwa lilikuwa la kipumbavu. Sheria ilisema, "aliyetundikwa amelaaniwa na Mungu. "[317] Kusema kwamba Yesu aliyeangikwa msalabani alikuwa Masihi ni kashfa nzito kwa wasikilizaji wa Kiyahudi.

Neno la msalaba kwa "mataifa lilikuwa ni upuuzi." Wayunani waliheshimu sana adhabu ya kifo cha mateso cha shahidi mfia dini. Ingetokea Yesu kuuawa katika mapambano dhidi ya Warumi, Wayunani mahiri wangemtunuku nishani ya heshima kwake ambaye amekuwa na ujasiri kutekeleza tendo hilo. Lakini kusulubiwa msalabani kulimwondolewa heshima

---

[316] Matendo 17:16-34
[317] Kumbukumbu la Torati 21:23

kabisa mhusika; hiki hakikuwa kifo cha kuweza kumtunuku mtu heshima. Waliopatikana na adhabu ya kufa kifo cha msalaba kwa kawaida walinyimwa haki ya kuzikwa kwa heshima kama watu wengine. Miili yao iliachwa iliwe na ndege wa angani au panya, na mifupa yao kutupwa katika shimo la uchafu. Kwa hali hiyo, kudai kwamba raia wa Kiyahudi aliyehukumiwa kufa msalabani alikuwa Bwana" lilikuwa ni jambo la kipumbavu (au upuuzi) kwa wasikilizaji Mataifa.

Msalaba kwa Wayahudi ulikuwa ni "kikwazo" na kwa Mataifa ni "upuzi," lakini Paulo alihubiri ujumbe wa msalaba bila ya kusita. Mfano wa Paulo ni wa kuigwa na sisi. Kwa wakati huu, kama ilivyokuwa katika karne ya kwanza, msalaba utawakwaza baadhi ya watu, na pia kuonekana kama ni upuuzi kwa watu wengine, lakini ndio ujumbe tunaotakiwa tuhubiri.

Ujasiri wetu kama wahudumu na viongozi wa kanisa hauji kutokana na uwezo tulio nao; ujasiri wetu uko katika msingi wa neno la msalaba. Paulo alikuwa msomi wa elimu ya juu sana, akili ya kipaji, na alikuwa na uwezo wa kuhojiana na wasomi waliobobea wa wakati wake. Lakini ujasiri wake wa mwisho ulikuwa kwenye msalaba. Tunapowapata watu kwa njia ya mahojiano ya kawaida peke yake, imani yao inaweza "kuegemea kwenye hekima ya watu"; lakini tunapowaelekeza kwenye msalaba, imani yao inabakia "kwenye uweza wa Mungu."

**Kuhudumia katika Nguvu Ya Kufufuka**

► Soma Matendo 2:22-36.

Kitabu cha Matendo kinaonyesha kwamba kufufuka kulikuwa ndio kiini cha mahubiri ya Wakristoo wa mwanzo. Wakati wa Pentekoste, Petro anaonyesha kufufuka kama ushahidi kwamba Yesu alikuwa ndiye mkamilishaji wa ahadi zilizokuwa zimetolewa na manabii.

Akijitetea mwenyewe mbele ya Agripa, Paulo alitoa kauli kwamba alikuwa kwenye mashtaka "kwa ajili ya tumaini la ahadi baba zetu waliyopewa na Mungu, ambayo kabila zetu kumi na mbili wanataraji kuifikia." Ahadi hii ilikuwa ni nini? Kufufuka. "Kwa nini limedhaniwa kwenu kuwa ni neno lisilosadikika, kwamba Mungu awafufua wafu?"[318]

► Soma 1 Wakorintho 15:12-34.

Katika 1 Wakorintho, Paulo anaonyesha kwamba huduma yake imejengeka siyo tu kwenye nguvu ya msalaba, bali katika nguvu ya kufufuka. Paulo anatoa msisitizo kwamba mbali na kufufuka, huduma yake itakuwa haina maana yeyote. "Tena kama Kristo hakufufuka, basi, kuhubiri kwetu ni bure na imani yenu ni bure." Kusingekuwepo na kufufuka, Yesu angekuwa siyo chochote zaidi ya Masihi aliyeshindwa. Pasipokuwepo na

[318] Matendo 26:6-8

kufufuka, Yesu angekuwa ni mfia dini aliyesababisha majonzi, lakini siyo Masihi aliyeahidiwa.

Kufufuka ndio msingi wa imani yetu ya Kikristo. "Na kama Kristo hakufufuka, imani yenu ni bure; mngalimo katika dhambi zenu." Akiwa juu ya msalaba, Yesu alileta upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu, lakini ilikuwa ni ufufuo uliothibitisha nguvu ya Kristo dhidi ya kifo na dhambi. Kama hakuna ufufuo, Paulo anasema, imani yenu ni bure; mngalimo katika dhambi zenu.

Kufufuka ndio msingi wa matumaini yetu ya Kikristo. "Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu, kadhalika na kiyama ya wafu ililetwa na mtu. Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa." Paulo anawahakikishia Wakorintho kwamba wanayo matumaini ya kufufuka *kwa sababu* Kristo naye alifufuka kutoka katika wafu.

Katika karne ya pili, Lucian, mwandishi wa riwaya wa Kigiriki, aliwadhihaki Wakristo kwa ajili ya Imani yao katika kufufuka.. Alisema, "Ha maskini fukara wanashawishika kwamba wataishi milele. Kwa sababu ya hiyo, wanakidhalilisha kifo na wako tayari kutoa dhabihu maisha yao kwa ajili ya imani yao." Lucian alikuwa akiwadihaki Wakristo, lakini maneno yake yalikuwa ya kweli. Kama Lucian alivyosema, Wakristo wa karne ya pili waliamini kwamba wataishi milele. Kwa sababu ya imani hiyo, walikuwa tayari kufa kwa ajili ya imani hiyo.

Hii inapasa iwe kweli hata wakati wa sasa. Kama kweli tunaamini kwamba Kristo amefufuka kutoka kwa wafu, itatupa ujasiri wakati wa kukutana na mateso au hata kifo. Kufufuka ndio kiini cha imani yetu ya Kikristo.

Kufufuka ndio msingi wa maisha yetu ya Kikristo. Paulo analeta matumizi ya vitendo ya kushangaza kuhusiana na imani ya kufufuka. "Wasipofufuliwa wafu, na tule, na tunywe, maana kesho tutakufa…Tumieni akili kama ipasavyo, wala msitende dhambi."[319] Kwa mujibu wa Paulo, kufufuka kunatupa sababu muhimu ya kuishi maisha ya kimungu. Kama hakungekuweko na kufufuka, tungeweza tukaishi kama Epicureans waliosema kwamba, "Tule na tunywe kwa sababu tutakufa hvi karibuni." Hakuna sababu ya kuishi kwa ajili ya milele kama hakuna kufufuka. Lakini, Paulo anaendelea, kwa kuwa kufufuka kupo, amka na uishi maisha yasiyokuwa na dhambi. Ushindi wetu dhidi ya dhambi unapewa msukumo na matumaini yetu katika kufufuka.

Kisa hiki cha kufufuka kinapaswa kituhukumu sisi kwa sababu ya ukosefu wetu wa imani tunapokutana na changamoto katika huduma zetu. Mara nyingi tunatarajia Mungu hatajibu maombi yetu. Kwa nini? Kwa sababu tumesahau nguvu ya kufufuka. Ni mara ngapi tunakutana na majaribu tukiwa na matumaini madogo ya kushinda? Kwa nini? Kwa

[319] 1 Wakorintho 15:32-34

sababu tunasahau ahadi ya Paulo: "Lakini, ikiwa Roho yake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu."[320]

Kama Kristo anaishi ndani yetu, hatuishi tna katika mwili:hatuko tenakama watumwa wa dhambi. Haya ni maisha yaliyo katika nguvu ya kufufuka. Nguvu ile iliyomfufua Kristo kutoka katika kaburi inatupa ushindi wa kila siku dhidi ya dhambi. Hii ndiyo maana ya kuishi na kuhudumia kwa nguvu za kufufuka.

## Hitimisho: Alama za Maisha yanayomfanania Kristo na Huduma

### Je, Maisha Yako Yanafanana na Kristo?

Luka aliandika," Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia."[321] Jinsi watu walivyokuwa wanawaangalia waamini wa Antiokia walianza kusema, "Hawa watu wanafanya kama Kristo. Tuwaite 'Wakristo.'" Ninapoisoma aya hii, mara nyingi hujiuliza mimi mwenyewe, "Je, majirani zangu wanaweza kuingia katika jina hili la "Mkristo" kwa kuiangalia tabia yangu, maneno yangu na mwenendo wangu? Je, ninaonekana kama Kristo? Waamini pale Antiokia waliishi maisha ambayo yaliakisi tabia ya Yesu Kristo; walikuwa Wakristo.

Baada ya miakamingi kama mchungaji, Dr. H.B. London kwa sasa anatumika kama mnasihi wa wachungaji vijana. Alionya kuhusu hatari za kiroho ambazo wachungaji hukutana nazo. "Mmoja anaweza kuwa karibu na vitu vitakatiu, lakini yeye mwenyewe asiwe mtakatifu. Inawezekana kuhubiri kuhusu kusamehe, na usiwe mtu wa kusamehe. Watumishi wengi wanaweza kutumia nguvu nyingi sana katika huduma kiasi kwamba wanazembea afya ya roho zao."[322] Inawezekana kuwahubiria watu wengine kasha ukawa mtu wa kukataliwa.[323]

Dr. London alipendekeza baadhi ya mambo ya vitendo yanayoweza kuwasaidia wachungaji kuepukana na kushindwa kiroho wakati wanapoongoza watu wengine. Haya ni maeneo ambayo yanaweza kutusaidia kudumisha maisha yanayomfanania Kristo. Aliandika kama ifuatavyo:

- **Ishi kile unachokihubiri.** Usihubirie watu wengine kile ambacho wewe hujakifanyia kazi kwanza kwenye maisha yako mwenyewe
- **Jali nafsi yako**. Madaktari wengine hawana afya. Wanajali kuangalia afya za watu wengine na wanazembea kuangalia afya zao wenyewe. Baadhi ya wachungaji

[320] Warumi 8:11
[321] Matendo 11:26
[322] H. B. London, *They Call Me Pastor.* (Grand Rapids: Baker Books, 2000), 145
[323] 1 Wakorintho 9:27

hawana afya ya kiroho. Kama mchungaji, tumia muda wako kutunza afya yako ya kiroho.

- **Kuwa mnyenyekevu**. Kumbuka kwamba mchungaji ni kama mchungaji wa kondoo, na siyo raisi wa benki. Kuwa mtumishi
- **Jiongeze katika mambo yanayokatisha tamaa**. Utakatishwa tama katika huduma. Mtu Yule unayemnasihi atakwenda kinyume chako. Rafiki yako wa karibu atakujeuka. Wafuasi wa kanisa lako watakukataa. Usiruhusu mambo haya ya kukatisha tamaa yakufanye upoteze matumaini. Yuda alimsaliti Yesu. Dema alimsaliti Paulo. Kupitia maombi ya machozi, endelea kukua na kulichunga kundi lako la kondoo.

**Je, Huduma yako inamfanania Kristo?**

Katika masomo haya ya maisha na huduma ya Yesu, tumeona tabia nyingi zahuduma ya Yesu. Je, tabia hizi zinaonekana katika huduma yako?

Hapa kuna maswali ya kujiuliza katika kufanya tathmini ya huduma yako:

- Je, wenye dhambi wanatubu? Wakati Yesu alipohubiri, watu walipokea maisha mapya. Je, wewe unawaleta watu kwenye maisha mapya ya wokovu?
- Je, waamini wanajazwa na Roho Mtakatifu? Yesu aliahidi "kumtuma Roho" kwa watoto wake, Je, ahadi hii inakamilishwa miongoni mwa wale unaowahudumia?
- Je Shetani anashindwa? Je, ngome kuu za Shetani zinavunjwa? Huduma ya Yesu ilifahamika kwa kuwa na mamlaka ya kiroho.
- Je, watu walioumizwa wanapata uponyaji? Je, familia zilizosambaratika zinapata suluhisho la marejeano? Je, maisha yaliyoharibika yanarejeshwa tena kwa upya? Je, mahusiano yaliyoharibika yanarejeshwa? Yesu aliwaponya watu waliokuwa wameumizwa kimwili, kimhemuko na vidonda vya kiroho.
- Je watu wanaona neema na ukweli? Je, ninawavutia watu kuja kwa Yesu au ninawatolea nje mbali na Yesu? Yesu alifundisha ukweli ulioleta kujisikia mwenye hatia na neema.

► Unapokuwa katika kujadili maswali haya, angalia maeneo ambayo huduma yako inaweza ikakua katika kumfanania Kristo. Kumbuka kwamba kila mhudumu anao uwanja wa kukulia, kwahiyo chukua orodha hii kama changamoto yako ya kukulia kuliko kuifanya iwe ya kukuhukumu wewe mwenyewe.

**Kazi za Somo la 8**

(1) Andaa mahubiri au somo la Biblia kuhusu Maneno Saba ya Msalabani. Wekea mkazo wa ujumbe wa maneno haya ya Yesu kwa Wakristo wakati wa sasa.

(2) Andaa mahubiri au somo la Biblia kuhusu maana ya kufufuka kwa maisha ya kila siku ya Mkristo. Tumia kwa pamoja maelezo ya kufufuka kutoka katika Vitabu vya Injili na maneno ya Paulo katika 1 Wakorintho 15:15-17 kwenye maandalizi yako.

# Somo la 9
# Kuacha Urithi

## Malengo ya Somo

Kufikia mwisho wa somo hili, kila mwanafunzi atapaswa:
(1) Kuelewa urithi wa mwisho wa Yesu kwa wanafunzi wake na kanisa.
(2) Kutambua umuhimu wa umisheni ulioko katika urithi wa Yesu
(3) Kukubaliana na matokeo endelevu ya huduma ya Yesu kupitia wanafunzi wake katika Kitabu cha Matendo
(4) Kukuza hatua za vitendo za kuacha urithi wa huduma yako wenyewe.

## Kanuni za Huduma

Kipimo cha huduma yetu ni kile tunachokiacha nyuma tutakapokuwa hatupo tena kwenye huduma.

## Utangulizi

Tim alikuwa anakaribia kustaafu baada ya miaka mingi ya utumishi kama mchungaji aliyepata kuheshimiwa. Nilimwuliza, " Unaliandaaje kanisa katika kustaafu kwako? Ni nini maono ya kanisa kwa miaka kumi ijayo? Jibu lake lilinifanya nikapigwa na bumbuazi. " Sitakuwepo tena hapa. Kwa hiyo sina cha kujali ni nini kitakachotokea baada ya kuwa nimendoka." Huyu mchungaji :hakuwa ameelewa kanuni muhimu ya huduma: kipimo cha mwisho cha huduma zetu ni kile kinachofanyika baada ya sisi kuondoka.

Fanya ulinganifu wa huyu mchungaji na mchungaji mwingine aitwaye Pete. Pete alifariki ghafla baada ya miaka ishirini na tano ya huduma. Wakati wa miaka hiyo, Pete alikuwa ameongoza huduma nyingi katika kanisa lake. Alikuwa ameanzisha huduma kwa watu wasio na makazi, programu ya kuhudumia walioathirika na madawa ya kulevya, na makongamano kwa ajili ya viongozi wa wafanyabiashara. Kwenye mazishi ya Pete, kiongozi wa huduma ya kushughulikia waathirika wa madawa ya kulevya alisema, "Mwezi uliopita, Pete na mimi tulijadiliana kuhusu bajeti ya mwaka ujao." Kiongozi wa huduma ya wasiokuwa na makazi alitoa ramani ya jengo jipya kwa ajili ya makazi ya familia hizo. Kwa uangalifu mkubwa, Pete alikuwa ameweka mipango ya baadaye ya huduma. Alikuwa ameacha urithi.

Katika somo hili la mwisho, tutajifunza kuhusu mafundisho ya mwisho ya Yesu kwa ajili ya wanafunzi wake, kukabidhi wanafunzi wake majukumu kwa mara ya mwisho, na huduma za wanafunzi wake baada ya kupaa mbinguni. Tutajifunza masomo yanayohusu jinsi ya kuacha urithi.

► Je, kama ulikuwa ufariki usiku wa leo, utaacha urithi gani?

- Nini urithi wako kwa familia yako?
- Nini urithi wako kwa jamii yako?
- Nini urithi wako kwa huduma yako?

## Mihadhara ya Yesu ya Kuaga

Yohana 13-16 inaweza kulinganishwana na “mihadhara ya kuaga” kwenye Agano la Kale ya Yakobo, Musa, Yoshua na Daudi. [324] “Mihadhara ya kuaga” ya Yesu inatoa baadhi ya mafundisho yake ya ndani sana na ya mwisho.

Yohana 13:1 inatoa muundo wa mafundisho haya ya kuaga: “Yesu, hali akijua ya kuwa saa yake imefika, atakayotoka katika ulimwengu kwenda kwa Baba.” Kama wewe ungejua utakufa katika kipindi cha masaa arobaini na nane yajayo, ungesemaje kwa wale ambao utawaacha kuendeleza huduma yako? Maneno hayo yatawakilisha kile ambacho ulikuwa umeamini kwamba ni muhimu sana kwa wafuasi wako.

Kwenye Chakula cha jioni cha Mwisho, Yesu alionyesha upendo wake wa mwisho kwa wanafunzi wake kwa matendo yake (ya kuwatawadha miguu) na kwa maneno yake kawa pamoja. Yesu ”aliwapenda watu wake katika ulimwengu.” Na sasa, “aliwapenda hadi mwisho.”[325] Neno “Hadi mwisho” linabeba nadharia kuu mbili:

1. Inamaanisha kwamba Yesu “aliwapenda hadi mwisho” wa muda wa kukaa nao.
2. Inaamaanisha kwamba “Yesu aliwapenda kwa upeo wake wote wa mwisho.” Yesu aliwapenda kabisa.

► Soma Yohana 13:31-14:31.

### Maamrisho na Ahadi katika Mihadhara ya Yesu ya Kuaga

#### *Amri: Mpendane (Yohana 13:34).*

“Amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo. ”Kwa kikundi cha wanafunzi kilichojulikana zaidi kwa kubishanabishana kuliko kupendana, amri hii ilikuwa ngumu.

Ilikuwaje hii “ikawa amri mpya?” Hata Agano la Kale liliamrisha watu wa Mungu kwamba “Mpende jirani yako.” Kuna vipengele viwili “vipya” vya Yesu kufundisha kuhusu upendo.[326]

Kipengele cha kwanza, Yesu alitoa **aina** ya upendo ambao aliuamrisha. Walikuwa wapendane kama yeye alivyowapenda. Baada ya kuwatawadha miguu yao kwa

---

[324] Mwanzo 49; Kumbukumbu la Torati 32-33; Yoshua 23-24; 1 Mambo ya Nyakati 28-29
[325] Yohana 13:1
[326] Darrell L. Bock, *Jesus According to Scripture* (Grand Rapids: Baker Book House, 2002), 498

unyenyekevu mkubwa, Yesu aliwaambia, "Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo." Aliingiza upendo ambao unadhihirishwa kwenye huduma ya unyenyekevu. Wanafunzi, kwa wakati ule na hata sasa, ni lazima wawe na uwezo wa kupenda kama Yesu alivyopenda. Upendo huu unachukua kitambaa cha kujifutia ili kutumika. Upendo huu unatumikia hata msaliti. Upendo huu unadumu hata kama ni kufikia mahali pa kufa.

Kipengele cha pili, Upendo kati ya Wakristo ulitakiwa uwe ushuhuda wa **aina yake** wa ukweli wa ujumbe wa Yesu. "Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi." Baada ya hapo, Yesu anaomba "Wote wawe na umoja; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma."[327] Upendo na umoja katika kanisa ni lazima uwe ushuhuda kwa ujumbe wa Yesu.

Wakristo wengi wamegundua kwamba ni rahisi zaidi kumpenda jirani ambaye bado hajaamini kuliko kumpenda ndugu wa Kikristo ambaye amejaa tele makosa ya kibinadamu. Lakini kama Wakristo, tumepewa amri "Mpendane." Miaka hamsini baadaye, Yohana akalikumbusha kanisa kuhusu ujumbe huu:

> Mtu akisema, Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona. Na amri hii tumepewa na yeye, ya kwamba yeye ampendaye Mungu, ampende na ndugu yake.[328]

Yesu alianza na ujumbe wake wa kuaga kwa amri ya mpendane. Amri hii ndio msingi wa kila kitu alichozungumza katika ujumbe huu.

### *Amri: Msifadhaike, Aminini (Yohana 14:1).*

Kama alivyokuwa anafanya mara kwa mara, Petro aliingilia kati kumwuliza Yesu, "Bwana unaenda wapi?" Katika jibu lake, Yesu alitabiri kuhusu Petro kumkana. Kisha Yesu akaendelea na ujumbe wake kwa Petro, kwa ajili a wanafunzi wake na kwa ajili yetu sisi wa leo. "Msifadhaike mioyoni mwenu."

Kwa kuwa kuna kituo cha sura baada ya Yohana 13:38, mara nyingi tunasoma Yohana 14:1 kana kwamba ndiyo tunaanza aya mpya. Yohana 14:1 ni sehemu ya jibu kwa Petro. Lisome kwa njia hii:

> Petro, utanikana mara tatu. Wewe ni mdhaifu kuliko unavyojifikiria. Lakini usikate tamaa; nina ujumbe wa matumaini kwa ajili yako, Petro, na kwa ajili ya wale wote ambao katika muda mfupi tu ujao watakimbia kwa hofu ya kukamatwa. "Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi."

---

[327] Yohana 17:23
[328] 1 Yohana 4:20-21

Petro alihitajika kujua kwamba pamoja na kushindwa kwake, Yesu alikuwa na ujumbe wa matumaini. Wanafunzi walihitaji kujua kwamba pamoja na kuwa na hofu, Yesu alikuwa na ujumbe wa matumaini. "Msifadhaike mioyoni mwenu" ni kwa wakati uliopo. Wakiwa wamepewa maonyo pamoja na upinzani wa viongozi wa kidini, wanafunzi tayari walishakuwa na mfadhaiko. Yesu anasema, "Acheni kufadhaika ….mnamwamini Mungu; niaminini na mimi."

Njia pekee tunayoweza kuepuka kuwa na "mfadhaiko" kutokana na msongo wa huduma ni "kuamini." Ninaandika somo hili katika siku ya Jumatatu asubuhi. Katika Jumatatu yeyote, kuna wachungaji duniani kote ambao wamekata tamaa. Jana, ulifundisha kwa uaminifu – na mmoja wa wafuasi wako akakasirika. Ulihubiri ujumbe wa kutubu – na hakuna hata mmoja aliyejitokeza. Uliita ambao hawajaokoka – hakuna hata mmoja aliyekuja.

Katika baadhi ya nchi, Kanisa linakabiliwa na upinzani wa serikali. Katika baadhi ya nchi, Kanisa linagubikwa na vitisho vya wajahidina wa Kiislamu. Katika baadhi ya nchi, kania linakabiliwa na vitisho vya tofauti za kijamii – hakuna anayejali. Yesu anasema, "Msifadhaike. Mnamwamini Mungu; niaminini na mimi."

### *Ahadi: Mimi ndimi njia. (Yohana 14:6).*

Yesu aliwapa matumaini wanafunzi wake kwamba yeye anaondoka kwenda kuwaandalia makao. Tomaso akaingilia kati, "Bwana, sisi hatujui uendako; nasi twaijuaje njia?"

Jibu la Yesu linafundisha kanuni muhimu sana ya maisha ya Mkristo. Yesu *hakusema*, "Hapa ndipo ninapokwenda." Badala yake alisema, "Mimi ndimi njia." Yesu hakuonyesha njia ya kupitia; alijionyesha yeye mwenyewe. Hakuna tamko lingine lililo wazi zaidi katika Maandiko linaloonyesha kwamba njia pekee ya kwenda kwa Baba ni kupitia kwa Yesu. Kinyume na madai ya wanatheolojia wanaopendelea mabadiliko ya wastani, Yesu alitamka wazi kwamba yeye peke yake ndiye njia ya kupitia kwenda kwa Baba.

### *Ahadi: Kazi kubwa kuliko hizo Mtafanya (Yohana 14:12-14).*

Yesu aliahidi kwamba, "Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba." Hizi kazi zitakuwa nyingi siyo kwa sababu zina mambo ya kushangaza zaidi, lakini ni kwa sababu zitakuwa kwenye uwigo mpana zaidi wa kufika. Wakati wa huduma yake duniani, kazi za Yesu zilikuwa zimesambaa katika eneo moja tu la kijeografia. Sasa, kwa sababu Yesu alikuwa anatuma Roho Mtakatifu, kazi zitakazofanywa na kanisa zitaufikia ulimwengu wote.

Yesu akaendelea, "Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana." Kuna nadharia kuu mbili zinazofungamana na ahadi hii:

#### (1) "Mkiomba lo lote kwa jina langu."

Hii ni zaidi ya kuongezea "Kwa jina la Yesu" katika kila mwisho wa maombi yetu. Siyo kila kitu tunachokiweka katika maombi kitakachomlazimisha Yesu atoe majibu ya maombi

yetu. Katika Biblia nzima, "jina" la Mungu linawakilisha tabia yake. Kuomba "Kwa jina la Yesu" inamaanisha ni kuomba kwa namna inayoendana na tabia ya Yesu na mapenzi yake.

Kuomba "kwa jina langu" inaweza ia ikamaanisha ni "kuja kwa Baba kupitia kwa mamlaka ya Yesu." Kwa maana tangu Musa "alipokwenda kwa Farao, kusema naye kwa jina lako," alikuja kwa mamlaka ya ya Mungu aliyemtuma.[329] Kuomba kwa Jina la Yesu inamaanisha kuomba katika kibali na mamlaka yake. Tunamwendea Mungu kupitia maombezi ya Mwanae ambaye "yu hai sikuzote ili awaombee."[330]

**(2) "…ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana."**

Maombi yetu ni lazima yawe kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Yakobo aliwaonya wale ambao "Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu."[331] Tunapodai ahadi za Mungu, ni lazima tuwe na hakika kwamba tunaomba kwa ajili ya utukufu wa Mungu, na siyo kwa ajili ya makusudi yetu binafsi.

***Amri: Mtazishika amri zangu (Yohana 14:15).***

Yesu alitoa kiwango ambacho tunaweza kuupima upendo wetu kwake. "Mkinipenda, mtazishika amri zangu." Yohana akakumbuka kauli hii wakati alipoandika barua yake ya kwanza: "Lakini yeye alishikaye neno lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli."[332] Kinyume na jinsi ambavyo wahubiri wengine wa wakati huu wanahubiri, Yesu kamwe hakufundisha kwamba wanafunzi wake wanaweza kuishi katika kutokutii kwa hiari amri zake. Upendo unaonekena katika utii wa hiari.

***Ahadi: Naye atawapa Msaidizi mwingine (Yohana 14:16).***

Neno lililotafsiriwa "Msaidizi" katika Yohana 14:16 ni *Paraclete.*[333] Neno hili linarejea kwa "wakili anayemtetea mtu mwingine kwenye shauri." Linarejea kwa "Msaidizi" au "Mfariji anayetoa huduma yake ya faraja wakati wa matatizo."

Yesu alisema kwamba, "Baba, naye atawapa Msaidizi **mwingine**, ili akae nanyi hata milele." Hii inaonyesha kwamba huduma ya Roho Mtakatifu itafanana na ile huduma ya Yesu. Roho Mtakatifu hakuja kama "nguvu" ya mtu binafsi lakini kama nafsi hai, sawa na vile Yesu alivyokuwa nafsi hai.

*Paraclete* ni "Roho Mtakatifu wa kweli" ambaye "anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu." Yeye "atawafundisha mambo yote ambayo niliwaambia ninyi." Huduma yake itakuwa na nguvu sana kiasi cha Yesu kutangaza kwamba, "yawafaa ninyi mimi niondoke,

---

[329] Kutoka 5:23
[330] Waebrania 7:25
[331] Yakobo 4:3
[332] 1 Yohana 2:5
[333] Msaidizi, *English Standard Version;* Mfariji, *King James Version*; Wakili, *New International Version*

kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu."[334]

Itakuwaje kwa faida ya wanafunzi kama Yesu ataondoka? Robert Coleman anafafanua:

> Wakati wanafunzi wake walipokuwa naye katika hali ya mwili wa kawaida, waliona umuhimu mdogo sana wa kumtegemea Roho Mtakatifu, kwa sababu hiyo walikuwa hawajawahi kujua kwa undani ukweli unaohusiana na maisha yake. Alipokuwa hayupo, hata hivyo, hawakuwa na msaada unaoonekana. Ili waweze kuendelea kuwepo, walipaswa wajifunze siri ya mahusiano yake ya ndani na Baba. Nje ya umuhimu wao, watapata uzoefu wa ushirika mkuu na Kristo kulikoni hata walivyokuwa wamejua kabla ya hapo.[335]

**Maisha katika Mzabibu**

► Soma Yohana 15:1-16:37.

Yesu aliendelea na moja ya sura zake zenye nguvu sana. "Mimi ndimi mzabibu wa kweli, na Baba yangu ndiye mkulima." Agano la Kale limekuwa likiirejea mara nyingi Israelini kama mzabibu.[336] Hata hivyo, kwa sababu ya dhambi yake, Israeli kamwe haikutimiza kusudi la Mungu la uzuri wa mzabibu alioupanda. Badala yake, jinsi Israeli ilvyofanikiwa kwa mali nyingi, alijenga madhdbahu kwa miungu ya uongo. [337] Badala ya kuzaa matunda ambayo yangekuwa ni baraka kwa ulimwengu, Israeli akazaa "mzabibu mwitu." [338] Israeli ilfanya maovu mengi kiasi kwamba Mungu hangeweza kufanya lolote na huu mzabibu isipokuwa kuchoma kuni kwa ajili ya mafuta. [339]

Yesu alikuja kama mzabibu wa kweli." Alikuja kutimiza kile ambacho taifa la Israeli lilishindwa kufanya; alikuja kukamilisha wito wa Israeli wa kufanyika baraka kwa ulimwengu wote.

Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba yeye alikuwa ni mzabibu, na wao ni matawi. Ujumbe wa Yesu ulikuwa wazi: Matunda hutegemea kabisa nia yetu ya "kukaa ndani yake."

> Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote.

---

[334] Yohana 16:7
[335] Robert Coleman, *The Mind of the Master* (Colorado Springs: WaterBrook Press, 2000), 29
[336] Zaburi 80:8-9; Isaya 5:1-7; 27:2-6; Hosea 10:1-2
[337] Hosea 10:2
[338] Isaya 5:2. "Mwitu" lina maana sawa na ladha "chungu" badala ya ladha tamu ya mvinyo utokanao na mizabibu iliyostawishwa mashambani.
[339] Ezekieli 15:1-6

Mbali na mzabibu, wanafunzi hawangeweza kufanya jambo lolote; mbali na mzabibu, sisi hatuwezi kufanya jambo lolote katika wakati wa leo. Tunapojaribu kufanya huduma kwa nguvu zetu wenyewe, tunajitafutia kuchanganyikiwa na kukosa nguvu kabisa. Kwa nini? Kwa sababu kamwe hatujakusudiwa kuzaa matunda tukiwa sisi wenyewe.

Maisha yetu ya kiroho yenyewe yanapatikana kutokana na mahusiano yetu na mzabibu. Mtu yeyote asipokaa ndani ya mzabibu, "hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea." Wakati aya hii ni onyo, lakini pia ni faraja kubwa. Mbali na mzabibu, hatufai wala hatuna thamani. Lakini kama tutaendelea kukaa ndani ya mzabibu, tunayo maisha na uzao wa matunda tele. Maisha yetu ya kiroho hayategemei nguvu zetu wenyewe; tunaishi ndani ya "mzabibu."

Dhamira hii inaonekana tena katika Waebrania. Kuhani wetu mkuu, Yesu, "yu hai sikuzote ili awaombee" wale "wamjiao Mungu kwa yeye."[340] Howard Hendricks aliwafariji wachungaji wanaojitahidi na ambao wanajisikia kama walioachwa: "Kama huna mtu yeyote anayekuombea, usisahau kwamba Kristo anakuombea." Yeye ni mwombezi wetu; yeye ni chanzo cha maisha yetu ya kiroho.

Yesu aliwakumbusha wanafunzi kwamba ni lazima wakae ndani ya mzabibu. Hiyo ni kweli hata sasa. Kama wachungaji na viongozi wa makanisa, hufanyi huduma kwa nguvu zako mwenyewe. Unaishi ndani ya nguvu ya msalaba na ndani ya Kuhani mkuu ambaye anakuombea wakati unapojikuta huna nguvu za kujiombea mwenyewe.

Kupitia mihadhara ya wazi yote ya mwisho ya Yesu, aliwafundisha wanafunzi wake tena kwamba ni lazima wapendane. Aliwaandaa katika kukabiliana na machukizo ya ulimwengu huu. Ulimwengu ulimchukia Yesu; ulimwengu huo huo utawachukia wafuasi wa kweli wa Yesu.

Kisha Yesu akafafanua zaidi kuhusu kazi za Roho Mtakatifu. Mwanzoni mwa mihadhara yake, alishaahidi kumtuma Roho. Sasa anawafundisha zaidi kuhusu kazi za Roho Mtakatifu. Roho atauhukumu ulimwengu; atawaongoza wanafunzi awatie katika kweli yote; atamtukuza Mwana.

Yesu pia aliwafafanulia kuhusu kuondoka kwake katika "kitambo kidogo kijacho." Akazungumza nao tena kuhusu amani kuwa matatani. Mapema katika mhadhara huu, Yesu aliagiza, "Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. "[341] Aliufunga mhadhara pamoja na kuwapa maneno ya kuwatia moyo: "Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu."[342]

---

[340] Waebrania 7:25
[341] Yohana 14:1
[342] Yohana 16:33

Kumbuka kwamba katika matukio yote kwa pamoja, matumaini yetu yako ndani ya Kristo peke yake. Hatupaswi kufadhaika kama pia tunaamini "ndani yake." Ni lazima "tuwe na moyo mkuu" kwa sababu anasema "mimi nimeushinda ulimwengu." Maisha ndani ya mzabibu ni maisha yenye amani ya uhakika. Matumaini yetu hayategemei hali za kidunia; matumaini yanamtegemea Kristo na ushindi wake dhidi ya dunia.

**Angalia kwa kuzingatia: Chakua cha Mwisho**

*Mishnah* ni kumbukumbu ya mila za kale za Kiyahudi. [343] Sehemu moja ya *Mishnah* inaonyesha jinsi Wayahudi walivyoshiriki chakula cha Pasaka. Kwenye Chakula cha Mwisho, Yesu na wanafunzi wake yumkini walifuata mtindo huu ambao bado unaendelea miaka 2,ooo baadaye.

Mvinyo wa mzabibu uliochanganywa na maji kwenye kikombe cha kwanza unatolewa utumike. Baraka juu ya kikombe cha mvinyo ni pamoja na ahadi iliyopo katika kitabu cha Kutoka "Nami nitawatoa ninyi mtoke."

Mvinyo wa mzabibu umechanganywa na maji kwenye kikombe cha pili, lakini bado haujatolewa utumike. Kijana mdogo anauliza, "Kwa nini usiku huu ni tofauti na usiku nyingine zote?' Baba anamjibu akitumia maelezo ya ukombozi wa Israeli kutoka Misri.

Baada ya maelezo hayo, familia inaimba *Haleluya* ya kwanza ya Pasaka, Zaburi 113-114. Kisha wanakunywa kikombe cha pili pamoja na ahadi hii: "Nami nitawaokoa na utumwa wao."

Baada ya Baraka, chakula kinagawanywa kitumike. Chakula kimechanganywa pamoja na mimea michungu, mikate isiyotiwa chachu, kondoo, na mchuzi mzito wa matunda ya msimu uliochanganywa na viungo na siki. Baba anaosha mikono yake, humega na kuombea mikate, anachukua kipande cha mkate, anakifungia kwenye mimea michungu, anakichovya kwenye mchuzi mzito kisha anakula. Baada ya hapo anashukuru na kula kipnde cha kondoo. Ndipo kila mwanafamilia naye hula.

Kikombe cha tatu kimebarikiwa na ahadi za Pasaka: "nami nitawakomboa."

Kikombe cha nne kimebarikiwa na ahadi za Pasaka: "nami nitawatwaeni kuwa taifa langu."

Kisha familia inaimba *Haleluya* ya mwisho ya Pasaka, Zaburi 115-118.[344]

Wakati wa chakula cha Pasaka, Wayahudi wanakumbuka jinsi Mungu alivyoikomboa Israeli kutoka utumwani. Zaidi ya hapo, wana mategemeo ya ukamilishwaji kamili wa

---

[343] Unaweza kuangalia video kuhusu chakula cha Pasaka ya Masihi ya Kiyahudi kutoka https://www.youtube.com/watch?v=bVolBDlWloQ, iliyopatikana mwezi Marchi 22, 2021. Unaweza kusoma zaidi kutoka http://www.crivoice.org/haggadah.html, iliyopatikana mwezi Marchi 22, 2021.

[344] Hii ni Zaburi ya mwisho ambayo Yesu aliimba pamoja na wanafunzi wake kabla ya kwenda (Mathayo 26:30).

ahadi za Mungu wakati Masihi atakapowakomboa kutoka kwenye utumwa kwa mara nyingine na ya mwisho kabisa.

Siku moja baada ya Pasaka, Yesu alikufa kama kondoo wa Pasaka kamili. Juu ya msalaba, ahadi ya ukombozi ilikamilishwa.

## Maombi ya Kuhani Mkuu

► Soma Yohana 17.

Maombi ya mwisho ya Yesu yaliyonukuliwa akiwa na wanafunzi wake ni muhimu sana katika kuelewa urithi wake kwa wanafunzi na kanisa la leo. Maombi haya yanaitwa "Patakatifu pa Patakatifu pa maombi ya Yesu." Ni maombi yake ya ndani sana.

### Yesu alijiombea mwenyewe (Yohana 17:1-5)

Yesu aliomba akasema Baba, "Mtukuze Mwanao, ili Mwana wako naye akutukuze wewe." Wakati wanafunzi hawakuelewa maombi haya, baadaye wanakuja kujifunza ukweli wa kushtusha kwamba majibu ya maombi haya yanakuja kujibiwa juu ya masalaba wa Warumi.

Siku ya Jumatatu ya wiki la mateso, Yesu alisema, "Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu." Yohana akafafanua, "Aliyanena hayo akionyesha ni mauti gani atakayokufa." [345] Yesu alitukuzwa siyo kwa kupitia ushindi, bali kwa njia dhahiri ya kushindwa. Yesu alitukuzwa kupitia msalaba.

### Yesu Aliomba kwa ajili ya Wanafunzi wake (Yohana 17:6-19)

Yesu aliombea mambo matatu kwa wanafunzi wake. Aliomba kwamba, Baba, "kwa jina lako ulilonipa uwalinde hawa," na akaomba tena kwamba "uwalinde na yule mwovu," na akaomba tena kwamba Baba,"Uwatakase kwa ile kweli."

### Yesu Aliomba kwa ajili ya Waamini wote (Yohana 17:20-26)

Yesu aliomba kwa ajili ya "wale watakaoniamini" baadaye. Aliomba kwamba, "wote wawe na umoja." Umoja huu ni kwa ajili ya ushuhuda kwa ulimwengu kwamba, "wewe ndiwe uliyenituma."

Yesu hakuomba kwa ajili ya ulimwengu: "mimi siuombei ulimwengu; bali hao ulionipa." Badala yake aliomba kwa ajili ya Wakristo ili ulimwengu upate kusadiki. Kwenye maombi yake ya mwisho kwa ajili ya kanisa, Yesu aliomba kwamba tuweze kuwa mashuhuda kwa ulimwengu kupitia umoja na uaminifu wetu.

Urithi wa Yesu ulikuwa ni kundi la watu walioamini ambao wataenda kukamilisha kusudi lake hapa duniani. Katika Agano la Kale, Israeli ilibarikiwa na Mungu ili iwe ni gari la

---

[345] Yohana 12:32-33

kupeleka baraka kwa mataifa mengine yote.[346] Katika Agano Jipya, Kanisa lilibarikiwa na Mungu ili liwe ni gari la kupelaka Baraka kwa watu wote. Yesu aliomba kwamba tutatimiza jukumu letu la kuwa Baraka kwa watu wote.

**Agizo Kuu la mwisho la Yesu kwa Wanafunzi wake.**

► Soma Mathayo 28:16-20; Marko 16:15; Luka 24:44-49; Matendo 1:6-11.

Ushawishi wa wisho wa kiongozi kwa sehemu kubwa unapimwa na uwezo wake wa kushirikisha maoni yake kwa watu wengine. Siku hizi tunasema ni "kutoa maono." Yesu anatoa mfumo wa kutoa maono katika njia ambayo itawahamasisha wafuasi waliojidhili kabisa. Kwa sababu ya maono yake, wanafunzi walijitolea maisha yao kusambaza injili ya ufalme wa Mungu katika Dola yote ya Kirumi.

Vitabu vya Injili vinashirikisha matamko matatu ya agizo kuu la Yesu. Kila tamko linalenga katika kipengele tofauti cha agizo kuu. Mathayo anasisitiza kuhusu mamlaka ambayo ni muhimu kwa ajili ya agizo kuu hilo. Marko anabainisha agizo kuu linakotakiwa lifike: "kwa kila kiumbe." Luka anatoa kwa muhtasari maudhui ya ujumbe ambao mitume wanapaswa kuhubiri.

Tamko kamili lililokamilika la agizo kuu la Yesu la mwisho liko katika Mathayo 28:18-20.

> Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.

Amri kuu ya msingi iliyoko katika hili agizo kuu ni "mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi." Ili kukamilisha amri hii kunatuhitaji sisi tuende, tubatize waamini wapya na kuwafundisha waamini wachanga. Shughuli hizi ndizo zinazounganisha amri kuu ya, "mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi." Uinjilisti, kazi za kijamii, elimu, na vipengele vyote katika huduma vinaongozwa na hii amri kuu: tumepewa agizo kuu la kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi.

**Kusudi la kufanya Huduma ya Kichungaji**

Ed Markquart, mchungaji wa Kimarekani, alikula chakula cha jioni na mchungaji Richard Wurmbrand kutoka Romania ambaye alikuwa amefungwa miaka mingi katika gereza la kikomunisti. Wakati wa chakula hicho cha jioni, Wurmbrand akamgeukia mfuasi mmoja wa kanisa la Markquart na kumwuliza, "Je, mchungaji wako ni mzuri?" Yule mfuasi alijibu, "Ndiyo."

---

[346] Mwanzo 12:1-3

Wurmbrand akauliza, "Kwa nini unaona ni mchungaji mzuri?" Yule mfuasi akajibu, "Kwa sababu anahutubu mahubiri mazuri."

Kisha Wurmbrand akamwuliza tena, "Lakini huwafanya watu kuwa wanafunzi?" Mchungaji Markquart akasema swali hilo limebadilisha kabisa mwelekeo wa huduma yake yote. Akasema, "

> Kusudi la Mungu kwa kwa wachungaji wote ni kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi wa Yesu Kristo. Watu wanaompenda Yesu Kristo, wanaomfuata Yesu Kristo, wanaomwita Yesu Kristo Bwana wao. Hiki ndicho tulichoitiwa kukifanya: kufanya wanafunzi kwa ajili ya Yesu Kristo. Siyo kuwafanya watu wawe wafuasi wa kanisa. Siyo kutengeneza shule za Jumapili. Siyo kujenga majengo. Tunapaswa kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi wa Yesu Kristo. Hilo tu ndilo linalohitajika.

**Angalia kwa kuzingatia: Kazi Maalumu ya Yesu**

Matukio ya wiki ya mwisho ya huduma ya Yesu yanaonyesha kazi yake maalumu ya kuanzisha ufalme unaohuzsisha mataifa yote, rangi zote, na watu wa aina zote. Sehemu za matukio ya wiki ya mwisho ya huduma ya Yesu zinaonyesha kazi yake maalumu kwa mataifa yote.

- Yesu aliingia kwenye jiji kwa kupanda punda. Mathayo na Yohana walinukuu unabii wa Zakaria, "Tazama, mfalme wako anakuja kwako; Ni mnyenyekevu, amepanda punda." Zakaria alielezea utawala wa huyu mfalme. "atawahubiri **mataifa yote** habari za amani; na mamlaka yake yatakuwa toka bahari hata bahari."[347]

- Alipousafisha uwanja uliokuwa mahali pa kuabudia kwa Mataifa, Yesu alimnukuu Isaya akasema, "Je! Haikuandikwa, Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote?"[348] Viongozi wa kidini wa Kiyahudi walikuwa wamegeuza uwanja ambao watu wa Mataifa walikuwa wakiabudia kuwa eneo la soko kwa ajili ya kubadilishana fedha na kuuza njiwa.

- Wakati wanafunzi walipomshutumu Mariamu kwa "kutumia" marhamu ya gharama kubwa, Yesu aliwajibu: "Amin, nawaambia, Kila ihubiriwapo Injili **katika ulimwengu wote,** na hili alilotenda huyu litatajwa kwa kumbukumbu lake."[349]

- Kwenye hotuba ya Oliveti, Yesu alitoa unabii wa siku ambayo "Habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda **kwa mataifa yote**; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja."[350] Kwa hawa wanafunzi wa Kiyahudi ambao

---

[347] Mathayo 21:5; Zakaria 9:9-10; Msisitizo umeongezwa
[348] Marko 11:17, Ikinukuu Isaya 56:7; Msisitizo umeongezwa.
[349] Marko 14:9; Msisitizo umeongezwa.
[350] Mathayo 24:14; Msisitizo umeongezwa

> walikuwa wanafikiri kwamba ufalme ulikuwa ni kwa ajili ya watu waliochaguliwa peke yao, Yesu alisema kwamba habari njema za ufalme zitahubiriwa duniani kote.

Manabii wa Agano la Kale walishaonyesha kwamba Masihi atakuja kwa ajili ya mataifa yote. Katika wiki ya mwisho ya huduma yake, Yesu alifundisha wanafunzi wake kwamba ufalme wa Mungu utahusisha watu kutoka mataifa yote. Ahadi za manabii zilikuwa zikamilishwe kupitia kanisa.

## Urithi wa Yesu: Kanisa katika Matendo

Vitabu vingi kuhusiana na maisha ya Yesu vinamalizikia kwenye kupaa kwake. Hata hivyo, Kupaa kwake hakukuwa mwisho wa huduma ya Yesu duniani. Huduma ya Yesu haikuwa tu kuuendea msalaba au kuiacha kaburi wazi; huduma yake iliendelea hata wakati wa Pentekoste. Yesu alitoa ahadi kwamba "atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele."[351] Ahadi hii ilitimizwa kwenye Matondo. Sehemu mbili za matukio katika Matendo zinaonyesha ukamilishwaji wa urithi wa Yesu.

### Kanisa Wakati wa Pentekoste

► Soma Matendo 1:4-11 na 2:1-41.

Kitambo kidogo kabla Yesu hajapaishwa, wanafunzi walimwuliza, "Je! Bwana, wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme?" Walikuwa wanategemea Yesu aanzishe ufalme wa kisiasa wa duniani. Kwa akili zao, kufufuka kwake kuliimarisha matumaini yao ya kuwepo ufalme wa kidunia. Alichohitaji tu Yesu kukifanya, walivyofikiria, ni kutumia uwezo wake kuwapindua Warumi. Yesu akawajibu,

> Si kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba aliyoyaweka katika mamlaka yake mwenyewe. Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.

Yesu anamaanisha "Nyakati na majira ya ufalme siyo jukumu letu." Badala yake, nilazima ukamilishe kazi maalumu niliyawapeni.: tumikeni kama mashahidi wangu hadi miisho yanchi. Lakni kabla hamjaenda, ni lazima mngojee. Katika Luka, Yesu alisema, "lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu."[352]

Siku hamsini baada ya Pasaka, wanafunzi wapatao 120 walikuwa wamekusanyika kwenye chumba cha juu, ambako ndiko ahadi ya Roho Mtakatifu ilipokamilishwa. Walianza kuzungumza kwa lugha za watu mbalimbali waliokuwa wamekusanyika kutoka kila taifa kwa ajili ya Sikukuu ya Kiyahudi ya Pentekoste.

---

[351] Yohana 14:16
[352] Luka 24:49

Hii iliashiria kukamilika kwa mpango wa Kristo wa kuanzisha kanisa lake kutoka mataifa yote. Orodha ya mataifa iliyoko katika Matendo 2 inatukumbusha sisi orodha ya mataifa iliyoko katika Mwanzo 10. Katika Mwanzo 11, Yesu alihukumu jaribio la mwanadamu la kuanzisha ufalme mmoja wa dunia nzima katika mji wa Babiloni kwa kuwachanganya wasisikilizane katika lugha zao. Katika Matendo 2, Mungu alianza kuujenga ufalme wake kwa kuugeuza ule mkanganyiko uliokuwepo wa kutoelewana lugha.

Pentekoste ulikuwa mwanzo wa "kazi kubwa kuliko hizo" ambazo Yesu aliahidi.[353] Kwa sababu ya kazi ya Roho Mtakatifu, watu wengi waliamini kuliko wakati wa huduma ya Yesu hapa duniani. Utimilifu wa urithi wa Yesu umeanza. Roho Mtakatifu aliyeahidiwa sasa anafanya kazi kupitia hudumaza mitume. Kuanzia wakati huu, kanisa litaanza kukamilisha kusudi kuu la Mungu la kuanzisha ufalme wake. Kama mahubiri ya Petro yalivyojifafanua kwa uwazi, ahadi za Agano la Kale sasa zinakamilishwa kupitia kanisa.

John Stott alielezea vipengele vinne vinavyohusiana na siku ya Pentekoste.[354]

- Siku ya Pentekoste ilikuwa ndiyo ya kitendo cha mwisho cha Yesu kuhudumu katika ulimwengu.
- Siku ya Pentekoste iliwapa mitume uwezo kwa ajili ya kutekeleza Agizo Kuu.
- Siku ya Pentekoste ilizindua enzi mpya ya Roho Mtakatifu. Kwenye Agano la Kale lote, Roho Mtakatifu aliwawezesha watumishi wa Mungu katika nyakati maalumu tu za huduma. Baada ya Pentekoste, Wakristo kwa nyakati zote na katika maeneo yeyote wanafaidika kutokana na huduma yake.
- Huduma ya uamsho ya kwanza ya Wakristo ilianza wakati wa Pentekoste.

Matokeo ya Pentekoste yanaonekana katika kitabu chote cha Matendo. Ishara zilizotokea wakati wa Pentekoste zilikuwa "ni maalumu na za kipekee." Furaha, ushirika wa waumini, uhuru wa kuabudu, ujasiri wa kushuhudia, na nguvu ya huduma viliweza kuwa ni ushahidi wa "kawaida" wa huduma katika uweza wa Roho Mtakatifu.

### Maisha ya kila siku katika Kanisa la Mwanzo

► Soma Matendo 2:42-47.

Sehemu ya pili ya tukio la ukamilishwaji wa urithi wa Yesu liko mwishoni mwa matendo 2. Sehemu hii inaonyesha maisha ya kila siku ya kanisa la mwanzo.

Katika maombi yake ya Kuhani Mkuu, Yesu aliomba umoja kwa ajili ya wafuasi wake. Aliomba kwamba, "wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja."[355] Jibu kwa ajili ya ombi hili

---

[353] Yohana 14:12
[354] John W. Stott, *The Message of Acts* (Westmont, Illinois: InterVarsity Press, 1990), 60-61
[355] Yohana 17:22

linaanziakatika Matendo 2. Wote walioamini "walikuwako wote mahali pamoja"; kwa pamoja walidumu ndani ya hekalu pamoja na kumega mkate nyumba kwa nyumba"; Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa."

Katika Matendo, neno "pamoja" linawakilisha umoja wakanisa la mwanzo. Licha ya matatizo ya kuanzisha kanisa moja la Wayahudi na watu wa Mataifa, mateso kutoka kwa viongoziwa Kiyahudi, na migogoro binafsi miongoni mwa mitume, kanisa liliendelea kubakia kuwa moja. Kinyume na magumu yote, maombi ya Yesu kwamba, "waweze kuwa wamoja" yalitimilizwa.

► Je, picha ya kanisa katika Matendo 2:42-47 inafanana na iliyopo kwenye kanisa lako? Je,unahudumu katika uweza wa Roho Mtakatifu? Kama sivyo, kuna vizuizi gani vinazuia kazi ya Roho Mtakatifu ndani na katika huduma yako yote? Je, ni ukosefu wa utii? Je, ni ukosefu wa maombi? Je, ni ukosefu wa imani? Je, ni ukosefu wa umoja? Je, unawezaje ukaona mmiminiko mpya wa Roho Mtakatifu katika huduma yako?

## Matumizi: Kuacha Urithi

Katika kuandaa sehemu hii, niliwafanyia usaili viongozi mbalimbali wastaafu wa huduma.[356] Niliwahoji kuhusu urithi wao, maandalizi yao ya kustaafu uongozi, na masomo ya kuwavusha. Sehemu hii inategemezwa na majibu kutoka kwao.

### (1) Viongozi wanaoacha urithi hupanga mpango ya baadaye.

Fikiria unamwuliza mtu anayejenga, "Je, unajenga nini?" Utashangaa kama huyu mjenzi atakujibu, "Sijajua bado. Nategemea kuona kitakachotokea."

Kabla hajaanza kujenga, mjenzi huwa na mipango ya matokeo ya mwisho ya ujenzi anaoufanya. Viongozi wanaoacha urithi wanajua wanachotaka kuacha baada ya wao kuondoka.

Viongozi wanaomaliza vizuri wanajua urithi wanaotaka kuacha baada ya wao kuondoka. Hawaendelezi huduma zao kama vipofu. Viongozi hawa waliamini kwamba, "Hili ndilo kusudi Mungu aliloniitia mimi kukamilisha kama sehemu yangu ya huduma."

Urithi wa Yesu ulikuwa ni kundi la wanafunzi ambao walitayarishwa kwa ajili ya kuliongoza kanisa. Tangu mwanzo wa huduma yake, alitoa mudawa kutosha na nguvu zake katika kuwaandaa hwa watu kama urithi wake.

---

[356] Usaili kwa ajili ya sehemu hii ulihusisha viongozi wafuatao:
+ Dr. Michael Avery, raisi wa zamani katika God's Bible School and College, Cincinnati, OH
+ Rev. Paul Pierpoint, mchungaji wa zamani katika Hobe Sound Bible Church na raisi wa FEA Missions, Hobe Sound, FL
+ Rev. Leonard Sankey, mchungaji mstaafu na kiongozi wa mashirika ya huduma mchanganyiko za kimisheni
+ Dr. Sidney Grant, raisi wa zamani wa huduma za umisheni za FEA, Hobe Sound, FL

> " Unauandaa urithi wako kila siku, na siyo pale kwenye mwisho wa maisha yako."
> - Alan Weiss

Kama unataka kuacha urithi, ni lazima uwe na mipango ya baadaye. Kwa masikitiko, watu wengi wanajenga maisha yao pasipokuwepo na umakini katika malengo. Kama utawauliza wakiwa katika umri wa miaka 30, 50 au hata 70 kwamba, "Unajenga nini na maisha yako?" Jibu litakuwa, "Sijui. Nangojea nione kitakachotokea."

**(2) Viongozi wanaoacha urithi hujiandaa kikamilifu kwa kipndi cha mpito**

Fikiria kumtembelea fundi ujenzi anayekaribia kumalizia ujenzi wa mradi mkubwa wa ujenzi. Kuta zimekamilika; paa limekamilika; liko tayari kuanza kutumika. Uliza, "Ni hatua gani zimebakia kabla jengo halijakamilika kabisa?"

Utashikwa na mshangao kama atajibu, "Sijui! Sina muda wa kufikiria kuhusu hatua za mwisho." Hapana! Fundi ujenzi anaacha kitu ambacho kitaendelea kudumu na kuwepo hata baada ya yeye mwenyewe akiwa hayupo hai tena. Anapanga kwa uangalifu kila hatua. Anaweza akakuambia, "Hii ni siku ambayo tutakamilisha ujenzi. Hii ni siku ambayo mwenye jengo anaweza kuingia kukaa." Kila kitu kimepangwa kwa ajili ya mpito.

Viongozi wanaoacha urithi hujiandaa kikamilifu kwa ajili ya kipindi cha mpito. Inapowezekana, wanapanga mapema kuhusu kustaafu kwao, kutoa nafasi kwa shirika kuchagua atakayekuwa badala yake, na hawa wapya kujiandaa kwa ajili ya majukumu mapya. Katika baadhi ya matukio, viongozi wanaoingia na wanaoondoka wanakuwa na kipindi cha "kufanya pamoja" ambacho kiongozi mpya anaanza kufanya maamuzi wakati kiongozi aliyekuwepo anayeondoka anakuwepo kwa ajili tu ya kutoa usia na ushauri.

Viongozi wanaoacha urithi huiandaa huduma wanayoiongoza kwa ajili ya kipindi cha mpito. Viongozi wanaoondoka wenye ufanisi wanawasilisha kujiamini katika utoaji wa Mungu kwa ajili ya baadaye. Wanawaanda watu kufanya kazi vizuri chini ya kiongozi wao mpya anayefuata. Wanahakikisha kwamba watu katika shirika wanajisikia kuwa salama kwenye kipindi cha mpito. Kiongozi mmoja aliandika, "Lengo langu lilikuwa ni kufanya mabadiliko yaliyotulia kiasi kwamba hata wafanyakazi hawangetambua kuondoka kwangu."

**(3) Viongozi wanaoacha urithi wanajua ni lini wataondoka.**

Viongozi ni lazima wawe na hiari ya kubadilishana majukumu na viongozi wanaoondoka na "waondoke bila ya kuwepo na majuto." Viongozi wa zamani wanatakiwa waweze kupatikana kwa ajili ya kutoa usia, lakini iwe ni pale tu anapoombwa na mrithi wake.

Katika kozi hii, tumeonajinsi Yesu alivyowaandaa wanafunzi wake kuchukua nafasi za kuongoza makanisa. Mapema, aliwapa mafunzo kwa uangalifu. Baadaye, aliwatuma nje kwenda kufanya huduma na baadaye kurejea kwa ajili ya kufanyiwa tathmini. Kwenye Chakula cha Mwisho cha Pasaka, aliwapa maelekezo ya mwisho kwa ajili ya huduma. Muda mfupi kabla ya kupaa, aliwapa ukumbusho wa mwisho kuhusiana na agizo kuu. Yesu aliwaandaa kwa uangalifu kwa ajili ya kipindi cha mpito.

Kwa masikitiko, viongozi wengi wa Kikristo hutumia muda mfupi kwa ajili ya kipindi cha mpito. Wanachukulia kwamba, "Nitafanya kazi yangu hadi nitakapopewa mtu wa kunibadilisha. Baada ya hapo, itakuwa tatizo lamtu mwingine." Bila shaka, kuna nyakati ambazo kunatokea dharura za maradhi, vifo, au mabadiliko makubwa ya huduma jambo ambalo hufanya maandalizi ya kipindi cha mpito kuwa finyu. Lakini kila inapowezekana, tunapaswa tupange kwa uangalifu kipindi cha mpito kwa ajili ya kiongozi mpya anayekuja. Hii ni moja ya hatua muhimu sana katika kuhifadhi urithi kwa ajili ya baadaye.

**Kazi za kufanya Somo la 9**

Andika insha ya kurasa 3-5 kwa ajili ya kujibu maswali matatu yafuatayo:

(1) Fikiria kuhusu kiongozi mmoja wa huduma ambaye ameacha urithi ambao ulishawishi maisha yako ya Ukristo na huduma. Katika ukurasa mmoja, toa kwa muhtasari ushawishi wao kwenye maisha yako. Jibu maswali mawili yafuatayo.

- Ushawishi wao ulikuwa ni nini kwenye maisha yako?
- Walifanya kitu gani au walisema nini hata vikafanya kuwepo na matokeo muhimu kama hayo?

(2) Unataka kuacha urithi gani kwa wanaobakia wakati utakapofariki? Kuwa makini kwenye majibu yako. Jibu kwenye kurasa 1-2.

- Unataka uache urithi gani kwa familia yako?
- Unataka uache urithi gani kwa jamii yako?
- Unataka uache urithi gani kwa huduma yako?

(3) Kwa kila kipengele katika vipengele vitatu vya jibu la 2, tambulisha mambo maalumu utakayopaswa kufuata sasa ili uweze kuacha urithi unaotaka uuache. Jibu kwenye kurasa 1-2.

Ihifadhi karatasi hii na kila wiki ifanyie marejeo kwa kipindi cha miezi sita ijayo kwa mfululizo. Itumie katika kuanza kupanga urithi wako kwa kizazi kijacho

# Kiambatisho:
# Injili kuhusiana na Ufalme (Mahubiri)

Profesa Danny McCain (Chuo Kikuu cha Jos, Nigeria)

Miaka michache iiyopita, Emiri wa Gombe alinialika nikamtembelee. Miezi michache baadaye, nilienda kwenye kasri lake. Afisa katika eneo hilo akatoa maelezo ambayo mtu anatakiwa kuyazingatia wakati wa kukutana na Emiri. Ni lazima uvue viatu vyako unapoingia kwenye kasri. Huruhusiwi kushikana mikono na Emiri kwa sababu hashikani mikono na watu wa kawaida. Huwezi kukaa eneo moja la usawa na Emiri. Ni lazima umtambue mfalme kama "mtukufu mfalme" au "mtukufu jalali."

Kila ufalme una taratibu zake, sheria zake na viongozi wake. Kama wewe ni sehemu ya huo ufalme, unapaswa uuelewe huo ufalme na sheria zake. Nitaanza na Maandiko mawili ambayo yatakuwa ndio msingi wa mahubiri haya.

Mathayo 6:9-10:

> Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.

Luka 9:1-2:

> Akawaita wale Thenashara, akawapa uwezo na mamlaka juu ya pepo wote na kuponya maradhi. Akawatuma wautangaze ufalme wa Mungu, na kupoza wagonjwa.

Katika ujumbe huu, ninataka nitoe picha kubwa ya ufalme wa Mungu na kuonyesha jinsi ambavyo ukweli huu unaweza kuwa kweli katika maisha yetu.

## Ufalme wa Mungu: Picha Kubwa

Nilipokuwa mtoto mdogo, nilifikiri kwamba "ufalme wa Mungu" ulikuwa ndiko **nyumbani kwa Mungu – mbinguni.** Aya nyingi zinazohusiana na ufalme zinarejea nyumbani kwetu kwa milele "Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni." (Mathayo 7:21).

Nilipojifunza zaidi, nilianza kuelewa kwamba ufalme ulikuwa ni zaidi ya kuwa nyumbani kwa Mungu kwa milele. Nilipanua mawazo yangu ili kuamini kwamba ufalmeulikuwa ni sawa na **kanisa.** Mifano kama ile ya samaki kwenye wavu ilionyesha kwamba baadhi ya kumbukumbu za ufalme hazihusiani na mbinguni.

> Tena ufalme wa mbinguni umefanana na juya, lililotupwa baharini, likakusanya samaki wa kila namna; hata lilipojaa, walilivuta pwani; wakaketi, wakakusanya walio wema vyomboni, bali walio wabaya wakawatupa. Ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia; malaika watatokea, watawatenga waovu mbali na wenye haki, na kuwatupa katika tanuru ya moto; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno. (Mathayo 13:47-50).

Hii ni lazima iwe inarejea kanisa. Kuna waumini waliomaanisha na waumini wanafiki ndani ya makanisa yetu. Hata hivyo, mwishoni kabisa mwa umri wa kanisa, Mungu atawachambua: "Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni." (Mathayo 7:21).

Jinsi nilivyokuwa naendelea kujifunza zaidi, ndio hivyo hivyo nilikuwa nagundua kwamba, ufalme wa Mungu ni **mpana zaidi kuliko hata kanisa**. Yesu alisema, "Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia." (Mathayo 12:28). Kama kanisa lilizaliwa wakati wa Pentekoste na ufalme tayari ulishakuja, basi kanisa na ufalme haviwezi kufanana.

Fikra hizi zilinilazimisha mimi kuuangalia ufalme kutokea kwenye mkabala wa jumla. Hicho ndicho ninachotaka kukifanya sasa.

## Ufalme wa Mungu katika Bustani ya Edeni

Wakati wa uumbaji, Mungu akasema, "Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi." (Mwanzo 1:26). Wakati Mungu alipoumba wanadamu aliwafanya wafanane na yeye kwa namna fulani.

Kama Mungu aliumba wanadamu kwa mfano wake, inaonekana kuwa busara kwamba Mungu ataumba eneo la wanadamu la kuishi ambalo kwa namna fulani litafanana na mazingira ambayo Mungu mwenyewe aliishi. Kama hivyo ni kweli, basi Bustani ya Edeni ilikuwa imetengenezwa katika sura ya mbinguni. Bustani ya Edeni ilifafanaje?

- Hapakuwa na dhambi au kosa la maadili pale; palikuwa kama mbinguni.
- Hapakuwa na maradhi au kifo au huzuni pale; palikuwa kama mbinguni.
- Hapakuwa na kitu kisichofurahisha pale; palikuwa ni mahali palipokuwa pamekamilika kama mbinguni.
- Hapakuwa pamekaa bila mpangilio pale. Kila kitu kilikuwa kinafanya kazi vizuri kama kilivyokuwa kimeumbiwa kiwe; palikuwa kama mbinguni.

Bustani ya Edeni palikuwa ni ufalme wa Mungu wa duniani kwa wakati ule. "Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni chema sana." (Mwanzo 1:31). Haya yalikuwa ndiyo maoni ya kwanza kuhusiana na ufalme wa Mungu hapa duniani. Kitu kinapokuwa ni kizuri, kila kitu kinakuwa mahali pake na katika utaratibu uliokaa sawasawa. Kila kitu

kwenye dunia hii kiko kama Mungu alivyotaka kiwe. Hii ilionyesha mpangilio, uzuri, na ukamilifu uliobainishwa na makao ya Mungu mbinguni. Kwa hiyo, kama unataka kujua ufalme wa Mungu ungefananaje hapa duniani, jifunze kuhusu Bustani ya Edeni.

**Kupotea kwa Ufalme wa Mungu katika Bustani ya Edeni.**

Kwa uanaglifu mkubwa Mungu alitoa maelekezo ya jinsi ya kudumisha na kuhifadhi ufalme wa Mungu duniani. Kwa bahati mbaya, mwanadamu alikiuka uaminifu wa Mungu mtakatifu na akatenda dhambi dhidi ya Mungu. Jambo hili lilisababisha hali kuu mbili ngumu sana.

Kwanza, dhambi iliingia ulimwenguni na kusababisha sura ya Mungu aliyokuwa nayo mwanadamu kuharibika. Pili, kwa kuwa wanadamu walikuwa wamepoteza sura hiyo ya Mungu, walikuwa hawana sifa tena ya kuishi mahali pakamilifu ambako kimsingi palionekana ni sura ya eneo ambalo Mungu alikuwa akiishi. Edeni haikuwa tena sehemu sahihi ya kuishi kwa mwanadamu.

Kwa hiyo, Mungu aliwafukuza kutoka katika eneo hilo akailaani nchi sawa na alivyomlaani mwanamume na mwanamke. Mundu "aliilaani ardhi" ili kwamba itengeneze "miiba na michongoma." Ulimwengu ulipoteza sehemu kubwa ya uzuri wake, utulivu, uzalishaji na usalama. Jinsi ambavyo wanadamu ni kivuli tu cha kile ambacho awali chenyewe kilikuwa ni kitakatifu, kadhalika na ardhi ni kivuli tu cha kile Mungu alichokiumba kiwe. Kuyaweka haya ili yaowane na mtiririko wa mahubiri haya: Ufalme wa Mungu duniani ulibomoka.

- Kile Mungu alichokuwa amekijenga kiliharibiwa.
- Kile Mungu alichokuwa amekifanya kizuri cha kuvutia, sasa kikawa na sura mbaya.
- Kile Mungu alichokuwa amekiumba kiwe kitulivu, sasakimekuwa ni maumivu.
- Kile Mungu alichokuwa amekiunda kiwe kitakatifu, sasa kimekuwa chenye dhambi na kilichojawa na uharibifu.
- Kile Mungu alichokuwa amekipanga kwa ajili ya ubinadamu na ulimwengu sasa havitaweza kutokea tena.

Hata hivyo, Mungu hawezi kupoteza chochote. Hawezi akashindwa. "Hapana hekima, wala ufahamu, Wala shauri, juu ya Bwana." (Mithali 21:30). Shetani alijaribu lakini kamwe hawezi akamshinda Mungu.

- Ni nani awezaye kubatilisha kile ambacho Mungu amekifanya?
- Ni nani awezaye kusema hapana kwa kile ambacho amesema ndiyo?
- Ni nani awezaye kuharibu kile ambacho Mungu amekiumba?

Mungu hatakubali kushindwa. Mungu anao uwezo wa kubadilisha na kurejesha vitu ambavyo vimekwenda vibaya, Mungu ni bwana wa kuboresha-kuokoa-kurejesha-kutakasa-kufanya upya- na kukarabati.

Mungu aliweka mpango wa kurejesha tena ufalme wake duniani.

> Maongeo ya enzi yake na amani Hayatakuwa na mwisho kamwe, Katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; Kuuthibitisha na kuutegemeza Kwa hukumu na kwa haki, Tangu sasa na hata milele. Wivu wa Bwana wa majeshi ndio utakaotenda hayo. (Isaya 9:7).

Hata kabla ya Adamu na Hawa kuanguka katika dhambi, Mungu alikuwa na mpango wake wa kurejesha na kuujenga upya ufalme wake hapa ulimwenguni. Mojawapo ya kusudi muhimu sana la Biblia ni kuelezea urejeshwaji wa ufalme wa Mungu duniani ili uwe kama ilivyo kule mbinguni. Hatua ya urejeshwaji bado ni endelevu. Tunaona hatua hiyo kuanzia Mwanzo 12:1-3

## Ufalme wa Mungu na Abrahamu

Abrahamu alikuwa katika Uri ya Wakaldayo alipopokea ujumbe huu:

> Bwana akamwambia Abramu, Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayokuonyesha; nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka; nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa. (Mwanzo 12:1-3).[357]

Ingawaje neno "Ufalme" halitumiki hapa, tunaamini kwamba Mungu anaanza kurejesha ufalme wake duniani kwa sababu ya ahadi kuu mbili katika taarifa hii.

### Mungu aliahidi Kuanzisha Taifa Kubwa kutoka katika Israeli

Taifa na ufalme havifanani lakini vinashabihiana katika mambo mengi. Inashangaza kwamba takribani theluthi inayofuata ya Agano la Kale imetumika kuelezea kuanzishwa kwa taifa hili kubwa.

Katika ujenzi wa taifa hili, tunamwona Mungu akitumia kanuni mbili ambazo anatazamia kuzitumia katika mradi huu.

1. Wakati Mungu anapofanya kazi katika dunia hii, siku zote hufanya akitumia wanadamu. Mungu kwa kawaida hatumi malaika kuja kufanya kazi ambazo anataka kuzifanya katika ulimwengu huu

2. Wakati Mungu anapofanya kazi katika dunia hii, anafanya katika njia ngumu, katika njia ya polepole, katika njia endelevu na katika njia ambayo ni kinyume kabisa na njia zetu za kufanyia mambo yetu. Ujenzi wa taifa ulikumbwa na vikwazo vingi. Hata hivyo, hatimaye ikawa ukweli.

---

[357] Msisitizo umeongezwa.

Sifikiri kwamba taifa hilo lilikuwa ni ukamilifu kamili wa urejeshaji wa Mugnu wa ufalme wake hapa duniani. Hata hivyo, ilikuwa ni hatua katika mwelekeo huo. Ufalme umethibitisha kwamba Mungu anao uwezo wa kutawala watu wake katika dunia hii. Kwa bahati mbaya, kwa sababu za kibinadamu, mafanikio yalifanikiwa kwa sehemu tu.

**Mungu Aliahidi kwamba Wazao wa Abrahamu watakuwa ni Baraka kwa watu wa dunia hii.**

"…na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa." (Mwanzo 12:3). Ahadi hii ilitimia wakati wa kuja kwake Yesu.

## Ufalme wa Mungu na Yesu

Taarifa ya kwanza anayoielezea Luka kuhusiana na Yesu baada ya ubatizo na kujaribiwa ni kutembelea sinagogi la Nazareti. Yesu alikwenda kwenye sinagogi la nyumbani kwake Nazareti na akajitolea kusoma maandiko. Somo la siku hiyo lilikuwa linatoka katika isaya 61

> "Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa, Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa. Akakifunga chuo, akamrudishia mtumishi, akaketi; na watu wote waliokuwamo katika sinagogi wakamkazia macho. Akaanza kuwaambia, Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu." (Luka 4:18-21).

Katika siku za mwanzo za huduma yake, Yesu alitoa angalizo zito kwamba alikuwepo ili aendeleze hatua ya matengenezo ambayo Baba amekuwa akiyafanya kwa mamia ya miaka iliyopita.

- Kwa sababu za matokeo ya dhambi, dunia imekuwa maskini kwa maana ya kiroho na ufahamu halisi kwa pamoja. Hata hvyo, Yesu alitangaza kwamba amepakwa mafuta "kuwahubiri maskini habari njema."
- Kwa sababu ya anguko, jamii ya wanadamu imekuwa wafungwa kwa ajili ya dhambi. Hata hivyo, Yesu alisema alikuja ili "kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao."
- Kwa sababu ya anguko, jamii ya wanadamu imekuwa vipofu kiroho, ikimaanisha kwamba watu hawana uwezo wakuelewa tena ukweli. Baadhiya watu wamekuwa vipofu kabisa kimwili. Hata hivyo, Yesu amekuja kwa ajili ya "vipofu kupata kuona tena."
- Kwa sababu ya anguko, ibilisi na maajenti wa ibilisi wamewagandamiza watu kwa njia nyingi. Hata hivyo, Yesu alisema kwamba amekuja ili "Kuwaacha huru waliosetwa."

Yesu alikuwa anasema kwamba kusudi lake lilikuwa ni kugeuza laana nyingi zilizokuwepo duniani kwa ajili ya dhambi. Kulisema hili kwa njia nyingine ni kwamba Yesu alikuwa amekuja duniani ili kuendeleza hatua za ujenzi za ufalme wa Mungu duniani. Na kuweza kulisema jambo hili kwa njia nyingne zaidi ni kwamba, Yesu alikuja duiani kuikamilisha ahadi ya pili kwa Abrahamu – kuwa baraka kwa watu wengine wote wa dunia hii. "Wakati umetimia,' alisema. "na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili!'" (Marko 1:14-15). Ufalme ndio uliokuwa kiini cha mafundisho ya Yesu katika huduma yake yote.

## Ufalme wa Mungu na Kanisa

Njia ambayo Mungu aliitumia kufanya kazi katika Agano la kale ilikuwa taifa la Israeli. Katika Agano Jipya, kanisa limekuwa ndiyo njia ya Mungu ya utendaji kazi. Kanisa lilikuwa na ukuu zaidi kuliko Agano la Kale kwa sababu chache zifuatazo:

- Kanisa lilihusisha atu wote wa duniani, na siyo Wayahudi tu.
- Kanisa lilikuwa na fursa ya kufikiwa na Roho Mtakatifu kwa kila mtu wakati katika kipindi cha Agano la Kale ni watu wachache tu mashuhuri waliokuwa na uwezo wa kumfikia Roho mtakatifu.
- Kanisa lilileta msisitizo mpya wa uhusiano binafsi wa mtu na Mungu.
- Kanisa lilitilia mkazo wa kuabudu "katika roho na kweli" kuliko kupitia dhabihu za wanyama na sherehe gumu au isiyobadilika.

## Masomo kutoka kwa Yesu kuhusu Ufalme wa Mungu

Kuna baadhi ya masomo tunayoweza kujifunza kuhusiana na ufalme kutoka katika maisha ya Yesu na mafundisho yake.

**(1) Ufalme wa Mungu hauna mipaka ya kijiografia lakini ipo kila mahali alipo Mfalme.**

- Wakati Yesu alipotembelea kwenye harusi, alitoa mvinyo kwa sababu ufalme wake ulienea eneo lile kutokana na uwepo wake.
- Wakati Yesu alipokutana na watu wagonjwa aliwaponya kwa sababu ufalme wake ulienea hadi kwenye maradhi na magonjwa.
- Wakati Yesu alipokutana na watu wenye njaa, aliwapa chakula kwa sababu ufalme wake uliunganika na mahitaji ya msingi ya watu.

Yesu anataka apanue ufalme wake leo kujumisha maeneo yote ambayo wafuasi wake wanaenda. Inakuwa ni sehemu ya ufalme wake kwa sababu watu wa mfalme wako pale. Hilo ni jukumu kama sehemu ya familia ya kifalme. Ni lazima tuhakikishe kwamba sheria ya Yesu inasambaa hadi kwenye eneo letu maalumu, eneo la dunia ambalo sisi tuna ushawishi juu yake.

- Ni lazima tuanzishe ufalme wa Mungu kwenye familia zetu.
- Ni lazima tuanzishe ufalme wa Mungu juu kwenye jamii zetu.
- Ni lazima tuanzishe ufalme wa Mungu kwenye kazi zetu na maeneo yetu ya kazi.
- Ni lazima tuanzishe ufalme wa Mungu kwenye serikali zetu za mitaa na serikali ya kitaifa.
- Ni lazimakwa uhakika tuanzishe ufalme wa Mungu kwenye makanisa yetu na mashirika/jumuia zetu za Kikristo.

Mahali popote ambapo mwana wa mfalme anaishi, ufalme ni lazima uanzishwe. Hivyo, kwenye nyumba zetu na ofisi zetu kunawakilishaufalme wa Mungu. Mahusiano yetu na wenzetu wa upande wetu huwakilisha ufalme. Petro aliandika,

> Wapenzi, nawasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na roho. Mwe na mwenendo mzuri kati ya Mataifa, ili, iwapo huwasingizia kuwa watenda mabaya, wayatazamapo matendo yenu mazuri, wamtukuze Mungu siku ya kujiliwa. (1 Petro 2:11-12).

Mungu anataka wasiokuwa bado kwenye ufalme wauone ufalme ndani yetu. Wanaweza tu kuona ufalme katika maisha yetu kama tutaishi kulingana na kanuni za ufalme. Je, watu wanaona ufalme wa Mungu ndani yako?

**(2) Ufalme wa Mungu siyo kwa ajili ya kikundi maalumu cha watu bali kwa watu wote watakaomfuata yeye.**

Wakati Yesu alipomponya mtumishi wa askari (Mmataifa) wa Kirumi, alisema

> Nami nawaambieni, ya kwamba wengi watakuja kutoka mashariki na magharibi, nao wataketi pamoja na Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo katika **ufalme wa mbinguni**. (Mathayo 8:11).[358]

Ufalme ulikuwa ni kwa ajili ya watu wote, bila kujali rangi, lugha, au historia ya nyuma (*usuli*) ya kabila. Kwa kuwa Mungu anachagua watu kutoka katika aina zote za historia za nyuma, tunapaswa tuwakubali watu kutoka katika aina zote za (*usuli*)- historia za nyuma ambazo ni wafuasi wa Yesu. Ubaguzi wa rangi, ukabila au utendaji wa vikundi viivyojitenga siyo sehemu ya ufalme wa Mungu.

**(3) Ufalme wa Mungu haufungamani na ikulu za kifahari na uvaaji wa mavazi ya nje bali thamani chanya za kijamii**

Tunapofikiria kuhusu falme mbalimbali, mara nyingi tunafikiria kuhusu nyumbani kwa mfalme –ikulu. Ikulu husema kitu kwa ajili ya mfalme. Hata hivyo, Yesu alisema, "Mbweha

---

[358] Msisitizo umeongezwa..

wana pango, na ndege wa angani wana viota; lakini Mwana wa Adamu hana pa kulaza kichwa chake." (Mathayo 8:20). Ufalme wa Yesu haujulikani kwa maonyeshoya utajiri au majengo ya kifahari au mavazi ya kigeni au mapambo ya vito vya thamani ya juu. Ufalme wa Kristo unajulikana siyo kupitia hivi vitu vya nje, bali kwa maadili chanya.

**(4) Ufalme wa Mungu hajulikani kwa mabaya na uharibifu bali kwa haki na ukweli**

Yesu alifundisha, "Haki yenu isipozidi hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni." (Mathayo 5:20). Haki hapa siyo kipengele cha theolojia, bali wema wa vitendo.Mafarisayo walikuwana haki ya nje iliyoundwa ili kuwapendezesha watu na kupata heshima. Haki ya kweli ni lazima iende mbali zaidi kuliko haki ya nje na wema wa nje. Ufalme wa Yesu unajulikana na wale wanaofanya mambo ya halali. Ufalme wa Mungu unaweza kustawi mahali palipo na utele wa vitu vingi. Ufalme wa Mungu unaweza kustawi mahali palipo na upungufu. Hii ni kweli kwa sababu ufalme wa Mungu siyo wa kimwili, au wa mali bali ni ufalme wa maadili na wema.

**(5) Ufalme wa Mungu haujulikani kwa kiburi na sherehe bali kwa unyenyekevu na huduma.**

Yesu alisema, "Heri walio maskini wa roho; Maana ufalme wa mbinguni ni wao." (Mathayo 5:3). Neno "maskini wa roho" linahusika na unyenyekevu. Unyenyekevu kwa kawaida haufungamani na viongozi wa kisiasa wa ulimwengu, Wanasiasa ni lazima wawaeleze wengine kwa nini wao ni bora kuliko wapinzani wao. Hata hivyo, ufalme wa Yesu unajulikana kwa unyenyekevu, kutokuwa na ubinafsi na kuwainua wengine.

Watu walioko katika familia za kifalme mara nyingi wanadekezwa na kusifiwa sana kiasi kwamba wanakuwa na majivuno na kujiona kwamba wao ni bora na muhimu kuliko watu wengine wote. Wanaweza kuwa watu wa kiburi katika tabia zao. Hata hivyo, Yesu alisema, "kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, **bali kutumika**, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi." (Mathayo 20:28).[359] Mfalme aliwachukua watu hawa kila mahali alipokwenda na kuwafundisha kile alichokijua.Mfalme alikuwa hata yuko tayari kuwatawadha wanafunzi wake miguu. Tunaonyesha asili ya ufalme huu kupitia unyenyekevu na wepesi, na siyo kwa mambo yaliyochanganuliwa na ugumu wa vitu.

**(6) Ufalme wa Mungu unakua siyo kupitia uzao wa kibinadamu bali kupitia kazi za wafuasi wa Kristo.**

Yesu alisema, "Nami nitakupa wewe **funguo za ufalme wa mbinguni**; na lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lo lote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni." (Mathayo 16:19).[360] Wakati ufalme ulioumbwa na

[359] Msisitizo umeongezwa.
[360] Msisitizo umeongezwa.

Mungu ulipoangukia kwenye dhambi na giza ukaharibika na kuhitaji kufanywa tena upya, ilimbidi Mungu aurejeshe tena ulimwengu. Mungu alikuwa amempa mwanadamu jukumulakuwaleta watu kwenye ufalme wake na kuujenga ufalme wake kwenye maeneo yote ya kijamii. Mungu hatatuma malaika ili kuujenga ufalme wake. Atakutumia wewe na mimi kuifanya kazi hii. Jukumu la watu walio sehemu ya ufalme huu ni:

- Kuwaleta watu wengine kwenye ufalme.
- Kuujenga ufalme mahali popote walipo.
- Kutekeleza kanuni zote za ufalme katika maeneo yote ya jamii.

Hili ni jukumu letu na upendeleo kwetu. Tujitahidi kuwa wepesi katika kuwaleta wengine kwenye ufalme wa Mungu.

## Kuifanyia mazoezi Injili ya Ufalme katika Matendo

Sasa tutaangalia ni kwa jinsi gani kanisa la mwanzo lilijaribu kutimiza ombi la Yesu la kuona jinsi ufalme uliokuwa umeanzishwa duniani utakavyokuwa kama ilivyo mbinguni. Chukua kumbukumbu ya mifano hii:

### Kuwahudmia Wahitaji

Mungu siku zote amekuwa na eneo maalumu kwa ajili ya wahitaji katika jamii, wakiwemo wajane, yatima na maskini. Haishangazi kuona wafuasi wa Yesu wakijiingiza kwa vitendo katika kazi ya kuujenga ufalme wa Mungu hapa duniani.

Katika Matendo 6, tunaona waumini wa mwanzo wakichukua jukumu la kuwatunza wajane. Mwanamke Mkristo aitwaye Dorkasi alikuwa “alikuwa amejaa matendo mema na sadaka alizozitoa.” (Matendo 9:36). Paulo na Barnaba walipeleka fedha na vyakula vya msaada kwa Wakristo wa Yerusalemu waliokuwa wanateseka kwa njaa (Matendo 11:29). Baadaye katika Matendo, Paulo alichukua sadaka na matoleo kutoka katika makanisa ya Makedonia na Akaya kwa ajili ya wahitaji wa Yerusalemu. (Matendo 24:17).

Kanuni ya ufalme wa Mungu kuhusu mahitaji yetu yamewekwa kwa muhtasari kwenye maelezo ya Paulo katika 2 Wakorintho 8:13-15:

> Maana sisemi hayo, ili wengine wapate raha nanyi mpate dhiki; bali mambo yawe sawasawa; wakati huu wa sasa wingi wenu uwafae upungufu wao, ili na wingi wao uwafae ninyi mtakapopungukiwa; ili mambo yawe sawasawa. Kama ilivyoandikwa, Aliyekusanya vingi, hakuzidi, wala yeye aliyekusanya vichache hakupungukiwa.

Kuna njia nyingi tunazoweza kutumia ili kusaidia wahitaji ambazo hazihitaji uwezo wa miujiza. Hatupaswi tumsubiri Mungu atupatie mahitaji yetu kwa njia za miujiza kabla hutujajaribu kushughulikia hali za madhaifu ya jamii yetu.

### Kushikilia Haki

Moja ya sehemu muhimu sana ya ufalme wa Mungu ni Haki. Ni kwa jinsi gani kanisa la mwanzo lilishughulikia suala la haki katika jamii? Wakati Petro na Yohana walipopigwa

marufuku ya kuhubiri kwa jina la Yesu, kwa upole waliwajibu viongozi wa Kiyahudi kwamba kwa kufanya hivyo watakuwa wanafanya uasi wa kiraia wa kutokutii kwa sabau wameagizwa kuihubiri injili. Waliwaambia wale viongozi, "Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu." (Matendo 5:29).

Wakati Paulo alipokamatwa na kupigwa kinyume cha sheria kule Filipi alikatalia kutoka jela hadi maafisa waliomweka pale waje na wamruhusu aondoke. Hiki hakikuwa kitendo cha uinjilisti. Hakuwa anajaribu kuwaleta watu kwa Kristo. Hiki kilikuwa ni kitendo kilichohusika na haki. Paulo alikuwa anawataka hawa maafisa waishi kwa mujibu wa kanuni za haki katika jamii.

Paulo hakuona tu kwamba kazi yake ni kufanya uinjilisti na kuanzisha makanisa. Aliishi katika jamii iliyokuwa na maradhi na alitumia kila nafasi aliyopata kutibu hayo maradhi, likiwemo ukosefu wa haki.

**Kurejesha Afya**

Paulo kama Bwana wake, alikuwa na uwezo wa kuponya kwa miujiza kwa baadhi ya watu. Hata hivyo, hiyo siyo njia peke yake aliyotumia. Paulo alimwandikia Timotheo, "Tokea sasa usinywe maji tu lakini tumia mvinyo kidogo, kwa ajili ya tumbo lako, na magonjwa yakupatayo mara kwa mara." (1 Timotheo 5:23). Mvinyo uliotengenezwa kutokana na matunda ya mzabibu una madini chuma mengi ndani yake. Ukitumiwa kwa kiasi, ni mzuri sana kwa ajili ya damu. Paulo alitoa maelekezo ya njia ya uponyaji kwa ajili ya kumsaidia Timotheo aweze kupona kutokana na maradhi yake.

Baada ya Yesu kuwatuma wanafunzi wake kwenye ziara ya mafunzo, aliwaambia, "Njoni ninyi peke yenu kwa faragha, mahali pasipokuwa na watu, mkapumzike kidogo." (Marko 6:31). Yesu alitambua kwamba kupumzika kulihitajika ili kufurahia afya njema.

Yakobo alitoa maelezo ya kuvutia sana kuhusu uponyaji.

> Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana. Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Bwana atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa. (Yakobo 5:14).

Kuna maneno mawili ya "upako" kwa Kiyunani, *aleipho* and *chrio*.

1. *Chrio* ni jina kwa ajili ya upako wa sherehe.
2. *Aleipho* ni neno kwa ajili ya matumizi ya mafuta kama dawa au kujipaka

Mafuta yalikuwa ni ya mtu wa kawaida ya huduma Ya kwanza katika ulimwengu wa zamani. Wakati Msamaria mwema alipomkuta yule mtu aliyekuwa amejeruhiwa vibaya na majambazi yenye silaha, alimwekea mafuta kwenye vidonda vyake. Mungu anaweza kuchagua kumponya mtu kwa njia ya miujiza kama majibu ya maombi *(chrio).* Hata hivyo, anaweza pia kuchagua kumponya mtu kwa njia ya madawa ya asili *(aleipho)*

**Hitimisho**

Mungu anataka kuanzisha ufalme wake duniani kama ule ulioko mbinguni. Ufalme huo unatawaliwa kwa kanuni, siyo zenye tabia za kijiografia, za kilugha au za kisiasa. Kwa kiwango kile tunachofundisha na kutekeleza kanuni za ufalme wa Mungu, tunakuwa tumeanzisha ufalme wa Mungu katika eneo hilo la maisha.

# Vianzo Vilivyopendekezwa

Kozi hii inahusu kujifunza maisha na huduma ya Yesu kama mfano wa kuigwa kwa maisha na huduma nyakati za sasa. Siyo mafunzo ya undani kuhusiana na Vitabu vya Injili. Badala yake, kozi hii inaangalia kwenye vipengele vilivyochaguliwa vya huduma ya Yesu ili kupata mafunzo ya huduma kwa wakati wa leo. Kama unataka kujifunza maisha yote ya Yesu Kristo, ninapendekeza kwako vitabu vilivyoorodheshwa hapa chini. Vitabu hivi ndivyo msingi wa vianzo vya kozi hii. Isipokuwa tu kwa tanbihi za wazi nilizonakilisha chini, sijanakilisha vitabu hivi katika masomo haya.

Vitabu vya *Jesus According to Scripture* cha Darrell Bock na *The Words and Works of Jesus Christ* cha J. Dwight Pentecost ni masomo kamilifu ya **kujifunza Maisha ya Yesu**. Kati ya vitabu vyote katika orodha hii, kitabu cha Ajith Fernando, *Jesus Driven Ministry* na cha Robert Coleman *The Master Plan of Evangelism* vimekuwa na mguso mkubwa sana kwangu katika mimi kufahamu **muundo wa huduma ya Yesu**. Ninapendekeza vitabu hivi kwenu kwa ajili ya mafunzo yenu.


Blomberg, Craig. *Jesus and the Gospels*. Nashville: Broadman & Holman, 1997.

Bock, Darrell L. *Jesus According to Scripture*. Grand Rapids: Baker Academic, 2002.

Coleman, Robert E. *The Mind of the Master*. Colorado Springs: Waterbrook Press, 1977.

Coleman, Robert E. *The Master Plan of Evangelism*. Grand Rapids: Baker Books, 1993.

Fernando, Ajith. *Jesus Driven Ministry*. Wheaton, Illinois: Crossway, 2002.

Pentecost, J. Dwight. *The Words and Works of Jesus Christ*. Grand Rapids: Zondervan, 1981.

Robertson, A. T. *Harmony of the Gospels*. New York: Harper & Row Publishers, 1922. Available online at http://www.gutenberg.org/files/36264/36264-h/36264-h.htm

## Maisha na Huduma ya Yesu
## Kumbukumbu ya Kazi Zilizofanywa

Jina la Mwanafunzi ______________________________________

Kwenye jedwali hapa chini, dhihirisha kwa alama za jina lako ukionyesha ni ulikamilisha kazi za kufanya ulizopewa. Kazi zote ulizopewa kufanya ni lazima zikamilishwe kwa ukamilifu ili uweze kupatiwa cheti cha kuhitimu kutoka Shepherds Global Classroom.

| Somo | Kazi ya kufanya 1 | Kazi ya kufanya 2 | Kazi ya kufanya 3 |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | | | |
| 6 | | | |
| 7 | | | |
| 8 | | | |
| 9 | | | |

## Ombi la Kupewa Cheti Kutoka Shepherds Global Classroom

Maombi kwa ajili ya kupewa Cheti cha Kufuzu kozi kutoka Shepherds Global Classroom yanaweza kukamilishwa kupitia ukurasa wetu wa wavuti www.shepherdsglobal.org. Vyeti vitatumwa kwa mfumo wa kidigitali kutoka kwa Raisi wa SGC kwenda kwa wakufunzi na wawezeshaji ambao watakamilisha maombi hayo kwa niaba ya mwanafunzi (au wanafunzi).

# Maelezo ya Kozi za
# Darasa la Wachungaji la Kimataifa

### Kuchambua Agano la Kale

Kozi hii inafundisha maudhui muhimu na mafundisho ya vitabu 39 vya Agano la Kale.

### Kuchambua Agano Jipya

Kozi hii inafundisha maudhui muhimu na mafundisho ya vitabu 27 vya Agano Jipya.

### Maisha na Huduma ya Yesu

Kozi hii inasoma maisha ya Yesu kama mfano kwa huduma na uongozi katika karne ya 21.

### Warumi

Kozi hii inafundisha theolojia ya wokovu na dhamira kama inavyoelezewa katika vitabu ya Warumi, kujadili masuala kadhaa ambayo yamekuwa ya kutatanisha katika kanisa.

### Kanuni za Tasfiri ya Kibiblia

Kozi hii inafundisha kanuni na njia za kutafsiri Biblia vizuri ili kuongoza maisha yetu na mahusiano na Mungu.

### Imani za Kikristo

Hii ni kozi ya theolojia ya kimfumo, inayoelezea mafundisho ya Kikristo kuhusu Biblia, Mungu, Mwanadamu, Kristo, Wokovu, Roho Mtakatifu, Kanisa, na Vitu vya Mwisho.

### Eskolojia

Kozi hii inafundisha vitabu vya kibiblia vya Danieli na Ufunuo pamoja na sehemu zingine za maandiko ya kinabii na inasisitiza mafundisho muhimu kama vile kurudi kwa Kristo, hukumu ya mwisho, na ufalme wa Mungu wa milele.

### Mafundisho na Mazoezi ya Maisha Matakatifu

Kozi hii inatoa maelezo ya kibiblia ya maisha matakatifu ambayo Mungu anatarajia na uwezesho kwa Mkristo.

**Mafundisho na Mazoezi ya Kanisa**

Kozi hii inaelezea ubunifu na mpango wa Mungu kwa kanisa na masomo ya kibiblia kama vile uanachama wa kanisa, ubatizo, ushirika, zaka, na uongozi wa kiroho.

**Historia ya Kanisa I**

Kozi hii inaelezea jinsi kanisa lilivyotimiza dhamira yake na kutunza mafundisho muhimu kuanzia kipindi cha kanisa la mwanzo mpaka Matengenezo.

**Historia ya Kanisa II**

Kozi hii inaelezea jinsi kanisa lilivyopanuka na lilivyopitia changamoto kuanzia kipindi cha Matengenezo mpaka nyakati za kisasa.

**Uundaji wa Kiroho**

Katika kozi hii wanafunzi wanajifunza kuwa na mitazamo ya yesu, kuwa na Mungu kama Yesu alivyokwa na baba yake, kujinyenyekeza kama Yesu alivyofanya, kufanya nidhamu ya kiroho na binafsi ya yesu, kuvumilia mateso kama Yesu alivyofanya, na kushiriki katika jamii ya Kikristo (Kanisa) lililoundwa na Yesu.

**Huduma ya Uongozi**

Kozi hii inahimiza tabia ya Kikristo wakati inafundisha viongozi kuongoza mashirika kupitia mchakato wa kugundua maadili, kutambua kusudi, kushirikishana maono, kuweka malengo, kupanga mkakati, kuchukua hatua, na kupitia mafanikio.

**Kanuni za Mawasiliano**

Kozi hii inafundisha theolojia ya mawasiliano, njia za kuzungumza kwa ufanisi, na njia za kuandaa na kuwasilisha mahubiri ya kibiblia.

**Uinjilisti wa Kibiblia na Uanafunzi**

Kozi hii inatoa kanuni za kibiblia ambazo huongoza mbinu za uinjilisti. Inaelezea aina za uinjilisti na kutoa masomo ya kutumia kufundisha wapya waliobadilishwa.

**Utangulizi wa Elimu ya Kuitetea Imani**

Kozi hii inafundisha misingi ya kisayansi, kihistoria, na kifalsafa kwa mtazamo wa ulimwengu wa Kikristo, na inaonyesha jinsi gani imani ya Kikristo ni thabiti katika hoja na hali halisi.

**Dini za Ulimwengu na Ibada**

Kozi hii huumpa muumini wa kiinjili uelewa wa mafundisho na majibu sahihi kwa vikundi kumi na nane vya dini.

**Utangulizi wa Kuabudu Kikristo**

Kozi hii inaelezea jinsi gani kuabudu huathiri nyanja zote za maisha ya muumini na hutoa kanuni ambazo humuongoza mtu binafsi na mkutano wote mazoezi ya kuabudu.

**Kuishi Kikristo kwa Vitendo**

Kozi hii hutumia kanuni za kiroho kwa utumiaji wa fedha, mahusiano, mazingira, mahusiano na serikali, haki za binadamu, na maeneo mengine ya kuishi kwa vitendo.